


**KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA
MWAKA WA FEDHA 2012/2013**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam. Simu ya Upepo:
'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527,
Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. FA.27/249/01/2012/2013/42/01
2014

Tarehe 28 Machi,

Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
Sanduku la Posta 9120,
DAR ES SALAAM.

**Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu
wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya
Umma kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (ilivyorekebishwa 2005), nawasilisha kwako ripoti yangu ya saba ya mwaka ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kama ilivyoielezewa katika Sehemu ya 3 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Ripoti hii inajumuisha taarifa za ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa vipindi vilivyoishia tarehe 30 Septemba, 2012, 31 Disemba, 2012 na tarehe 30 Juni, 2013.

Nawasilisha kwako ripoti hii kwa ajili ya kuiwasilisha Bungeni kulingana na matakwa ya sheria.

Ludovick S.L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(Imeanzishwa kwa Mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

Kazi na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali vimeainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (ilivyorekebisha 2005) na kufafanuliwa na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 (ilivyorekebisha) na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

Dira ya Ofisi

Kuwa kituo bora kwenye ukaguzi wa hesabu katika sekta ya ukaguzi wa umma.

Lengo la Ofisi

Kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji unaozingatia thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Katika kutoa huduma zenye ubora unaostahili, Ofisi inaongozwa na vigezo vya misingi vifuatavyo:

Kutopendelea	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki.
Ubora	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalam inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma vya Kimataifa.
Uadilifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha maadili ya kazi kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria.

Kujali Watu	Tunajali mahitaji ya wadau kwa kujenga utamaduni mzuri wa kujali wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na tija.
Ubunifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya Taasisi.
Matumizi bora ya Rasilimali za Umma	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayozingatia matumizi bora ya rasilimali zilizokabidhiwa kwake.

YALIYOMO

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	v
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi	v
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania	v
Dira ya Ofisi.....	v
Lengo la Ofisi	v
Yaliyomo	vii
Vielelezo	ix
Shukrani	xi
Muhtasari.....	xv
SURA YA KWANZA	1
Utangulizi na Taarifa za Jumla.....	1
1.0 Uanzishwaji wa Ofisi ya Ukaguzi Kisheria	1
SURA YA PILI	9
Aina za Hati za Ukaguzi Zilizotolewa	9
2.0 Utangulizi.....	9
2.2 Misingi ya Hati Zilizotolewa.....	14
SURA YA TATU	19
Muhtasari wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya.....	19
Ukaguzi wa Miaka Iliyopita	19
3.0 Utangulizi.....	19
SURA YA NNE.....	37
Masuala Muhimu ambayo Hayakutolewa Taarifa katika Ripoti ya Mwaka Uliopita	37
4.0 Utangulizi.....	37
SURA YA TANO	49
Usimamizi wa Sheria ya Manunuzi na Mikataba	49
5.0 Utangulizi.....	49
SURA YA SITA	69
Usimamizi wa Mali za Umma.....	69
6.0 Utangulizi.....	69
SURA YA SABA	85
Usimamizi wa Rasilimali Watu.....	85
7.0 Utangulizi.....	85

SURA YA NANE	97
Utawala Bora.....	97
8.0 Utangulizi.....	97
SURA YA TISA	117
Uwekezaji wa Serikali na Ukaguzi Baada ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma	117
9.0 Utangulizi.....	117
SURA YA KUMI.....	149
Matokeo ya Kaguzi Maalum	149
10.0 Utangulizi.....	149
SURA YA KUMI NA MOJA	165
Hitimisho na Mapendekezo	165
Viambatisho	184

VIELELEZO

Kielelezo 1:	Mgawanyo wa Kazi za Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka 2012/2013	8
Kielelezo 2:	Hati za ukaguzi zilizotolewa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 zimeonyeshwa kwenye kielelezo kifuatacho:	13

JEDWALI

Jedwali 1:	Hati zilizotolewa kwa kipindi cha miaka minne mfululizo kutoka 2009/2010 hadi 2012/2013 kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:	13
------------	--	----

SHUKRANI

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za mara kwa mara za kutilia msisitizo maswala mbalimbali yanayoandikwa kwenye ripoti zangu.

Shukrani zangu za dhati pia ziende kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wenyeviti na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge na Wabunge wote kwa kujitoa kwa dhati kujadili na kutoa maelekezo ya mambo yaliyojitokeza kwenye ripoti zangu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa ajili ya utekelezaji.

Napenda, kutoa shukrani zangu za dhati kwa Bodi za Wakurugenzi, Watendaji Wakuu na wafanyakazi wote wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zilizokaguliwa, kwa ushirikiano walioutoa kwa wakaguzi wakati wa zoezi zima la ukaguzi.

Vilevile, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mpiga Chapa kwa kukamilisha uchapaji wa ripoti hii na hivyo kuifanya itoke na kuweza kupelekwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge kwa muda uliowekwa kisheria.

Zaidi, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wabia wa maendeleo ambao wamekuwa wakitoa msaada kwa Ofisi yangu hususani Mpango wa Maboresho wa Menejimenti ya Fedha za Umma (PFMRP) chini ya usimamizi wa Benki ya Dunia, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden (SNAO), Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Watu wa Sweden (SIDA), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID) ya Uingereza, Benki ya Maendeleo ya Africa (ADB), Wakala wa Maendeleo wa Kimataifa wa Canada (CIDA), Umoja wa Ofisi za Taifa za Ukaguzi za Nchi za Kiafrika zinazotumia Kiingereza (AFROSAI-E), Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya India (SAI India) kupitia Serikali ya India, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya China (SAI China) kupitia Serikali ya China, Serikali ya watu wa Marekani kupitia Shirika lao la Maendeleo (USAID), Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la Maendeleo (GIZ) na

wadau wote wanaoitakia mema Ofisi yangu na waliochangia kwa sehemu kubwa kuifanya kuwa ya kisasa kwa kufadhili mafunzo ya wafanyakazi na kutupatia vifaa mbalimbali zikiwemo kompyuta na magari.

Zaidi ya hayo, napenda kuzishukuru Kampuni Binafsi za Ukaguzi ambazo zimekuwa zikifanya kazi za ukaguzi kwa niaba ya Ofisi yangu katika ukaguzi wa Hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

Kwa ujumla wigo wa ukaguzi umepanuka baada ya ofisi yangu kuungana na Ofisi ya Ukaguzi wa Hesabu ya Uingereza pamoja na Ofisi ya Ukaguzi wa Hesabu ya China kuunda Bodi ya Ukaguzi wa Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia tarehe 1 Julai, 2012. Kwa kushirikiana na Ofisi ya ukaguzi wa Hesabu ya China na Uingereza tumeweza kutoa ripoti ya kwanza ya ukaguzi wa Hesabu za Umoja wa Mataifa ambapo tumepongezwa kwa kazi nzuri tuliyoifanya.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru sana wafanyakazi wangu wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kujitolea kwao na uvumilivu waliouonyesha katika kukamilisha ripoti hii, umekuwa wa manufaa na faraja sana kwangu. Nawasihi wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi waendeleo kuwa na moyo wa kufanya kazi kwa bidii na umoja kwa siku zijazo ili kuendelea kudumisha heshima ya Ofisi yetu katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora, kuhimiza uwajibikaji na kuzingatia thamani ya fedha katika makusanyo na matumizi ya rasilimali za umma.

DIBAJI

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya saba ya mwaka ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2013. Ripoti hii ni mkusanyiko wa ripoti za kaguzi mbalimbali za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zilizofanyika kwa kipindi husika. Ripoti hii inaainisha masuala yanayozorotesha ufanisi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma katika kutekeleza na kufikia malengo waliyojiwekea.

Lengo la ripoti hii, ni kuwataarifu wadau kama vile Serikali, Bunge, Mahakama, Wadau wa Maendeleo, Asasi za Kijamii na Umma wa Watanzania kwa ujumla, kuhusu muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013, pamoja na kutoa mapendekezo kwa lengo la kuboresha ufanisi wa Mashirika na Taasisi hizo. Ripoti hii imechambua mambo mbalimbali ambayo yameonekana kwa njia moja au nyingine kuathiri ufanisi na uwajibikaji wa Mashirika hayo katika kufikia malengo yake. Katika kipindi hiki ambacho kimekuwa na ongezeko kubwa la uwajibikaji kwa umma, uwazi na utawala bora ni jambo la muhimu kwa watendaji kutoa taarifa zao za utendaji ikiwa ni pamoja na taarifa za fedha na usimamiaji wa mali za umma ndani ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Napenda kueleza kuwa ripoti hii imetayarishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008.

Ili kuhakikisha kuwa kazi yangu inachangia katika maendeleo ya Taifa, ofisi yangu imekuwa ikipitia na kuboresha mbinu za ukaguzi mara kwa mara ili kuona kuwa matokeo ya kaguzi yanakidhi haja za wadau. Kujenga uwezo wa wakaguzi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni jambo linalopewa kipaumbele kikubwa ili kuhakikisha wanapata uelewa wa sheria, miongozo, kanuni na matoleo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na mabadiliko yanayofanywa na Taasisi za taaluma za uhasibu na ukaguzi za kimataifa kama vile “IFAC”, “INTOSAI” na nyinginezo ambazo ofisi yangu ni mwanachama.

Kutokana na jitihada hizo, Wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wamekuwa wakipewa mafunzo, ili kuongeza ubora na ufanisi katika kufanya kazi. Kwa mtazamo huo, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina mpango wa kujenga Kituo cha mafunzo ya ukaguzi katika eneo la Gezaulole Kigamboni-Dar es Salaam. Ninayo imani kubwa kuwa Serikali kwa kutambua umuhimu wa mafunzo kwa wakaguzi, itaisadia ofisi yangu katika maeneo yote ya msingi ili kufanikisha mradi huu.

Ni vyema ikafahamika kwamba, wakati vyombo vyenye dhamana ya uangalizi (Oversight Organs) vina jukumu la kuhakikisha kuwa Sheria na taratibu zinafuatwa ndani ya Taasisi za umma, Bodi za Wakurugenzi na Maafisa Watendaji Wakuu wa Taasisi hizo kwa upande wao wana jukumu la kuweka mifumo imara ya udhibiti wa ndani na miongozo ili kuhakikisha kwamba sheria na taratibu hizo zinafuatwa.

Juu ya yote, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake kwa ujumla, Kamati za Bunge za usimamizi wa utendaji, Bunge kwa ujumla, Wadau wa Maendeleo, Taasisi zisizo za Kiserikali na vyombo vya Habari kwa michango yao katika kufanikisha uwajibikaji ambao umeboresha utawala katika nchi yetu.



Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

MUHTASARI

Utangulizi

Muhtasari huu unaainisha kwa kifupi hoja mahususi zilizojadiliwa kwa kina katika sura husika za ripoti hii na zinazohitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa Mashirika ya Umma.

Ripoti hii inajumuisha hoja mbalimbali zilizotolewa kutoka katika ripoti za ukaguzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinazoonekana kukwamisha utendaji wa Mashirika na Taasisi hizo ambazo zinahitajika kufanyiwa kazi. Hoja hizo kwa kifupi ni kama ifuatavyo:-

- i. Hali za Ukaguzi na Ripoti Zilizotolewa
Kufikia tarehe 7 Machi, 2014 nilikamilisha kaguzi 103 kati ya kaguzi 179 zilizotakiwa kukaguliwa ambazo zipo chini ya uwanda wangu wa ukaguzi. Ripoti za mashirika 93 ziliridhiwa na Bodi za wakurugenzi na maoni ya ukaguzi kutolewa, wakati kaguzi 10 zilikuwa hazina Bodi za Wakurugenzi kuidhinisha hesabu zao. Kaguzi 74 zilizobakia zilikuwa katika hatua mbalimbali za ukaguzi kutokana na kuchelewa kuwasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi, mashirika mengine kutoandaa vikao vya Bodi za wakurugenzi kwa wakati kama sheria inavyotaka na kushindwa kwa baadhi ya wakaguliwa kujibu hoja za wakaguzi kwa wakati hali iliyosababisha zoezi la ukaguzi kutomalizika kwa wakati.

Vile vile napenda kubainisha kwamba, baadhi ya Mashirika ya Umma yanakumbana na uzorotaji wa hali ya kifedha uliosababishwa na hasara kwa zaidi ya miaka miwili mfululizo. Hii imesababisha matatizo ya ukwasi kwenye mashirika hayo hali iliyosababisha yashindwe kulipa madeni ya muda mfupi. Angalizo pia lilitolewa kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yaliyokuwa yanakabiliwa na madeni tarajiwa (contingent liabilities) yapatayo shilingi bilioni 712. Madeni haya tarajiwa yalitokana

na uwepo wa mashauri yaliyokuwa yakiendelea katika mahakama ambayo hatima ya matokeo yake haijulikani.

- ii. **Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka Iliyopita**
Katika ripoti zangu za kila mwaka huwa ninatoa mapendekezo kwa Serikali pamoja na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuchukua hatua zinazokusudiwa kutatua kasoro ambazo zimejitokeza wakati wa ukaguzi.

Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, kuna jumla ya mapendekezo 26 ambayo bado hayajatekelezwa na yameandikwa kwa muhtasari katika sura ya tatu ya ripoti hii. Baadhi ya mapendekezo hayo hayajafanyiwa kazi na watendaji wakuu na Bodi za Mashirika husika kwa zaidi ya miaka mitano. Hii inamaanisha kuwa watendaji husika hawatekelezi majukumu yao ipasavyo. Mapendekezo ya muda mrefu ambayo hayajatekelezwa yanarudiwa katika ripoti zangu na hivyo kupunguza juhudi za ofisi yangu katika kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Umma.

Napenda kupongeza jitihada za Mlipaji Mkuu wa Serikali katika kujibu mapendekezo yaliyojitokeza katika ripoti yangu ya mwaka 2011/2012. Napenda kuisistiza kwamba utekelezaji wa mapendekezo niliyotoa hauridhishi kwani mengi yapo katika hatua za utekelezaji na mengine bado hayajatekelezwa kabisa.

- iii. **Masuala Muhimu Ambayo Hayakutolewa Taarifa Katika Ripoti ya Mwaka Uliotangulia**

Mashirika ya umma ambayo kaguzi zake hazikukamilika kwa muda muafaka kutokana na sababu mbalimbali hazikuingia katika ripoti ya mwaka uliopita. Hivyo basi, sehemu hii inaelezea kwa kifupi masuala muhimu ambayo taarifa zake hazikujumuishwa kwenye ripoti iliyopita.

Nilibaini kuwa, fedha kutoka Wizara ya Fedha kwenda kwenye baadhi ya Mashirika ya umma hazitolewi kulingana na bajeti iliyoidhinishwa, hivyo kuzuia mashirika hayo kufikia malengo yake yaliyojiwekea kwa mwaka. Kwa Mfano, bajeti ya EPZA iliyoidhinishwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilikuwa shilingi bilioni 4.8. Katika bajeti hiyo, EPZA ilipokea shilingi milioni 959.9 sawa na asilimia 19.8.

Katika Bohari ya Dawa kwa kipindi cha robo ya kwanza na ya pili ya mwaka 2011/2012 Wizara ilitoa jumla ya shilingi bilioni 4.3 kati ya shilingi bilioni 32 sawa na asilimia 13 ya bajeti.

Ukaguzi niliufanya katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ulibaini kuwa, mikopo ya shilingi milioni 214.5 ilitolewa kwa wanafunzi waliofeli na wengine walioahirisha masomo kinyume na mwongozo wa ukopesaji na kanuni za fedha ya Bodi. Pia nilibaini ucheleweshwaji wa mikopo kwa baadhi ya vyo mfano Chuo Kikuu cha Mkwawa kiasi cha shilingi milioni 440.8, Zanzibar shilingi milioni 70.6 na Ruaha shilingi milioni 89.2 hivyo kuathiri maendeleo ya wanafunzi wanaotegemea mikopo hiyo.

Katika ukaguzi wa VETA, nilibaini mashine zenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1 zilizotelekezwa katika kituo cha Mpanda. Hata hivyo, mashine hizo zingeweza kutumika katika vituo vingine.

iv. **Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba**

Shughuli za manunuzi zimeendelea kuwa moja ya maeneo makubwa ya matumizi katika bajeti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Kwa mantiki hii ninazidi kusesitiza umuhimu wa kufuata miongozo, sheria na kanuni za kusimamia manunuzi katika sekta za Umma.

Hoja muhimu zilizojitokeza mwaka huu katika ukaguzi wa usimamizi wa sheria ya manunuzi na mikataba ni pamoja na kuwepo kwa muingiliano wa utendaji kazi katika shughuli za manunuzi kwenye Shirika la Umeme Tanzania. Hoja hii

ilitokana na manunuzi ya mafuta ya mitambo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.137 na Euro milioni 1.173 kupitia zabuni Na. PA/001/10/HQ/W/033. Kadhalika, ukaguzi wa mwaka huu ulibaini uwepo wa manunuzi yasiyoidhinishwa katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kiasi cha shilingi bilioni 69.957 (Dola za Kimarekani 12,300 and Euro 15,000).

Kutozingatiwa kwa muda katika mchakato wa manunuzi ni tatizo lililobainika wakati wa ukaguzi wa Shirika la Umeme Tanzania kwenye zabuni Na.PA/001/10/HQ/N/024 ya shilingi bilioni 1.8 na zabuni Na.PA/001/11/HQ/G/121 ya shilingi bilioni 1.137.

Hali kadhalika nilibaini manunuzi ya bidhaa kwa kugawanya zabuni ili kuruhusu matumizi ya dondoo za bei (Quotations) katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kwa kiasi cha shilingi bilioni 4.594. Udhaifu katika usimamizi wa mikataba ulijitokeza katika ukaguzi wa Shirika la Madini Tanzania (STAMICO) kwa manunuzi ya shilingi milioni 428.375. Hali hiyo ilibainika pia katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (shilingi bilioni 1.578) ambapo kwa Shirika la Umeme Tanzania ilihusu manunuzi ya shilingi bilioni 12.972 ; EURO 2,551,091 na Dola za kimarekani 1,711,939.12. Pia Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imekuwa ikitumia gharama kubwa za kushughulikia manunuzi iliyofikia shilingi milioni 268.730 katika mwaka wa ukaguzi kinyume na miongozo ya sheria za manunuzi.

Zaidi ya hayo, zabuni zisizo za kiushindani zilibainika CARMATEC kwenye manunuzi yenye thamani ya shilingi milioni 84.593 wakati kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, udhaifu huo ulibainika kwenye manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi bilioni 1.872. Manunuzi ambayo hayakuwa na mikataba yalibainika kwenye Mamlaka ya Bandari Tanzania yakiwaa na thamani ya shilingi bilioni 3.754 wakati manunuzi yaliyo nje ya mpango wa manunuzi yakibainika kwenye Shirika la Nyumba la Taifa ya shilingi milioni 127.349 na kwenye

Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, manunuzi yenye thamani ya shilingi bilioni 1.297. Pia kulibainika kubadilika kwa bei ya zabuni katika Shirika la Umeme Tanzania ambapo ilionekana kwamba badala ya kuwa Euro 210,283 bei ya zabuni ikawa Euro 176,357.80.

Hali ilikuwa mbaya katika Shirika la Umeme Tanzania ambapo upembuzi yakinifu haukufanywa kwenye miradi hivyo kusababisha gharama za ziada za manunuzi zilizofikia shilingi bilioni 9.5. Pia kulikuwa na manunuzi yaliyozidi ukomo uliowekwa na sheria ya manunuzi ya umma ya shilingi bilioni 12.461. Pia kulikuwa na manunuzi ya dharura ambayo hayakuidhinishwa ya shilingi milioni 264.320 pamoja na kuwepo kwa maamuzi yenye viashiria vya upendeleo katika kutoa zabuni yenye thamani ya shilingi bilioni 7.9.

V. Usimamizi wa Rasilimali

Nilibaini matumizi yasiyo sahihi ya rasilimali katika baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yanayosababisha mashirika hayo yashindwe kupata mapato stahiki. Mfano, katika Bodi ya Pamba Tanzania, Kiasi cha Dola za Kimarekani 775,000 hazikukusanywa kutokana na kutokuwa na mpanganji katika ghorofa mbili kati ya sita za jengo la Pamba Dar es salaam kwa kipindi cha miaka mitano sasa.

Mamlaka ya Bandari Tanzania ilinunua mita ili kudhibiti mapato yatokanayo na mafuta yanayoingizwa nchini kwa kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni 2.458. Hata hivyo, mita hizo zilitelekezwa na Mamlaka ya Bandari baada ya kusimamishwa na Wakala wa Vipimo bila sababu za msingi.

Pia kuna upotevu mkubwa wa mapato katika mamlaka za maji unaotokana na wateja kutokuwa na mita. Kwa mfano, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba ilipoteza kiasi cha asilimia 56.6 ya mapato yatokanayo na maji wakati Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya walipoteza kiasi cha asilimia 35.16.

Pia, nilibaini matumizi yasiyo sahihi kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Mfano kulikuwa na upotevu wa fedha wa kiasi cha shilingi milioni 652.6 katika Mamlaka ya Elimu Tanzania na shilingi milioni 314 katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea.

Kumekuwepo na maendeleo makubwa katika teknolojia yanayoongeza tija, usahihi na kupunguza gharama na muda unaotumika kufanya shughuli mbalimbali. Hata hivyo baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma hazijaanza kutumia mifumo hiyo ya kompyuta. Mfano, Chuo cha Ustawi wa Jamii, Mamlaka ya Bandari Tanzania na Chuo cha Mipango Dodoma vimeshindwa kutumia mifumo ya kompyuta ya uhasibu.

Vi. Usimamizi wa Rasilimali Watu

Rasilimali watu ina umuhimu mkubwa sana katika taasisi yeyote ile. Ili mashirika ya umma yaweze kufikia malengo yake, yanahitaji usimamizi bora wa rasilimali watu.

Mapungufu yaliyobainika katika eneo hili ni pamoja kutokuwa na mipango ya mafunzo ya wafanyakazi, kutofuata sheria za kazi hususan waraka wa kudumu wa utumishi wa umma kama ilivyobainika katika Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA).

Zaidi ya hayo, baadhi ya Mashirika ya Umma yalikuwa yakiendesha shughuli zake yakiwa na upungufu wa wafanyakazi, mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu za wafanyakazi katika taasisi za Mfuko wa Pension wa GEPF, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), DAWASA na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya, kutofanyika kwa tathmini ya utendaji wa wafanyakazi katika mashirika ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara (MTUWASA), TEMDO, UTT, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba (BUWASA), na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Ucheleweshawaji wakulipa makato ya kisheria ya shilingi bilioni 8 katika kampuni ya usambazaji maji ya Dar es salaam, mapungufu katika udhibiti wa

uandaaji na utunzaji wa jedwali la mishahara katika shirika la Bodi ya Pamba Tanzania (TCB), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) na Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), ukuaji wa madeni ya wafanyakazi kufikia shilingi bilioni 2.18 kwa mwaka 2012/13 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.53 kwa mwaka 2011/12 katika Mfuko wa Uwekezaji Tanzania (UTT) na uwepo wa mchanganyiko wa wafanyakazi usio na uwiano mzuri kitaaluma.

Vii. Utawala Bora katika Mashirika ya Umma

Ili kuwa na uwazi na uwajibikaji katika utendaji wa shughuli za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, utawala bora ni jambo la muhimu. Katika kuendesha shughuli za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, nilibaini kuwepo kwa vitendo vya kutozingatia kanuni za utawala bora.

Katika Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), nilibaini kuwepo kwa maagizo na sheria ambazo zinaitaka TANAPA kuchangia fedha ili kuendesha shughuli za serikali na baadhi ya taasisi za umma. Katika kipindi cha miaka mitatu, TANAPA ilichangia jumla ya shilingi bilioni 10.4 kwenda serikalini na baadhi ya taasisi zake. Kati ya fedha hizi, kiasi cha shilingi bilioni 8 kililipwa kwa taasisi za umma kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Pia ilikuwepo mijadala baina ya TANAPA na wadau wengine juu ya wazo la kuishirikisha TANAPA katika kuanzisha shirika jipya la ndege. Pamoja na kuwa hili ni wazo zuri, lakini kuna uwezekano wa mpango huo kuiathiri TANAPA kifedha na hivyo kuathiri shughuli za msingi za uhifadhi.

Katika mwaka huu wa fedha, Mamlaka ya Bandari ililipa shilingi milioni 44.3 kwa niaba ya Wizara ya Uchukuzi. Malipo haya yalikuwa ni kwa ajili ya kuhudhuria mikutano na gharama za hoteli na yalifanywa kwa kuzingatia maagizo ya wizara.

Mikataba ya utendaji baina ya Bodi za Wakurugenzi na Msajili wa Hazina ni muhimu ili kufuatilia na kupima utendaji wa Bodi za Wakurugenzi. Nimebaini kuwa mikataba hii haijatiwa saina licha ya kuwepo waraka wa Msajili wa Hazina unaosisitiza jambo hilo.

Katika ripoti zilizotangulia, nimekuwa nikiripoti haja ya kufanyika kwa uteuzi wa Bodi mpya kwa wakati baada ya Bodi zilizopo madarakani kumaliza muda wake. Hata hivyo, hakuna maendeleo makubwa kwani tatizo hili limekuwa likijitokeza mara kwa mara. Hali hii inaathiri shughuli za utendaji wa mashirika kwa upande wa miongozo, maamuzi muhimu na ukamilishaji wa ukaguzi wa hesabu kwa wakati.

Viii. Vitega Uchumi vya Serikali Pamoja na Mchakato wa Ubinafsishaji

Upitiaji wa ufanisi wa serikali ulibaini kuongezeka kwa kwa uwekezaji wa ndani wa serikali kutoka shilingi trilioni 12.215 na kufikia shilingi trilioni 14.01 mpaka ilipofika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013. Ongezeko hilo lilisababishwa na uwekezaji katika hisa kwenye makampuni ya kibiashara na ongezeko la mitaji katika mashirika yasiyo ya kibiashara. Kiwango kikubwa cha ongezeko la mtaji kilitokana na uthamini wa tengo la faida, mali za shirika, limbikizo la faida na ongezeko la taasisi za serikali kutoka taasisi 213 mwaka 2011/2012 na kufikia taasisi 215 mwaka 2012/2013.

Uwekezaji wa serikali katika makampuni 9 ya kigeni ulifikia shilingi bilioni 222.8 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013 ikilinganishwa na shilingi bilioni 145.9 katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012. Pia ilibainika kwamba mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2013 jumla ya dhamana za serikali zilifikia shilingi bilioni 485.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 498.7 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012.

Ukaguzi baada ya ubinafsishaji wa Mashirika kumi (10) ulibaini kwamba, pamoja na mafanikio ya ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, kulikuwa na kutoridhika kwa baadhi ya

wadau juu ya mchakato uliotumika katika zoezi zima la ubinafsishaji ambao ushahidi wake ni kutofanya vizuri kwa mashirika yaliyo binafsishwa pamoja na baadhi ya mashirika kutoanza shughuli zake kabisa kinyume na mikataba ya mauzo iliyosainiwa.

Sura ya tisa (9) inaainisha mambo muhimu yaliyoangaliwa katika ukaguzi ili kubaini kama sheria na vigezo vya uwekezaji vilifuatwa na iwapo mtazamo mpana wa kiuchumi utokanao na ubinafsishaji kama ulifikiwa.

Katika mchakato wa kubinafsisha Mgodini wa Makaa ya Mawe wa Kiwira, nilibaini kwamba taratibu za ubinafsishaji zilikiukwa. Uuzaji ulisimamiwa na serikali kuu kupitia Wizara ya Nishati na Madini hali kukiwa na uhusishaji mdogo sana wa PSRC/CHC.

Katika mikataba ya uuzaji wa Southern Paper Mills, ilibainika kwamba bei iliyokubalika ya uuzaji ilikuwa dola za kimarekani milioni 26. Ilikubalika kwamba kati ya kiasi hicho dola za kimarekani milioni 22 zilitakiwa kuwekezwa kwenye kampuni hiyo na dola za kimarekani milioni 3 ziwekwe kwenye akaunti ya “escrow”. Zaidi ya hayo, ilikubalika kuwa kiasi kilichowekwa kwenye akaunti ya escrow ni sharti kitolewe na mwekezaji baada ya kuwekeza jumla ya kiasi cha dola za kimarekani milioni 22. Hii inamaanisha kwamba SPM iliuzwa kwa dola za kimarekani milioni 1 tu.

Serikali ilitoa dhamana ya mkopo wa shilingi bilioni 6.65 uliotolewa na NSSF kwa ajili ya Kiwira Coal and Power Limited (KCPL) chini ya “Export Credit Guarantee Scheme” ilihali KCPL haikuwa na sifa ya kupewa dhamana chini ya mpango huo.

Zaidi ya hayo, KCPL ilipata mkopo wa shilingi bilioni 28.998 kutoka NSSF, PSPF na benki ya CRDB kwa ajili ya kuongeza mtaji, ukarabati na upanuzi wa shughuli za KCPL. Utumiaji wa mikopo hii na KCPL unaleta maswali kwa kuwa hakuna

uwekezaji wowote uliofanywa. Pia, mikopo hii haikuwahi kulipika tangu ilipochukuliwa.

ix. Matokeo ya Kaguzi Maalum

Ukaguzi maalumu wa Benki ya Posta Tanzania (TPB), ulibaini kutozingatiwa kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma katika mkataba wa kukarabati nyumba ya Mkurugenzi Mkuu. Zabuni hiyo ilipewa kwa kampuni ya Kiaren Investment kwa jumla ya shilingi 92.63 lakini jumla ya shilingi milioni 104.5 zililipwa kwa kampuni hiyo ambapo kiasi cha shilingi milioni 11.9 ilikuwa ni malipo ya kazi za ziada ambayo hayakuthibitshwa na Benki ya posta. Pia, Kampuni ya Kiaren Investment ilipewa zabuni ya ukarabati wa jengo la Benki ya Posta tawi la Mkwepu bila kuzingatia sheria ya manunuzi.

Kampuni za NACOD Enterprises Co. Ltd na Havillah Business ambazo hazikuwa zimesajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi zilipewa kazi na Benki ya Posta. Malipo ya kodi ya ongezeko la thamani ya Shilingi milioni 61,851 yalilipwa kwa kampuni ya NACOD Enterprises Co. Ltd na shilingi milioni 16.692 yaliyojumuisha kodi ya ongezeko la thamani kwa kampuni ya Havillah Business yalilipwa kwa kampuni hizo lakini hayakupelekwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Ilionekana pia kuwepo kwa ajira za watumishi ambazo hazikufuata Miongozo ya Utumishi (Scheme of Service) ya Benki ya Posta.

Ukaguzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), uligundua kuwepo kwa limbikizo la deni la ankara za maji la jumla ya Shilingi milioni 147 ambazo hazikulipwa na taasisi mbalimbali za Serikali.

Ilibainika kuwa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), haijawasilisha fedha za makato ya mishahara kwenye Mamlaka husika ya kiasi cha Shilingi milioni 716. Ilionekana pia hakukuwepo na upembuzi yakinifu uliofanyika kabla ya kuomba mkopo wa kiasi cha bilioni 3.280 kutoka Benki ya Rasilimali ya Tanzania (TIB) na Benki ya CRDB. Jumla ya

Ng'ombe 376 walipotea kutoka Ranchi ya Ruvu kwa sababu ya kutokuwepo kwa uangalizi na udhibiti mzuri.

Ukaguzi wa Bodi ya Korosho ya Tanzania, ulionyesha kuwepo kwa Sheria mbili zinazokinzana ambazo ni Sheria iliyoanzisha Bodi ya Korosho Na.18 ya mwaka 2009 na ile ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 kuhusu matumizi ya fedha za ushuru wa Korosho. Kiasi cha shilingi milioni 223.8 zililipia pembejeo za wakulima ambazo hazijapokelewa kwa kipindi cha miaka minne. Hali kadhalika, Afisa Kilimo wa Wilaya (DAO) ya Masasi aliidhinisha malipo ya kiasi cha shilingi milioni 292 kwa ajili ya pembejeo ambazo nusu yake bado hazijapokelewa kwa kipindi cha miaka minne. Pia, Bodi ya Korosho ilitumia shilingi bilioni 1.075 za ushuru wa korosho kwa matumizi ya kawaida ya ofisi wakati fedha hizo zilikuwa ni kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho mkoani Mtwara. Bodi ya korosho haijawasilisha shilingi milioni 735 zilizotengwa kwa ajili ya wakulima wa korosho wa wilaya za Masasi, Newala na Nanyumbu.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulilipa madai ya shilingi milioni 20.4 ikiwa ni malipo ambayo hayakustahili. Kurugenzi ya uendeshaji haikuweza kuhakiki usahihi wa rekodi za wanachama kwenye mfumo wa kumbukumbu wa Mfuko ili kupunguza udanganyifu na makosa kwenye malipo ya madai ya afya. Ilionekana pia kuwepo malipo mengine yaliyolipwa kwa wagonjwa ambao majina yao hayakuwasililishwa kwenye Mfuko na vituo vinavyotoa huduma za Afya.

Ukaguzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade), ulibaini kuwepo kwa tiketi na stika za kughushi za kuingia katika maonyesho ya Kimataifa ya 36 ya Dar es Salaam ya kiasi cha shilingi milioni 158.816. Bodi na Menejimenti ya TanTrade hawajaweza kuwa na udhibiti wa mipaka ya viwanja vya maonyesho ya biashara kuepukana na uvamizi. Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara haikuwa na vielelezo vya kuthibitisha madeni ya kiasi cha shilingi milioni 108.486. Ukaguzi pia ulibaini, Bodi na Menejimenti ya Mamlaka

hawajaweza kurejesha mali zilizokuwa chini ya Bodi ya Biashara za Ndani (BIT) na iliyokuwa Bodi ya Biashara za Nje (BET) zilizohamishiwa serikalini. Kwa upande mwingine ukaguzi ulibaini magari 11 yaliyonunuliwa kwa ajili ya Mamlaka lakini hayakupokelewa na Mamlaka hiyo.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA

1.0 Uanzishwaji wa Ofisi ya Ukaguzi Kisheria

Ofisi ya Mdhobiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni ofisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kama inavyorekebishwa mara kwa mara. Ukaguzi wa Umma Tanzania umeelezwa zaidi kwenye Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 na sehemu ya 44 (2) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004.

Aya ya 5 ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamtaka Mdhobiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma angalau mara moja kwa mwaka wa fedha. Vilevile kifungu cha 33 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 inampa mamlaka Mdhobiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kumruhusu mtu yeyote ambaye anaweza kuchaguliwa kuwa mkaguzi wa Shirika ama afisa yeyote kukagua kwa niaba yake vitabu vya hesabu vya taasisi yoyote ambayo Mdhobiti na Mkaguzi Mkuu anapaswa kukagua kwa mujibu wa Sheria. Hata hivyo, jukumu la kutoa maoni ya ukaguzi ni la Mdhobiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma nchini zinafanya kazi kwa kutumia ‘accrual basis of accounting’ ambayo inayalazimu kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSASs). Miongozo zaidi ya kisheria inayotumika kuandaa hesabu ni pamoja na Sheria ya Makampuni Na. 12 ya mwaka 2002 au sheria yeyote iliyopitishwa na Bunge ya kuanzishwa kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

1.1 Ukaguzi na Mamlaka ya Kuripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu

1.1.1 Mamlaka ya Ukaguzi

Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma umeelezewa katika Ibara ya 143 (2) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara hii inaelezea majukumu ya kikatiba ya kukagua Taasisi za Serikali.

Madhumuni ya ibara hii ya katiba yameelezwa zaidi katika kifungu Na. 34 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 ambayo inasema kuwa baada ya kupokea mahesabu kwa ajili ya ukaguzi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ndiye atakayehakikisha kuwa ukaguzi unafanyika na ndani ya kipindi cha miezi tisa baada ya mwaka kuisha inabidi atoe hati ya kitaalamu kuhusiana na hesabu pamoja na matokeo ya ukaguzi.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ana mamlaka ya kufanya ukaguzi wa hesabu na ukaguzi wa thamani ya fedha au kaguzi nyinginezo katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kama ilivyoainishwa kwenye vifungu Na. 26, 27, 28 na 29 vya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008. Kifungu cha 12 cha sheria hiyo kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kutoa maoni kwa nia ya:-

- Kuzuia na kupunguza matumizi ya fedha za Umma yasiyokuwa na tija,
- Kuongeza makusanyo ya maduhuli ya Umma,
- Kuzuia hasara inayoweza kutokea kwa uzembe, wizi, kukosa uaminifu udanganyifu au rushwa kuhusiana na fedha na rasilimali za Umma.
- Kuongeza uchumi, Tija na Ufanisi katika kutumia fedha za umma.

1.1.2 Mamlaka ya Kuripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha ripoti za mwaka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyo katika Ibara ya 143 (4) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Katika kanuni ya 88 ya kanuni za ukaguzi wa umma, ripoti hizo zinatakiwa kuwasilishwa kwa Rais ifikapo tarehe 31 Machi ya kila mwaka. Baada ya kupokea ripoti hizo, Rais atawaelekeza Mawaziri wanaohusika kuwasilisha ripoti hizo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge ambacho kitafanyika baada ya Rais kupokea ripoti. Ripoti hizo zinabidi ziwasilishwe ndani ya siku saba tangu kikao hicho cha Bunge kilipoanza.

Kama Rais hatachukuwa hatua zozote za kuwasilisha taarifa hizo Bungeni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu atawasilisha nakala za ripoti kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano (au Naibu wa Spika ikiwa kiti cha Spika kiko wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yeyote Spika hawezi kutekeleza majukumu yake) ambaye atawasilisha ripoti hiyo Bungeni. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inayohusu Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma inajadiliwa kwanza na Kamati za Bunge za Hesabu (PAC) au Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa niaba ya Bunge na kuandaa ripoti ambayo itawasilishwa Bungeni.

1.2 Wigo na Matumizi ya Viwango vya Ukaguzi

1.2.1 Wigo na Madhumuni ya Ukaguzi

Wigo wa ukaguzi wangu unajumuisha tathmini ya ufanisi wa mifumo ya kihesabu na vidhibiti vya ndani katika shughuli za taasisi husika, ukaguzi na uhakiki wa hesabu, ripoti za utekelezaji na mbinu nyingine za kikaguzi ambazo ni muhimu katika kukamilisha ukaguzi. Ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia vihatarishi na umuhimu wa kufanya uhakiki “risk and materiality” hivyo matokeo ya ukaguzi yanatokana na

kiwango cha kumbukumbu, nyaraka na taarifa zilizoombwa kwa madhumuni ya ukaguzi na zikawasilishwa kwangu.

Nia na madhumuni ya kufanya ukaguzi ni kutimiza jukumu la kutoa maoni yaliyo huru kwenye hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka 2012/2013 kama zimeandaliwa kutokana na viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu. Ukaguzi huu unahusiana na hesabu zilizokaguliwa kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Septemba, 2012, tarehe 31 Disemba, 2012 na tarehe 30 Juni, 2013. Pia ripoti hii inajumuisha mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwenye ripoti za ukaguzi za miaka iliyopita ambayo hayajatekelezwa na mambo muhimu yaliyokuwa kwenye ripoti za Mashirika husika ambayo hayakuandikwa kwenye ripoti ya mwaka uliopita.

1.2.2

Utumiaji wa Viwango Vinanvyokubalika vya Kimataifa
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni mwanachama katika Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi Duniani (INTOSAI), Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi za nchi za Afrika (AFROSAI) na Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi kwa nchi za Afrika zinazoongea Kiingereza (AFROSAI-E). Hivyo ofisi inatumia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vya Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi Duniani (ISSAI) vinavyotolewa na INTOSAI na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu (ISA) vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu duniani (IFAC).

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina majukumu ya kipekee kuhakikisha kunakuwepo na nidhamu katika matumizi, uwajibikaji na uwazi katika nchi. Pia, Ofisi ya Ukaguzi Tanzania ina jukumu la kutoa ripoti iliyo bora na kwa wakati unaofaa inayoelezea namna rasilimali za Taifa zilivyotumika.

- 1.3 Majukumu ya Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinalo jukumu la kutayarisha kwa usahihi hesabu kama inavyotakiwa katika Viwango vya Kimataifa vya utayarishaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya Kimataifa vya utayarishaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSAS). Majukumu hayo yanajumuisha na kuhakikisha taarifa za hesabu zinaandaliwa kwa kiwango cha kimataifa ikiwa ni pamoja na kuweka, kutekeleza na kudumisha mifumo thabiti ya ndani itakayoweza kuandaa mahesabu yaliyo huru yasiyo na makosa au mapungufu yatokanayo na udanganyifu, kupanga na kutumia sera za mahesabu, na makadirio ya mahesabu yanayoendana na mazingira halisi. Uandaaji na uwasilishaji wa hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ni jukumu la kisheria lililoainishwa kwenye Sheria zilizoanzisha Mashirika na Taasisi husika, Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002 na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu (IFRS 1), Viwango vya Kimataifa vya Kihesabu (IAS 1) na Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu za Taasisi za Umma (IPSAS 1) vinaainisha aina za hesabu zinazotakiwa kuandaliwa. Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma Tanzania zinatakiwa kuandaa hesabu kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu (IFRS) au Viwango vya Kimataifa vya utayarishaji wa Hesabu za Taasisi za Umma (IPSAS) kutokana na aina/asili ya shughuli na madhumuni ya Mashirika na Taasisi husika. Hii inatokana na maamuzi yaliyochukuliwa na Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA) iliyopitishwa na Serikali ya kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, 2004 Mashirika Tanzania yanatakiwa kuandaa taarifa za hesabu kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu na ukaguzi utafanyika kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) na itaongozwa na viwango na miongozo inayotolewa

mara kwa mara na Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA).

Ripoti ya mwaka ya Mashirika ya Umma inatoa taarifa ambazo zinasaidia umma kutathmini ustawi wa mashirika na uwajibikaji wa Watendaji Wakuu katika kutumia rasilimali za taifa. Kwa hali hiyo kupata taarifa kwa wakati muafaka ni kitu muhimu. Hii ndio dhima nzima ya uwazi na uwajibikaji katika kutumia rasilimali za umma.

1.4 Mifumo ya Udhibiti wa Ndani

Mifumo ya udhibiti wa ndani ni namna ambavyo rasimali za umma zinavyopangiliwa, zinavyosimamiwa na kupimwa. Udhibiti wa ndani unatumika kama chombo muhimu katika kudhibiti ubadhirifu na matumizi mabaya ya mali za umma zinazoshikika na zisizoshikika. Kwenye taasisi yoyote lengo la mfumo wa udhibiti wa ndani ni kuhakikisha shughuli za taasisi husika zinafanywa kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni. Tukiongelea malipo na manunuzi, udhibiti wa ndani una maana ya hatua zilizochukuliwa ili kufikia malengo mbalimbali yaliyowekwa mfano; namna ya kuhakikisha malipo yanayolipwa kwa ajili ya huduma na mali za shirika ni halali.

1.5 Majukumu ya Msajili wa Hazina

Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 418 na kifungu Na. 6 cha Sheria ya Mashirika ya Umma Na.16 ya mwaka 1992, zinahusiana na kazi za Mashirika ya Umma. Sheria hizo zinaelezea kuwa Msajili wa Hazina ana kazi na majukumu ya kusimamia vyema uendeshaji wa shughuli za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa kushirikiana na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika husika. Wanafanya hivyo kwa ukaribu katika kusimamia na kuongoza Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa ufanisi kwa njia ya kutoa maelekezo ya kusimamia.

1.6 Kuwasilisha Hesabu kwa Ajili ya Ukaguzi

Kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008, kinataka Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuwasilisha hesabu kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi ndani ya miezi mitatu baada ya kuisha mwaka wa fedha unaohusu hesabu hizo.

1.7 Mpangilio na Uteuzi wa Makampuni Binafsi kwa kazi ya Ukaguzi


Ili ofisi yangu iweze kutimiza majukumu ya ukaguzi kwa ufanisi katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, natumia mamlaka yangu ya kikatiba kuteua makampuni binafsi ya ukaguzi kukagua Mashirika ya Umma kwa niaba yangu. Hii ni kama inavyoelekezwa kwenye kifungu Na. 33 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, ambacho kinampa mamlaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kumruhusu mtu au kampuni yeyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Wakaguzi wa Hesabu na Wahasibu Na. 33 ya mwaka 1972 (iliyorekebishwa mwaka 1995) kufanya ukaguzi kwenye Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa niaba yake. Wakaguzi watakaoteuliwa watafuata Sheria kama inavyotakiwa na hawatakuwa na mgongano wa kimaslahi katika kutekeleza wajibu wao na pia hawatatoa siri za mashirika zinayoyakagua. Wajibu wa kutoa maoni ya ukaguzi ni wa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Katika kutekeleza majukumu hayo, ofisi yangu inakagua yenyewe Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma au kwa kushirikina na makampuni binafsi ya ukaguzi na pia kaguzi nyingi zinakaguliwa na makampuni binafsi peke yao. Kazi za ukaguzi zilizofanywa na makampuni binafsi kwa niaba yangu zinawasilishwa kwenye ofisi yangu ili kuhakikiwa ubora wake kabla hazijapelekwa kwa wakaguliwa.

Kati ya mashirika 179, mashirika 21 sawa na asilimia 12 yalihakikuliwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, na mashirika 18

sawa na asilimia 10 yalikaguliwa kwa kushirikiana na makampuni binafsi, pia mashirika 140 sawa na asilimia 78 yalikaguliwa na makampuni binafsi peke yao.

Kielelezo 1: Mgawanyo wa Kazi za Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka 2012/2013



Idadi ndogo ya Mashirika ya Umma, yaani asilimia 12% inayokaguliwa na ofisi yangu ni ishara ya upungufu wa wafanyakazi katika Ofisi ya Mdhiditi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ofisi yangu inahitaji wafanyakazi wa kutosha na wenye ujuzi ili kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali inazokumbana nazo katika ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Majina ya makampuni binafsi ya ukaguzi yaliyofanya kazi ya ukaguzi kwa niaba ya ofisi yangu yameorodheshwa kwenye kiambatanisho Na.1 cha taarifa hii.

SURA YA PILI

AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

2.0 Utangulizi

Kulingana na kanuni za ukaguzi, sababu ya kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumwezesha Mkaguzi kutoa hati ya ukaguzi inayoeleza iwapo hesabu zinaonyesha hali halisi ya kifedha ya shirika na kama zimeandaliwa kwa kufuata viwango vinavyokubalika. Ukaguzi wa hesabu unafanyika ili kumuongezea imani mtumiaji wa Hesabu husika kwamba zimetengenezwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika, na kumfanya Mkaguzi kupata sababu za uhakika ya kwamba hesabu kwa ujumla wake hazina makosa makubwa na pia kutoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi.

Hati ya ukaguzi ni maoni ya mkaguzi kuhusu Hesabu zilizokaguliwa ili kumwezesha mtumiaji kujua kama Hesabu hizo zimeandaliwa kwa kufuata viwango vinavyokubalika vya uhasibu, vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu na vile vinavyotolewa na Bodi za Taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi za Kimataifa vinavyokubalika kwenye Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo.

Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2013 watendaji wakuu wa mashirika 177 kati ya 179 waliwasilisha hesabu zao kwenye ofisi yangu kwa ajili ya kukaguliwa. Mashirika mawili (2) ambayo ni Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) na Kampuni ya Huduma za Majini hayakuwasilisha hesabu zake. Shirika la Usafiri Dar es salaam halikuwasilisha hesabu zake kwa mantiki kuwa umiliki wake haueleweki.

Katika hesabu zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, kaguzi 103 zilihitimishwa na ripoti zake kutolewa kwa mashirika husika hadi kufikia tarehe 7 Machi, 2014. Kati ya kaguzi zilizohitimishwa, ripoti za kaguzi za mashirika 93 ziliridhiwa na bodi za wakurugenzi na hati za ukaguzi kutolewa, wakati

mashirika 10 hayakuwa na Bodi za Wakurugenzi kuidhinisha hesabu hizo. Kaguzi 74 zilizobaki zilikuwa katika hatua mbalimbali za ukaguzi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuchelewa kuwasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi, mashirika mengine kutoandaa vikao vya Bodi za wakurugenzi kwa wakati kama sheria inavyotaka na kushindwa kwa baadhi ya wakaguliwa kujibu hoja za wakaguzi kwa wakati. Hali halisi ya uwasilishaji wa hesabu na ukaguzi wa hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kufikia tarehe 7 Machi, 2014 ni kama ilivyoonyeshwa kwenye Kiambatisho Na. II cha ripoti hii.

2.1 Aina za Hati za Kaguzi zilizotolewa

2.1.1 Hati Inayoridhisha

Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, na vile vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika kimataifa. Kaguzi 51 zilizokamilika zilipata hati inayoridhisha.

2.1.2 Hati Inayoridhisha na Yenye Suala la Msisitizo

Suala la msisitizo halibadilishi hati ya ukaguzi kutoka hati inayoridhisha, bali huongeza uelewa zaidi wa hali ilivyo ndani ya Taasisi iliyokaguliwa ingawa imepewa hati inayoridhisha. Ripoti ya Mkaguzi inaweza kuhuishwa au kubadilishwa kwa kuongeza aya yenye suala la msisitizo kuainisha/kuonyesha suala linaloathiri hesabu ambalo limeonyeshwa au kujumuishwa kwenye maelezo ya hesabu lenye kuhitaji uzingatiaji wa makini kwa watumiaji wa hesabu katika kufanya maamuzi sahihi. Masuala hayo ya msisitizo yanajumuisha matatizo ya uwezo wa shirika kujiendesha lenyewe na kuwepo kwa mashaka ambayo matokeo yake yanategemea maamuzi ya baadae. Mkaguzi pia anaweza kurekebisha ripoti ya ukaguzi kwa kutoa aya yenye suala la msisitizo kuripoti mambo ambayo hayaathiri

hesabu kama vile masuala ambayo hayafuati utaratibu kwenye hesabu zilizokaguliwa ambazo taasisi inayokaguliwa inakataa kuzifanyia marekebisho. Kaguzi 41 za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zilipata hati zinazoridhisha na zenye masuala ya msisitizo.

2.1.3 Hati Yenye Shaka

Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anapokutana na mazingira ya kutokukubaliana na menejimenti au mazingira yenye shaka ambayo yana athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa hesabu. Maelezo ya hati yenye shaka yanafanana sana na hati inayoridhisha lakini aya ya ufafanuzi inaongezwa ili kuelezea sababu zinazoleta shaka. Kwa hiyo, hati itaonyesha kuwa hesabu kwa ujumla zinaonyesha vizuri hali ya kifedha isipokuwa kwa kasoro zitokanazo na masuala yaliyohojiwa. Hati yenye shaka haikutolewa kwenye shirika lolote.

2.1.4 Hati Yenye Shaka na Suala la Msisitizo

Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anapokutana na mazingira ya kutokukubaliana na menejimenti au mazingira yenye shaka ambayo yana athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa hesabu. Aya ya suala la msisitizo inaambatanishwa kama kuna jambo linalotakiwa kujulikana na watumiaji wa hesabu hizo au kama kunahitajika uzingatiaji wa haraka kutoka kwa Watendaji Wakuu na watumiaji wa taarifa za fedha kuwatahadharisha kuhusu masuala hayo yanayohitaji kushughulikiwa haraka. Hata hivyo, lengo kuu la suala la msisitizo ni kuleta karibu uelewa wa hali ilivyo ndani ya Shirika au Taasisi iliyokaguliwa ingawa imepewa hati yenye shaka. Kwa hiyo, hati itaonyesha kuwa hesabu kwa ujumla zinaonyesha vizuri hali ya kifedha isipokuwa kwa kasoro zitokanazo na masuala yaliyohojiwa. Hati yenye shaka na suala la msisitizo ilitolewa katika shirika 1.

2.1.5 Hati Mbaya


Aina hii ya hati ni mojawapo ya sababu zinazoweza kubadilisha hati ya ukaguzi. Hati hii hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu hesabu zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo inaathiri hesabu kiasi cha kushindwa kutoa maoni kuhusiana na hesabu hizo. Hakuna hati mbaya iliyotolewa kwenye shirika lolote.

2.1.6 Hati Isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapoon kuwa, taarifa za fedha za Shirika au Taasisi Nyinginezo za Umma kwa kiasi kikubwa zina makosa, na zikiangaliwa kwa ujumla wake zinakuwa hazikuandaliwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika vya uhasibu vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, na vile vinavyotolewa na Taasisi za kitaaluma za Uhasibu na Ukaguzi za Kimataifa. Hati hii inaonekana kuwa ni kinyume cha hati inayoridhisha. Kimsingi hati hii hueleza kwamba, taarifa zilizomo katika hesabu za Shirika au Taasisi kwa kiasi kikubwa si sahihi wala za kuaminika kwa ajili ya kutathmini hali ya kifedha na matokeo ya kiutendaji ya Shirika au Taasisi husika. Hakuna hati isiyoridhisha iliyotolewa kwa shirika lolote.

Uchanganuzi wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika kipindi cha mwaka 2012/2013 kinapatikana kwenye kiambatisho cha III na mgawanyo wake umeainishwa hapa chini.

Kielelezo Na. 2: Hati za ukaguzi zilizotolewa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 zimeonyeshwa kwenye kielelezo kifuatacho:



Jedwali 1: Hati zilizotolewa kwa kipindi cha miaka minne mfululizo kutoka 2009/2010 hadi 2012/2013 kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

Aina ya Hati	Mwaka			
	2009/ 2010	2010/ 2011	2011/ 2012	2012/ 2013
Hati zinazoridhisha	92	84	62	51
Hati zinazoridhisha zenye masuala ya msisitizo	12	12	23	41
Hati zenye shaka	10	7	2	0
Hati zenye shaka na masuala ya msisitizo	7	4	7	1
Hati mbaya	1	0	1	0
Hati Zisizoridhisha	0	0	0	0
Jumla	122	107	95	93

2.2 Misingi ya Hati Zilizotolewa

2.2.1 Ripoti Zenye Hati Inayoridhisha na Zenye Masuala ya Msisitizo

Hati safi zenye masuala ya msisitizo zipatazo 41 zilitolewa kwenye Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Hati hizi zilitokana na uzorotaji wa hali ya kifedha uliochangiwa na hasara mfululizo na matatizo ya kifedha yanayokwamisha Mashirika ya Umma kulipa madeni yake. Mchanganuo wa upungufu na matatizo ya kifedha unaozikabili baadhi ya taasisi umeonyeshwa kwenye kiambatisho cha IV.

Umakini pia uliainishwa kwa baadhi ya mashirika ya umma yaliyokuwa yanakabiliwa na madeni yasiyo na uhakika yaliyopelekea uwepo wa mashauri mbalimbali zilizokuwa zikiendelea kwenye hatua mbalimbali ambazo matokeo yake hayajulikani yatakuwaje. Madeni yasiyokuwa na uhakika na mambo mengine yaliyopelekea utolewaji wa Hati zenye masuala ya msisitizo yanaelezwa hapa chini kama ifuatavyo;

Bodi ya Pamba Tanzania ilikuwa na madeni tarajiwa (contingent liabilities) yenye madai ya shilingi bilioni 1.36 ikiwa ni ruzuku ya ziada kwenye mazao kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010. Pia Chuo cha Ustawi wa Jamii kilikuwa na mashauri yaliyofunguliwa na wafanyakazi wake ambayo hayajaamuliwa ya madai ya shilingi bilioni 2.041. Kwa kuongezea Shirika la Hifadhi za Taifa lilikuwa na madeni tarajiwa yaliyotokana na kesi ambazo hazijaamuliwa zipatazo kumi (10) zenye madai ya shilingi milioni 285 (2011/2012: shilingi milioni 186) na shilingi milioni 33 (2011/2012: shilingi milioni 5) zilizofunguliwa dhidi yake na waliokuwa wafanyakazi wake.

Mamlaka ya Bandari Tanzania ilikuwa na kesi iliyofunguliwa dhidi yake na Kampuni ya Ujenzi ya Mvita ikiidai mamlaka kiasi cha shilingi bilioni 337.7 (zilizopendekezwa kwenye usuluhishi). Vile vile Mamlaka ilikuwa na mashauri ambayo

yalikuwa hayajatolewa hukumu katika mahakama mbalimbali ya kiasi cha shilingi bilioni 20.6 (2011/12: shilingi bilioni 20.05) ambazo maamuzi yake hayajulikani. Pia Mamlaka ilikuwa na mashauri yaliyohusu makadirio ya kodi yapatayo kiasi cha shilingi bilioni 75.5 ambayo yalikuwa yanasubiri maamuzi ya Bodi ya Rufani za Kodi.

Mapato ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA) yanajumuisha ankara za uendeshaji zinazowasilishwa kwa wateja na ada za kukodi miundombinu inayolipwa na mwendesha huduma za usambazaji wa maji. Mamlaka iliweza kurekodi tozo ya mapato iliyokuwa ya gharama za maji yenye kiasi cha shilingi bilioni 16.296 ambayo yanawakilisha mapato yaliyotokana na asilimia 47 ya maji yote yaliyozalishwa katika kipindi cha mwaka. Pia, Mamlaka iliweza kurekodi maji ambayo yalipotea kwa uwiano wa asilimia 53 ya kiasi cha maji yote yaliyozalishwa ambayo ni asilimia 28 juu zaidi ya kiwango kinachokubalika cha asilimia 25 kilichokadiriwa kufikia fedha za kitanzania bilioni 8.947. Mamlaka inadhani ya kwamba uwiano wa maji yaliyopotea ulitokana na watu kujiunganishia maji kinyume cha sheria au kutosajiliwa, waliounganishiwa maji na kusajiliwa lakini wanatambuliwa kimakosa kama wamekatiwa au hawapo (inactive) hali inayopelekea wasipelekewe ankara. Vile vile mamlaka ilipata hasara ya shilingi bilioni 17. 159 (2012 shilingi bilioni 21.052) na hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013 madeni ya muda mfupi ya mamlaka yalizidi mali za mamlaka za muda mfupi kwa shilingi bilioni 19.624.

Baraza la Uwezeshaji wa Kiuchumi lina madeni yasiyokuwa na uhakika yapatayo shilingi milioni 980.232 yaliyotokana na SACCOS 26 kushindwa kulipa mikopo yao kwenye benki ya CRDB ambayo Baraza lilidhamini. Hii inaashiria uwepo wa mashaka juu ya uendeshaji wa Baraza katika shughuli zake za kila siku endapo itatakiwa kulipa deni lote hilo bila kupata msaada kutoka serikalini.

Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) lilikuwa na madeni tarajiwa yaliyotokana na mashauri mbalimbali yaliyopo mahakamani yapatayo shilingi bilioni 274. Pia Shirika lilikuwa linadaiwa madeni ya iliyokuwa LART yaliyojumuisha salio la wadeni lililotokana na ufilisi wa Mashirika ya Umma na mali zisizozalisha zilizokuwa zikimilikiwa hapo awali na LART. Mauzo yaliyopatikana kutokana na zoezi la ufilisi yalikuwa shilingi bilioni 25.844. Mauzo yaliyopatikana kwenye ufilisi hayakutengwa hivyo Shirika linaweza lisiwe na kiasi cha fedha cha kutosha kulipa madeni yaliyokuwepo wakati wa ufilisi yatakapotakiwa kulipwa.

Vile vile ilionekana kwamba hesabu za Benki ya Posta Tanzania zinaonesha umiliki wa hisa wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Shirika la Posta Tanzania na Chama cha Kuweka na Kukopa cha Shirika la Posta na Simu Tanzania katika uwiano wa 80.4:4.1:11.8:3.7 ambao ni kinyume na uwiano 41:10:30:19 ulioainishwa kwenye kifungu cha 12(1) na (2) ya Sheria ya Benki ya Posta Tanzania Na. 11 ya mwaka 1992.

Ukaguzi wa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) ulibaini kwamba kutokana na uthamini wa uwezo wa mfuko kulipa wanachama wake (Actuarial Valuation) iliyofanyika mwaka 2010, Mfuko ulipata mapungufu (nakisi) katika uwezo wa kulipa (Actuarial Deficit) ya shilingi trilioni 6.49 kama nilivyoripti kwenye ripoti ya mwaka uliopita. Pia mfuko uliingiza kwenye hesabu zake kiasi cha shilingi bilioni 107.843 zilizotumika kujenga Chuo cha Elimu cha Chuo Kikuu Dodoma kama mkopo. Hii ni kinyume na masharti ya mkataba ambao unataka mradi kuwa katika mfumo wa kubuni, kujenga, endesha na kuhamisha jengo (Design, Build, Operate and Transfer) ambapo Mfuko utapokea kodi iliyokokotolewa kwa misingi ya gharama za uwekezaji na riba ya uwekezaji ambayo ni asilimia 15 kwa kipindi cha miaka 10.

Mwishoni mwa mwaka, Tume ya Ushindani ilikuwa na mashauri mbalimbali yaliyokuwa yakiendelea yenye madai ya shilingi milioni 255. Utengefu wa kiasi cha shilingi milioni 166 ulifanywa kwa ajili ya kukabili madeni ya siku za mbele. Hata hivyo kiasi cha shilingi milioni 89 hazikufanyiwa utengefu kwa sababu matokeo ya mwisho bado hayajatolewa au kuamuliwa.

2.2.2 Ripoti Zilizopata Hati Yenye Shaka na Masuala ya Msisitizo

Katika kipindi cha mwaka 2012/2013 Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara ilipata hati yenye shaka iliyotolewa kwa kigezo cha mamlaka kuwa na madeni yaliyotokana na mauzo ya maji yapatayo shilingi milioni 409.617 ambayo menejimenti waliyafanyia utengefu (impairment provision) kiasi cha shilingi milioni 108.461. Utengefu uliofanywa ulihusu madeni yenye umri wa miaka mitano tu. Hakukuwa na sera ya mamlaka kuhusu utengefu wa madeni. Zaidi ya hayo hakuna utengefu wa ziada uliofanywa kwa wadaiwa waliobaki na mchakato wa utengefu ulikuwa haukidhi viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu (IAS 39.63).

Vile vile ilibainika kuwa viwango vya tozo za huduma ya maji na gharama za uendeshaji vinatokana na aina ya wateja. Nilibaini kuwa tozo za maji kwa baadhi ya wateja ikijumuisha shule za msingi ziliingizwa kwenye “Smart Billing System” kama watumiaji wa nyumbani ingawa walikosa sifa za kuwa watumiaji wa nyumbani. Hali hii ilipelekea Mamlaka kukosa mapato yanayokadiriwa kufikia shilingi milioni 48.4. Kutokana na kukosekana kwa tathmini ya kina ya wateja na makundi yao ili kuweza kutambua wateja waliotozwa ndivyo sivyo, sikuweza kuthibitisha ukamilifu wa taarifa ya mapato na wadaiwa wa Mamlaka.

SURA YA TATU

MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MIAKA ILIYOPITA

3.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha kwa muhtasari mapendekezo ya Ukaguzi wa ripoti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa miaka iliyopita, ambayo bado hayajatekelezwa. Mapendekezo hayo yapo aidha kwenye hatua za utekelezaji au hayakutekelezwa kabisa hadi ilipofikia wakati wa kuandaa ripoti hii. Uwajibikaji na utawala bora hautafikiwa kama hapatakuwa na jitihada binafsi kutoka kwenye shirika la umma husika kutekeleza mapendekezo ambayo hayajatekelezwa.

3.1 Majibu ya Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka Uliopita (2011/2012)

Nimepokea majibu ya Serikali ya ripoti ya mwaka uliopita kupitia barua ya Katibu Mkuu Hazina na Mlipaji Mkuu wa Serikali yenye kumbukumbu Na. EB/AG/AUDIT/12/VOL.I/53 ya tarehe 25 Juni, 2013. Napenda kutambua juhudi zilizofanywa na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa majibu aliyotoa kwa mapendekezo yaliyotolewa kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Pamoja na juhudi alizofanya Mlipaji Mkuu wa Serikali, mapendekezo mengi bado hayajatekelezwa. Kwa hali hiyo malengo na madhumuni ambayo mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo za Umma yamejiwekea hayatafikiwa kama hatua za ziada hazitachukuliwa katika kutekeleza mapendekezo yaliyokwisha tolewa.

Ningependa kuifahamisha Serikali kwamba mapendekezo ninayoyotoa mara kwa mara yana lengo la kuhakikisha kwamba kunakuwa na hatua madhubuti na umakini katika kuimarisha ukusanyaji na utumiaji wa mapato na rasilimali za Taifa. Mapendekezo hayo pia yanalenga kuhakikisha

matumizi ya fedha za umma yanaidhinishwa na wenye mamlaka na fedha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Kwa hali hiyo, kwa kuzingatia sheria na kanuni katika kutumia rasilimali za taifa, thamani ya fedha, tija na ufanisi vyaweza kufikiwa.

Kwa misingi hiyo nimeona ni vyema kuyarudia tena mapendekezo niliyoyatoa katika ripoti zilizopita ambayo hayajatekelezwa au yametekelezwa kwa kiwango kidogo na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma.

3.2 Muhtasari wa Mapendekezo Ambayo Hayajatekelezwa Katika Mwaka wa Fedha 2007/2008

3.2.1 Kuongezewa Mtaji kwa Mashirika ya Umma yenye Mtaji Mdogo

Msajili wa Hazina (Mmiliki) anapaswa kuhakikisha kuwa Mashirika ambayo hayana mitaji ya kutosha, yanapatiwa fedha kwa ajili ya kuyaendesha. Hili linaweza kufanyika kwa kuanzisha vyanzo mbalimbali vya mapato ili yaweze kufanya kazi kwa ufanisi na kutoa huduma bora kwa umma.

Pamoja na jibu la Mlipaji Mkuu kutaja Mashirika aliyoyapatia mtaji ni mashirika manne tu ndio yaliyopewa mitaji kama Benki ya Posta Tanzania, Mzinga Corporation, Benki ya Wanawake Tanzania na Benki ya Uwekezaji Tanzania ambayo bado ni machache ikilinganishwa na Mashirika ambayo yana mitaji midogo.

3.2.2 Kuongeza wigo wa Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma

Katika ripoti zangu za mwaka zilizopita nilimshauri Mheshimiwa Spika afikirie kuongeza wigo wa majukumu ya Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma na kuipa jina la Kamati ya Uwekezaji wa Umma ili iweze kuangalia na kuhoji maswala ya taarifa za fedha za Taasisi na

makampuni yote ambayo Serikali ina hisa, hata kama ni chini ya asilimia 50.

Kwa kuwa Mheshimiwa Spika ameona ni vyema hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zijadiliwe na Kamati ya hesabu za Serikali (PAC), kuna haja ya kuona umuhimu wa kuongeza wigo wa kamati na kuiongezea wajumbe na vitendea kazi ili kuweza kutekeleza majukumu makubwa ya kusimamia rasilimali za Umma.

Mlipaji Mkuu wa Serikali ametolea majibu swala la kubakiza wajumbe wa zamani wa kamati ya hesabu za Mashirika ya Umma kwenye kamati ya PAC. Hata hivyo napendekeza idadi ya wajumbe wa PAC iongezwe ili kuhakikisha idadi kubwa ya Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine za Serikali zinajadiliwa na PAC.

3.2.3 Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu

Kanuni za Utawala Bora zinataka Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wateuliwe na Bodi za Wakurugenzi badala ya kuteuliwa na Rais. Ili kumpunguzia mzigo mheshimiwa Rais, ninashauri Rais angeachiwa jukumu la kuteua wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi wakati uteuzi wa Maafisa Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma lingekuwa ni jukumu la Bodi za Wakurugenzi ili Bodi za Wakurugenzi ziweze kuziwajibisha menejimenti za Mashirika pale ambapo viongozi hao watahindwa kuwajibika ipasavyo.

3.3 Mapendekezo ya Mwaka 2008/2009 Ambayo Bado Hayajatekelezwa

3.3.1 Mgongano wa Kimaslahi kwa Wabunge Kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Bunge ndicho chombo kikuu kinachowakilisha wananchi na chenye majukumu ya kutathmini utendaji kazi wa Serikali

ikiwa ni pamoja na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kupitia Kamati za Kudumu za Bunge. Ili kuepuka mgongano wa kimaslahi, wabunge hawastahili kuteuliwa kuwa wajumbe wa bodi za Wakurugenzi katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwani wana jukumu la kusimamia mashirika hayo. Katika mkutano wa uwajibikaji uliofanyika tarehe 23 hadi tarehe 24 Januari, 2009 iliamuliwa kuwa Wabunge wasiteuliwe kuwa wajumbe katika Bodi za Mashirika ya Umma. Mwenendo huu ni wa kipekee na upo tu Tanzania na hautumiki mahali popote katika Jumuiya ambayo Tanzania ni mwanachama, kwa mfano EAC, SADCOPAC, SADC, AFROSAI-E, AU na hata nchi yoyote duniani. Nimerudia pendekezo hili kwa miaka mitano mfululizo bila kutekelezwa na mamlaka husika.

3.3.2 Mikataba ya Uwajibikaji wa Bodi za Wakurugenzi

Serikali inapaswa kuingia mikataba ya utendaji na Wakurugenzi wa Bodi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ili kuwekeana malengo wanayotakiwa kufikia kwa kipindi chao cha kazi na yawekwe wazi. Mlipaji Mkuu wa serikali amejibu mapendekezo haya kwa kutoa maelekezo kupitia waraka wa Msajili wa Hazina Na. 1 wa mwaka 2012 wenye Kumb Na. TYC/T/200/566/29 wa tarehe 5 Januari, 2012. Hata hivyo waraka huo haujaanza kufanyiwa kazi. Ni vizuri Serikali iweke mkakati wa kuhakikisha Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinasaini mikataba ya utendaji. Bodi ambazo hazitasaini zichukuliwe hatua za kinidhamu.

3.3.3 Haja ya Kuanzishwa Mfuko wa Umma wa Uwekezaji

Ni dhahiri kwamba Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zimegubikwa na matatizo mengi, kubwa ikiwa ni ukosefu wa mitaji ya kutosha ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya mashirika hayo.

Serikali inapaswa kuanzisha Mfuko wa Umma wa Uwekezaji ili kuweza kukabiliana na changamoto hizi. Bunge

linatakiwa kila mwaka kuidhinisha fedha kwa ajili ya mfuko huo, vilevile gawio kutoka kwa mashirika na misaada inayotolewa na wafadhili inayopokelewa kwa madhumuni hayo iweze kuwekwa kwenye mfuko huo. Fedha hizo hazipaswi kutumiwa katika shughuli za matumizi ya kawaida bali kwenye miradi ya maendeleo kama vile miradi mipya, kuongeza mitaji na kutoa mikopo nafuu kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinazohitaji.

Serikali iongeze juhudi katika uanzishwaji wa Mfuko wa Umma wa Uwekezaji kulingana na majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali.

3.3.4 Kutokuwepo kwa Usawa Katika Marupurupu Yatolewayo na Mashirika ya Umma

Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wana majukumu yanayofanana katika mashirika wanayosimamia. Kwa maana hiyo kuna haja ya serikali kuhakikisha kuwa kuna uwiano katika marupurupu wanayopata Menejimenti na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, kutokana na ukweli kwamba rasilimali wanazotumia (kama posho za vikao, ada za Bodi za Wakurugenzi n.k.), ni rasilimali za Umma. Hii itasaidia kuondoa tofauti zilizopo, kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Japokuwa mlipaji Mkuu wa Serikali amesema kuwa serikali imeanzisha “Salaries and Remuneration Rationalization Board” bado hakuna ushahidi unaonyesha kuanzishwa kwa Bodi hiyo.

3.3.5 Mkopo wa PSPF Shilingi Bilioni 58 kwa Bodi ya Mikopo na Marejesho ya Mikopo ya Wanafunzi Shilingi Bilioni 51.1

Serikali kuingilia maamuzi katika mifuko ya Pensheni ndio chanzo cha matatizo ya kifedha katika mifuko ya pensheni. Mikopo ambayo kwa Taasisi za Serikali kutoka Mifuko ya Jamii ambayo imedhaminiwa na serikali inachukua muda mrefu kulipwa huku serikali ikiwa imekaa kimya. Ningependa kusesitiza kuwa serikali inapaswa ichukue hatua kuhakikisha kwamba bakaa ya deni lote la mkopo (ikiwa

ni kiasi cha mkopo na riba) uliokopwa kutoka PSPF inalipwa, ili kuepuka gharama zaidi za riba na adhabu itokanayo na kuchelewa kulipa mikopo hiyo. Kuhusu na kutolipika kwa deni la kiasi shilingi 51.1, Bodi ya Mikopo inashauriwa kuchukua hatua za kisheria kwa waajiri na wakopaji binafsi ambao hawatoi ushirikiano kama ilivyoainishwa kwenye Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na kuhakikisha Mfuko unarudishiwa fedha za wanachama zilizokopwa.

3.4 Mapendekezo ya Mwaka 2010/2011 ambayo Hayajatekelezwa

3.4.1 Usimamizi wa Rasilimali

Katika ukaguzi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) nilibaini kwamba mfuko ulitumia shilingi bilioni 234.1 kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), chini ya makubaliano ya buni, jenga, endesha na kisha hamisha miliki baada ya miaka kumi (10). Mifuko mingine iliyochangia ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma kwa makubaliano hayo hayo ni Mfuko wa Pensheni kwa wafanyakazi wa Serikali Kuu (PSPF), Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mtaa (LAPF), Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma (PPF) ambayo yalichangia jumla ya shilingi bilioni 181.3.

Majengo haya hayapo kwenye vitabu vya Chuo Kikuu cha Dodoma wala katika vitabu vya mifuko ya hifadhi ya jamii. Hii inatokana na uelewa tofauti uliopo kati ya pande mbili zinazohusika. Mifuko ya hifadhi ya jamii inafahamu kwamba kiasi cha fedha kilichotumika kujenga majengo hayo kilikuwa ni mikopo kwa serikali, wakati serikali inafahamu kwamba ilikuwa ni uwekezaji wa mifuko hiyo. Mifuko ya jamii inatakiwa kufuata mikataba wa makubaliano iliyowekeana kati yao na serikali ili kuweza kuonyesha majengo hayo kwenye vitabu vyao vya hesabu.

3.4.2 Haja ya Kuwa na Taarifa za Msingi (Database) kwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma

Kwa kuzingatia ukweli kwamba Bodi za Wakurugenzi humaliza muda wake kwa nyakati tofauti, inakuwa vigumu kwa mamlaka za uteuzi kufuatilia kwa urahisi. Hivyo basi, ni maoni yangu kuwa Msajili wa Hazina anapaswa kutengeneza kumbukumbu “database” ya bodi zote za wakurugenzi ambayo itakuwa imeandaliwa ili kutoa ishara ya kumalizika kwa muda wa bodi ya wakurugenzi na kuiwezesha mamlaka ya uteuzi kupata taarifa mapema kwa ajili ya uteuzi wa bodi mpya. Pamoja na majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali kukiri kuwepo kwa kumbukumbu za Msingi (Database) inayowapa ishara waliopewa mamlaka ya kupendekeza Bodi za Wakurugenzi miezi sita kabla ya muda wao kwisha bado tatizo lipo kama ilivyodhihirishwa kwa kuchelewa kuteuliwa kwa Bodi za Wakurugenzi za NCCA, TEMDO, TAWIRI, TAFORI na Bodi ya Mkonge Tanzania.

3.4.3 Uhakika wa Vyanzo vya Fedha za Uwekezaji

Tanzania ikiwa ni nchi inayoendelea, inatakiwa kuwa na mpango wa namna ya kuwa na fedha za kuwekeza kwa masharti nafuu. Kuna haja ya Serikali kupitisha sheria ya kuyataka Mashirika muhimu kuwekeza kwenye soko la hisa la Dar es Salaam. Mfano wa Mashirika hayo ni kampuni za madini, kampuni za simu, kampuni za saruji na kampuni za vinywaji.

Kuna haja ya serikali kusimamia sheria itakayowezesha Taasisi za Umma kurejesha hazina mali kama amana katika mabanki ambazo zimetelekezwa au zimeachwa na wamiliki kwa zaidi ya miaka mitano. Mali hizo ambazo hazina wamiliki zinaweza kuwekwa kama amana katika mfuko wa uwekezaji uliopendekezwa na kutumika kama chanzo cha fedha za uwekezaji. Fedha nyingine zitakazowekwa kwenye Mfuko ni zile ambazo zitapatikana katika gawio linalotokana na uwekezaji katika mashirika ya

umma na fedha zitokanazo na mauzo ya mali za serikali ili kuhuisha uwezo wa Mfuko.

3.5 Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kwa mwaka 2011/12

3.5.1 Manunuzi ya Dharura Ambayo Hayakupata Kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali

Katika Mamlaka ya Bandari Tanzania ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ilifanya manunuzi ya dharura yenye thamani ya dola za Kimarekani 810,000 na Euro 13,915,783 bila idhini mrejesho kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hali kadhalika ukaguzi ulibaini kuwa Chuo Kikuu cha Mzumbe kilifanya manunuzi ya dharura yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.987 kwenye ujenzi wa majengo matano ya stoo katika kampasi ya Dar es Salaam bila idhini mrejesho kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

3.5.2 Utoaji wa Zabuni Kinyume na Taratibu Zilizowekwa-NSSF

Ukaguzi umegundua kwamba Bodi ya Zabuni ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) iliidhinisha na kumpa mkataba wa kununua vipooza hewa katika nyumba za biashara za NSSF zilizopo Kaloleni katika Manispaa ya Arusha kwa muuzaji ambaye bei yake ilikuwa shilingi milioni 430. Bei waliyokubaliana ni kubwa kwa shilingi milioni 230 zaidi ya makadirio ya wahandisi (Ongezeko la asilimia 87%). Katika maelezo yaliyotolewa na menejimenti ni kwamba makisio haya yalikuwa ni ya mwaka 2009 na hivyo yalikuwa yameshaathiriwa na mfumuko wa bei. Hata hivyo sababu hii haikutosheleza kuelezea sababu za kupanda kwa gharama kwa zaidi ya asilimia (87%) kama ilivyoelezwa kwenye dokezo la kamati ya tathmini waliyoituma kwenye Bodi ya zabuni ya tarehe 29/02/2012. Katika hali ya kawaida tofauti inayokubalika na makisio ya mhandisi yanatakiwa yawe kati ya 10%.

3.5.3 Usimamizi Mbovu wa Mkataba wa Ujenzi wa Gati Katika Ziwa Tanganyika

Mamlaka ya Bandari Tanzania mnamo tarehe 20 Novemba, 2009 iliingia makubaliano na kampuni ya Modspan Enterprises Ltd kusanifu na kujenga Gati katika Ziwa Tanganyika kwenye maeneo ya Logasa, Kyala, Karema na Kirando kwa gharama ya shilingi bilioni 4.870 ikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani. Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizokaguliwa mkataba huu ulikuwa wa miezi kumi na nane (18) uliotarajiwa kukoma mwezi Julai, 2011.

Mapitio ya utekelezaji wa mkataba huu yaligundua kwamba mkandarasi ambaye ni Modspan Enterprises Ltd hakusimamia mradi vizuri kitu ambacho kimesababisha mkandarasi kutumia muda mrefu na matokeo yake kuongezeka kwa gharama za manunuzi bila sababu. Pamoja na mapungufu yote hayo menejimenti ilitoa nyongeza ya kazi kwa mkandarasi kwa kiasi cha shilingi milioni 647.865 hivyo kusababisha gharama za mradi huu kuongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 5.518 kutoka gharama za awali za shilingi bilioni 4.870. Hadi kufikia kipindi nilichokuwa nakamilisha ukaguzi huu jumla ya shilingi bilioni 3.127 sawa na asilimia 56.6 ya jumla ya gharama za mradi zilishalipwa kwa mkandarasi ambapo sehemu ya kazi iliyokamilika ilikuwa asilimia 34 tu.

3.5.4 Kusitishwa kwa Mkataba Kulikosababisha Malipo Yasiyo na Tija kwa Mamlaka ya Bandari

Mamlaka ya Bandari Tanzania iliingia mkataba na kampuni ya Oceana Advanced Industries Ltd mwezi Novemba, 2008 kukarabati eneo la meli kutia nanga katika lango Na.1 - 11 na kituo cha kupakulia mafuta cha Kurasini katika Bandari ya Dar es Salaam. Kwa mujibu wa makubaliano gharama za mkataba huu zilikuwa shilingi bilioni 4.634 bila kodi ya ongezeko la thamani. Ukarabati huu ulitakiwa ukamilike kufikia tarehe 11 Mei, 2009. Mapitio niliyofanya katika mkataba huu nilibaini kuwa mradi haukukamilika kwa muda hivyo kulazimu nyongeza ya miezi minne (4) hadi Agosti,

2009. Hii ni kutokana na menejimenti ya Bandari kushindwa kumkabidhi mkandarasi eneo husika la kazi gati (berth) 7 kama walivyokubaliana. Kushindwa kutekelezwa kwa mkataba huu kulisababisha kuibuka kwa kazi za ziada zilizogharimu kiasi cha Dola za Kimarekani 753,807.60.

Kufikia tarehe 15 Mei, 2010 mamlaka iliamua kusitisha mkataba na Oceana Advanced Industries Ltd kwa kisingizio kwamba kulikuwa na msongamano wa meli katika Bandari ya Dar es Salaam hivyo kazi isingeweza kuendelea. Kusitishwa kwa mkataba huu kuliilazimu Mamlaka kumlipa mkandarasi kiasi cha shilingi bilioni 1.657 zikiwa ni gharama za fidia kwa vitendea kazi vyake kukaa muda mrefu bila kufanya kazi. Hata hivyo mpaka kufikia tarehe 1 Julai 2010 ni kiasi cha shilingi milioni 641.844 ambacho kililipwa na kiasi cha shilingi milioni 955.338 kililipwa Aprili, 2011 miezi tisa baadae, baada ya majadiliano ya muda mrefu ya kumalizia malipo ya mwisho. Kutokana na malipo haya kutolipwa kwa wakati ilisababisha mkandarasi kutoza riba ya shilingi milioni 584.634. Kwa hali hiyo ilisababisha Mamlaka kulipa kiasi cha shilingi bilioni 2.242 bila kunufaika kwa huduma yoyote.

3.5.5 Michango ya Wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Kutowasilishwa kwa Wakati

Ukaguzi wa Chuo Kikuu Huria ulibaini kuwa chuo hakijawasilisha michango yenye thamani ya shilingi bilioni 2.481 kwa mfuko husika. Mapungufu kama haya yalibainika pia katika ukaguzi uliofanyika katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mtwara, TEMDO, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, Chuo cha Elimu ya Watu Wazima, CARMATEC, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida na Mamlaka ya Udhibiti wa Hisa na Mitaji.

Waraka wa Hazina Na.C/BA 54/ 328/01/15 wa tarehe 19 Julai, 2011, uliwafahamisha watendaji wa taasisi zote za umma kuwa jukumu la makato yote ya michango ya watumishi wa Umma kama PSPF, LAPF, PPF, NSSF, GEPF na

NHIF yatakatwa na kupelekwa moja kwa moja kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Hazina.

3.5.6 Ukiukwaji wa Waraka wa Serikali kuwalipa Pensheni Watumishi wa Mikataba katika Shirika la Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)

Waraka wa Serikali Na. C/AC.45/257/01/Temp./26 wa tarehe 1 Disemba, 2009 unataka watumishi wa mikataba kulipwa kiinua mgongo baada ya mkataba na wasilipwe mafao ya pensheni kama watumishi wa ajira za kudumu. Wafanyakazi wa ajira ya kudumu wanatakiwa kulipwa mafao ya Pensheni yanayotokana na asilimia fulani iliyopo kisheria na sio mafao ya mkataba.

Katika ukaguzi wa Shirika la Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ilibainika kuwa Mfuko ulikiuka waraka huo wa serikali na kuwalipa shilingi milioni 13.062 watumishi wake wa mkataba na shilingi bilioni 1.965 watumishi wa ajira ya kudumu kama malipo ya mkataba (gratuity) ambapo wafanyakazi wa Pensheni wanatakiwa kulipwa mafao ya kiinua mgongo peke yake. Kukiukwa huku kwa waraka huo wa serikali kumeliingiza shirika kwenye matumizi yasiyokuwa ya lazima na yasiyoleta tija kwa Shirika.

3.5.7 Uteuzi Wenye Mapungufu wa Menejimenti ya Shirika la Masoko Kariakoo Uliofanywa na Halimashauri ya Jiji

Kifungu cha 5 kifungu kidogo cha 2(a) cha sheria iliyoanzisha shirika la masoko kimeelekeza kuwa Mwenyekiti wa Bodi atateuliwa na Rais na kifungu cha 5 kifungu kidogo 2(b) kinaeleza kuwa wajumbe wengine wa Bodi watateuliwa na Waziri mwenye dhamana.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa shirika la masoko limekuwa likiendeshwa bila ya Bodi ya Wakurugenzi ambayo imeundwa kwa mujibu wa Sheria tangu mwaka 2000 ambapo Bodi iliyopo iliwekwa madarakani na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Pia Meneja Mkuu aliyetakiwa

kuteuliwa na Rais aliwekwa madarakani na Waziri mwenye dhamana kinyume na Kifungu cha 5 (4) cha Sheria iliyoanzisha shirika.

3.5.8 Shirika la Utangazaji la Tanzania Katika Matatizo ya Kifedha

Katika mwaka uliopita nilibaini kwamba Shirika la Utangazaji la Tanzania limeripotiwa kuwa na hasara ya shilingi bilioni 1.590 (2011: shilingi 3.547). Shirika lina madeni yanayofikia shilingi bilioni 2.738 (2011; shilingi bilioni 1.136). Hata hivyo linaitegemea serikali kwa kiasi kikubwa katika mahitaji yake ili kujiendesha na kulipia madeni mbalimbali. Hali hii inaleta wasiwasi na endapo itaendelea kwa kipindi kirefu shirika linaweza kushindwa kujiendesha.

3.5.9 Hali Mbaya ya Mwenendo wa Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali Kuu (PSPF)

Katika ukaguzi uliopita Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali Kuu (PSPF) ulibaini kwamba, uthamini wa uwezo wa Mfuko kuwalipa wanachama wake (actuarial valuation) ulifanyika mara ya mwisho tarehe 30 Juni, 2010 na Kampuni ya kujitegemea ya Genesis Actuarial Solutions. Kampuni ilionyesha kuwa hali ya kifedha ya Mfuko iliendelea kuwa mbaya na uthaminishaji huo ulibaini mapungufu (nakisi) katika uwezo wa Mfuko (actuarial deficit) ya shilingi trilioni 6.487 kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2010.

Pia nilibaini kwamba katika mwaka wa 2011, serikali ilikubali kuanza kurejesha mafao yaliyolipwa awali na Mfuko kuanzia mwaka 2004 hadi 2010 kiasi cha shilingi bilioni 716. Kiasi hiki kilipaswa kurejeshwa kidogo kidogo na serikali kila mwaka katika mgawanyo wa shilingi bilioni 71.6 kwa muda wa miaka kumi kuanzia mwaka 2011. Kufikia mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 kulikuwa na malimbikizo ya marejesho ya mwaka 2011 na 2012 yalifikia kiasi cha shilingi bilioni 133.

3.5.10 Kuongezeka Matukio ya Uwindaji Haramu Katika Hifadhi ya Taifa Tanzania

Katika ripoti yangu ya mwaka jana nilibaini katika taarifa zinazotokana na ripoti za robo mwaka za Idara ya Ulinzi ya Shirika la Hifadhi za Taifa kuwa vitendo vya uwindaji haramu hususani tembo vimeongezeka kwa kasi. Kutokana na taarifa zilizotolewa kutoka mbuga saba, jumla ya tembo 110 waliuwawa katika kipindi cha mwaka 2011/2012.

Napenda kutambua mikakati iliyowekwa na Shirika la Hifadhi za Taifa kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasiri na Utalii katika kuzuia na kupambana na shughuli za uwindaji haramu mfano kuongezwa kwa askari wa wanyama pori, kushirikisha vikosi vya askari polisi, kuimarisha idara ya upelelezi ya wanyamapori, kuboresha zana za kutendea kazi na hatua nyinginezo.

Kwa sasa ujangiri ni janga la kitaifa na kimataifa ambapo kama lisipodhibitiwa kwa miaka ya hivi karibuni litahatarisha uhai wa wanyamapori Tanzania. Hivyo basi serikali kwa kushirikiana na wadau wengine ni muhimu wakatafuta mbinu za kuzuia hali hiyo ambayo ni ishara mbaya kwa ustawi wa wanyama pori.

3.5.11 Kontena Mbili za Vitabu vya Maktaba Kutoka Shirika la Kimataifa la Kufadhili Watoto Hazijatolewa Bandari ya Dar es Salaam Tangu Mwaka 2009

Katika ripoti yangu ya mwaka jana nilibaini kuwa Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imeshindwa kutoa mzigo wa vitabu katika Bandari ya Dar es salaam tangu mwaka 2009. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2012/2013 vitabu hivyo vilikuwa bado havijatolewa bandarini vikisubiria malipo ya kodi na gharama za kuhifadhi mizigo ambayo imefikia kiasi cha shilingi milioni 147. Hadi kufikia tarehe 7 Machi, 2014 Mlipaji Mkuu wa Serikali hajaweza kujibu utekelezaji wa mapendekezo yangu.

3.5.12 Malipo ya Leseni ya Biashara Yaliyolipwa kwa TCRA na TBC Kwa Niaba ya Star Media

Nilibaini kuwa kiasi cha shilingi milioni 618.3 kililipwa na Shirika la Utangazaji Tanzania kwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa niaba ya Star Media (Tanzania) Limited (startimes) katika mwaka 2010 kwa ajili ya leseni ya biashara. Hata hivyo, Star Media (Tanzania) Company ina mkataba wa utendaji uliosainiwa na Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC) ambapo Kampuni ya Star Media (Tanzania) imepewa msamaha wa kulipa ada ya leseni ya biashara kwa kipindi cha miaka kumi na hivyo imesababisha malipo ya awali ya leseni ya biashara yaliyolipwa na TBC kwa TCRA kutotambuliwa kama Mtaji wa hisa za TBC katika Kampuni ya Star Media (Tanzania). Kampuni ya Star Media (Tanzania) ilipata hasara ya dola za Kimarekani 710,456 katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi huo (Dola za kimarekani 1,463,253,158 kwa kipindi cha miezi 18 ya mwanzo kwa kipindi kilichoishia 31 Disemba, 2010). Hakuna kumbukumbu iliyoonyeshwa katika taarifa za hesabu kuhusiana na kiasi cha hasara ya hisa za TBC katika Star Media.

3.5.13 Majengo ya NDC Kwenye Kitalu Na.2338 yaliyopo Mbezi Beach, Barabara ya Bagamoyo Hayana Mkataba wa Pango

Nilibaini kuwa Shirika la Maendeleo la Taifa halina mkataba wa pango na mpangaji wa sasa wa jengo hilo, Messrs Vignan Education Foundation (IMTU) baada ya mkataba na Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) kuisha mwezi Agosti, 2011. Vignan Education Foundation amekataa kukubali masharti ya mkataba ulioandaliwa na NDC ambao pamoja na mambo mengine una kodi ya mwezi ya shilingi milioni 60. Kodi ambayo ilikadiriwa na mthamini (valuer) aliyebobea. Hadi kufikia tarehe 7 Machi, 2014 Mlipaji Mkuu wa Serikali hajaweza kujibu utekelezaji wa mapendekezo yangu.

3.5.14 Nyumba ya Bodi ya Sukari Tanzania Anayoishi Waziri wa Zamani wa Kilimo, Hifadhi ya Chakula na Ushirika Nilibaini kuwa Bodi ya Sukari Tanzania ina nyumba kwenye kiwanja Na. 482 iliyopo katika barabara ya Bray Masaki. Kwa muda mrefu nyumba hiyo amekuwa akiishi Waziri wa zamani wa Kilimo, Hifadhi ya Chakula na Ushirika. Licha ya juhudi zilizofanywa na Bodi kumuandikia barua Katibu Mkuu Kiongozi kuomba kuimiliki tena nyumba hiyo, Waziri aliahidi kurudisha nyumba hiyo ifikapo Disemba, 2011. Mpaka sasa hivi nyumba hiyo haijakabidhiwa kwa Bodi ya Wakurugenzi. Waziri kuendelea kukaa katika nyumba hiyo ni kuinyima Bodi haki yake ya kutumia nyumba hiyo ili kujipatia mapato. Bodi inabidi iweke juhudi zaidi kufuatilia ili kuweza kurudisha nyumba ya shirika katika mamlaka ya Bodi. Hadi kufikia tarehe 7 Machi, 2014 Mlipaji Mkuu wa Serikali hajaweza kujibu utekelezaji wa mapendekezo yangu.

3.5.15 Usafiri Dar es Salaam (UDA)

(a) Uuzwaji wa Hisa za UDA

Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) lilikuwa na jukumu la kuuza hisa za UDA na sio Bodi ya Wakurugenzi kama ilivyofanyika. Mwezi Julai, 2010, CHC iliishauri Bodi ya Wakurugenzi wa UDA kupata idhini ya serikali kabla ya kuendelea na uuzaji wa hisa za UDA. Bodi ya Wakurugenzi wa UDA iliendelea na uuzaji wa hisa hizo bila kupata kibali cha serikali. Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) lilitoa ushauri kwa Bodi ya Wakurugenzi wa UDA kuwa njia ya wazi itumike kulingana na sheria ya Manunuzi ya Umma ili kumpata mwekezaji bora katika Shirika la UDA. Bodi ya Wakurugenzi wa UDA ilipuuza ushauri huo na kuendelea na uuzaji huo wa hisa za UDA ambazo zilikuwa hazijagawiwa (unallotted shares).

- Hisa za Shirika la UDA zilithaminiwa kwa bei ya shilingi 744.79 kwa kila hisa mwezi Oktoba, 2009 na mwezi Novemba, 2010 thamani ya kila hisa ikawa 656.15. Hata hivyo, katika uuzaji huo, Bodi ya Wakurugenzi ya UDA

ilitoa punguzo la asilimia 60 kwa kila hisa kwa mwekezaji huyo (kwa tathimini ya bei ya hisa ya mwezi Oktoba, 2009), bila kuwepo na sababu za kufanya hivyo. Kwa hiyo kila hisa ilitakiwa kuuzwa kwa shilingi 298 kutoka shilingi 744.79 kwa hisa moja ambayo ilithaminishwa mwezi Oktoba, 2009 na hivyo kusababisha UDA kupata hasara ya shilingi bilioni 1.559.

Vile vile ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya UDA iliingia mkataba wa kumuuzia mwekezaji hisa 7,880,303 ambazo hazikugawiwa kwa bei ya shilingi 145 kwa kila hisa kwa jumla ya shilingi bilioni 1.143 badala ya shilingi 744.79 kwa hisa kulingana na ripoti ya mshauri ambapo hisa hizo zingekuwa na thamani ya shilingi bilioni 5.869. Hii ilisababisha shirika kupata hasara ya shilingi bilioni 4.727. Kwa kutumia bei ya hisa ya shilingi 298 na 145 badala ya shilingi 744.79 kwa hisa moja iliisababishia serikali hasara ya jumla ya shilingi 6.285 (shilingi 1.559 na shilingi 4.727).

- Mnunuzi (mwekezaji) alilipa kiasi cha shilingi 145 kwa hisa moja na kulipa jumla ya shilingi milioni 285 kinyume na thamani ya hisa ya shilingi 744.79 au 656.15 kwa hisa moja. Bodi ya Wakurugenzi ya UDA ilitoa punguzo la bei ya hisa hadi kufikia shilingi 145 kwa hisa moja ambazo hazikugawiwa, ukilinganisha bei ya punguzo iliyokuwa imeshafanyika mwanzoni ya Shilingi 298 kwa hisa moja ambapo inaonekana iliongeza tena punguzo la asilimia 53.

(b) Ripoti ya Makadirio ya Thamani ya Hisa na Mali za UDA

Ripoti ya makadirio ya thamani ya hisa iliyoandaliwa tarehe 30 Oktoba, 2009 na tarehe 15 Novemba, 2010, ilionyesha thamani ya mali za UDA ikiwa ni pamoja na mitambo na vifaa. Makadirio yaliyofanyika mwezi Agosti, 2009 hayakuainisha jumla ya mali za Shirika ukiondoa

madeni yote (Net Assets). Pia haikuonyesha madeni ya Shirika ambayo ni jumla ya shilingi milioni 473.241 ambayo yaliripotiwa kuwa yalishahamishiwa kwa Msajili wa Hazina.

- (c) **Kuthibitishwa Kiasi Kilicholipwa na Mnunuzi**
Mkataba wa kuwasilisha hisa wa tarehe 11 Februari, 2011 unaeleza kwamba mnunuzi (mwekezaji) atalipa jumla ya shilingi bilioni 1.143 kama bei ya ununuzi ya hisa zote ambazo hazijagawiwa na UDA ingawa mkataba haukuonyesha akaunti ya benki ambayo malipo yangefanyika. Mnunuzi (mwekezaji) alilipa kiasi cha shilingi milioni 285 katika akaunti namba OJ1021393700 ya benki ya CRDB inayomilikiwa na UDA. Kulikuwa hakuna malipo mengine ya ziada yaliyofanywa na mwekezaji kuhusiana na ununuzi wa hisa za UDA. Malipo haya ni sawa na asilimia 24.9 ya bei ya kuuza iliyokubaliwa.

Mwekezaji alidai kumlipa aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya UDA kiasi cha shilingi milioni 320 kama ada ya kukubali kununua UDA mwaka 2009. Mwenyekiti wa Bodi alikubali kupokea kiasi cha shilingi milioni 320 katika akaunti yake binafsi kutoka kwa Mwekezaji ikiwa kama ada ya ushauri alioutoa kwa Mwekezaji, ambayo ilizua mgongano wa kimaslahi.

SURA YA NNE

MASUALA MUHIMU AMBAYO HAYAKUTOLEWA TAARIFA KATIKA RIPOTI YA MWAKA ULIOPITA

4.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea kwa kifupi masuala muhimu ambayo yapo katika ripoti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuhusiana na ukaguzi wa mwaka 2011/2012, lakini kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wangu hazikuvingia katika ripoti ya mwaka uliopita.

Kwa mujibu wa kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ni wajibu wa kila Shirika la Umma kuwasilisha hesabu kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kufunga mwaka wa fedha. Kwa vile kumekuwa na kiasi kikubwa cha kutokuzingatiwa kwa matakwa haya ya sheria katika baadhi ya Mashirika ya Umma, ukaguzi katika baadhi ya Mashirika ya Umma umekuwa unachelewa kuanza na hivyo kusababisha Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kushindwa kutoa ripoti za kaguzi hizo katika ripoti ya mwaka husika. Ni muhimu ikaeleweka kuwa Mashirika ya Umma ambayo kaguzi zake zitashindwa kukamilika katika kipindi kinachotakiwa na hivyo kutoripotiwa katika ripoti ya mwaka ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kaguzi hizo zitaripotiwa katika mwaka unaofuata.

Hadi kufikia kipindi cha kuandaa ripoti ya mwaka jana (2011/2012) iliyowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais mwishoni mwa mwezi Machi, 2013, ni kaguzi za mashirika 95 tu zilitolewa taarifa. Kaguzi za Mashirika 79 zilikuwa kwenye hatua mbalimbali kutokana na kuchelewa kuwasilishwa kwa hesabu, kutokuwepo kwa Bodi za Wakurugenzi baada ya zile za awali kumaliza muda wake na menejimenti za mashirika husika kushindwa kujibu kwa wakati hoja za ukaguzi.

Mambo muhimu ambayo hayakutolewa taarifa kwenye ripoti yangu iliyopita na nimuhimu kutolewa taarifa katika ripoti hii ni pamoja na:

- 4.1 Taasisi ya Utafiti na Uvuvi (TAFIRI) Haijathaminisha Mali zake kwa Zaidi ya Miaka Tisa
- Viwango vya uhasibu vya Kimataifa (IAS 16 Para 34) vinahitaji mali za Shirika kuthaminishwa wakati thamani yake halisi inapotofautiana na thamani iliyoripotiwa kwenye vitabu vya Shirika. Zaidi ya hayo sheria inataka mali ambazo hazina mabadiliko ya thamani kwa uharaka zithaminishwe kila baada ya miaka mitatu hadi mitano. Hata hivyo, nilibaini kuwa Taasisi ya Utafiti na Uvuvi Tanzania (TAFIRI), haikuthaminisha mali zake tangu mwaka 2003 kama inavyotakiwa kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vya kimataifa.

Kwa sababu hiyo, TAFIRI iliripoti baadhi ya mali ambazo bado zinatumiwa kwa thamani ndogo sana, hivyo, kusababisha hesabu zake kutoonyesha uhalisia. Kwa Mfano, mitambo na mashine viliripotiwa kwa thamani ya shilingi moja, Gia za uvuvi shilingi saba na vyombo vya baharini kwa shilingi milioni 1.450. Hivyo, menejimenti inashauriwa kuthaminisha mali zake kwa wakati ili kuonyesha thamani halisi kwenye taarifa ya fedha za Taasisi.

- 4.2 Fedha Hazitolewi Kulingana na Bajeti Iliyoidhinishwa
- Malengo ya EPZA ni kuvutia, kukuza ukanda wa uwekezaji (EPZ) na ukanda maalum wa kiuchumu (SEZ) katika uwekezaji ili kufuatilia mchakato wa maendeleo ya Viwanda kwa haraka, kutoa huduma ya uwezeshaji kwa wawekezaji wa EPZ na SEZ kwa ufanisi, kuhamasisha uongezaji thamani wa malighafi, kujenga na kuongeza fursa za ajira pamoja na uongezaji wa mapato ya fedha za kigeni. Malengo hayo yote hayawezi kutimia iwapo hakuna upatikanaji wa fedha za kutosha.

Ukaguzi wa hesabu hususani katika utendaji wa Mamlaka ya Ukanda wa Uwekezaji Tanzania (EPZA) kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 ulibaini kuwa, EPZA ilishindwa kufikia malengo yake iliyojiwekea kutokana na kukosa fedha za kutosha serikalini. Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilikuwa shilingi bilioni 4.8. Kati ya hiyo bajeti iliyoidhinishwa, EPZA walipokea shilingi milioni 959.9 tu ambayo ni sawa na asilimia 19.8 hivyo kusababisha shilingi bilioni 3.9 kutokutolewa ambayo ni sawa na asilimia 80.2 hivyo kusababisha kutotekelezwa kwa shughuli zilizopangwa na Mamlaka.

Bohari ya Dawa (MSD) ni idara inayojitegemea chini ya Wizara ya Afya inayofanya kazi zake kwa misingi ya kibiashara. MSD ina wajibu wa kujiendesha yenyewe kwenye masuala ya kifedha. Kazi yake kubwa ni kununua, kutunza na kusambaza dawa na vifaa vya hospitali vyenye viwango vizuri nchini na kwa bei ya chini. Pia, inasambaza dawa zake kupitia mawakala walioidhinishwa na serikali nchi nzima.

Nilibaini kuwa utoaji wa fedha kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwenda Bohari ya Dawa kwa ajili ya utoaji wa huduma za hospitali za serikali haukuwa wa kuaminika wala kutabirika. Kwa Mfano, kipindi cha robo ya kwanza na ya pili ya mwaka 2011/2012, Wizara ilitoa jumla ya shilingi bilioni 4.3 sawa na asilimia 13 ya bajeti ya Bohari ya Dawa (MSD) ambayo ilikuwa ni shilingi bilioni 32. Hii inaweza kusababisha Bohari ya Dawa kutofikia malengo iliyojiwekea. Pia inaipa ugumu MSD kuweka mipango kwa ajili ya manunuzi ya dawa kutokana na hali ya upatikanaji wa fedha kutokuwa ya kuaminika, hivyo inaweza kusababisha bohari kuishiwa dawa na vifaa.

- 4.3 Manunuzi Yaliyofanyika Bila Ushindani wa Zabuni**
Kanuni ya 71 ya kanuni za Manunuzi ya Umma ya tangazo la serikali Na. 97 ya mwaka 2005 inatamka kwamba "Taasisi inaweza kununua bidhaa, huduma au kazi ndogo ndogo

moja kwa moja kutoka kwa muuzaji, mtoa huduma au mkandarasi kama gharama yake haitazidi shilingi 10,000,000”.

Nilibaini kwamba katika Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA) kuna vitu vilivyounuliwa vyenye thamani ya shilingi milioni 109.4 bila kuzingatiwa kwa mchakato wa ushindani wa zabuni. Pia manunuzi hayo hayakupitishwa na bodi ya zabuni kinyume na kanuni za fedha za Chuo.

Pia katika Kampuni ya Huduma za Majini (Marine Service Company), niliweza kubaini manunuzi yaliyofanyika moja kwa moja kutoka kwa wauzaji wa vifaa vya ofisini vya zaidi ya shilingi milioni 80 kwa kutumia fedha taslimu. Kwa vile gharama ilikuwa kubwa, Kampuni ya Huduma za Majini ilitakiwa kutumia njia ya ushindani katika ununuzi wa vifaa hivyo. Hii ina maana kwamba, kampuni ilikosa fursa ya kupata bei nzuri na yenye unafuu. Pia Mfumo huu unajenga mianya ya udanganyifu katika kampuni.

4.4 Ubungo Plaza Limited Inaidai Hoteli ya Blue Pearl Malipo ya Huduma ya kiasi cha shilingi Milioni 139.1

Malipo ya huduma ni ada ya ziada ambayo mmiliki wa Ubungo Plaza Limited anawatoza wapangaji wake kama gharama za uendeshaji jengo pamoja na huduma za jamii kama vile maji, umeme, ulinzi, usalama na usafi wa eneo kwa ujumla. Huduma hizo zinazotumiwa na wapangaji hulipwa tofauti na kodi ya jengo.

Mnamo tarehe 19 Oktoba, 2006, Ubungo Plaza Limited iliingia mkataba wa kukodisha sehemu ya jengo lake kwa mmiliki wa hoteli ya Blue Pearl. Moja ya makubaliano yao ilikua ni mpangaji kulipia gharama zote za huduma zinazopatikana katika viwango vilivyoafikiwa na pande zote mbili. Kwa mujibu wa nyaraka zilizotolewa na meneja wa jengo (M/s Gimco Africa), Hoteli ya Blue Pearl ilitakiwa kulipa shilingi milioni 223 kama gharama zitakazotumika kwa mwaka 2011 kama walivyokubaliana kwenye mkataba.

Hata hivyo, kulingana na taarifa ya fedha ya Ubungo Plaza Limited kwa mwaka 2011, Blue Pearl ililipa kiasi cha shilingi milioni 83.9 ambayo ni sawa na asilimia 37.6 ya kiasi kilichotakiwa kulipwa katika mwaka 2011 na kubakiza kiasi cha shilingi milioni 139.1 bila kulipwa. Mikataba mingine midogo midogo ilionekana kulipwa kwa wakati na Hoteli hiyo, tofauti na mkataba huu wa malipo ya huduma. Hivyo bodi ya wakurugenzi ya Ubungo Plaza Limited inatakiwa kuchunguza kiasi kinachotakiwa kulipwa na mpangaji kulingana na makubaliano ya mkataba uliosainiwa na pande zote mbili. Hii ni kutokana na Hoteli ya ya Blue Pearl kuwa mtumiaji mkuu wa huduma hizo za maji na umeme, pamoja na hayo mmiliki ndio anayeonekana kubeba mzungo wote endapo kama mpangaji hataweza kutimiza majukumu yake ya ulipaji.

4.5 Chuo cha Ufundi Stadi MPANDA kina Mali Ambazo Hazitumiki Zenye Thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni Moja

Chuo Cha Ufundi Stadi Mpanda ni mojawapo ya vyo 21 vinavyoendesha na Mamlaka ya Ufundi Stadi (VETA). VETA ni Shirika la umma linalojitegemea, limeanzishwa chini ya sheria No. 1 ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1994 na iliyorekebisha mwaka 2006 (CAP 82).

Katika ukaguzi wa hesabu za Mamlaka za mwaka ulioishia 30 Juni, 2012 nilibaini kwamba Chuo cha Ufundi Stadi Mpanda kina mashine zenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni moja kuwa zimetelekezwa, na baadhi ya mashine zilikosa vifaa vyake. Pia nilibaini kuwa walimu wa VETA hawakupata mafunzo ya utumiaji wa mashine hizo mpya kulingana na teknolojia, hivyo kusababisha mashine hizo kutotumika. Mifano ya mashine hizo zilizotelekezwa ni pamoja na mashine na "drilling machines", "rolling machines", "thicknessing planner" na "saw spiddle machine".

Menejimenti ya VETA, inapaswa kuweka mikakati wa kuhamisha mashine zote ambazo hazitumiki kwenye baadhi ya vituo kama vile kituo cha Mpanda na kupelekwa kwenye vituo vingine vyenye uhitaji wa mashine hizo. Pia menejimenti inapaswa kutoa mafunzo kwa walimu wake jinsi ya kutumia mashine kulingana na utandawazi, badala ya kuzitelekeza mashine ambazo zililigharimu shirika fedha nyingi.

4.6 Ucheleweshwaji wa Michango ya Wanachama kwenda kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Kwa mujibu wa sheria, mwajiri anatakiwa kukata asilimia fulani ya kipato cha mwajiriwa wake kwa ajili ya Mchango katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama vile Mfuko wa Pansheni wa Mashirika ya Uma (PPF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) n.k. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa baadhi ya mashirika ya umma kama vile Shirika la Masoko Kariakoo (KMC) na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) hayajawasilisha michango kwenye mashirika ya Hifadhi ya jamii kwa mujibu wa sheria.

Shirika la Masoko Kariakoo halikuwasilisha michango yenye thamani ya shilingi milioni 297 kwenye mifuko husika. Suala hili lilitolewa taarifa kwenye miaka ya nyuma, ingawa shirika linaendelea kupata ugumu wa kuwasilisha makato kwenye Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii.

Pia Kampuni ya Ranchi za Taifa ilishindwa kuwasilisha makato yake kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa wakati. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 michango ya kiasi cha shilingi milioni 777.9 ilikuwa haijawasilishwa kwenye mifuko husika. Deni hilo limekua likiongezeka kila baada ya mwaka. Kwa mujibu wa taarifa ya mwaka wa fedha 2010/2011, kampuni ilikuwa inadaiwa kiasi cha shilingi milioni 604.6.

Ucheleweshwaji huo wa michango ya hifadhi ya jamii inapelekea mashirika/kampuni kutozwa riba ikiwa kama

adhabu ya ucheleweshwaji. Pia hali hii inawanyima fursa wafanyakazi kupata mafao yao pindi watakapostaafu.

4.7 Ucheleweshwaji Wa Mikopo kwa Wanafunzi

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ipo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Bodi hii ilipewa mamlaka na serikali kuwa na jukumu la kutoa mikopo kwa wanafunzi katika ngazi ya stahada ya juu na shahada katika taasisi za elimu ya juu ndani na nje ya nchi. Katika taarifa ya fedha ya HESLB inayoishia tarehe 30 Juni, 2012, nilibaini kuwa wanafunzi katika vyuo mbalimbali walicheleweshewa mikopo yao. Mifano ya vyuo ambavyo vilicheleweshewa mikopo kwa wanafunzi wake ni pamoja na Chuo kikuu cha Ushirika na Stadi za Biashara (MUCCOBs) kiasi cha shilingi milioni 500.2, Chuo Kikuu Mkwawa shilingi milioni 440.8, Chuo Kikuu Cha Ruaha milioni 89.2 na Chuo Kikuu cha Zanzibar milioni 70.6. Hali hii inaweza kusababisha kutokuelewana kati ya Menejimenti ya vyuo husika na wanafunzi wanaostahili kupata mikopo hiyo. Pia ucheweleshwaji huu wa utoaji wa mikopo unaweza kuathiri maendeleo ya wanafunzi.

4.8 Wanafunzi Walioacha/Kuahirisha Masomo Wapatiwa Mikopo

Ibara ya pili (2) sehemu ya kwanza ya Mwongozo wa Ukopesaji (Lending Manual) wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) inaelezea vigezo vya wanaostahili kupata mikopo. Moja ya vigezo ni ufaulu kwa wanafunzi kuelekea mwaka wa masomo unaofuata. Uhakiki uliofanywa kwenye baadhi ya vyuo uliniwezesha kubaini kuwa mikopo ya kiasi cha shilingi milioni 214.5 kilitolewa wanafunzi walioshindwa mitihani na kutoendelea na chuo na wengine walioahirisha masomo. Baadhi ya vyuo hivyo ni pamoja na vyuo vikuu katika nchi ya Algeria na Cuba shilingi milioni 132, Chuo Kikuu cha Dodoma shilingi milioni 43.9, Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) shilingi milioni 28.9 na Chuo Kikuu cha Urusi shilingi milioni 9.6.

Pia nilibaini wanafunzi walipewa mikopo bila ya kuzingatia matokeo ya mitihani yao kama ilivyoainishwa katika kanuni za fedha za HESLB, hivyo kukosesha fursa kwa wanafunzi walio stahili kupata mikopo. Hii inasababisha matumizi mabaya ya fedha kwenye vyuo na hasara kwa umma kutokana na Bodi kushindwa kukusanya fedha kutoka kwa watu walionufaika na mikopo hiyo.

4.9 Kushuka Kwa Hali ya Kifedha Katika Shirika La Masoko Kariakoo

Shirika la Masoko Kariakoo ni muhimili katika kusimamia na kudhibiti Soko la Kariakoo pamoja na uanzishwaji wa masoko mengine katika jiji la Dar es Salaam. Katika utekelezaji wa kazi zake, menejimenti inatakiwa kutazama kwa makini masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii pamoja na kutoa huduma za jamii kwa umma ikiwa ni pamoja na afya.

Hata hivyo, Shirika limekuwa likiingia hasara kwa kipindi cha miaka sita mfululizo, ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 Shirika limelimbikiza hasara ya shilingi bilioni 1.4. Vivyo hivyo Shirika la Masoko Kariakoo limetokea kuwa na hali mbaya katika uendeshaji wake. Hii ni kutokana na mali za muda mfupi (current assets) za Shirika kuwa za kiasi ya shilingi milioni 135.2 ambazo zinashindwa kulipa madeni yake ya muda mfupi (current liabilities) ya kiasi cha shilingi milioni 613.7 katika kipindi cha mwaka 2012. Uwiano wa mali na madeni ya muda mfupi kwa Shirika hilo ulikuwa ni 0.22:1 ukiwa chini ya uwiano wa 2:1 unaokubalika. Kwa hiyo endapo hali hii itaendelea, Shirika linaweza kushindwa kujiendesha.

4.10 Uchakavu wa Miundombinu ya Maji Safi na Mazingira Pamoja na Hali Mbaya ya Mabweni TIA

Taasisi ya uhasibu Tanzania (TIA) ilianzishwa chini ya Executive Agency Act No.30 ya mwaka 1997. Taasisi hii inajishughulisha zaidi na masuala ya kitaaluma, utafiti,

ushauri wa kiuhasibu, manunuzi na taaluma nyingine za ufundishaji.

Taasisi ya Uhasibu Tanzania ina vyuo katika mikoa ya Mbeya, Singida na Mtwara. Vyuvo hivyo vinaongozwa na mameneja ambao wanaripoti moja kwa moja kwa Mkurugenzi Mtendaji. Lengo kuu la taasisi ni kuboresha elimu, kuongeza idadi ya wahitimu kupitia mitihani ya kitaaluma yaani NBAA na NBMM, pamoja na kupanua miundombinu ya malazi ya kutosha kwa wanafunzi wake.

Katika Chuo cha Mbeya, mabweni yalijengwa mwaka 1972, kwa nia ya kila chumba kulaza wanafunzi wawili. Hata hivyo, ziara iliyofanywa katika kampasi ya Mbeya mnamo Januari, 2013 tulibaini kuwa kila chumba wanalala wanafunzi wanne kutokana na mahitaji makubwa ya malazi kwa wanafunzi. Pamoja na mabweni kuwa na wanafunzi wengi kuliko ilivyotarajiwa lakini hayakuwa kwenye hali nzuri. Mfano paa kuvuja maji, uchakavu wa miundombinu ya maji safi na mazingira ambayo haiwezi kuhudumia ongezeko la wanafunzi.

4.11 Kukosekana kwa Umiliki wa Kisheria wa Mali katika Baadhi ya Mashirika ya Umma

Hati miliki ni nyararaka za kisheria ambazo zinaonyesha umiliki wa mali. Pia zinampa mmiliki haki na mamlaka ya mali zinazomilikiwa. Nyaraka hizo pia ni muhimu kwa sababu zinaweza kutumika kama dhamana endapo shirika litahitaji mkopo kutoka Benki.

Uhakiki wa mali katika baadhi ya mashirika kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Disemba, 2011 na 30 Juni, 2012 niliweza kubaini taasisi kadhaa zisizo na umiliki wa kisheria kwenye baadhi ya mali zake. Baadhi ya mashirika hayo ni pamoja na Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA), Taasisi ya Utafiti na Uvuvi Tanzania (TAFIRI), Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Kampuni ya

Ranchi za Taifa (NARCO). Hatari ambayo inaweza kujitokeza kwenye mamlaka hizo ni pamoja na kupoteza haki kwenye mali zao na kutokuwa na msingi thabiti kwenye madai ya mali zao endapo kutatokea migogoro.

4.12 Fedha zilizotolewa Kwenye Miradi ya Maendeleo VETA Hazijatumika

Wakati wa mapitio ya bajeti ya VETA dhidi ya matumizi halisi, niliweza kubaini kuwa fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 hazikutumika kulingana na bajeti iliyoidhinishwa. Mfano, bajeti iliyoidhinishwa katika kituo cha VETA Kihonda ilikua ni shilingi milioni 175, lakini ni shilingi milioni 48.3 tu zilitumika katika miradi michache na kuacha shilingi milioni 126.7 kutotumiwa ambazo ni sawa na asilimia 72.4. Pia bajeti iliyoidhinishwa kwa matumizi ya maendeleo katika kituo cha VETA Dakawa, ilikuwa ni shilingi milioni 49.8, kati ya hizo, kiasi kilichotumika ni shilingi milioni 13.7 tu na kuacha shilingi milioni 36.1 kutotumika ambazo ni sawa na asilimia 72.4.

4.13 Ubora Usioridhisha wa Ghala la Shirika la Rasilimali za Reli Tanzania Mkoani Shinyanga

Kampuni ya kusimamia Rasilimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO) lilianzishwa mwaka 2002 chini ya sheria ya makampuni Tanzania na kupewa cheti chenye namba 60578. Malengo yake ni kuendeleza miradi mipya ya reli, kuwekeza kwenye miundombinu, pamoja na kukuza na kusimamia miundombinu iliyopo.

RAHCO ilifanya uwekezaji wa ujenzi wa ghala katika mkoa wa Shinyanga. Ghala hilo ambalo liligharimu kiasi cha shilingi bilioni 3.27 lilitakiwa kumalizika mwishoni mwa mwaka 2012. Mnamo mwisho wa mwaka, menejimenti ilikuwa inasubiri cheti cha mwisho cha uthibitisho kutoka kwa mkandarasi. Wakati wa ukaguzi nilibaini uvujaji wa

paa na uwepo wa nyufa kadhaa kubwa ndani ya jengo hilo jambo linaloashiria uwezekano wa kazi iliyofanyika kuwa chini ya kiwango. Ni wazi kwamba thamani ya fedha katika ujenzi huo haikupatikana.

SURA YA TANO

USIMAMIZI WA SHERIA YA MANUNUZI NA MIKATABA

5.0 Utangulizi

Tanzania imefanya maboresho makubwa ya ya mifumo ya manunuzi iliyosababisha kuanzishwa kwa sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2001 kama ilivyorekebisha mwaka 2004 ili kuhakikisha manunuzi ya Umma yanafanyika kwa mujibu wa Sheria za Manunuzi ya Umma. Hivyo basi, ili kuhakikisha kwamba Sheria ya Manunuzi inafuatwa, kifungu Na. 44 (2) cha Sheria ya Manunuzi kinamtaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuainisha katika ripoti zake kama taratibu zote za manunuzi zimezingatiwa na Taasisi husika.

Sura hii, inatoa majumuisho ya taarifa za usimamizi wa manunuzi na mikataba katika Taasisi za Umma zilizoonekana muhimu kuripotiwa. Ukaguzi wa manunuzi na mikataba ulifanyika sambasamba na ukaguzi wa kawaida wa hesabu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Septemba, 2012, 31 Disemba, 2012 na 30 Juni, 2013. Matokeo ya ukaguzi wa mikataba iliyoingiwa na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yameainishwa ndani ya sura hii.

5.1 Usimamizi wa Manunuzi

Kulingana na kifungu Na.3(a) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004, manunuzi inamaanisha kununua, kukodisha, kupata bidhaa, ujenzi au huduma inayofanywa na taasisi kwa kutumia fedha za umma, kwa niaba ya Wizara au Idara ya Serikali au Shirika la Umma na ikijumuisha kazi zote zinazohusiana na upatikanaji wa bidhaa au huduma ikiwa ni pamoja na kuainisha mahitaji, kuteua na kutangaza zabuni na kutoa mikataba. Yafuatayo ni mambo ambayo yalionekana kuwa na kasoro kwenye kaguzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

5.1.1 Muungiliano wa Majukumu kati ya Mihimili Mikuu ya Manunuzi

Kifungu cha 37 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004 kinaelekeza kuwa tathmini zote za zabuni zifanywe na kamati ya tathmini chini ya Kitengo cha Manunuzi. Kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma wajumbe wa kamati ya tathimini ya zabuni watapendekezwa na kitengo cha Manunuzi na kudhibitishwa na Mkuu wa Taasisi husika. Kadhalika kifungu cha 38 cha sheria hii kinataka kamati ya tathmini ya zabuni, Kitengo cha Manunuzi, Bodi ya Zabuni na Mtendaji Mkuu kufanya kazi zao bila kuingiliana.

Ukaguzi wangu juu ya utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 ulibaini kuwa zipo baadhi ya taasisi za umma ambazo kamati zake za tathmini ya zabuni zilijumuisha wajumbe toka kitengo cha manunuzi kinyume na matakwa ya sheria. Hali hii inaweza kuleta muungiliano wa maamuzi na hivyo kusababisha taratibu kukiukwa. Dosari hii ilibainika katika ukaguzi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa, Chuo cha Ushirika na Mafunzo ya Biashara Moshi na Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro.

Kadhalika nilibaini uteuzi usio sahihi wa wajumbe wa kamati ya zabuni kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambapo wajumbe waliteuliwa na Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi badala ya Mkuu wa Taasisi husika. Hii ni kinyume na kifungu cha 37 (2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma namba 21 ya mwaka 2004 kinachomtaka Mkuu wa Taasisi kuwateua wajumbe wa tathimini ya zabuni baada ya kupata mapendekezo kutoka Kitengo cha Manunuzi.

Kwa kuzingatia sheria hii, ukaguzi katika Shirika la Umeme Tanzania ulibaini muungiliano wa maamuzi kati ya Idara za Watumiaji (user departments) na Bodi ya Zabuni ambapo mtumiaji alionekana kupendekeza jina la mtoa huduma na njia ya manunuzi. Dosari hii ilibainika katika zabuni Na.

PA/001/10/HQ/N/024 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 (Dola za kimarekani 1,225,703.37), zabuni Na. PA/001/11/HQ/G/121 yenye kiasi cha Dola za kimarekani 711,139 (shilingi bilioni 1.138) na zabuni Na. PA/001/10/HQ/W/033 yenye kiasi cha Euro 1,172,741. Zabuni hizi zilitolewa kwa kampuni ya 'Infratech Ltd and Comfix & Engineering Ltd' na 'Total (T) Ltd'.

5.1.2 Manunuzi Yasiyoidhinishwa Kutokana na Mapungufu ya Mpango wa Manunuzi

Kifungu cha 45 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004, kinazitaka Taasisi za Umma kuandaa mpango wa manunuzi ambao (a) utaepusha manunuzi ya dharura; (b) utaweka pamoja mahitaji ya taasisi; (c) utaweka utaratibu maalum wa kuagiza bidhaa au huduma zinazohitajika mara kwa mara kwa makubaliano na watoa huduma husika.

Ukaguzi wangu katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ulibaini mapungufu katika uaandaaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka kwa baadhi ya taasisi. Hali hii ilisababisha kuwepo kwa manunuzi yasiyoidhinishwa na mamlaka husika katika baadhi ya Taasisi za Umma. Kwa mfano nilibaini kutotangazwa kwa mipango ya manunuzi kwenye tovuti na magazeti ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinyume na Kanuni ya 24 ya Tangazo la Serikali Na.98 ya Kanuni za Manunuzi za mwaka 2005. Kasoro hii ilibainika katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara na katika Kampuni ya Simu Tanzania ambapo menejimenti haikuandaa mpango madhubuti wa manunuzi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Katika ukaguzi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro nilibaini kuwa mpango wa manunuzi kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2013 haukuandaliwa vizuri kukidhi mahitaji ya mamlaka. Kwa mapungufu haya jumla ya zabuni tatu ambazo ni zabuni ya usafirishaji wa mahindi yenye thamani ya shilingi milioni 69.958; manunuzi ya programu za tehama yenye thamani ya Dola za

Kimarekani 12,300 na manunuzi ya huduma za kitaalamu juu ya uandaaji wa fomu za mradi wa Geopark yenye thamani ya Euro 15,000.

5.1.3 Kukosekana kwa Taarifa za Ukaguzi wa Bidhaa

Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 inaelekeza kuwepo kwa ukaguzi wa bidhaa zinazonunuliwa na taasisi za serikali. Matakwa haya ya sheria yamewekwa katika Kanuni ya 126 ya tangazo Na.97 la Kanuni za Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2005 ambayo inataka bidhaa zilizoagizwa kutopokelewa hadi pale ambapo mnunuzi atakaporidhika baada ya kuzikagua.

Mapitio ya nyaraka mbalimbali za manunuzi katika Mamlaka ya Bandari Tanzania yalibaini kuwepo kwa ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005 katika manunuzi ya magari 25 toka kampuni ya Toyota. Ukiukwaji huu ulitokana na manunuzi hayo kukosa ushahidi wa kuteuliwa kwa kamati ya ukaguzi na taarifa ya ukaguzi.

5.1.4 Kukosekana kwa Taarifa za Kila Mwezi za Manunuzi

Kifungu cha 35(o) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 kinataka Kitengo cha Manunuzi kuaandaa taarifa ya Manunuzi kwa kila mwezi na kuziwasilisha kwenye Bodi ya Zabuni ya taasisi husika. Ukaguzi niliufanya katika Mamlaka ya Bandari Tanzania, Chuo cha Elimu ya Biashara na nilibaini kuwa vitengo vya manunuzi vya mashirika haya havikuandaa taarifa za mwezi za manunuzi na kuzipeleka katika bodi zao za zabuni kwa utekelezaji. Pia Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ilichelewesha uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za manunuzi za kila mwezi kwa miezi nane bila sababu za msingi. Kutokuandaliwa au kucheleweshwa kwa taarifa hizi kunasababisha ucheleweshwaji katika kutekeleza na kusimamia shughuli mbali mbali za manunuzi katika mamlaka husika.

5.1.5 Kurefushwa kwa Muda katika Michakato wa Manunuzi

Kwa mujibu wa jedwali la tatu la Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2005 (Tangazo la Serikali Na.97) muda wa kuandaa mchakato wa manunuzi kwa zabuni zinazotangazwa ndani ya nchi ni siku 123 wakati zabuni za kimataifa zitatangazwa kwa siku 130.

Mapitio ya taarifa mbali mbali za manunuzi katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yamebaini kuwepo kwa ucheleweshwaji wa mchakato wa manunuzi kwa zaidi ya muda uliowekwa kisheria. Katika Mamlaka ya Bandari Tanzania nilibaini kuwa jumla ya zabuni 44 zilizopangwa kutekelezwa, mchakato wake ulichukua takribani miezi kumi na mbili (zaidi ya siku 490). Muda huu ni zaidi ya muda unaotakiwa na Kanuni za Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005 ambao ni miezi minne na nusu.

Hali kama hii pia ilijitokeza katika Shirika la Umeme Tanzania ambapo mchakato wa zabuni Na. PA/001/10/HQ/N/024 yenye thamani ya Dola za kimarekani milioni 1.226 (shilingi bilioni 1.8) ulichukua miezi ishirini na moja (21) na zabuni Na. PA/001/11/HQ/G/121 yenye thamani ya Dola za kimarekani 711,139 (shilingi bilioni 1.138) ulichukua muda wa miezi nane kukamilika.

5.1.6 Kugawanywa kwa Manunuzi Makubwa ili Kuruhusu Matumizi ya Nukuu za Bei (Quotations)

Kwa mujibu wa jedwali la pili la Kanuni za Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005 (Tangazo la Serikali Na.97) manunuzi kwa kutumia fomu za nukuu ya bei yamewekewa ukomo wa aina tatu. Kwa manunuzi ya bidhaa ukomo ni shilingi milioni 80, kwa shughuli ujenzi ni shilingi milioni 100 na kwa kazi zisizo za ushauri ni shilingi milioni 50.

Kadhalika, kifungu cha 59(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 kinaeleza kwamba taasisi yeyote ya umma itakayohusika na manunuzi ya bidhaa, ujenzi na kazi

zisizo za ushauri au huduma au mauzo ya mali za umma kwa zabuni lazima itumie njia ya ushindani.

Katika ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Bandari Tanzania nilibaini kuwa Mamlaka ilinunua bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 4.595 kwa kutumia mfumo wa kugawanya mahitaji katika mafungu madogo madogo ili kuruhusu matumizi ya nukuu za bei (Quotations). Mfumo huu ni kinyume na jedwali la pili la kanuni za manunuzi ya 2005 na kifungu Na.45 (d) cha sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2004.

- 5.1.7 Upungufu wa Watendaji Kwenye Vitengo vya Manunuzi**
Katika mapitio ya shughuli za vitengo vya manunuzi katika Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo nilibaini kwamba vitengo vya manunuzi vilikuwa na upungufu wa watendaji kinyume na sheria inavyoelekeza.

Kwa mujibu wa kifungu cha 34 (2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 kitengo cha manunuzi ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo kinapaswa kuwa na idadi inayotosheleza ya watumishi kulingana na ukubwa wa taasisi husika. Ukaguzi huu ulibaini kuwepo kwa idadi ndogo ya watendaji katika vitengo vya manunuzi katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Jiji la Dar Es Salaam na katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba.

- 5.1.8 Udhaifu Katika Usimamizi wa Mikataba**
Ukaguzi uliofanyika katika Shirika la Taifa la Madini kwa kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 ulibaini uwepo wa limbikizo la deni la jumla ya shilingi milioni 228.375 kutoka kampuni ya Tanmin Mining & Explore baada ya Kampuni hii kurejesha leseni yake ya utafutaji madini kwa Shirika la Madini chini ya makubaliano yaliyoingwa tarehe 30 Julai, 2010. Ukaguzi ulibaini kuwa kampuni hii haikubadilisha jina kwenye leseni iliyokuwa inamiliki kwenda kwenye jina la Shirika la Taifa la Madini kinyume na matakwa ya Sheria ya Madini Tanzania.

Ukaguzi huu pia ulibaini uwepo wa makubaliano kati ya serikali na Shirika la Madini ambapo Serikali iliahidi na kutoa Shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuwezesha uanzishwaji wa kituo cha kukopesha zana za uchimbaji madini kwa gharama nafuu katika mji wa Geita. Katika mkopo huu serikali kupitia wizara ya nishati na madini ilitoa shilingi milioni 140 kwa ajili ya kununulia zana za uchimbaji na shilingi milioni 60 kwa ajili ya uendeshaji wa kituo. Katika makubaliano haya Shirika lilitakiwa kulipa mkopo pamoja na riba ya asilimia 6 kwa mikupuo 54. Hadi kipindi cha kuandika ripoti hii Shirika halikuwa limenunua kifaa chochote na wala hakuna mrejesho wa mkopo uliofanywa kwa mkopeshaji (Serikali).

Katika ukaguzi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania nilibaini kuwa mamlaka iliingia mkataba na kampuni ya Canopies International Limited kujenga gati katika ziwa Nyasa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.579. Mkataba huu ulipangwa kumalizika baada ya miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuingiwa kwa mkataba huu tarehe 2 Augosti, 2012. Kufikia tarehe ya kuandika ripoti hii Machi, 2014 mkandarasi alikuwa hajakamilisha ujenzi. Pia nilibaini madhaifu katika kuusimamia mkataba huu ambapo mkandarasi alitakiwa kununua gari aina ya Pick Up na jenereta mpya kwa ajili ya kuhudumia mradi lakini hakufanya hivyo licha ya kulipwa fedha. Udhaifu wa usimamizi wa mkataba ulionekana pia katika mkataba wa ujenzi wa uzio wa bandari ndogo ya Kiwira uliogharimu shilingi milioni 418.132 chini ya kampuni ya ALUTECH ENGEENERS (E.A) LTD ilyoshindwa kukamilisha ujenzi huo kulingana na matakwa ya mkataba.

Kadhalika udhaifu ya usimamizi wa mikataba yalibainika katika mikataba iliyoingwiwa na watoa huduma mbalimbali na Bohari ya Dawa ambapo dawa zilizoagizwa hazikuweza kumfikia muagizaji kwa wakati. Katika ucheleweshwaji huu hakuna tozo zilizolipwa na wauzaji na hakukua na hatua zozote zilizochukuliwa na menejimenti. Pia hali kama hii ilijitokeza katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

ambapo menejimenti haikuweza kudai fidia kutoka kwa mkandarasi kutokana na kuchelewa kuleta bidhaa. Hii ni kinyume na kanuni namba 121, 122, na 123 ya tangazo la serikali namba 97 la Kanuni za Sheria ya Manunuzi za mwaka 2005.

Katika ukaguzi wa Shirika la Umeme Tanzania kituo cha Mara, nilibaini kuwa kulikuwa na mkataba wa ulinzi uliokuwa umeisha muda wake wenye thamani ya shilingi milioni 43.282 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani. Kampuni hiyo iliendelea kutoa huduma kwenye ofisi za shirika kabla ya kusaini mkataba mwingine kwa kipindi cha miezi nane kuanzia mwezi Juni, 2012 hadi Februari 2013.

Kadhalika nilibaini kuwa kuna mkandarasi aliyelipwa kiasi cha dola za kimarekani 1,711,939 ikiwa ni malipo ya fidia kwa kipindi ambacho alikaa bila kufanya kazi yeyote. Kampuni ya MGS International (T) Ltd ililipwa kiasi cha shilingi bilioni 1.638, vilevile shilingi bilioni 1.175 zililipwa kwa kampuni ya MPS Oil (T) Ltd kama fidia ya kuchukuliwa ardhi. Gharama hizi zililipwa kutokana na udhaifu wa menegimenti ya TANESCO kutofanya upembuzi yakinifu juu ya maeneo ambayo mradi ungepita.

Pia tuligundua kuwa mshauri wa mradi alizidisha gharama za ushauri kutoka kiasi cha Euro milioni 1.702 kufikia Euro milioni 2.551 sawa na ongezeko la Euro 848,910 bila idhini ya Bodi ya Zabuni. Hakukuwa na sababu iliyotolewa na menejimenti ya kutofanya uhakiki wa kina kabla ya kuanza kwa mradi.

Pia Shirika la umeme Tanzania lilifanya manunuzi ya dharura ya shilingi bilioni 10.115 kutoka kampuni ya East Africa Fossils kwa ajili ya kuleta lita 4,536,000 za mafuta ya dizeli ya mitambo ya kufua umeme ya Agreko iliyoko Tegeta na Ubungo. Menejimenti ya Shirika ilikuwa inajua kuwa mkataba kati yake na Agreko ulikuwa unaisha mwezi Octoba, 2012 na ingeweza kuanza mchakato wa manunuzi

mapema lakini haikufanya hivyo badala yake iliacha mkataba ukaisha muda na kufanya manunuzi ya dharura kinyume na kanuni za sheria ya manunuzi Na.42 ya mwaka 2005.

5.1.9 Udhhibiti wa Gharama katika Mchakato wa Manunuzi

Kifungu cha 58 (2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya Mwaka 2004 kinazitaka taasisi za umma na Serikali kufanya michakato ya manunuzi katika hali ambayo italeti tija, ufanisi, manufaa ya kiuchumi, uwazi na thamani ya fedha. Njia pekee ya kufikia matakwa haya ni kuhakikisha kuwa gharama za michakato ya manunuzi zinadhhibitiwa. Sheria hii inaelekeza kuwa ni wajibu wa watendaji wakuu wa taasisi za umma na Serikali kuhakikisha gharama hizi zinadhhibitiwa na pale ambapo gharama zitaonekana kuwa kubwa ofisa atakae husika awajibishwe.

Kadhalika, kwa mujibu wa kifungu cha 89 cha sheria ya manunuzi ya umma Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi ya Umma imepewa mamlaka kisheria kutoa miongozo ya mara kwa mara kusaidia utekelezaji wa sheria. Kwa kuzingatia mamlaka haya tarehe 7 Julai, 2007, Mamlaka ilitoa muongozo Na. PPRA/CPR/253/41 kwa taasisi za umma na Serikali kuhusiana na njia bora ya kudhibiti gharama za matumizi katika michakato ya manunuzi.

Wakati wa ukaguzi kwenye Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma nilibaini ukiukwaji wa sheria na miongozo inaelekeza udhibiti wa matumizi katika michakato ya manunuzi. Kasoro hizi zilizibainika katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambapo jumla ya shilingi milioni 268.731 zilitumika kama gharama kwenye mchakato wa manunuzi kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ukilinganisha na shilingi milioni 182.572 mwaka uliotangulia (2011/2012) ikiwa ni ongezeko la asilimia 47. Kwa wastani jumla ya shilingi milioni 7.678 zilitumika kama gharama kwenye zabuni moja.

5.1.10 Manunuzi ya Bidhaa Ambayo Hayakupitishwa na Bodi ya Zabuni

Kifungu cha 30 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004 kinaelekeza manunuzi yote kuidhinishwa na bodi ya zabuni. Hata hivyo, ilibainika kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo hazikuzingatia kifungu hiki.

Wakati wa ukaguzi wa hesabu za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Serikali Kuu nilibaini kwamba Mfuko uliingia mkataba na kampuni ya huduma za usafiri wa anga Antelope Tours and Travel Services Ltd bila mkataba na bila kuihusisha bodi ya zabuni. Pia Mfuko ulinunua mafuta ya magari kutoka kampuni ya International Co. Ltd na SUPCO na ukarabati wa magari toka makampuni ya Toyota Tanzania na PATEL Trading Company kwa garama ya shilingi milioni 128.854 bila kihusisha bodi ya zabuni. Hii ni kinyume na kifungu cha 30 (a)-(g) cha sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 na kinyume na Kanuni ya 80 (1)-(7) ya tangazo la serikali Na.97 ya mwaka 2005.

Hali kadhalika Bodi ya Kahawa Tanzania ilitumia jumla ya shilingi milioni 36.427 kukarabati banda la maonyesho ya nane nane Morogoro bila kuidhinishwa na bodi ya zabuni. Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro ilitumia jumla ya shilingi milioni 23.498 kufanya manunuzi bila kuidhinishwa na bodi ya zabuni. Ukaguzi huu pia ulibaini matumizi ya shilingi milioni 17.976 zilizotumika kwa ajili ya manunuzi mbalimbali na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara bila kuidhinishwa na bodi ya zabuni. Baadhi ya manunuzi Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya hayakupitishwa na bodi ya zabuni.

Vilevile mashirika yafuatayo yalifanya manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali bila ya kuidhinishwa na bodi za zabuni kinyume na kifungu cha 31 (2) cha Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 na Kanuni ya 54 (1) ya Kanuni za Sheria ya Manunuzi ya Umma tangazo la Serikali Na.97 ya mwaka 2005.

Benki ya Posta Tanzania (shilingi 75,252,000), Bodi ya Chai (shilingi 8,315,470) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (shilingi 2,033,526,382). Pia Shirika la Nyumba la Taifalilifanya manunuzi mengi ambayo hayakuidhinishwa na bodi ya zabuni.

5.1.11 Manunuzi ya Huduma Kutoka Kwa Watoa Huduma

Wasioidhinishwa katika Mamlaka ya Bandari Tanzania

Kifungu cha 46(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 kinasema kwamba, ili taasisi ya umma au serikali iweze kushiriki katika mchakato wa manunuzi kwa kutumia watoa huduma, wakandarasi na washauri ni lazima pawepo na vigezo vilivyopitishwa na bodi za zabuni. Kadhalika, kifungu cha 47 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 kinatoa nafasi kwa taasisi za umma na serikali kuchagua watoa huduma, wakandarasi na washauri kwa kuitisha zabuni na kuchambua ili kuweza kuwa na orodha ya makampuni ambayo yanaweza kutoa huduma pale inapohitajika.

Ukaguzi katika Mamlaka ya Bandari Tanzania ulibaini uwepo wa manunuzi ya bidhaa na huduma kutoka kwa watoa huduma ambao hawakua wameidhinishwa na mamlaka. Hii ilitokana na kuvunjwa kwa bodi teule ya zabuni katika bandari ya Dar es Salaam na shughuli zake kuhamishiwa makao makuu ya mamlaka ambapo manunuzi yalilazimika kufanyika kwa kutumia nukuu za bei. Katika uchambuzi wa manunuzi yaliyofanyika kwa njia hii nilibaini kuwa watoa huduma hawa hawakuwa kwenye orodha ya wale walioteuliwa na bodi ya zabuni ya mamlaka.

5.1.12 Manunuzi ya Bidhaa na Huduma bila Ushindani

Ukaguzi wa nyaraka mbali mbali za manunuzi katika shirika la CARMATEC ulibaini malipo ya shilingi milioni 121.181 zilizolipwa kwa kampuni ya 'Mngara General Enterprise' ya mkoani Tanga kwa kazi ya kusambaza vifaa kwenye mradi wa Wakala wa Umeme Vijijini mkoani Kigoma na Shinyanga. Zabuni hii haikutangazwa na hapakuwepo na njia yeyote ya ushindani iliyotumika kumpata mtoa huduma.

Ukaguzi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ulibaini kuwa shilingi bilioni 1.6 zilitumika kununulia bidhaa bila kutumia njia ya ushindani. Hali kadhalika kulikuwa na mazingira ya upendeleo katika kuwapata watoa huduma kwa kuweka vigezo ambavyo vinalenga kampuni husika tu. Udhaifu huu ulibainika katika zabuni ya kununua magari aina ya Ford Ranger kwa gharama ya shilingi milioni 63.537 na Land Rover Defender kwa shilingi milioni 209.447.

5.1.13 Udhaifu katika Utunzaji wa Nyaraka na Kumbukumbu za Manunuzi

Ukaguzi wa nyaraka mbalimbali za manunuzi ulibaini mapungufu katika kutunza nyaraka zilizotumika katika mchakato wa manunuzi kwenye baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

Katika kaguzi za Mashirika ya; Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira za miji ya Bukoba na Kahama, Bohari ya Dawa Tanzania na Shirika la Umeme Tanzania, hayana taratibu nzuri za kutunza nyaraka muhimu za manunuzi kinyume na matakwa ya Kanuni ya 19 (1) ya Kanuni za Sheria za Manunuzi na tangazo la serikali namba 97 la mwaka 2005.

5.1.14 Kukosekana kwa Mikataba na Nyaraka Muhimu Katika Manunuzi ya Bidhaa katika Mamlaka ya Bandari Tanzania

Ukaguzi ulibaini matumizi ya shilingi bilioni 2.805 zilizolipwa kwa kampuni ya PUMA Energy kutokana na mauzo ya mafuta ya petroli na dizeli. Katika mapitio ya nyaraka mbalimbali wakaguzi hawakupewa mkataba kati ya Mamlaka ya Bandari na PUMA Energy licha ya mkataba huo kuombwa. Pia kitengo cha manunuzi katika Bandari ya Dar es Salaam kilikuwa na nakala ya mkataba ambayo ni sehemu moja ya nane tu ya mkataba husika uliotiwa sahihi tarehe 18/1/2011 kwa muda wa miaka miwili.

Hali kadhalika ukaguzi huu ulibaini matumizi ya shilingi milioni 364.499 zilizolipwa kwa kampuni ya “Southern Engineering Co.” kwa ajili ya ukarabati wa boti ndogo ya kusukuma meli aina ya Elizabeth Luhigo na shilingi milioni 584.634 zilizolipwa kwa kampuni ya B.M.Benmar Marine LTD kwa ajili ya kukarabati maegesho ya meli na kituo cha kupakulia mafuta Kurasini. Mamlaka haikuweza kuonyesha mikataba ya malipo katika huduma hizi ambapo ni kinyume na sheria.

5.1.15 Manunuzi Yaliyofanyika Nje ya Mpango wa Manunuzi na Bajeti

Kanuni ya 46 (9) ya tangazo la Serikali Na.97 la Kanuni za sheria ya manunuzi ya umma za mwaka 2005 inazitaka taasisi za umma na serikali kufanya manunuzi yake pale tu ambapo manunuzi hayo yako ndani ya mpango wa manunuzi wa mwaka na ndani ya bajeti.

Ukaguzi wa manunuzi yaliyofanyika katika Shirika la Nyumba la Taifa ulibaini uwepo wa matumizi ya shilingi milioni 127.349 ambayo hayakuwa ndani ya mpango wa manunuzi na ndani ya bajeti ya mwaka 2012/2013. Mapungufu haya pia yalibainika katika ukaguzi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambapo shilingi bilioni 1.298 zilitumika nje ya mpango wa manunuzi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

5.1.16 Kuwepo kwa Baadhi ya Wajumbe wa Bodi ya Zabuni Waliomaliza Muda Wao Katika Shirika Hodhi la Mali za Serikali

Kifungu cha 3 (1) cha jedwali la pili katika sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2004 kinaelekeza kuwa mwenyekiti na wajumbe wa bodi za zabuni wanapaswa kuteuliwa kwa vipindi vya miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa miaka mitatu pale itakapoonekana inafaa.

Hata hivyo licha ya uwepo wa sheria hii, ukaguzi wa Shirika Hodhi la Mali za Umma ulibaini kuwa bodi ya zabuni ya shirika iliendelea kufanya kazi baada ya kuisha kwa muda wake kinyume na matakwa ya sheria.

5.1.17 Matangazo ya Fursa za Zabuni nje ya Utaratibu wa Sheria ya Manunuzi

Wakati wa mapitio ya utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005 nilibaini kwamba, baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo hazikutangaza fursa za zabuni katika magazeti na tovuti kama sheria inavyoelekeza. Katika ukaguzi wa hesabu za Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania zabuni hazikutangazwa ili kutoa mwanya kwa wazabuni kushindanishwa. Hii ni kinyume na kanuni ya 80(5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005. Hali kama hii ilijitokeza pia katika ukaguzi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara.

5.1.18 Utofauti wa Bei katika Mkataba na Bei katika Barua ya Kujulishwa Ushindi wa Zabuni

Ukaguzi wa nyaraka za manunuzi katika Shirika la Umeme Tanzania ulibaini kuwa barua ya kujulishwa ushindi wa zabuni kwa kampuni ya M/s SAFT AB LTD kwa ajili ya mauzo ya betri ya vituo vya kufua umeme ilikuwa inaonyesha bei ya Euro 176, 358. Hata hivyo bei iliyoonyeshwa kwenye mkataba ilikuwa ni Euro 210, 283. Menejimenti ya Shirika ilieleza kuwa bei ya kwenye mkataba ya Euro 210,283 ilitokana na kosa la uchapishaji ingawa ndio bei iliyotumika kulipa malipo ya awali kwa mkandarasi.

5.1.19 Malipo ya Gharama za Ziada Shilingi Bilioni 9.5 Yaliyotokana na Udhaifu katika Upembuzi Yakinifu

Ukaguzi wa usimamizi wa mikataba katika Shirika la Umeme Tanzania ulibaini kuwa Shirika lilipa gharama za ziada jumla ya shilingi bilioni 9.5 kwa kampuni za SEMCO Martine

AS na Rolls Royce Maritime AS. Malipo haya yalitokana na mapungufu ya menejimenti katika kufanya upembuzi yakinifu juu ya dosari za kimazingira katika mradi wa mafuta mazito. Hali hii ilipelekea kufanyika upya kwa utafiti ambao ulichelewesha mradi kwa miezi kumi na kuligarimu Shirika kiasi cha shilingi bilioni 9.5.

5.1.20 Manunuzi Yanayozidi Ukomo na Yasiyo na Ushindani - Shirika la Umeme Tanzania

(i) Jedwali la pili la Kanuni za Manunuzi ya Umma limebaiinisha njia mbalimbali za manunuzi kutegemeana na kiasi cha manunuzi kinachohusika. Kwa mfano kwa manunuzi ya njia ya 'restricted tendering' hayapaswi kuzidi kiasi cha shilingi milioni 200 vinginevyo manunuzi apate idhini cha Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi Tanzania (PPRA) kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 31(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma.

Hata hivyo, Ukaguzi wa zabuni Na. No.PA/001/10/HQ/N/024 iliyotolewa kwa kampuni ya Infratech Ltd na Comfix & Engineering Ltd wa gharama ya shilingi bilioni 1.8 (bila kodi) ulibaini kuwa shirika lilitumia njia ya 'restricted tendering'

(ii) Hali kadhalika, nilibaini uwepo wa utata katika vigezo vilivyotumika kupitisha zabuni tajwa hapo juu kwa mkandarasi Infratech Ltd and Comfix & Engineering Ltd kwa kile kilichoonekana kuwa bei yake ya shilingi bilioni 1.8 (bila kodi) sawa na shilingi bilioni 2.124 (pamoja na kodi) ilikuwa ndogo ukilinganisha na mshindani wake kampuni ya Techno brain shilingi bilioni 1.9 (pamoja na kodi).

(iii) Pia nilibaini kuwa Shirika liliingia mkataba kwa njia isiyo ya ushindani (single source) na kampuni ya Itron Measurement na Systems (Pty) Limited tarehe 31 Octoba, 2012 kuliuzia shirika vifaa aina ya Eclipse

Manager and EVG license kwa gharama ya shilingi bilioni 1.3. Manunuzi haya yalizidi kiwango cha manunuzi bila ushindani kama inavyoelekezwa kwenye jedwali la pili la kanuni za manunuzi ya umma ya mwaka 2005 yaani shilingi milioni 100. Kwa ukiukwaji huu wa sheria haikuweza kufahamika kama Shirika lilipata idhini kutoka Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ndani ya siku kumi na nne (14) kama inavyoainishwa kwenye kifungu cha 31(3) cha sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2004.

- (iv) Shirika la Umeme Tanzania katika zabuni Na. PA/001/11/HQ/G/092 iliyohusiana na usambazaji, ufungaji na kuweka katika hali ya matumizi jenereta mbili aina ya 90 MVA, 132/33 KV. Mkataba huu ulikuwa wa gharama ya shilingi milioni 238.663 na Dola za kimarekani milioni 4.570 kiwango ambacho ni zaidi ya kile kilichoidhinishwa katika sheria kwa njia ya zabuni maalumu yaani shilingi milioni 400.
- (v) Ukaguzi wa zabuni Na. PA/001/11/HQ/G/121 ulibaini kuwa Shirika liliingia katika mkataba usio na ushindani na kampuni ya Total Tanzania Limited tarehe 27 Agosti, 2012. Katika mkataba huu mkandarasi alikubali kuiletea mamlaka mafuta ya kulainishia mitambo aina ya CAPRANO SPECIAL 30 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.138. Mapitio ya kina katika mkataba huu yalibaini kuwa bei ya mkataba ilizidi kikomo elekezi kilichoko kwenye jedwali la pili la Kanuni za Manunuzi ya umma yaani shilingi milioni 500. Kadhalika hapakuwepo na mawasiliano kati ya Shirika na Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kuhusiana na manunuzi yaliyozidi kikomo.
- (vi) Mapitio ya zabuni Na. PA/001/10/HQ/W/033 yalibaini kuwa shirika lilitumia Euro milioni 1.173 kujenga kituo cha uendeshaji Pangani kwa kutumia

njia ya manunuzi ya uteuzi wa mzabuni maalumu (restricted tendering). Njia hii inamtaka mnunuzi wa umma kutoingia zabuni inayozidi shilingi bilioni 1.5

- (vii) Zabuni Na.PA/001/12/HQ/N/034 iliyohusu usafirishaji wa transfoma kumi na moja (11) kwenda mikoa ya Shinyanga na Dar es Salaam kwa kutumia njia ya zabuni maalumu haikuzingatia ukomo wa viwango vilivyoko kwenye sheria. Zabuni hii ilikuwa ya gharama ya shilingi milioni 256.710 ambapo ukomo wake ni shilingi milioni 200. Pia katika zabuni Na.PA/001/11/HQ/G/125 ya ununuzi wa transfoma mbili zenye thamani ya shilingi bilioni 7.880 (zabuni maalumu) ambayo ukomo wake ni shilingi milioni 400.

- 5.1.21 Udhaifu uliojitokeza katika Zabuni ya Kujenga “Optical Fibre Cable Free Span”- TANESCO
- Katika ukaguzi wa shirika la umeme nilibaini madhaifu katika zabuni Na. PA/001/11/HQ/W/023 iliyohusiana na ujenzi wa “Optical Fibre Cable Free Span”kati ya swichi na bwawa la maji ya kufulia umeme Kidatu. Kwa mara ya kwanza, ilishauriwa kwamba kampuni ya Supertech Limited ipewe zabuni hii kwa gharama ya shilingi milioni 148.481, lakini Katibu wa Bodi ya zabuni akaishauri bodi kuyaongeza pia makampuni ya Misiga Communications na Primetech Offices & School Solutions kwenye ushindani kwa sababu yalikuwa yameomba zabuni hiyo kwa bei ndogo kulinganishana na Supertech ltd. Ushauri huo ulikubaliwa na Bodi na kuagiza kupitia upya machakato wa zabuni hiyo. Zaidi, hatukupata ushahidi wowote kwamba mchakato wa zabuni hiyo ulirudiwa, badala yake kampuni ya Supertech Ltd ilishinda zabuni hiyo pamoja na kwamba makampuni ya Misiga Communications na Primetech Offices & School

Solutions ndiyo yaliyo kuwa na bei ndogo kuliko Supertech Limited.

- 5.1.22 **Manunuzi ya Dharura Ambayo Hayakupata Kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali**
Katika ukaguzi wangu wa zabuni Na. PA/001/12/HQ/N/027 juu ya kukarabati transifoma katika Shirika la Umeme Tanzania, ilibainika kuwa njia ya manunuzi iliyotumika haikuwa ya ushindani na haikupata kibali toka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Zabuni hii ilipewa kampuni ya M/s ABB Ltd kwa bei ya Shilingi 264,320,000 kama manunuzi ya dharura kinyume na kanuni ya 42 ya Kanuni za Sheria za Manunuzi za mwaka 2005.
- 5.1.23 **Matumizi Yasiyo Sahihi ya Njia ya Manunuzi ya zabuni Maalumu**
Shirika la Umeme Tanzania liliingia mkataba na kampuni ya "Usangu Logistics Tanzania Ltd" kusafirisha transifoma kumi kutoka ghala la shirika Kurasini kwenda vituo vidogo vya usambazaji umeme -Dar es salaam na transifoma moja kwenda mkoani Shinyanga kwa gharama ya shilingi milioni 256.710 na mkataba kutiwa sahihi tarehe 5 Agosti, 2012. Hata hivyo, iligundulika kwamba, utaratibu uliotumika kumpata mzabuni huyo ulikuwa ni kwa njia ya zabuni maalumu katika makubaliano ya kumalizika ndani ya siku saba (7). Vile vile ukaguzi ulibaini kuwa mzabuni wa kwanza kampuni ya SARAM ilitoa ofa ya shilingi milioni 10 na kukataliwa kwa kigezo kwamba haina uzoefu wa kusafirisha mizigo. Badala yake mkandarasi aliyetoa bei ya shilingi milioni 256.710 ndiye aliyeshinda bila maelezo ya ziada juu ya sababu zilizopelekea yeye kushinda zabuni hii kinyume na kanuni ya 67 ya kanuni za sheria ya manunuzi za mwaka 2005.

5.1.24 Utata Katika Manunuzi ya Transifoma 2 Kwa Gharama ya Shilingi Bilioni 7.879

Shirika la Umeme lalinunua transifoma mbili kwa gharama ya shilingi bilioni 7.879 kwa kushindanisha wazabuni 12 kwa njia ya zabuni maalumu. Baada ya zoezi la awali la kuwapendekeza washindani kumalizika na kamati kuwasilisha ripoti yake, Kaimu Mkurugenzi wa Usambazaji aliongeza jina la kampuni ambayo haikuwa kwenye orodha ya awali. Kampuni hii ni Shandong Taikai Power Engineering, na ndiyo kampuni ambayo ilipitishwa na bodi ya zabuni ya shirika kuwa mshindi wa zabuni hii. Ukaguzi huu haukuweza kupata sababu za kisheria zilizopelekea bodi ya zabuni kupitisha jina la ziada la kampuni ambayo haikuwa miongoni mwa kampuni zilizopitishwa kipindi mchakato ulipokuwa unaanza.

Mapitio ya taarifa ya tathmini yalionyesha kwamba kampuni ya Shandong Taikai Power Engineering haikuwa na sifa za kutosha kupewa kazi kwa kuwa haikuwa na uwezo kitaalamu na pia kifedha. Hata hivyo Bodi ya Zabuni ilipitisha kuwa kampuni hii ipewe kazi baada ya kutathiminiwa upya tarehe 14 Februari, 2012 kwa makubaliano kwamba maofisa wa shirika watatembea makao makuu ya kampuni nchini China kujiridhisha na utendaji kazi wake. Hata hivyo tarehe 24 Februari, 2012 kabla ya safari ya kuelekea China kuanza Shirika lilipitisha uamuzi wa kuipa kazi kampuni hii bila kuzingatia maamuzi ya awali ya kuifahamu zaidi utendaji kazi wake. Tarehe rasmi ya safari ya China ilikuwa 5/3/2012. Matokeo yake baada ya miezi miwili kabla ya mkataba kuisha muda

wake kampuni ililiandikia shirika barua ya kutaka kubadilisha aina ya malighafi ambayo ingetumika kutengenezea transifoma kwa mujibu wa mkataba. Hali hii ilipelekea ongezeko la kazi na bei kwa jumla ya shilingi bilioni 3.707 bila maelezo ya ziada juu ya ongezeko hili ambalo kimsingi halikuwa na faida yeyote kwa shirika. Makubaliano ya ya ongezeko hili yalifanyika tarehe Aprili, 2013.

SURA YA SITA

USIMAMIZI WA MALI ZA UMMA

6.0 Utangulizi

Rasilimali ni mali zinazomilikiwa na Taasisi au Shirika kwa ajili ya matumizi yake ya kila siku katika kuendesha shughuli zake. Rasilimali zinajumuisha mali zinazoshikika na zisizoshikika ambazo taasisi inazimiliki. Mali hizo ni kama mitambo, vifaa mbalimbali, uwekezaji, fedha taslimu, madeni yanayodaiwa, akiba ya vifaa, mifumo ya ndani ya kompyuta, tovuti na malipo ya awali.

Sura hii ni muhimu kwa sababu ya changamoto zinazoyakabili Mashirika ya Umma katika kufuatilia na kusimamia rasilimali za Taifa. Pia, pamoja na changamoto hizo, hili ni eneo ambalo kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na watumishi ambao siyo waaminifu wanaoweza kufanya ubadhirifu wa mali za umma. Kwa mwaka huu wa ukaguzi, nimeainisha masuala ambayo ni muhimu kwa Serikali na Bunge kuyatolea maelekezo ya namna nzuri ya kuyatekeleza kama ifuatavyo:

6.1 Matumizi Yasiyo Sahihi ya Rasilimali za Bodi ya Pamba na Mamlaka ya Usimamizi wa Nishati na Maji

Bodi ya Pamba Tanzania (TCB) ina jengo (Pamba House) lenye ghorofa sita (6) lililoko kwenye kitalu namba 21 barabara ya Pamba, Dar es Salaam. Wakati wa ukaguzi ilibainika kwamba ni ghorofa nne (4) tu zinazotumika. Ghorofa ya nne (4) na tano (5) hazitumiki kwa zaidi ya miaka mitano (5) kutokana na kuvuja hasa wakati wa mvua. Kutotumika kwa ghorofa hizo, kumesababisha Bodi kupoteza mapato yapatayo Dola za Kimarekani 155,000 kwa mwaka sawa na Dola za kimarekani 775,000 kwa miaka mitano ambayo ghorofa hizo mbili zimekuwa wazi. Vilevile, Bodi ya Pamba ilionyesha kwenye hesabu zake mapato ya shilingi bilioni 1.689 yatokanayo na kodi ya pango la nyumba badala ya shilingi bilioni 1.796 ambazo ndizo

zilizotakiwa kuonyeshwa. Makosa hayo yalisababisha Bodi kuonyesha upungufu wa mapato ya shilingi milioni 106.9 kwenye vitabu vyake. Upotoshaji huu huenda ukawa ni wa makusudi ili kuficha uwezekano wa matumizi ya fedha visivyo.

Vile vile, Mamlaka ya Usimamizi wa Nishati na Maji (EWURA) walipewa kiwanja na Wizara kwa ajili ya kujenga jengo lao. Lakini ujenzi wake haujaanza, na bado Mamlaka imepanga kwenye jengo la Harbour View Towers kwa shilingi bilioni 1.2 kwa mwaka 2012/13 ikiwa ni ongezeko la shilingi milioni 100 ukilinganisha na kodi ya pango la mwaka 2011/2012. Bila Mamlaka kujenga jengo lake, itaendelea kulipa pango kwa ajili ya ofisi, gharama ambazo zingeweza kuepukika.

6.2 Mapungufu Kwenye Usimamizi wa Fedha

Fedha ni kile kiasi ambacho taasisi inakimiliki kama taslimu au kilichohifadhiwa benki na kinachozunguka kwenye shughuli za kawaida za taasisi, ambacho ni rahisi sana kuibiwa kuliko rasilimali zingine.

Kuzuia na kugundua wizi/matumizi yasiyo sahihi ya fedha za umma kunahitaji usimamizi sahihi unaohusisha kuweka mifumo ya usimamizi wa ndani ya taasisi inayogusa maeneo yote husika. Maeneo ambayo ni lazima yazingatiwe ni pamoja na ukusanyaji, na usimamizi wa matumizi ya fedha hususani ya fedha taslimu. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka wa fedha 2012/2013, niligundua mapungufu mbalimbali ambayo kama yasiporekebishwa yatasababisha matumizi yasiyo sahihi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na wizi.

Kwa mfano, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea, ilipata hasara ya shilingi milioni 314 kwa mwaka wa fedha 2012/13 kwa sababu zinazodhaniwa kuwa ni ubadhirifu uliofanywa na baadhi ya wafanyakazi wa Mamlaka. Ubadhirifu huo ulichelewa kugundulika kutokana

na ucheleweshwaji wa usuluhishi wa hesabu ambao ulikuwa haufanyiki kwa wakati.

Vilevile iligundulika kwamba, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ilipata upotevu wa fedha zipatazo shilingi milioni 652.650 Upotevu huu wa fedha ulifanywa na Mhasibu mwandamizi kwa kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Kwenye akaunti ya rasilimali zilizofutwa ya Benki ya Posta Tanzania, kulikuwa na kiasi cha shilingi milioni 105.701 zilizotokana na wizi kwenye “Western Union”. Pamoja na kwamba wizi wa fedha za Western Union umepungua toka shilingi milioni 510 kwa mwaka 2010 mpaka kiasi cha shilingi milioni 105 kwa mwaka 2012/13, tatizo bado lipo ambalo linaashiria kwamba mifumo ya ndani ya benki sio madhubuti kuweza kudhibiti ubadhirifu.

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara, ilikuwa haitayarishi usuluhishi wa Hesabu wa akaunti yake ya NBC. Akaunti zingine, zilikuwa na baadhi ya vitu vilivyo shindikana kusuluhishwa na ilikuwa haiwezekani kuvifuatilia.

Usuluhishi wa hesabu wa akaunti namba 01J1082678700 ya Chuo cha Mipango Dodoma, ilionyesha kwamba kulikuwa na makusanyo ya maduhuli ya kiasi cha shilingi milioni 9.6 ambazo hazikuwa zikionekana kwenye taarifa ya benki ya akaunti hiyo. Kulikuwa na kiasi kingine kipatacho shilingi milioni 21 kwenye akaunti namba 01J1082678700 ambacho kilikuwa hakionekani kwenye kitabu cha kumbukumbu za hesabu (cash book) cha chuo hicho. Usuluhishi wa hesabu wa akaunti za miradi ya Chololo na NICHE ulikuwa haufanyiki kila mwezi. Akaunti ya NICHE ilionyesha kuwa kulikuwa na makosa ya kihesabu ya mara kwa mara na makosa hayo hayakuwa yakirekebishwa kwa haraka.

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Tanga ilikuwa na hundi ambazo zilikuwa hazijalipwa benki kwa muda mrefu bila ufuatiliaji wowote kufanyika.

Baraza la Wafugaji Ngorongoro lilikuwa na kiasi cha shilingi milioni 90 zikiwa zimekaa benki kwa zaidi ya mwaka mmoja. Fedha hizi zilitokana na mauzo ya hisa ambazo baraza lilikuwa linamiliki kwenye hoteli ya Rhino. Kama fedha hizi zingewekezwa kwenye akaunti ya muda maalum, zingeweza kuwa zinazalisha faida isiyopungua shilingi milioni 7.2 (8%) kwa mwaka.

6.3 Msaada wa Dola za Kimarekani 300,000 Kutoka Jamhuri ya watu wa China Haukuwa Kwenye Vitabu vya Bodi ya Maktaba ya Taifa

Kwa mujibu wa dondoo za kikao cha uongozi wa Maktaba cha tarehe 06/11/2012, Maktaba ilipokea msaada wa fedha wa Dola za Kimarekani 300,000 tarehe 24 Septemba, 2012. Msaada ulijumuisha vitabu 1000, kompyuta na samani 20. Hata hivyo, kiasi hicho cha fedha hakikuonyeshwa kwenye vitabu vya hesabu za Maktaba, hivyo kushusha kiasi cha rasilimali kwenye vitabu vya Maktaba kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 300,000.

6.4 Wadaiwa wa Muda Mrefu

Madeni ya kibiashara ni fedha ambazo shirika au taasisi linamdai mtu binafsi, shirika au taasisi nyingine kutokana na mauzo ya bidhaa au huduma iliyotolewa na kutumika kabla ya malipo kufanyika. Kwa kawaida, wastani wa kipindi cha ukusanyaji wa madeni ni muda usiozidi mwaka mmoja ili kuepuka kushikilia rasilimali za shirika. Kwenye mizania ya hesabu, madeni ya kibiashara huwekwa upande wa rasilimali kwa sababu huonyesha kiasi cha fedha kitakachopokelewa kwa kipindi kifupi kijacho.

Tofauti na madeni ya kibiashara, taasisi au shirika laweza kufanya malipo kwenda kwa mtu binafsi, taasisi au shirika lingine kwa ajili ya kupatiwa huduma au bidhaa. Wakati

ambapo bidhaa au huduma hiyo itakuwa haijafika, shirika au taasisi iliyolipa huweka kumbukumbu za fedha hizo kama malipo ya awali. Kama ilivyo kwa madeni ya kibiashara, kwenye mizania ya hesabu kiasi hicho huwekwa upande wa rasilimali za taasisi. Baada ya kupitia hesabu za mashirika mbalimbali, iligundulika kuwa kuna madeni ya kibiashara na malipo ya awali ambayo yalikuwa yamekaa kwa muda mrefu sana bila kulipwa au bila ya huduma/bidhaa husika kutolewa.

Kwa mfano, baada ya kupitia hesabu za Taasisi ya Bahari Dar es salaam (DMI) iligundulika kuwa Dola za Kimarekani 76,000 zililipwa kama malipo ya awali kwenda Chuo Kikuu cha Dalian Maritime cha China kwa ajili ya kununua “Simulator”. Jumla ya bei ya simulator hiyo ilikuwa ni Dola za Kimarekani 360,000. Mkatoba wa manunuzi hayo ulikuwa unanza Juni, 2009 na kumalizika mwishoni mwa 2010 baada ya kiasi kilichobaki kuwa kimelipwa. Hata hivyo, DMI imeshindwa kulipa kiasi kilichobaki na badala yake huenda ikapoteza malipo ya awali ya Dola za Kimarekani 76,000 yaliyokwishafanyika.

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza, ilikuwa na madai ya muda mrefu ya shilingi bilioni 3.5 hadi tarehe 30 Juni, 2013 yakiwa yamepitisha muda wake kwa zaidi ya miaka mitatu. Kiasi cha madai kwa mujibu wa mfumo wa kompyuta wa madai “Billing System” kilikuwa hakilingani na kiasi kilichokuwa kwenye hasabu za Mamlaka zilizokuwa zimetengenezwa na mfumo mwingine wa kompyuta wa kutengeneza hesabu wa Pastel. Tofauti hiyo ilikuwa ni ya kiasi cha shilingi milioni 41.157. Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Kahama ilikuwa na madai ya shilingi milioni 510.469 ya zaidi ya miaka mitatu wakati shilingi milioni 478.850 yalitokana na mauzo ya maji.

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara (MTUWASA) ilikuwa na madai ya muda mfupi ya jumla ya shilingi milioni 409.617 yaliyotokana na mauzo ya maji. Vile

vile, uongozi wa Mamlaka hiyo ulikuwa umetenga kiasi cha shilingi milioni 108.461 kama madai tengefu, kikiwa ni kiasi chote cha miaka mitano ambacho mamlaka ilikuwa ikidai toka kwa wadaiwa mbali mbali, wengi wakiwa ni wadaiwa wa maji. Hata hivyo, hakuna utaratibu/sera inayotoa mwongozo wa kuandaa tengu kwenye madai. Hivyo basi, maamuzi haya yalifanywa bila kuwa na mwongozo wowote.

Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Songea ilikuwa na madai ya kiasi cha shilingi bilioni 1.028. Madai ya muda mfupi ya Mfuko wa Uwekezaji Tanzania (UTT) yalikuwa ni shilingi milioni 654.392 kiasi ambacho ni kikubwa ukilinganishwa na riba ya shilingi milioni 44.740 iliyotokana na mfuko wa kukopesha wafanyakazi.

6.5 Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW), Chuo cha Mipango Dodoma na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) zilishindwa kutumia Mifumo ya Kompyuta kwa ajili ya Uhasibu

Mifumo ya kielektroniki ya kiasibu ni aina ya mifumo inayotumiwa na wanataaluma wa uhasibu kusimamia na kuendesha shughuli mbalimbali za kiuhasibu. Mifumo hii hutumika kwenye nyanja mbalimbali za uhasibu kama kusimamia madeni, mishahara na kadhalika. Mifumo hii ni bora na hupendelewa na wanataaluma kwa sababu huendesha shughuli za kiuhasibu kwa usahihi na kasi ya hali ya juu na hupunguza gharama za uendeshaji.

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa, Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW) kilinunua mfumo wa kielektroniki ya kiasibu ujulikanao kama Pastel na mkataba wake kwa ajili ya ununuzi, uwekaji na kuendesha mfumo huo ulisainiwa tarehe 30 Septemba, 2011 na tarehe rasmi ya kuanza utekelezaji wa mkataba huo ilikuwa tarehe 1 Octoba, 2011 na kumalizika tarehe 31 Desemba, 2011. Wakati wa ukaguzi wa hesabu za chuo hicho ilikuwa yapata miaka miwili imepita na bado Chuo kilikuwa kinatumia mfumo wa uhasibu usio wa kielektroniki pamoja na kwamba mzabuni

analipwa fedha kila mwezi kwa ajili ya ukarabati na usimamizi wa mfumo huo. Iligunduliwa vilevile kwamba, Mamlaka ya Bandari Tanzania ina mfumo wa uhasibu wa kielektroniki (COBOL) ambao umepitwa na wakati, hivyo Mamlaka inaendelea kutumia mfumo usio wa kielektroniki hadi sasa. Mamlaka ilingia kwenye mkataba na Soft Tech Consultants tarehe 14 Julai, 2010 wa shilingi milioni 694.143 kwa kipindi cha miezi mitano (5) kwa ajili ya kuweka, kufundisha na kukabidhi mfumo wa kielektroniki wa pamoja unaojumuisha mifumo midogo midogo kama ya mishahara, usimamizi wa rasilimali watu, uhasibu na mifumo ya ghalani. Hata hivyo mpaka wakati wa kufanya ukaguzi wa Mamlaka, mifumo hiyo ilikuwa haijaunganishwa pamoja na ukweli kwamba mkandarasi alishalipwa fedha yote. Chuo cha Mipango Dodoma kilinunua na kuweka Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ujulikanao kama Vote Book tangu mwaka 2009. Mfumo huu ulikuwa ni kwa ajili ya kutumia kwenye mifumo midogo midogo kama, kukusanya takwimu za kifedha, kuzichanganua na hatimae kutoa ripoti. Lakini mpaka muda wa kumaliza ukaguzi, chuo bado kiliendelea kutumia mifumo isiyo ya kielektroniki.

6.6 Mita za Kupima Mafuta Zilizotelekezwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania

Vifaa vya kupimia mafuta bandarini 'flow meters' hutumika kupima shehena za mafuta zinazoingia nchini hivyo basi hupima mafuta yenye ujazo mkubwa kwa muda mfupi.

Mamlaka ya Bandari Tanzania ilinunua mita nane kwa ajili ya kudhibiti upimaji wa shehena za mafuta yanayoingia nchini kwa kiasi cha shilingi bilioni 2.458 kutoka kwenye kampuni ijulikanayo kama FMC Energy System. Mita hizo ziliwekwa tayari kwa matumizi kwenye bandari za Tanga na Dar es Salaam kwa ajili ya kusaidia kudhibiti mapato yanayopotea kutokana na kutokuwa na vifaa vizuri vya kupimia shehena za mafuta zinazoingia nchini. Vifaa hivyo vilinunuliwa na kuwekwa kwenye bandari hizo baada ya serikali kuagiza ununuzi wake kwa ajili ya kupata vipimo

sahihi na hatimaye kutoza kiwango sahihi cha kodi. Hata hivyo, vifaa hivi vimetelekezwa kwa miaka kadhaa sasa. Sababu iliyotolewa na Kamishina wa vipimo ni kwamba vifaa hivyo havikidhi viwango vinavyotakiwa. Pamoja na kwamba kamishina wa vipimo ndiye aliyeidhinisha ununuzi wa vifaa hivyo, baadae aliidhinisha utumikaji wa vifaa hivyo kwa barua yenye kumbu kumbu.Na.HB.111/597/01/111 ya tarehe 27 Disemba, 2004. Vilevile, barua hiyo iliainisha mapungufu kadhaa ambayo baadaye yalishindikana kupatiwa ufumbuzi. Baada ya matatizo hayo kushindikana, Mamlaka ikaamua kuendelea kutumia njia zisizo za kielektroniki kwenye kupima shehena za mafuta yanayo ingia nchini. Kitendo hicho kina athari kwa mapato ya Mamlaka ya Mapato katika uhakiki wa usahihi wa kiasi cha kodi kinacholipwa kutokana na upimaji wa shehena hizo za mafuta bila ya kutumia vifaa stahiki na athari katika uendeshaji wa shughuli za Mamlaka ya Bandari Tanzania.

6.7 Kukosekana kwa Uthibitisho wa Malipo Yaliyofanywa na Shirika Hodhi la Raslimali za Umma (CHC) na Bohari ya Dawa

Shirika Hodhi la Rasilimali za Umma (CHC) lilipata fedha kiasi cha shilingi bilioni 1.824 kutoka Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuilipa kampuni ya Alexander Forbes (Mtaalamu/Mshauri wa Bima) kwa niaba ya Shirika la Ndege la Tanzania. Wakati wa kupitia malipo kwenda kwa Forbes, ilibainika kuwa mchakato wa manunuzi wa kumpata mtaalamu huyo haukufuatwa. Vile vile hakukuwa na ushahidi kama shirika la ndege lilipata huduma hii ambayo kiasi hicho cha fedha kililipwa kwa ajili yake. Hii inamaanisha kwamba, udhibiti wa mfumo wa manunuzi na ulipaji si thabiti na unaweza kuwa na mianya mingi inayoweza kusababisha ubadhirifu wa fedha za Umma.

Wakati wa ukaguzi wa Bohari ya Dawa (MSD), kulikuwa na matumizi yapatayo shilingi milioni 55.398 ambayo

hayakuwa na vielelezo vinavyojitosheleza. Hivyo basi hatukujiridhisha kama malipo hayo yalifanyika na iwapo bidhaa au huduma zilizolipiwa zililetwa au la.

6.8 MUCE Kushindwa Kuhakiki Dhamana ya Benki ya Shilingi Milioni 362.351

Chuo kikuu cha Ualimu cha Mkwawa kiliingia mkataba na mkandarasi 'MNM Engineering Services Limited' kujenga jengo la maktaba na madarasa ya kusomea chuoni hapo kwa makubaliano yaliyohitaji mkandarasi kuwasilisha dhamana ya benki ya shilingi milioni 362.351 itakayolipwa kwa chuo iwapo mkandarasi atashindwa kukamilisha ujenzi huo kwa sababu mbalimbali. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba, dhamana Na 2010/100 iliyowasilishwa na mkandarasi ikisemakana kutolewa na Benki ya KCB haikua halisi na Benki ilikana kuitambua. Hali hii imekiweka chuo katika hatari ya kupata hasara ya shilingi milioni 362.651 hasa baada ya mkandarasi huyo kushindwa kuendelea na ujenzi.

6.9 Kushindwa Kuunganishwa kwa Mifumo ya Kompyuta Inayohusiana

Uendeshaji wa biashara wa kisasa duniani unahitaji mifumo mbalimbali ya taarifa iloyopo katika Mashirika na Taasisi, kama mifumo ya uhasibu, manunuzi, rasilimali watu na mifumo mengine ya taarifa kuunganishwa ili iweze kufanya kazi kwa pamoja ili kuongeza tija, ufanisi na usahihi kwa muda mfupi.

Hata hivyo, ilibainika kuwa baadhi ya Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma zina mifumo mbalimbali ya kompyuta inayohusiana lakini haijaungwanishwa. Hali hii inasababisha uunganishwaji wa taarifa kutoka mfumo mmoja kwenda mwingine kufanyika kwa njia isiyo ya kompyuta. Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma yaliyobainika kutoungwanishwa kwa mifumo yake ni kama; Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro (Mishahara, bili na Uhasibu), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira

Mwanza (Mfumo wa kubili na uhasibu), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara (Usimamizi wa taarifa na uhasibu), Chuo cha Ustawi wa Jamii (udahili, Usajili na Mitihani), Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (Mishahara, Usimamizi wa Taarifa na Uhasibu).

6.10 Idadi Kubwa ya Watu Wasiopata Maji Safi Katika Mji wa Bukoba

Moja wapo ya madhumuni ya kuanzisha Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba ni kuhakikisha uwepo wa maji safi kufikia eneo la mji wa bukoba lenye kilometa za mraba 55. Hata hivyo ni eneo la kilometa 25 tu za mraba zilizofikiwa na huduma ya maji safi na salama ambayo ni sawa na asilimia 45.4 ya wakazi wote.

Wananchi wanaohitaji huduma ya maji kutoka kwa Mamlaka ni 128,796 ambapo kati yao ni 73,280 tu wanaopata maji safi na salama, na kuacha watu 55,096 bila huduma ya maji safi na salama, ambao ni sawa na asilimia 43.2. Hali hii inaashiria kuwa Mamlaka haitumii fursa ya mahitaji ya maji kuongeza miundombinu ili kujiongezea mapato yake. Kwa mantiki hiyo, Mamlaka imeshindwa kufikia utekelezaji wa majukumu yake.

6.11 Upotevu wa Maji Unaopelekea Upungufu wa Mapato Unazozikabili Mamlaka za Maji Safi na Mazingira za Bukoba na Mbeya

Kwa kawaida kiasi cha Maji yanayozalishwa kwa ajili ya kusambazwa hutofautiana na kiasi cha maji yanayosambazwa. Baadhi ya maji hupotelea njiani, na hivo kuziongezea mamlaka za maji gharama zaidi, na kuzikosesha mapato. Maji haya hupotea kwa namna tofauti kama vile kujiunganishia isivyo halali, uharibifu wa mita, kuvuja kwa mabomba na uharibifu wa miundo mbinu ya maji.

Mapitio ya ripoti za ukaguzi yanaonyesha kuwa, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba ilizalisha kiasi cha

mita za ujazo 3,146,937 za maji ambapo kati ya hizo mita za ujazo 1,365,996 ndizo wateja wake walidaiwa sawa na asilimia 43.3 wakati maji yaliyopotea yalikuwa ni mita za ujazo 1,780,941 sawa na asilimia 56.6.

Pia, kwa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya ilionekana kuwa upotevu wa maji uliongezeka kwa kipindi cha miaka minne mfululizo, yaani, 31.2% (2009/2010), 31.4% (2010/2011), 34.5% (2011/2012) and 35.16% kwa mwaka 2012/2013. Hii inaonesha kuwa hakuna uboreshaji wowote unaofanyika kupunguza upotevu wa maji. Kiwango kinachoruhusiwa kupotea kama ilivyoainishwa katika mkataba kati ya Mamlaka na Wizara ya Maji ni 20%. Mamlaka ilijiwekea malengo ya kuruhusu 29% ambayo hata hivyo wameshindwa kuyafikia. Upotevu wa maji unasababisha upotevu wa mapato kwa Mamlaka.

6.12 Kutokuwepo kwa Mkataba wa Kugharamia Ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Afya

Ukaguzi ulibaini kuwa, katika ujenzi wa kituo cha afya unaondelea Chuo Kikuu Dodoma hapakuwa na mkataba halali kwa fedha zilizotolewa na mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2013 kiasi cha shilingi bilioni 29.539 zilikwishalipwa kwa mkandarasi bila kuwepo kwa mkataba. Pia, imebainika kuwa, mshauri wa ujenzi wa awamu ya pili (Hospitali ya Mafunzo) katika chuo kikuu cha Dodoma tayari ameshapatikana kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.671. Ubunifu wa majengo hayo unaendelea na pia michoro ya majengo iko tayari na inasubiri kuthibitishwa. Kukosekana kwa mkataba kunasababisha kukosekana kwa ufafanuzi wa mambo mbalimbali kama vile haki na wajibu wa kila upande katika mkataba huo, namna marejesho yatakavyokuwa yanafanyika na pia mfuko uko katika hatari ya kupoteza fedha nyingi iwapo litatokea tatizo la kisheria.

- 6.13 Kuvunjwa kwa Makubaliano ya Uwiano wa Umiliki wa Hisa Kufuatia magawio mbalimbali ya hisa za ziada kwa Serikali ya Tanzania, Umiliki wa hisa wa benki ya posta kufikia tarehe 31 disemba, 2012 ulikua ni uwiano wa 80.4:4.1:11.8:3.7 kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Shirika la Posta Tanzania na Chama cha kuwekaa na kukopa cha TP&TC.

Hata hivyo, sheria ya Benki ya Posta Tanzania ya mwaka 1991 inaelekeza kuwa umiliki wa hisa uwe kwa uwiano wa 41:10:30:39 kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Benki ya Posta Tanzania na ushirika wa TP&TC. Hali hii inaweza kuleta matatizo ya kisheria wakati wa ugawanywaji wa gawio la faida.

- 6.14 Kutokuwapo kwa Usimamizi Sahihi wa Mali Zilizokodiwa

- 6.14.1 Gharama kutoka kwa M/s TANCOAL Energy Limited

Mamlaka ya Bandari Tanzania inamiliki majengo mbalimbali ambayo inayakodisha na kuyafanya kuwa chanzo cha mapato. Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka iliingia mkataba na TANCOAL Energy Limited tarehe 15, Agosti 2012 wakati huduma za kutumia ardhi na huduma za Mamlaka zilianza tarehe 1 Oktoba, 2011. Makubaliano yalikuwa ni kukodisha eneo la mita za mraba 13,000 kwa kiwango cha dola za kimarekani 0.3 kwa mita ya mraba katika bandari ya Kiwira na mita za mraba 20,000 kwa kiwango cha dola za kimarekani 0.2 kwa mita ya mraba katika bandari ya Ndumbi. Kodi hiyo ilipaswa kulipwa katika kila robo mwaka. Hata hivyo, mpangaji (TANCOAL Energy Limited) ameshindwa kulipa limbikizo la kodi yote unaofikia kiasi cha shilingi milioni 225.743. Mpaka kufikia Agosti, 2013 mpangaji ameweza kupunguza deni lake kufikia shilingi milioni 105.412. Ingawa kulikuwepo na uchelewashwaji huo, Mamlaka ilishindwa kumshtaki mpangaji huyo kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 7.1.1 cha makubaliano.

Pia hakukuwa na bima kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 3.3.1 cha mkataba.

Zaidi ya hapo, nilibaini kuwa kuna wapangaji watano (5) wa Mamlaka ya Bandari (Kigoma) ambao wamepanga vyumba kutoka Julai, 2012 na Januari 2013 bila kuwa na mikataba. Kati ya hao ukiacha Ms. NCCC hawakua wakilipa kodi ya pango kabisa ambao ni ANOR, CARTEEN, FULGO and ABS MARY. Pia nilibaini hakukua na ankara zilizopelekwa kwa wapangaji, wala hapakuwepo na daftari la usajili wa wapangaji.

6.14.2 Kodi ya Upangaji ambayo Haijalipwa Kwa Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)

Kampuni ya Simu Tanzania ina majengo yake ambayo inayapangisha kwa wizara, taasisi za serikali na makampuni mengine binafsi ambayo kwa mujibu wa mkataba yanatakiwa kulipa kabla ya muda. Hata hivyo baadhi ya wapangaji hawajalipia kodi ya pango kwa zaidi ya mwaka mmoja. Kwa mfano mpaka mwisho wa mwaka wa ukaguzi, Makampuni yafuatayo hayakuwa yamelipa madeni yao; Airtel (shilingi milioni 687.631), Wizara ya Afya (shilioni milioni 419.394), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (shilingi milioni 267.187), Universal Communications (Sh. 216,966,831), Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi (shilingi milioni 213.125) na e-government (shilingi 211.359). Kutokukusanywa kwa kodi hii kunasababisha Kampuni ya Simu kukosa fedha za kujiendesha na kuendeleza miradi ya maendeleo.

6.15 Ukosefu wa Umiliki Halali wa Mali

Umiliki wa mali zisizohamishika unamaanisha umiliki wa kisheria unaohibitishwa na hati miliki au nyaraka nyingine zinazoweza kuthibitishwa kisheria. Kinyume cha hapo shirika au taasisi haina itakuwa katika hatari ya kukosa uhalali wa kisheria juu ya mali inayomiliki endapo kutakuwa na madai ya umiliki na mtu mwingine. Uhakiki wa mitambo, vifaa na majengo yanayomilikiwa na Mashirika na

Taasisi Nyinginezo za Umma ulibainisha kuwa mali nyingi hazikuwa na uthibitisho wa umiliki wa kisheria. Matokeo ya kutokuwa na umiliki halali kunafanya mkaguzi ashindwe kuthibitisha umiliki wa mali hizo na thamani zake katika vitabu vya hesabu. Baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo hazikuwa na umiliki halali wa mali zao ni kama Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (Viwanja 25), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza (Mali 5), Bohari ya Dawa (Viwanja 5), Chuo cha Mipango (Viwanja 15), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi Mazingira Tanga (Viwanja 2), Shirika la Maendeleo ya Viwanda (Viwanja 19), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara (vyanzo vya maji, ardhi na majengo).

6.16 Kutokuwepo kwa Namba za Utambuzi Katika Mali Mbalimbali

Kufuatilia mwenendo wa rasilimali ni jambo la muhimu katika kutambua mali na kufahamu maeneo zilipo. Pia inaleta urahisi wa kujua hali, idadi, thamani na mahitaji ya marekebisho yake. Kufuatilia mwenendo huu ni muhimu katika kuhakikisha hakuna upotevu wa mali.

Ukaguzi ulibaini kuwa, Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yana rasilimali ambazo ama hazijawekewa alama, au alama hazikidhi haja katika kutambua mali hizo. Mfano, Bodi ya shughuli za Maktaba haikufanya uhakiki wa mali zake ipasavyo. Samani za ofisi zilizokuwa makao makuu ziliwekewa alama kama mpya na zamani. Pia, katika Bohari ya Dawa kanda ya Mwanza rasilimali hazikuwekewa alama. Rasilimali 3,670 (35%) zilionunuliwa katika kipindi cha mwaka 2011/2012 na 2012/2013 hazikuwekewa alama. Kumbukumbu za rasilimali katika rejista ya Mfuko wa Uwekezaji Tanzania (UTT) zilikuwa sawa. Hata hivyo rasimali hizo hazikuwekewa alama yoyote kuzioanisha na rejista hivyo kusabababisha ugumu wa kutambua mali zenye thamani ya shilingi milioni 994.065.

6.17 Uwepo wa Vifaa Visivyotumika Katika Bandari ya Dar es Salaam

Wakati wa zoezi la kuhesabu na kukagua mali za Shirika la Bandari Tanzania, nilibaini uwepo wa vifaa na mali zenye thamani kubwa ya shilingi bilioni 1.598 ambazo zimekaa kwenye maghala hayo kwa zaidi ya miaka kumi na mbili (12) bila ya matumizi yoyote. Menejimenti ya Shirika la Bandari ilieleza kuwa mali hizo zimebaki katika maghala hayo kwa kipindi kirefu baada ya ubinafsishaji wa kitengo cha makontena mwaka 2000. Uwepo wa vifaa na mali zisizotumika unaliongezea shirika gharama zisizo za lazima. Pia vifaa na mali hizo zinaharibika na kupoteza thamani yake.

6.18 Matumizi Yasiyo Sahihi ya Mifumo ya Kompyuta Katika Kuhifadhi Kumbukumbu za Mali

Utunzaji wa kumbukumbu kwa usahihi ni muhimu kwa kuwa unarahisisha ufuatiliaji wa mali na kuhakikisha hakuna upotevu. Matumizi ya mifumo ya kompyuta katika uhifadhi wa kumbukumbuku huongeza tija na ufanisi. Hata hivyo, baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yamekua hayana mfumo ulio bora katika uhifadhi wa kumbukumbu na mwenendo wa mali.

Kwa mfano Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro wana mfumo wa kompyuta wa uhasibu wa “SAGE Accpack”. Hata hivyo kumekuwa na makosa mengi katika kuingiza taarifa katika mfumo huo. Pia rejista ya mali haikuwa ikiwekwa kwa wakati na kupelekea ulinganifu kati ya rejista na kumbukumbu za kompyuta kuwa mgumu. Katika chuo cha Mipango Dodoma, mfumo wa kompyuta wa “VoteBook MIS” haufanyi kazi kwa kiwango kinachokidhi mahitaji. Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama ilikuwa na baadhi ya wateja ambao hawakuwa wakitozwa kutokana na mfumo uliotumika kutofungwa kwa usahihi. Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza ilikuwa na wateja 438 ambao hawakuwa wametumiwa ankara. Hii inamaanisha kuwa zoezi la usomaji wa mita

halifanyiki kwa usahihi. Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara inatoa vyeti na malipo kwa kutumia mfumo wa MIS. Hata hivyo taarifa zilizopo kwenye MIS haziendani na tarifa za kahasibu. Kampuni ya Simu Tanzania ilikuwa na miradi iliyokamilika yenye thamani ya shilingi milioni 262 lakini haikujumuishwa kwenye mali za kampuni. Ilibainika pia kuwa jengo la ofisi ya mkuu wa Mamlaka ya Bandari - Kyela ambalo lilianza kutumika kuanzia 2008/2009 halikujumuishwa katika hesabu za Mamlaka ya Bandari.

6.19 Kutokuwepo kwa Nyaraka za Kuthibitisha Mapato Yatokanayo na Mradi wa Bukoba (Mauzo ya Viwanja) Shilingi Milioni 663.57

Mfuko wa Uwekezaji Tanzania (UTT) uliripoti kiasi cha shilingi milioni 663.57 kama mapato yaliyotokana na mauzo ya viwanja. Msingi wa kutambua kiasi cha makusanyo umewekwa bayana katika mkataba wa makubaliano uliosainiwa baina ya UTT na Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, ambapo UTT itapata asilimia 60 na Manispaa asilimia 40 ya faida. Hata hivyo menejimenti haikuonyesha namna gawio la faida lilivyopatikana. Pia menejimenti ilionyesha mapato ya shilingi bilioni 8.837 yaliyopatikana kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2013 kutokana na mauzo ya viwanja 3,389 kwa watumiaji mbalimbali. Hata hivyo gharama zilizotumika katika viwanja hivyo hazikuonyeshwa. Mapungufu haya yanaleta mashaka makubwa katika uhalali na uhalisia wa makusanyo yaliyopatikana.

SURA YA SABA USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU

7.0 Utangulizi

Usimamizi wa rasilimali watu ni mpango mahsusi wenye lengo la kusimamia watu katika utumishi. Mpango huu unalenga mambo yahasuyo uajiri na mwelekeo wa watumishi wafanyao kazi katika taasisi husika.

Mpango huo ukisimamiwa kwa ufanisi huchangia mafanikio kwa taasisi katika kutoa mwelekeo wa ujumla uhusuo utekelezaji wa malengo ya taasisi husika.

Sura hii inaonyesha mapungufu yaliyoleta vikwazo katika kufikia usimamizi ulio bora wa rasilimali watu katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

7.1 Mashirika ya Umma yenye Upungufu wa Wafanyakazi

Ni muhimu kuwepo kwa idadi stahiki ya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kuwa na aina sahihi na idadi ya kutosha ya wafanyakazi, kwa wakati muafaka na mahali husika. Hii huenda sambamba na kuhakikisha kwamba wafanyakazi hao wana elimu, ujuzi na uzoefu wa kutosha katika utendaji kazi. Hivyo, utambuzi na utunzaji wa idadi stahiki ya wafanyakazi ni muhimu katika ufanisi.

Nimebaini uwepo wa Mashirika ya Umma yenye idadi ndogo ya wafanyakazi kuliko kiwango kinachihitajika. Mashirika haya ni pamoja na Mamlaka ya Soko la Hisa na Mitaji (CMSA) ambapo kati ya nafasi 36 zilizotakiwa kujazwa, ni nafasi 21 tu sawa na asilimia 58 zilijazwa. Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogovidogo (SIDO) walikuwa na nafasi zilizo wazi 66 zikiwemo nafasi za kiuongozi. Katika Chuo cha Uongozi wa Maendeleo Vijijini (IRDP) ilibainika kuwa kati ya nafasi 14 zilizotengwa kwa ajili ya wahasibu, ni nafasi 8 tu ndizo zilijazwa. Pia kwenye Tume ya Ushindani (FCC) ilibainika kuwa na upungufu wa wakaguzi wa ndani. Pia ilibainika kwamba, Ofisi ya Kurugenzi ya

Fedha ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) ilikuwa na wafanyakazi 9 tu walioajiriwa kati ya nafasi 24 zilizotakiwa kujazwa. Ilibainika pia, katika Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kulikuwa na mpango wa kuwa na wafanyakazi 182 ambapo nafasi 84 tu ndizo zilijazwa. Pia upungufu wa wafanyakazi ulijitokeza katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga.

Ukaguzi ulibaini kuwa upungufu huo ulisababishwa na kuchelewa au kutotolewa kwa vibali vya uajili kutoka kitengo cha Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO PSM). Sababu nyingine ni ufinyu wa bajeti katika mashirika hayo.

Zaidi ya hayo, ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya mashirika hayakuwa na wafanyakazi waliobobea kwenye taaluma mbalimbali kwa ajili kushughulia changamoto zinazoyakabili mashirika hayo. Baadhi ya mashirika yalikuwa na upungufu wa wafanyakazi waliobobea katika fani ya uhasibu kwa ajili ya kuongoza vitengo vya uhasibu na fedha au kushughulikia changamoto mbalimbaali za uhasibu. Mfano wa mashirika hayo ni Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Chuo cha Ushirika Moshi (MUCCoBs).

- 7.2 Kutokuwepo kwa Utaratibu wa Kuandaa Mpango wa Kurithisha Madaraka Katika Baadhi ya Mashirika ya Umma Urithishaji wa nafasi za uongozi ni mchakato wa kutambua na kuendeleza wafanyakazi ili kuwajengea uwezo wa kushika nafasi za uongozi za taasisi. Upangaji huu huwezesha kupata wafanyakazi wenye uzoefu na uwezo wa kushika nafasi nyeti za uongozi mara nafasi hizo zinapoachwa wazi.

Matokeo ya ukaguzi yamebaini uwepo wa Mashirika ya Umma ambayo hayakuandaa mpango wa urithishaji wa madaraka. Kwa mfano taarifa ya wafanyakazi kulingana na ngazi ya utumishi ya TANAPA imeonyesha kuwa wafanyakazi wengi walio kwenye ngazi za juu wanakaribia kustaafu. Ni

muhimu kutambua kuwa watumishi wa ngazi za juu ndio walio na kiwango cha juu cha elimu na wafanyakazi waliobaki ni wale walio na kiwango cha chini cha elimu kuwawezesha kushika nafasi za kiuongozi endapo zitaachwa na viongozi waliowatangulia.

Imefahamika kuwa kufanya kazi katika timu na kiushirikiano ni muhimu katika kufikia lengo la urithishaji wa uongozi. Wakati wa ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi katika bandari ya Mwanza, ukaguzi ulibaini kuwa mfanyakazi mmoja pekee ndiye aliyekuwa na ujuzi wakati wengine wakiwa hawajui lolote kuhusu mchakato husika wa kazi. Hii inaonyesha kutokuwepo kwa utaratibu wa urithishaji wa uongozi au ujuzi wa kazi husika ambapo matokeo yake ni kusababisha hatari katika uendelezaji wa shughuli husika mara tu aliye na ujuzi akiondoka kazini.

Zaidi ya hayo, uchambuzi wa mpango wa mafunzo wa mashirika ya umma na taasisi nyinginezo haukujikita ipasavyo katika kuandaa viongozi wa baadae wa mashirika hayo. Hii inaonyesha kuwa usimamizi wa rasilimali watu haukufanywa kulingana na sera na taratibu bora za usimamizi wa rasilimali watu.

7.3 Mapungufu Katika Utunzaji wa Kumbukumbu za Wafanyakazi

Katika utaratibu bora, utunzaji wa taarifa za ajira ya mfanyakazi ni muhimu katika usimamizi wa rasilimali watu ili kulinda haki za mwajiri na mwajiriwa. Kumbukumbu hizi zinapaswa kutunzwa katika majalada ya wafanyakazi. Baadhi ya taarifa hizi ni barua za maombi ya kazi, vyeti vya elimu, sifa, taarifa binafsi, majukumu ya kazi na fomu za upimwaji utendaji kazi wa mfanyakazi na barua za nyongeza ya mshahara.

Kinyume na utaratibu tajwa hapo juu, imebainika kwamba baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma hayakuweza kutunza taarifa za mwajiriwa katika majalada

yao. Mifano ya mashirika hayo ni Mfuko wa Pensheni wa GEPF, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) ambapo zaidi ya asilimia 58 ya majalada ya wafanyakazi yalikosa majukumu ya kazi ya mfanyakazi husika. Pia katika chuo cha ustawi wa jamii (ISW) yalibainika majalada ya wafanyakazi ambayo hayakuwa na majukumu ya kazi ya mfanyakazi husika. Mapitio ya taarifa za wafanyakazi wa NCAA pia yalibaini kukosekana kwa taarifa zinazohusu sifa za mfanyakazi, vyeti vya kuhitimu masomo mbalimbali na majukumu ya kazi. Katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma, baadhi ya majalada ya wafanyakazi yalikosa mikataba ya ajira na barua za kuthibishwa kazini. Kwa upande wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya, majalada ya wafanyakazi hayakuwa na picha za wafanyakazi husika.

7.4 Upimaji wa Utendaji Kazi wa Wafanyakazi

Upimaji wa utendaji kazi wa wafanyakazi ni mchakato wa kupitia na kujadili utendaji kazi wa mfanyakazi kulingana na kazi na majukumu aliyokabidhiwa. Upimaji huu ni njia ya utambuzi wa maeneo ya utendaji bora wa kazi na kusaidia ukuaji wa taaluma ya mfanyakazi.

Serikali kupitia Kanuni za Kudumu D62 za utumishi wa umma ilielekeza kwamba, upimaji wa utendaji kazi ufanywe kwa uwazi kwa njia ya OPRAS. Kaguzi zilibaini kwamba baadhi ya Mashirika ya Umma hayakufanya upimaji wa utendaji kwa njia ya uwazi au hayakufanya kabisa aina yeyote ya upimaji wa utendaji kazi. Mashirika hayo ni Chuo cha Ardhi, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara, TEMDO, Mfuko wa Uwekezaji Tanzania (UTT), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba (BUWASA), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

7.5 Mapungufu katika Miongozo ya Usimamizi wa Fedha na Kanuni za Utumishi

Miongozo na taratibu mbalimbali za taasisi huwekwa ili kutoa maelekezo kwa wafanyakazi wakati wa utekelezaji wa shughuli za kila siku. Mapitio ya miongozo ya fedha na kanuni za utumishi umebaini kuwa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma wana miongozo ambayo ina upungufu wa vipengele muhimu na nyingine kupitwa na wakati.

Kwa mfano katika Benki ya Uwekezaji (TIB), masuala ya maslahi ya wafanyakazi yameorodheshwa katika nyaraka tofauti na kanuni za utumishi kama vile dondoo za mikutano, taarifa za mawasiliano ya ndani ya taasisi na maazimio ya bodi za wakurugenzi. Nyaraka hizo ndizo zilizotumika kama miongozo.

Pamoja na kanuni kuwa katika hatua za kuandaliwa, tumebaini baadhi ya mambo ambayo ni muhimu kujumuishwa kwenye kanuni hizo. Mifano ya mambo hayo ni sera ya usimamizi wa utendaji kazi, sera ya Utumishi wa muda mrefu, Sera ya mikopo ya wafanyakazi, Sera ya Matibabu na ya ulipaji posho maalum na ya kazi za ziada.

Kukosekana kwa miongozo ya utumishi na fedha inayojitoshela yaweza kuleta kutokuwa na msawazo katika matumizi ya taratibu zilizopo na inaweza kusababisha wafanyakazi kukosa mwongozo sahihi. Mapungufu haya yalibainika katika Benki ya Uwekezaji Tanzania, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea (SUWASA) na TEMDO ambapo kanuni mbalimbali za uendeshaji kama vile kanuni za utumishi zilionekana kupitwa na wakati na hivyo kuhitaji maboresho.

7.6 Mapungufu Katika Utoaji wa Mafunzo kwa Watumishi

Madhumuni ya mafunzo kwa watumishi ni kuboresha uwezo wa mtumishi na taasisi katika kufikia dira ya ofisi. Mafunzo yaliyopangwa vizuri ya wafanyakazi ni yale ambayo

yanaendana na sera ya mafunzo, yamepangwa kulingana na mahitaji ya mafunzo kwa wafanyakazi na pia kusimamiwa na kufanyiwa tathmini iliyo bora.

Sera ya mafunzo ni muhimu kwa kuwa inaongoza menejimenti katika kutoa mafunzo. Mpango wa mafunzo ulioandaliwa kulingana na tathmini ya mahitaji ya mafunzo ni lazima utiliwe maanani.

Baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo zilionekana kuwa na mapungufu ya kukosekana kwa sera ya mafunzo, tathmini ya uhitaji wa mafunzo na uandaaji wa mpango wa mafunzo ni; Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), MTUWASA, MWAUWASA, TANAPA, NCAA and DUWASA.

- 7.7 Ucheleweshwaji wa Kuwasilisha Mafao ya Wafanyakazi**
Wafanyakazi hukakwa michango mbalimbali inayoongozwa na sheria mbalimbali hivyo kuitwa makato ya kisheria. Makato hayo hukakwa na waajiri na kuwasilishwa kwa mamlaka husika.

Uchambuzi katika mashirika ya umma kuangalia utii katika kuwasilisha makato ya kisheria uligundua kuwa baadhi ya mashirika ya umma hayakuwasilisha makato ya wafanyakazi kwa wakati na hivyo kusababisha kutozwa adhabu kwa mashirika hayo.

Mifano ya mashirika ambayo hayakutii uwasilishaji wa makato ya wafanyakazi kwa wakati ni Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (MTUWASA) ambapo katika kipindi cha mwaka uliokaguliwa kulikuwa na bakaa ya makato ambayo hayakuwasilishwa ya pensheni ya shilingi milioni 191.696 na makato ya kodi ya shilingi milioni 35.494. Ucheleweshawaji huo ulisababisha tozo ya adhabu ya shilingi milioni 1.791 iliyotozwa na TRA, shilingi milioni 18.001 iliyotozwa na NSSF na shilingi milioni 4.508 iliyotozwa na NHIF. Adhabu hizi zina madhara ya kupunguza

mtiririko wa taslimu ambayo ingeweza kusaidia utekelezaji wa shughuli nyingine za shirika.

Ucheleweshwaji mkubwa ulionekana katika kampuni ya Usambazaji Maji ya Dar es Salaam (DAWASCO) ambapo michango ya PPF ya shilingi bilioni 2.794 haikuweza kuwasilishwa kwenye mamlaka husika. Suala hili liliripotiwa mwaka uliopita, lakini bado hakukuwa na uwasilishwaji wa makato kwa wakati.

Makato mengine ya kisheria yanayohusu mishahara ambayo hayakuwasilishwa na DAWASCO yanajumuisha michango ya PSPF ya shilingi milioni 4.710, shilingi milioni 174.460 za NSSF, shilingi milioni 31.610 za LAPF, shilingi bilioni 3.3460 kodi za wafanyakazi (PAYE) na shilingi bilioni 1.745 ikiwa ni michango ya SDL. Pia shilingi milioni 21.578 ikiwa ni makato ya wafanyakazi kulipa deni la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu kinyume na Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya mwaka 2004. Kutowasilishwa huku kuna madhara kwa waajiriwa na waajiri kutozwa tozo ya adhabu kutokana na ucheleweshwaji.

Kutokana na ucheleweshaji wa kuwasilisha makato ya kisheria DAWASCO walilipa tozo ya adhabu ya shilingi milioni 18.465 kwa ucheleweshwaji wa michango ya PPF kwa watumishi waliostaafu mwaka huu wa fedha. Pia DAWASCO walilipa adhabu ya shilingi milioni 161.644 kwa ucheleweshwaji wa kulipa michango ya PPF. Zaidi ya hayo DAWASCO wana uwezekano wa kupata adhabu ya kulipa shilingi bilioni 5.6 kutokana na ucheleweshwaji wa ulipaji makato ya kisheria. Deni hilo ni la mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2013.

Mashirika mengine ya umma ambayo hayakutii uwasilishaji wa makato ya kisheria kwa wakati ni Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA) ambayo mpaka mwisho wa mwaka wa ukaguzi, mamlaka haikuweza kulipa shilingi milioni 363.616 ikiwa ni michango ya pensheni ya

wafanyakazi na kodi ya mapato. Mashirika mengine ambayo hayakuwasilisha makato kwa wakati ni BAWASA, BUWASA na Bodi ya Chai Tanzania.

- 7.8 Mapungufu katika Udhhibiti wa Usimamizi wa Mishahara
Kuhakikisha udhibiti mzuri wa gharama za mishahara, ni muhimu kuwa na chanzo kimoja cha taarifa za ulipaji mishahara ambapo mabadiliko yoyote yataratibiwa. Pia ambapo mishahara ya shirika la umma itatoka UTUMISHI, ni muhimu kuhakikisha kwamba taarifa za utumishi zinahakikiwa ili ziweze kuwa na ulinganano na taarifa za shirika husika. Ulinganifu huu unapaswa kufanywa mara kwa mara ikiwa ni njia mojawapo ya udhibiti.

Tathmini ya uandaaji wa mishahara katika Bodi ya Pamba ulibaini kuwa baada ya kupokea pesa za mishahara kutoka utumishi, bodi hiyo iliandaa mishahara ya wafanyakazi wa makao makuu pekee na kuacha wale wa kanda ya Mwanza ambao walitumiwa pesa wajiandalie mishahara wenyewe.

Utaratibu huo hapo juu, si tu kwamba ni hatari kwa udhibiti uliopo, ila pia husababisha mlolongo usio na faida. Utaratibu unaopendekezwa ni kufanya uandaaji wa mishahara mahala pamoja na baadae kutumwa kwa wafanyakazi kupitia akaunti zao za benki.

Nilibaini kuwa Bodi ya Pamba Tanzania ilikuwa na tarifa za watumishi zinazokinzana kati ya idara ya fedha na idara ya rasilimali watu.

Mapungufu mbalimbali yalibainika TAFORI yakiwemo makosa ya kiuhasibu katika uandaaji wa mishahara ya wafanyakazi 42. Wafanyakazi 2 wa TAFORI walikuwa na namba 2 za kuajiriwa, wafanyakazi 4 waliostaafu bado walikuwa hawajaondolewa katika daftari la mishahara la hazina. Pia wafanyakazi 39 walilipwa mishahara midogo kuliko kiwango wanachostahili na wafanyakazi 10 hawakurekodiwa kabisa katika daftari la mishahara la

hazina kwa kukosa namba ya uajiri. Makosa haya yote yalitokana na kutofanya ulinganifu wa mara kwa mara kati ya hazina na TAFORI.

Imebainika pia kuwa katika Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), mishahara ya wafanyakazi haikupitiwa na kupitishwa na idara ya rasilimali watu kinyume na matakwa ya kifungu E.5 cha Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za 2009.

7.9 Kukua kwa Deni la Wafanyakazi

Sera ya mikopo ya Mfuko wa Uwekezaji (UTT) iliyopitishwa mwaka 2009 inajumuisha mikopo ya nyumba kwa wafanyakazi, mikopo ya usafiri na mikopo ya sehemu ya mshahara. Sera hiyo ya mikopo ilitaja chanzo cha pesa za kukopesha kuwa ni mfuko maalumu wa kukopeshea uliotokana na bajeti ya mwaka kwa miaka mitatu tangu tarehe ya kupitishwa kwa sera ya mikopo.

Mikopo iliyokopeshwa kwa wafanyakazi imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa ikilinganishwa na faida inayotokana na mfuko wa kukopeshea na jumla yote ya mikopo iliyotolewa. Katika kipindi kilichokaguliwa, mikopo iliyokopeshwa wafanyakazi ilifikia shilingi bilioni 2.181 ikilinganishwa na mikopo iliyokopeshwa kwa wafanyakazi ya shilingi bilioni 1.526 kwa mwaka 2012 wakati riba iliyopatikana kwa mikopo hiyo kupitia mfuko wa ukopeshaji ni shilingi milioni 44.740 ikilinganishwa na shilingi milioni 15.147 ya mwaka wa 2012.

Ukilinganisha na jumla ya madeni yote yaliyokopeshwa ya shilingi bilioni 4.353 kwa mwaka uliokaguliwa na shilingi bilioni 5.455 kwa mwaka 2012, madeni yaliyokopeshwa kwa wafanyakazi yalikuwa ni 50% (2012: 25%) ya jumla ya mikopo yote. Ukuaji huu wa deni la wafanyakazi unaweza kuhatarisha uimara wa uchumi wa taasisi iwapo hatua za usimamizi za mikopo hiyo na wa mfuko wa ukopeshaji hazitachukuliwa.

7.10 Kukosekana kwa Mchanganyiko Unaostahili wa Watumishi katika Idara ya Ukaguzi na Uchunguzi ya Shirika la Bima ya Afya (NHIF)

Mchanganyiko stahili wa wafanyakazi ni miongoni mwa mambo muhimu yanayopaswa kushughulikiwa kwa umakini wakati wa uajiri wa wafanyakazi kwa ajili ya kufanya kazi fulani.

Ukaguzi katika Shirika la Bima ya Afya ulibaini kuwa idara ya ukaguzi wa ndani na uchunguzi haikuwa na mchanganyiko wa wafanyakazi ulio sawia kushughulikia masuala ya kitabibu kwa kukosa madaktari na wafamasia. Watumishi waliopo ni wataalamu wa uhasibu ambao hupata changamoto za kitaalamu wanapotaka kufanya ukaguzi wa kichunguzi na uzuiaji wa wizi.

Utaratibu unaotumika sasa ni kuazima madaktari na wataalamu wa madawa kutoka idara nyingine mara wakaguzi wanapotaka kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi au uzuiaji wa wizi. Utaratibu huu si mzuri kwa kuwa unaweka dhana ya watumishi kutoka idara nyingine kana kwamba wanajikagua wenyewe.

7.11 Mapungufu Yaliyobainika Katika Ulipaji wa Posho kwa ajili ya vikao vya CJIC, JIC na Baraza Kuu la Wafanyakazi Katika Mamlaka ya Bandari Tanzania

Vyama vya wafanyakazi ni muhimu sana kwa ajili ya kuhakikisha kuwa amani na utulivu vinakuwepo katika taasisi. Ni mahala muhimu panapowawezesha wafanyakazi kuzungumza masuala yanayoathiri uzalishaji wa taasisi na kusaidia utatuzi wa migogoro.

Mapitio ya matumizi ya Mamlaka ya Bandari Tanzania kuhusiana na mabaraza ya wafanyakazi ya “Central Joint Industrial Council (CJIC)”, “Joint Industrial Council (JIC)”, “Workers Council”, “COTWU/DOWUTA” na “Master Workers Council (MWC)” yalibaini kwamba Mamlaka ya Bandari Tanzania yalifanya mikutano na kutumia kiasi cha shilingi

bilioni 3.277. Matumizi hayo yalifanyika kwa kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013.

Nilibaini kwamba malipo ya posho kwa ajili ya mikutano hiyo yalilipwa kwa wajumbe mara mbili au tatu kwa siku bila uthibitisho ulio wazi. Mikutano hiyo iligawanywa katika vipindi ambapo kwa siku kulikuwa na vipindi viwili mpaka vitatu ambapo wajumbe walilipwa kulingana na idadi ya vipindi ambavyo walishiriki katika vikao. Malipo ya posho ya zaidi ya mara moja kwa siku hayakufuata sera na taratibu za ulipaji wa posho hizo za CJIC, JIC, WC na MWC.

Zaidi ya hayo, mapitio ya matumizi hayo yalibaini kwamba, CJIC ilifanya mikutano mitatu mwaka 2012/2013, mmoja ukiwa ni mkutano maalum na mingine ya kawaida. Kiasi cha matumizi haya kilikuwa ni jumla ya shilingi bilioni 2.122. Uchambuzi wa matumizi yaliyofanyika ulibaini kwamba, matumizi haya yalilipwa kwa vipindi vya miezi tisa kuanzia Julai, 2012 mpaka Machi, 2013 badala ya miezi miwili ya Septemba na Disemba kipindi mikutano hiyo ilipofanyika. Hali hii inaonyesha kwamba pamoja na kuwepo kwa malipo ya posho ya zaidi ya mara moja kwa siku kwa ajili mkutano huo huo, pia kulikuwa na malipo yaliyofanywa ambayo hayakuhusu posho za mikutano lakini yalionekana katika vifungu vya matumizi ya mikutano.

SURA YA NANE

UTAWALA BORA

8.0 Utangulizi

Utawala bora kwa ujumla unahusu taratibu, mfumo na sheria ya namna ambayo makampuni yanavyoendeshwa, yanavyosimamiwa na kuelekezwa. Unahusu majukumu na mahusiano baina ya utawala wa shirika husika, bodi ya wakurugenzi, kamati ndogo za bodi ya wakurugenzi, wanahisa na wadau wengineo. Madhumuni ya utawala bora ni kuhakikisha kuwepo uwajibikaji, haki na uwazi katika shughuli za kampuni au shirika. Uwepo wa utawala bora unajenga muundo ambao unahakikisha tija kwa kila mdau anayehusika kwa kuhakikisha uwepo wa maadili na namna bora ya kufanya kazi kwa kufuata taratibu na sheria.

Hivi karibuni, masuala yahusuyo utawala bora wa makampuni yamekuwa ni jambo la kujadiliwa kutokana na kashfa mbalimbali zitokanazo na matumizi mabaya ya madaraka na kesi nyingi za jinai zinazowahusu wafanyakazi wa makampuni mbalimbali. Katika nchi ya Tanzania, Bodi za Wakurugenzi na Mabaraza wamekabidhiwa dhamana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wa Wizara mama kusimamia shughuli za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa niaba ya watanzania wote.

Katika taarifa hii, wakati wa ukaguzi nimebaini mambo kadhaa yahusuyo utawala bora ambayo yamezungumzwa katika aya zinazofuata.

Katika kipindi cha miaka kadhaa, katika sura hii nimekuwa nikitoa taarifa kuhusu matatizo katika utawala bora na mapendekezo ya namna ya

kuyarekebisha. Mambo mengi yaliyohojiwa katika miaka hiyo ya nyuma yamefanyiwa kazi na serikali pamoja na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za umma. Nimefarijika na mipango na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali na mashirika hayo katika kutekeleza mapendekezo niliyoyatoa katika eneo la utawala bora kama ilivyobainishwa na majibu ya Katibu Mkuu wa Hazina na Mlipaji Mkuu wa serikali. Kutokana na juhudi hizo, baadhi ya mapendekezo yametekelezwa na mengine yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Baadhi ya mambo yaliyoibuliwa katika ripoti zilizopita na hayajafanyiwa kazi ni pamoja mikataba ya Bodi za Wakurugenzi, kuingiliwa kwa Bodi za Wakurugenzi katika kufanya maamuzi ya kuongoza mashirika, uwepo wa wabunge katika Bodi za Wakurugenzi, mapungufu katika Idara za Ukaguzi wa ndani pamoja na uchache wa wafanyakazi katika idara hizo.

Wakati wa ukaguzi wa kisheria wa kila mwaka katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, nilibaini kuwepo kwa mambo kadhaa ambayo ni kinyume cha kanuni na taratibu za utawala bora. Baadhi ya mambo hayo ni kama yalivyoorodheshwa hapa chini :

- 8.1.0 Wizara Mama Kuingilia Utendaji wa Mashirika na Taasisi Zilizo Chini Yake

- 8.1.1 Ukosefu wa Mwongozo Unaoeleweka Kuhusu Michango Inayotolewa na TANAPA Kwa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo za Umma
Sura ya 282 kifungu cha 9 cha sheria ya Hifadhi za Taifa inaelekeza kuwa fedha na rasilimali za wadhamini zinajumuisha kiasi chochote kitakachoidhinishwa na bunge iwe ni msaada, mkopo, ruzuku kutoka serikalini, michango kutoka kwa wadhamini au mwananchi yeyote kwa ajili ya hifadhi za jamii, tozo au fedha yoyote iliyopokelewa

au kukusanywa na wadhamini au mali ambayo itawekwa chini ya wadhamini kwa ajili yao kufanyia shughuli za uhifadhi. Fedha ambazo zitapatikana kwa mujibu wa kifungu hicho hapo juu zilikusudiwa zitumike kwa ajili ya uendeshaji na uimarishaji wa Hifadhi za Taifa na si vinginevyo.

Nilibaini kuwa TANAPA inakabiliwa na michango kadhaa ya kisheria, michango na misaada kama inavyoelekezwa na wizara mama kupitia nyaraka mbalimbali na sheria zilizoanzishwa na bunge. Baadhi ya sheria za bunge za kuanzisha Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo zimetamka wazi kuwa moja ya vyanzo yake vya mapato itakuwa asilimia fulani ya makusanyo ghafi ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA). Kwa mfano Kanuni ya 3(a) ya Utalii (*Tourism Development Levy*) ya mwaka 2012 imetamka kuwa asilimia 3 itakusanywa kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa kwa ajili kuendeleza utalii na itawekwa chini ya Usimamizi wa Katibu Mkuu, Wizara ya Mali Asili na Utalii.

Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2010/11 hadi 2012/13, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) lililipa kiasi cha shilingi bilioni 10.369 kwa serikali na Mashirika ya Umma na Taasisi mbalimbali. Katika kiasi hiki, shilingi bilioni 2.2 ni mchango wa moja kwa moja kwenda Hazina na shilingi milioni 190 kwa ajili ya Makubaliano ya Lusaka (*Lusaka Agreement*). Kiasi cha shilingi bilioni 7.979 kilichobakia kililipwa kwa ajili ya Mashirika ya Umma mbalimbali ili kutekeleza shughuli za mashirika hayo. Kuhusu fedha inayolipwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali, utaratibu wa sasa ni kukubaliana na Msajili wa Hazina juu ya kiasi cha kulipa.

Miongoni mwa mashirika yaliyonufaika na michango kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) ni Bodi

ya Utalii iliyopokea shilingi bilioni 4.5 katika kipindi cha miaka mitatu kinachoishia 2012/13. Kwa upande mwingine, lengo mojawapo (lengo namba 4) linalohusu kuendeleza utalii katika nchi, kazi ambayo pia inafanywa na Bodi ya Utalii Tanzania. Hili linaonekana ni kurudia juhudi ambapo kazi moja ya kuendeleza utalii inafanywa na mashirika mawili tofauti. Kama hatua za makusudi hazitachukuliwa kulinda rasilimali fedha za TANAPA, inaweza kusababishia shirika kushindwa kutekeleza mipango yake ya muda mrefu kwa kukosa fedha.

8.1.2 Malipo yaliyofanywa na Mamlaka ya Bandari (TPA) kwa Niaba ya Wizara ya Uchukuzi

Wizara ya Uchukuzi imekuwa ikitoa miongozo mbalimbali kwa Mamlaka ya Bandari ikiagiza kufanya matumizi kwa ajili ya Wizara hiyo kinyume na taratibu za utawala bora. Katika mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2013, nilibaini kuwa kiasi cha shilingi milioni 44.320 zililipwa na Mamlaka kwa niaba ya Wizara hiyo.

Kiasi cha shilingi milioni 18.156 kililipwa kwa ajili ya kugharimia safari ya Naibu Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Wizara ya Uchukuzi ya kwenda Ghana kwa safari ya kikazi. Mamlaka ya Bandari (TPA) ilipata mwaliko wa watu wanne (4) kuhudhuria maadhimisho ya siku ya wafanyakazi Afrika yaliyofanyika huko Accra Ghana kuanzia tarehe 16 hadi 23 Juni, 2013. Mamlaka ilimteua Kaimu Mkurugenzi wa Rasilimali Watu kuiwakilisha Bandari na Wizara ikamteua Naibu Mkurugenzi wa Rasilimali Watu ili kuiwakilisha Wizara katika maadhimisho hayo. Gharama za washiriki wote wawili ziligharamiwa na Mamlaka ya Bandari.

Pia, jumla ya shilingi milioni 15 zililipwa kwa Wizara ya Uchukuzi tarehe 25 Machi, 2013 kwa ajili ya

Baraza la Wafanyakazi lililofanyika tarehe 25 Aprili, 2013. Maagizo ya kulipa yalitolewa kupitia barua yenye Kumb. JA 230/553/01 ya tarehe 25 Machi, 2013. Kwa maoni yangu malipo kama haya ya Baraza la Wafanyakazi wa Wizara yanatakiwa yalipwe kwa kutumia fedha za Wizara.

Vilevile, tarehe 16 Aprili, 2013, wizara iliandika barua nyingine yenye kumbukumbu Na. CB. 94/436/01/69 ikiagiza Mamlaka ya Bandari kulipa posho kwa ajili ya afisa atakayehudhuria kikao cha kamati ya ufundi juu ya Fedha na Uhamasishaji wa Rasilimali kilichoendeshwa na ISCOS (*Intergovernmental Standing Committee on Shipping*)

Tarehe 14 Machi, 2013, Wizara ya Uchukuzi iliandika barua yenye kumbukumbu Na. CB 230/364/01/A ili kuomba Mamlaka ya Bandari ilipe gharama ya kiasi cha shilingi milioni 11.164 katika Hoteli ya New Africa kwa ajili ya Naibu Waziri wa Uchukuzi. Malipo haya yalilipwa na bandari tarehe 28 Machi, 2013.

Ni maoni yangu kuwa wizara mama kuingilia masuala ya kifedha ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kunaathiri uwajibikaji wa Bodi za Wakurugenzi kwenye masuala ya fedha.

8.1.3 Maagizo ya Serikali Yanavyoweza Kusababisha TANAPA Kushindwa Kutekeleza Majukumu Yake ya Msingi

Sura ya 282 ya sheria iliyoanzisha Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) inaeleza kuwa shughuli kuu ya TANAPA ni kulinda maliasili, vifaa vya hifadhi na watalii, utawala wa hifadhi, kuendeleza hifadhi, kulinda mazingira na kufuatilia afya za wanyama pori, kuendeleza utalii na kushiriki kwenye shughuli za kijamii katika uhifadhi.

Katika kikao cha Bodi ya Wadhamini ya TANAPA cha 177, Bodi ilitaarifiwa juu ya uamuzi wa serikali kupitia wizara ya uchukuzi kuanzisha shirika jipya la ndege ili kutoa huduma za ndani na za kimataifa. Waziri wa Uchukuzi na Waziri wa Maliasili na Utalii wakiwa na watendaji wakuu wa baadhi ya mashirika ikiwemo TANAPA walikutana kujadili suala hili mnamo mwezi Oktoba, 2012. Bodi iliridhia mapendekezo na kuungana na wadau wengine wakiwamo Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Shirika la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Bodi ya Utalii Tanzania ili kuanzisha shirika jipya la ndege. Pia, Wizara ya Maliasili na Utalii iliandika barua yenye kumbukumbu Na. CGA.376/517/01/C/16 ya tarehe 29 Novemba, 2012 ikimelekeza Mkurugenzi Mkuu wa TANAPA kupeleka maamuzi yaliyofikiwa kuhusiana na uanzishwaji wa shirika jipya la ndege.

Kuanzisha Shirika jipya la ndege ni wazo zuri kwa ajili ya kuimarisha huduma za kijamii na kiuchumi. Hata hivyo, ninavyoona wazo hilo lililoanzishwa na Wizara ya Uchukuzi na kuungwa mkono na wadau wengine na hatimaye wizara kutoa agizo, linaweza kuwa na athari mbaya kwa TANAPA kwani inaweza kusababisha shirika kushindwa kutimiza malengo yake ya kipindi cha 2008 hadi 2013 ambayo ni muhimu kwa ustawi na maendeleo ya hifadhi.

8.2.0 Mapungufu ya Utendaji Wa Idara za Kaguzi za Ndani na Kamati za Ukaguzi za Bodi

8.2.1 Mapungufu katika Mwongozo za Kamati za Ukaguzi za Bodi

Taasisi ya wakaguzi wa ndani (*Institute of Internal Auditors in Tanzania*) ilitoa mwongozo wa namna ya kuandaa Kanuni za Kamati za Ukaguzi. Wakati wa kupitia kanuni za Kamati ya Ukaguzi zilikilinganishwa

na mwongozo kutoka taasisi ya wakaguzi wa ndani nilibaini mapungufu kadhaa yaliyojotokeza katika baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kama ifuatavyo.

Katika Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), nilibaini kuwa mwongozo huo hauna vigezo muhimu mfano, hauelezi idadi ya wajumbe katika Kamati ya Ukaguzi, kipindi chao cha kuwa wajumbe na haja ya kuwa na angalau mjumbe mmoja mwenye ujuzi wa masuala ya fedha katika kamati ya ukaguzi. Mwongozo hausemi lolote kuhusu uhuru wa kamati na ujuzi wa masuala ya fedha. Kuhusu uteuzi, ada na majukumu ya wakaguzi wa nje, mwongozo haulezi bayana ya kuwa kwa mujibu wa sheria mkaguzi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) ni Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya katiba ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania na kama ilivyoelezewa katika Kifungu cha 30 (1) na 30(3) e cha Sheria ya Ukaguzi Namba 11 ya mwaka 2008.

Pia, katika Bohari ya Dawa nilibaini kuwa miongozo ya kanuni za ukaguzi wa ndani na kamati ya ukaguzi ya Bodi hazikuwa zimethibitishwa na Bodi ya Wadhamini.

8.2.2 Mapungufu katika Idara za Kaguzi za Ndani

Vitengo imara vya ukaguzi wa ndani ni muhimu katika kutathmini kama shughuli za shirika zinafanyika kama inavyotakiwa. Uimara wa kitengo cha ukaguzi wa ndani unatokana na nafasi ya kitengo katika shirika, kinaripoti kwa mamlaka ipi, idadi na ujuzi wa wafanyakazi wa kitengo.

Wakati wa mapitio ya namna vitengo vya kaguzi za ndani vinavyofanya kazi, nilibaini kuwa vitengo vingi vya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

vilikuwa na wafanyakazi wasiotosha kufanya kazi za ukaguzi kwa ufanisi. Hali hiyo imejidhihirisha katika Shirika la TEMDO ambapo kuna mfanyakazi mmoja tu. Hali kama hiyo pia imeonekana katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga ambapo kuna mfanyakazi mmoja. Kwa kuangalia ukubwa wa mashirika husika, mfanyakazi mmoja hawezi kufanya kazi za ukaguzi kwa ufanisi. Katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA), idara ya ukaguzi wa ndani inaongozwa na mtu mmoja ambaye ni mkaguzi mwandamizi msaidizi. Nafasi ya Mkaguzi Mkuu wa ndani iko wazi. Katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), kuna wafanyakazi wawili ambao ni Kaimu Mkaguzi Mkuu na Mkaguzi Msaidizi. Nafasi ya Mkaguzi Mkuu imekaa wazi bila kujazwa tangu mwaka 2009.

Katika mpango kazi wa ukaguzi, nilibaini kuwa idara nyingi za ukaguzi wa ndani katika baadhi ya mashirika na taasisi nyinginezo hazina mpango wa ukaguzi kwa mwaka ambao ni wa kina. Mipango hii ni muhimu kwa ukaguzi kwani inabainisha rasilimali zinazohitajika ili kufanya ukaguzi, maeneo yatakayokaguliwa, muda wa kukagua na kipindi cha kutoa ripoti. Nikiwa katika shughuli za ukaguzi, mipango hiyo ni muhimu ili kuniwezesha kupanga sehemu za kukagua na uzito wa kuweka kwa kila eneo. Mapungufu katika mipango ya kazi yamebainika katika baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Mifano hiyo ni pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) ambapo mipango kazi haikupanga maeneo ya kukagua kwa kuangalia vihatarishi (*risk*) kama inavyoelekezwa na miongozo inayotolewa na Taasisi Kimataifa ya Wakaguzi wa Ndani (IPPF). Kutozingatiwa kwa mipango kazi kunasababisha matumizi mabaya ya rasilimali za idara ya ukaguzi wa ndani. Katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa

Mazingira Kigoma mipango kazi iliandaliwa lakini haikuridhiwa na Kamati ya Ukaguzi.

8.2.3 Kuchelewa Kuchukua Hatua kwenye Ripoti za Wakaguzi wa Ndani

Ukaguzi wa ndani ni chombo muhimu cha kuhakikisha mfumo wa udhibiti wa ndani ya shirika unafanya kazi vizuri. Mfumo huu wa udhibiti ni kipengele muhimu cha kuhakikisha shughuli za shirika zinaendeshwa vizuri na kulinda mali za shirika. Dhumuni kuu la mfumo hii ya udhibiti wa ndani ni kuhakikisha malengo ya kiutendaji ya shirika yanakamilishwa kwa wakati na ubora unaotakiwa kwa kuzingatia sheria mbalimbali, taratibu na kanuni na kuwa na hesabu za shirika zilizokamilika.

Nimebaini kuwa katika baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuna vitengo vilivyokamilika na ambavyo hutoa ripoti kama inavyotakiwa. Hata hivyo, utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi umekuwa haufanyiki au unafanyika kwa kuchelewa. Mfano wa mashirika ambayo ripoti hazikufanyiwa kazi kwa wakati au kutofanyiwa kazi kabisa ni pamoja na kituo cha CAMARTEC na Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi (MUCCoBs).

Ripoti ya CAMARTEC iliyotolewa tarehe 8 Oktoba, 2012 ilijibiwa Januari, 2013 na ripoti iliyotolewa Machi, 2013 ilijibiwa tarehe 15 Oktoba, 2013. Hali kadhalika, kulikuwa na hoja katika ripoti ambazo hazikujibiwa kabisa. Hoja hizo ni pamoja na shilingi milioni 290 zilizopokelewa kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara ambazo zilitumika kufanya shughuli nyingine zaidi ya zile za maendeleo yaliyokusudiwa na shilingi milioni 156.285 ambazo zilipokelewa kutoka Wakala wa Umeme Vijijini (REA) tarehe 3 Julai, 2012 ambazo hazikutumika katika mradi wa REA.

Katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA) ripoti za vipindi viwili hazikuweza kufanyiwa kazi na Kamati ya Ukaguzi.

8.3 Kuchelewa kusaini Mikataba na Bodi za Wakurugenzi

Kifungu cha 10 (2) (k) cha Sura ya 370 ya sheria ya Msajili wa Hazina ya mwaka 2002 pamoja na ile ya Mashirika ya Umma ya 1992 kama ilivyorekebishwa mwaka 2010 ambayo inamtaka Msajili wa Hazina (*Treasury Registrar*) kutia saini mikataba ya makubaliano ya malengo baina yake na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Mikataba hiyo ikiwa na nia ya kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Bodi na kuinua mapato na uchumi wa nchi kwa ujumla. Kwa upande mwingine, mikataba na Bodi ya Wakurugenzi ni muhimu katika kuhakikisha kuwepo kwa vigezo vya kufuatilia uwajibikaji na utawala bora. Hali kadhalika, mikataba hii katika utawala bora ni muhimu ili kuinua uwajibikaji na utawala bora katika shirika ikiwa ni pamoja na kuweka nguzo za kulisimamia shirika na kuwapima wakurugenzi kwa utekelezaji wa majukumu yao.

Katika ripoti zangu zilizopita, nilipendekeza utekelezaji wa mikataba baina ya serikali na wakurugenzi wa mashirika ingawaje pendekezo hili bado halijatekelezwa katika mashirika mengi na taasisi nyinginezo. Ninatambua kuwepo kwa juhudi za serikali katika kutekeleza jambo hili kama inavyooneshwa katika waraka na. 1 wa Msajili wa Hazina wa tarehe 1 Januari, 2012 ukiyakumbusha mashirika kuzingatia sheria ya Msajili wa Hazina ya mwaka 2002 na barua yenye kumb. Na. CNA 114/572/01/8 ya tarehe 13 Februari, 2014. Pamoja na juhudi hizo bado tatizo la kutokuwepo mikataba baina ya Msajili wa Hazina na Bodi za Wakurugenzi

limeendelea kuonekana katika mashirika na taasisi mbalimbali katika mwaka huu wa ukaguzi. Sehemu ambako tatizo hili limejitokeza ni pamoja na Baraza la Elimu ya Ufundi Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro. Kukosekana kwa mikataba hiyo kunasababisha kutokuwepo vigezo vya kutumia kupima uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya Bodi za Wakurugenzi.

Kwa hiyo, naendelea kusesitiza kuwa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ziongeze kasi katika kufuatilia na kuhakikisha zinazingatia sheria ya Masajili wa Hazina.

8.4.0 Mapungufu katika Utendaji wa Bodi za Wakurugenzi
Bodi za Wakurugenzi ni chombo kilichochaguliwa au wajumbe walioteuliwa na kupewa dhamana ya kusimamia na kuelekeza shughuli za shirika au kampuni ili kutimiza malengo ya uanzishwaji wake. Kazi za Bodi zinategemea nguvu, majukumu na wajibu ambao bodi zimekasimiwa na mamlaka nyingine. Kuna sheria zinazoainisha idadi ya wajumbe wa bodi, taratibu za uteuzi na idadi ya mikutano kwa mwaka. Bodi ni nguzo muhimu ya uwepo na ushamiri wa shirika la umma.

8.4.1 Uteuzi wa Mfanyakazi wa Bandari katika Bodi ya Wakurugenzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 6(2) cha sheria ya Mamlaka ya Bandari Na.17 ya mwaka 2004, Waziri wa Uchukuzi anayo mamlaka ya kuteua wajumbe watano (5) ili kuungana na Mwenyekiti aliyeteuliwa na Rais kuunda Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania. Nilibaini mfanyakazi mmoja anayewakilisha wafanyakazi katika chama cha wafanyakazi wa bandari (DOWUTA) ameteuliwa kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi. Katika kupitia

vyeti vyake, nilibaini kuwa mjumbe huyu ana kiwango cha elimu ya msingi na hajawai kushika nafasi ya juu katika uongozi katika shirika la umma au kampuni binafsi yoyote. Ninavyoona, hii ni kinyume na kanuni na taratibu za utawala bora katika kuliongoza shirika kwa kuzingatia kuwa Bodi inalo jukumu kubwa la kusimamia na kulielekeza shirika katika utendaji wa shughuli zake. Hii inaweza kusababisha mgongano wa kimaslahi na utendaji usioridhisha wa Bodi ya Wakurugenzi.

8.4.2 Mapungufu katika Bodi ya Wakurugenzi ya MORUWASA

Mikutano ya Bodi za Wakurugenzi ni muhimu kwa utendaji wa shughuli za Bodi. Katika mikutano hii ndipo maamuzi muhimu ya kuendesha shirika hujadiliwa. Kumbukumbu za maamuzi yanayotokana na mijadala hutunzwa kwa njia ya muhtasari wa vikao.

Wakati wa kupitia mihtasari ya mikutano ya Bodi, nilibaini kuwa vikao vya 76 na 77 vya Bodi za wakurugenzi havikuwa na mihtasari ya kumbukumbu za vikao hivyo. Pia, muhtasari wa kikao cha Bodi cha 83 haukuwa umesainiwa na mwenyekiti na katibu wa Bodi ya Wakurugenzi. Kwa kukosekana kwa kumbukumbu hizi kunasababisha kukosekana kwa ufuatiliaji na utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa katika vikao.

8.4.3 Malipo ya Posho za Wakurugenzi wa Bodi ya MORUWASA Bila Idhini

Wakati wa kukagua matumizi ya MORUWASA, nilibaini kuwa kila Mjumbe wa Bodi alilipwa shilingi milioni 5 katika jumla ya wajumbe kumi (10) na hivyo kuwa na malipo ya shilingi milioni 50 kama mkono wa heri baada ya wajumbe hao kumaliza kipindi chao cha uongozi kwa mujibu wa mkataba

kati ya Wizara ya Maji na wajumbe wa Bodi kifungu cha 4.4(d). Mkurugenzi Mkuu alimwandikia Katibu Mkuu barua yenye kumbukumbu Na. UWSA/M/4/Vol.V/166 ya tarehe 10 Julai, 2013 akimwomba kuidhinisha malipo ya posho za wakurugenzi. Posho hizi zilikuwa zimelipwa kabla ya kuidhinishwa na Wizara ya Maji kinyume na taratibu.

8.4.4 Gharama Kubwa za Kuwasafirisha Wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

Nilibaini kuwa mfuko haukuzingatia thamani ya fedha katika kupanga namna ya kuwasafirisha wajumbe kuhudhuria vikao. Bima ya Afya ilitumia kiasi cha shilingi milioni 2.880 kulipia gharama ya kumsafirisha mjumbe wa Bodi kutoka Mwanza kwenda Dar es Salaam na kurudi kwa njia ya barabara kutumia usafiri binafsi. Kwa mantiki hiyo, mfuko wa Bima ya Afya ungetumia usafiri wa ndege ambao gharama halisi ingekuwa ni shilingi 450,000 kwenda na kurudi. Pia mjumbe mmoja kutoka Mwanza alilipwa jumla ya shilingi milioni 5.520 ikiwa ni gharama ya kusafiri kutoka Mwanza kwenda Dares Salaam, Morogoro na kurudi Mwanza kwa safari ya kikazi. Safari hizi zingeugharimu Mfuko jumla ya shilingi laki 9 na hivyo kuokoa jumla ya shilingi milioni 7.050.

8.4.5 Ukiukwaji wa Taratibu za Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha sheria ya maji (*Water Works Ordinance 1949 Rev: Act 12 of 2009*) ; uteuzi unapaswa kufanywa na Waziri aneyehusika na Maji. Wakati wa kupitia kumbukumbu za vikao vya Bodi ya wakurugenzi, niliona taarifa za mjumbe aliyejiuzulu na kumpendekeza mjumbe atakayerithi nafasi yake kinyume cha sheria. Utaratibu huu wa kumpendekeza anayemtaka kuchukua nafasi

aliyokuwa anashikilia unaondoa taratibu zinatozatakiwa kwa mujibu wa kanuni za utawala bora. Uteuzi wa wajumbe wa bodi ni jukumu la Waziri anayehusika na shirika hilo.

8.4.6 Watumishi Waliohamishiwa Mamlaka ya Bandari Tanzania Kutoka Wakala wa Barabara Tanzania na Wizara ya Ujenzi Bila Idhini ya Bodi

Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 kifungu cha 31 na sheria ya mashirika ya umma kifungu cha 8(2) kinatamka kuwa watumishi wote wa mashirika ambao ni wakala wa serikali katika utendaji wataongozwa kwa kuzingatia sheria zilizoanzisha taasisi husika. Katika taasisi hizo madaraka ya kuajiri wafanyakazi yamekasimiwa kwa Bodi za Wakurugenzi za mashirika na taasisi husika.

Nilibaini kuwa nafasi mbalimbali za kazi katika Mamlaka ya Bandari zilijazwa na Wizara ya Uchukuzi bila kupata idhini ya Bodi ya Wakurugenzi. Kwa mfano, wizara ilimhamisha Mkadiriaji Majengo (*Quantity Surveyor*) kutoka Wizara ya uchukuzi kuwa mkuu wa kitengo cha usimamizi wa manunuzi katika Bandari ya Dar es Salaam. Afisa huyu hana sifa zinazotakiwa jambo ambalo ni kinyume na kifungu cha 34 (4) ya Sheria ya Manunuzi ya umma ya mwaka 2004 ambayo inahitaji mkuu wa kitengo cha manunuzi awe na taaluma ya ugavi na uzoefu wa shughuli za manunuzi. Wizara pia iliamisha watumishi wengine wakiwamo wahandisi, maafisa ugavi, dereva na katibu mukhtasi.

Kwa mujibu wa kanuni za utawala bora, wajibu wa kuajiri wafanyakazi katika mashirika ya umma ni wa Bodi ya Wakurugenzi.

8.4.7 Kukithiri kwa Mikutano ya Makamishna wa Tume ya Ushindani wa Kibiashara (FCC)

Vikao vya makamishna wa tume ni jukwaa muhimu kwa ajili ya maamuzi muhimu ya kimkakati. Tume ilipanga kuwa vikao vinane (8) vya kawaida na vya ziada ishirini (20) vya kusikiliza mashauri. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2012/13 makamishna walifanya jumla ya vikao 49. Vikao vitano (5) vilikuwa vya kawaida, vikao 36 vya ziada, vikao viwili (2) vya kusikiliza mashauri na vikao (6) vya kuendeleza mashauri yaliyopo. Vikao vyote vilikadiriwa kugharimu shilingi milioni 113. Kwa kuongezeka kwa vikao ikilinganishwa na makadirio, kamisheni ilitumia shilingi milioni 174 kwa posho za vikao na kuvuka makadirio kwa kiasi cha shilingi milioni 61 (35%).

Katika kutimiza majukumu yao, makamishna wa tume wanatakiwa kuzingatia makadirio ya matumizi kama walivyopanga na kuidhinisha.

8.5 Uchelewashaji wa Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi

Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania analo jukumu la kuwateua wenyevidi wa Bodi za Wakurugenzi. Wajumbe wengine huteuliwa na mawaziri wenye dhamana kutoka katika wizara mama za mashirika husika. Katika ripoti zilizopita, nimekuwa nikiandika juu ya uchelewashaji wa uteuzi wa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi. Majibu ya serikali yamezungumzia juu ya waraka namba SAB 55/204/01/159 wa Septemba 2010 ukiwaelekeza maafisa masuuli kupendekeza wajumbe wapya wa Bodi miezi sita (6) kabla ya kipindi cha Bodi kuisha. Kama miaka iliyotangulia, ucheleweshaji wa uteuzi wa Bodi umeendelea kuonekana katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

Nilibaini kuwa ucheleweshaji wa kuteua Bodi umeendelea kuwepo japokuwa taarifa ya kuisha kwa vipindi vya Bodi za Wakurugenzi zilitolewa kwa wakati kama inavyotakiwa. Kwa mfano, Taarifa ya kuisha kwa kipindi cha Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la TEMDO ilipelekwa kwa Wizara ya Viwanda na Biashara mwezi Januari, 2012 mwaka mmoja kabla ya Bodi kumaliza muda wake mnamo Januari, 2013. Bodi ya Wakurugenzi ya Ngorongoro ilimaliza muda wake tarehe 5 Oktoba, 2012 na taarifa hii kupelekwa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii japokuwa Bodi haikuwa imeteuliwa hadi Disemba, 2012 wakati ukaguzi unakamilika. Kukosekana kwa Bodi ya Wakurugenzi kunasababisha uongozi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kujiendesha bila miongozo kutoka kwa wenye mamlaka ya kufanya hivyo. Pia nilibaini kuwa, Chuo cha Wanyama Pori kilitangaza nafasi sita (6) za wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi tarehe 25 Agosti, 2012. Hata hivyo, mpaka Disemba, 2013, Bodi ya Wakurugenzi ilikuwa haijateuliwa.

Kama ilivyoripotiwa katika miaka ya nyuma, kuchelewa kuteua Bodi za Wakurugenzi kuna madhara katika utendaji wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Miongoni mwa madhara hayo ni pamoja na kutoweza kuajiri wafanyakazi katika ngazi za juu, kuidhinisha makadirio, kufanya mipango ya kimkakati, kufuatilia masuala ya kimaadili katika kutoa ripoti na kuidhinisha hesabu za mashirika na taasisi zao.

- 8.6 Gharama Kubwa katika Kuwapata Wanasheria wa Kutetea Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umeingia mikataba na wanasheria mbalimbali ili kuutetea katika kesi zinazoukabili mahakamani. Nilibaini kuwepo kwa mikataba minne (4) ambayo ilitiwa saini na Mkuu wa

Kitengo cha sheria. Katika mikataba hiyo, shirika liliingia gharama ya shilingi milioni 100 yaani 18.9% ya gharama ya shilingi milioni 527.990 inayodaiwa katika kesi hizo. Mikataba hii yote haikusainiwa na Mkurugenzi. Hata hivyo utawala wa NSSF bado unaamini kuwa ni vigumu kwa Mkurugenzi Mkuu kutia saini mikataba yote ya shirika bila kujali aina ya mkataba. Bado ninaamini kuwa kiasi cha fedha kilichotozwa ni kikubwa (18.9%) kulinganisha na fedha ambazo zinadaiwa katika kesi hizo. Kitendo cha Mkuu wa Kitengo cha sheria kutia saini katika mikataba na wanasheria bila kumhusisha Mkurugenzi Mkuu kinaweza kusababisha mgongano wa kimaslahi kwa kuzingatia kuwa anatoka katika idara inayotumia huduma hiyo.

8.7 Zuio kwa Wafanyakazi wa Bandari Kuomba Nafasi za Ajira zilizotangazwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania

Wakati wa kufanya mabadiliko katika Mamlaka ya Bandari Tanzania, nafasi nyingi za kazi katika ngazi ya uongozi ziliachwa wazi. Bodi ya Wakurugenzi ilitangaza nafasi hizi kwa watanzania wenye sifa zinazohitajika wakiwemo wafanyakazi wa Bandari. Katika kikao cha Bodi ya Wakurugenzi kilichofanyika tarehe 9 Julai, 2013, Kaimu Mkurugenzi Mkuu alipendekeza kwa Bodi kuwa wafanyakazi watakaoomba nafasi za kazi katika ngazi ya uongozi pia nafasi zao zitangazwe. Kaimu Mkurugenzi wa Bandari alitoa mwongozo kwa wafanyakazi kama inavyoonyesha barua yenye kumbukumbu Na. DG/3/5/01 ikitaarifu kuwa watakaoomba nafasi za kazi basi na nafasi zao zitatangazwa. Kwa maoni yangu hii ni kinyume na maadili ya utawala bora kwa kuwa inaondoa ile dhana nzuri ya kutoa fursa za kazi kwa watanzania wote. Utaratibu huu unaathiri upatikanaji wa wafanyakazi wenye sifa na ujuzi unaotakiwa.

8.8.0 Umiliki Usio Dhahiri wa Serikali katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

8.8.1 Benki ya Azania

Benki ya Azania (hapo mwanzo ikiitwa 1st Adili Bancorp Limited) ni benki binafsi iliyoanzishwa mnamo mwaka 1995. Wanahisa wake ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) 34.8%, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) 30.1%, Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali (PSPF) 17.2%, Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali za Mitaa (LAPF) 14.2%, Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB) 2.3%, wafanyakazi wa Benki ya Azania na wanahisa wengine (1.4%).

Mifuko ya pensheni kwa pamoja inamiliki asilimia 96.3 ya hisa zote katika benki ya Azania. Hali hii inamaanisha kuwa mifuko hii ina uwezo wa kuisimamia benki hii kwa kutoa miongozo na maamuzi muhimu yanayohusu shughuli za uendeshaji. Kwa upande mwingine, mifuko yote ya pensheni inamilikiwa na serikali kupitia Msajili wa Hazina. Kwa kuzingatia uhusiano huu, ni wazi kuwa benki ya Azania inamilikiwa na serikali kupitia Mifuko ya Pensheni. Hapo mwanzo, benki hii ilianzishwa kama benki binafsi iliyoandikishwa kwa kutumia Sheria ya Makampuni (Companies Act) na hivyo kutokuwa na sheria ya bunge ya kuianzisha. Hii imesababisha shirika hili kutokuwepo katika orodha ya mashirika yanayosimamiwa na Msajili wa Hazina na hivyo halijawahi kuwasilisha hesabu kwenye ofisi yangu kwa ajili ya ukaguzi kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 9(a)iii na iv cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

8.8.2 Benki ya Wanawake Tanzania (TWB)

Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) ilianzishwa na kuandikishwa mnamo mwaka 2007 kwa kutumia sheria ya makampuni. Benki hii inamilikiwa kwa asilimia 99 na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na taarifa ya Msajili wa Hazina ya tarehe 30 Juni, 2013 na watu binafsi wanamiliki asilimia moja (1%). Jumla ya mtaji wa kampuni kufikia tarehe 31 Disemba, 2012 ulikuwa shilingi bilioni 6.732. Kwa kuzingatia umiliki wa serikali katika shirika hili, ni wazi kwamba Benki inastahili kuwa Shirika la Umma hata kama halikuanzishwa kwa sheria ya bunge.

Kifungu na 30(1) na 30(3)e na f cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma kinaeleza kuwa kila Shirika la Umma ambalo serikali inamiliki sehemu kubwa ya hisa au linapokea ruzuku yenye thamani ya zaidi ya nusu ya mapato yake, linatakiwa kupeleka hesabu zake kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kukaguliwa. Hata hivyo, shirika hili halijawahi kuwasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi japokuwa linamilikiwa na serikali karibu asilimia 100.

8.8.3 PRIDE Tanzania Limited

Taasisi ya PRIDE Tanzania ilianzishwa mnamo tarehe 5 Mei, 1993 chini ya sheria ya makampuni (CAP 212) kwa dhamana (*limited by guarantee*). Dhumuni la kuanzishwa kwa chombo hiki ni kutoa mikopo midogo midogo kwa wajasiriamali. Chanzo kikuu cha fedha za kuanzisha taasisi hii kilitoka NORAD kwa makubaliano baina ya Serikali za Tanzania na Norway. Pia Serikali ya Sweden ilijiunga kukifadhili chombo hiki mwaka 2001.

Kwa mujibu wa taarifa ya Msajili wa Hazina iliyoonyesha uwekezaji wa serikali katika makampuni kufikia tarehe 30 Juni, 2008, ilionyesha kuwa hisa

zote za PRIDE zinamilikiwa na serikali ambapo mtaji wa PRIDE Tanzania ulikuwa shilingi bilioni 2.301 na fedha za wanahisa wengine zilikua jumla ya shilingi bilioni 2.198 na hivyo kuufanya mtaji mzima kuwa shilingi bilioni 4.499.

Kwa mujibu wa taarifa ya Msajili wa Hazina inayoishia tarehe 30 Juni, 2013 nimebaini kuwa shirika hili halipo tena kwenye orodha ya Mashirika ya Umma. Uhalali na sababu za kuondolewa kwa shirika hili katika orodha ya Msajili wa Hazina hazikuweza kubainika.

Niliandika barua yenye kumbukumbu Na. CB.27/31/63 ya tarehe 20 Juni, 2012 ili kupata maelezo juu ya umiliki wa shirika hili ambayo hadi sasa haijajibiwa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, kila shirika la umma linatakiwa kupeleka hesabu kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukaguliwa katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha. Hata hivyo, hesabu za PRIDE Tanzania hazijawahi kuwasilishwa kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyotakiwa na sheria.

SURA YA TISA

UWEKEZAJI WA SERIKALI NA UKAGUZI BAADA YA UBINAFSISHAJI WA MASHIRIKA YA UMMA

9.0 Utangulizi

Sura hii inahusu masuala ya uwekezaji ya serikali katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Serikali na hatua ya ubinafsishaji kama ilivyoonyeshwa kwenye taarifa ya hazina kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013. Zaidi ya hayo, sura hii inaonyesha matokea ya tafiti juu ya mashirika yaliyobinafsishwa, ukaguzi ambao ulifanywa na Kampuni ya Ukaguzi ya Tanscot kwa niaba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

9.1 Uwekezaji wa Serikali na hatua ya Uwekezaji

Taarifa ya uwekezaji inaonyesha hatua ya uwekezaji iliyofikiwa katika mashirika mbalimbali na taasisi za serikali.

9.1.1 Uwekezaji Katika Makampuni ya Kigeni

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 Serikali ilikuwa na uwekezaji wenye thamani ya shilingi bilioni 222.8 kwenye kampuni tisa za kigeni. Kiwango cha uwekezaji kimeongezeka kufikia shilingi bilioni 145.9 ikilinganishwa na uwekezaji wa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012.

Hisa za serikali katika makampuni ya kigeni hazikubadilika katika makampuni yote. Hata hivyo, thamani ya uwekezaji imeongezeka kutokana na kubadilika kwa viwango vya kubadilishia fedha, uthamini wa limbikizo la faida na faida ya mwaka kutokana na shughuli za makampuni hayo.

9.1.2 Uwekezaji Katika Makampuni ya Ndani

Mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2013, Serikali ilikuwa inamiliki hisa katika mashirika na taasisi nyingine za serikali 215 ambazo ziliwasilisha hesabu zao. Jumla ya uwekezaji katika makampuni ya ndani uliongezeka kutoka shilingi

trilioni 12.215 mnamo tarehe 30 Juni, 2012 mpaka kufikia shilingi trilioni 14.031 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013.

Ongezeko la uwekezaji wa ndani ulisababishwa na ongezeko la uthamini wa limbikizo la faida katika hisa za serikali, ongezeko la idadi ya taasisi za serikali kutoka taasisi 213 mwaka 2011/2012 mpaka kufikia taasisi 215 mwaka 2012/2013. Zaidi ya hayo, uwekezaji wa hisa katika makampuni ya kibiashara pia uliongezeka.

9.1.3 Mapato ya Serikali

Jumla ya mapato yaliyokusanywa na Msajili wa Hazina kama gawio, marejesho ya mikopo na mapato mengine kutoka Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yamepungua kufikia shilingi bilioni 61.5 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 kutoka shilingi bilioni 208.1 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012, ambayo ni tofauti ya shilingi bilioni 146.6 sawa na asilimia 70.47. Bajeti iliyopangwa kwa mwaka 2012/2013 ilifikia shilingi bilioni 121.8. Sababu za kupungua huko ni;

Baadhi ya mashirika kama vile BOT, In flight Catering Services Ltd, IPS, Airtel na TDFL hazikufanya vizuri. Hata hivyo, kuna baadhi ya mashirika ambayo yaliweza kufanya vizuri na hivyo kulipa gawio kwa Msajili wa Hazina. Mashirika hayo ni TPC -LIMITED, NMB, PUMA Energy (T) Ltd, TIPPER na TCC.

Ulipaji wa madeni uliofanywa na TPA kwa Serikali uliosababisha kupungua kwa kiasi cha mikopo na malipo ya riba kutoka shilingi bilioni 1.8 kwa mwaka 2011/2012 kufikia shilingi bilioni 1.1 mwaka 2012/2013, na kusababisha tofauti ya shilingi milioni 703.4 sawa na asilimia 38.65.

Kutokukusanywa kwa marejesho yaliyobaki yanayofikia shilingi bilioni 94.3 kwa sababu zifuatazo:-

- Mashirika yasiyofanya vizuri na ambayo yako katika ufilisi kupitia CHC. Makusanyo ya mapato yaliyotarajiwa kutoka mashirika haya yanaweza kupatikana kupitia mapato ya mauzo.
- Mashirika ya umma kama vile TANESCO, TRL (ambayo kwa sasa ni Reli Assets Holding Company - RAHCO) na TTCL zimekuwa na uhaba wa fedha kuweza kulipa mikopo.
- Kuna madeni ya mikopo ya serikali ya Zanzibar ambayo hayajaamuliwa na serikali mbili namna ya kuyashughulikia.

9.1.4 Mikopo ya Serikali kwa Mashirika ya Umma

Aya hii inalenga kuonyesha kiwango cha madeni ambayo mashirika ya umma yanaidai Serikali. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2013. Kiasi kilichokusanywa kama mikopo na riba kimepungua kwa shilingi milioni 506.7, yaani kutoka shilingi bilioni 2.1 mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 kufikia shilingi bilioni 1.6 ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 sawa na asilimia 24.

Kati ya madeni yanayodaiwa, shilingi bilioni 20.7 zilidawa kwa Serikali ya Zanzibar, shilingi 50 kwa RAHCO na shilingi bilioni 21.3 kwa TANESCO. Taasisi hizi kwa ujumla wake zilidaiwa asilimia 95.23% ya madeni yote yaliyopaswa kulipwa kulingana na vipengele vya mkataba.

SONGAS walikuwa na deni lililofikia shilingi bilioni 238.3 sawa na asilimia 51% ya mikopo yote inayodaiwa. Kulingana na mkataba, malipo ya mikopo ya SONGAS yanapaswa kutokana na malipo ambayo TANESCO inayafanya kwa SONGAS kutoka mauzo ya gesi. Iwapo TANESCO ikishindwa

kulipa kutokana na hali mbaya ya kifedha, SONGAS haitakuwa na uwezo wa kulipa deni.

Bakaa la kufungulia mwaka la mikopo kwa tarehe 1 Julai, 2012 ya shilingi bilioni 467.925 ilitofautiana na bakaa ya kufungua mwaka tarehe 30 Juni, 2012 kutokana na mkopo wa DUWASA wa shilingi bilioni 1.376 ambao haukujumuishwa kwenye taarifa za hesabu.

Zaidi ya hayo, mikopo iliyokuwa inadaiwa mpaka tarehe 30 Juni, 2013 ilipungua kufikia shilingi bilioni 466.549 kwa mwaka 2011/2012. Kupungua huko kulisababishwa na malipo ya mikopo yaliyofanywa na Tanzania Automech Ltd, Kampuni ya Uendelezaji wa Uwanja wa ndege wa Kilimanjaro, Mamlaka ya viwanja vya ndege, Mamlaka ya Usafiri wa anga (TCAA) na Kampuni ya Cement ya Portland (TPCC) na DUWASA. Makampuni haya yamekuwa yakilipa mikopo kulingana na majedwali ya kulipa deni.

Kuna mikopo mingine zaidi ya ile iliyotolewa kwa makampuni binafsi kama ifuatayo Loans to De Lauw Cather International, Ginaac Industries Ltd, Mansons Ltd and African Marble Co. Ltd. Also other loans were issued to Zanzibar Government.

9.1.5 Dhamana za Serikali

Dhamana za Serikali zilizotolewa kwa Mashirika mbalimbali na Taasisi Nyingine za Serikali mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2013 inaonyesha kwamba deni linalotokana na dhamana ya serikali lilifikia shilingi bilioni 485.735 ikilinganishwa na shilingi bilioni 498.67 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012.

Madeni hayo yako katika makundi yafuatayo;

- (a) Mashirika ambayo hayafanyi kazi na yako katika kubinafsishwa kama vile Mamlaka ya Mkonge Tanzania, Shirika la Usafirishaji (State Motor Cooperation), SUKITA na Kampuni ya Matairi (General Tyre East Africa). Kundi

hili lina jumla ya shilingi bilioni 33.13 (6.82%) ya kiwango cha mikopo kilichodhaminiwa.

- (b) Mashirika ambayo malipo yake ya mikopo yamepangwa upya kama vile Kiwanda cha nguo cha urafiki. Kiasi cha shilingi bilioni 5.781 (5.31%) ndio salio la dhamana katika kundi hili.
- (c) Mashirika yenye hali ngumu ya kifedha. Mashirika haya ni Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu yenye dhamana ya serikali ya shilingi bilioni 121.607; Shirika la Ndege la Taifa lenye dhamana ya dola za kimarekani sawa na shilingi bilioni 29.1 na Chama cha Ushirika Mara chenye dhamana ya serikali ya shilingi bilioni 8.503. Dhamana hizi zinafikia jumla ya shilingi bilioni 208.034 sawa na asilimia 42.83%.
- (d) Mashirika ambayo mikopo yake imelipwa inajumuisha mikopo iliyotolewa kwa ushirika kwa TANESCO yenye thamani ya shilingi bilioni 203 na kitivo cha biashara cha chuo kikuu cha Dar es salaam yenye bakaa ya mkopo wa shilingi milioni 789.544. Mikopo hii inafikia jumla ya shilingi bilioni 203.790 ambayo ni sawa na asilimia 41.95% ya dhamana yote.
- (e) Mashirika ambayo mikopo yake haifutwi kwa uuzwaji wa shirika inajumuisha shirika la usafirishaji (State Motor Corporation). Bakaa la mkopo huo ni shilingi bilioni 3.065 sawa na asilimia 0.63 ya dhamana yote ya serikali.
- (f) Dhamana ya shilingi bilioni 5 ilitolewa kwa Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA) ili kupata mkopo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha taaluma kwa wahasibu na wakaguzi. Kiwango cha udhamini ni sawa na asilimia 3.09 ya jumla ya dhamana yote yaa serikali.

Kama ilivyoielezwa hapo juu, jumla ya dhamana za serikali mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2013 imepungua kwa asilimia 2.59% yaani kwa shilingi bilioni 12.936 kutoka shilingi bilioni 498.670 mwaka 2011/2012 kufikia shilingi bilioni 485.734 mwaka 2012/2013. Bakaa hiyo inatokana na limbikizo la riba, adhabu na mabadiliko ya kiwango cha kubadilishia fedha

9.2 Ukaguzi wa Mashirika Yaliyobinafsishwa

9.2.1 Utangulizi

Ubinafsishwaji wa mashirika ya umma ulilenga kupunguza mzigo wa uendeshaji wa mashirika ya umma, uboreshaji wa kiuchumi wa mashirika na uchangiaji wake katika pato la taifa, kuchochea ukuaji wa sekta binafsi na ukuzaji wa ewekezaji wa ndani na nje.

Hata hivyo kumekuwa na kutoridhika kwa jamii kuhusu jinsi ubinafsishwaji wa mashirika ya umma ulivyofanyika kutokana na udhaifu wa utendaji wa baadhi ya mashirika yaliyobinafsishwa wakati mashirika mengine yakiwa hayajaanza kazi kinyume na vipengele vya mikataba ya ubinafsishwaji.

Kutokana na hali hiyo, Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliagiza ukaguzi wa utaratibu uliotumika katika ubinafsishwaji kwa mashirika kumi ufanywe ili kubaini kama sheria, taratibu na vigezo vya ubinafsishwaji vilifuatwa na kama malengo ya kiuchumi ya ubinafsishwaji yalifikiwa. Ukaguzi huu ulifanywa na kampuni ya ukaguzi ya Tanscot kwa niaba ya Ofisi ya Mdhiliti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

9.2.2 Hoja Zilizotokana na Ukaguzi wa Mashirika Yaliyobinafsishwa

Matokeo ya tathmini ya ubinafsishwaji yamegawanywa kama hoja za kiujumla na hoja maalum kama ifuatavyo;

9.2.3 Hoja za jumla

9.2.3.1 Maamuzi Katika Mchakato wa Ubinafsishaji

Maamuzi katika mchakato wa ubinafsishaji yalicheleweshwa kwa muda mrefu hali ambayo iliwakatisha tamaa wawekezaji na pia ilisababisha kupungua thamani ya mali na hivyo kusababisha hasara wakati wa uzaaji. Sababu kubwa ya kuchakaa kwa mali zilikuwa ni kutotumika kwa mali husika na kuachwa muda mrefu bila matengenezo.

Shirika	Namba ya Tangazo la Serikali	Tangazo la kwanza	Hitimisho la uuzaji	Kipindi (miaka)
NMC- Head office	1996/ GN 23	1996	7 Mei, 2001	5
NMC- Kurasini Wheat Complex	1996/ GN 23	1997	16 Novemba, 2005	8
Kiwira Coal Mine Ltd.	1997/ GN 543	Aprili 1999	8 Agosti, 2005	6
Morogoro Canvas Mill Ltd.		Aprili 1994	5 Octoba, 1998	4
Mufindi Paper Mill Ltd		1991-kabla PSRC	16 Januari, 2004	12
Ubungo Farm Implements Ltd		1996	20 Disemba, 2003	7
General Tyre			Mchakato unaendelea	
Tanganyika Packers Ltd-Kawe		1993 (chini ya LART)	Mchakato haujakamilika ingawa mkataba wa uuzaji wa mali ulisainiwa tarehe 19 Aprili, 2002	19
Tanganyika Packers Ltd-Shinyanga		1993 (chini ya LART)	15 Oktoba, 2007	14

Chanzo: Taarifa ya utekelezaji wa ubinafsishwaji kutoka Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) na tathmini ya mshauri

9.2.3.2 Muungiliano wa Kiutendaji Kati ya Shirika Hodhi la Mali za Serikali na Serikali Kuu

Kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Mashirika ya Umma (Iliyorekebishwa) ya mwaka 1993 inataja madaraka, mamlaka, nguvu na majukumu ya Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma/Shirika Hodhi la Mali za Serikali katika utekelezaji wa sera ya ubinafshwaji. Kutokana na Sheria hiyo, Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma/Shirika Hodhi la Mali za Serikali ilikuwa na madaraka ya kutekeleza sera ya ubinafsishaji na mpango wa urekebishaji wa mashirika ya umma kwa kushirikiana na wizara husika. Hata hivyo imebainika kuwa mara kadhaa serikali kuu kupitia wizara inayohusika na ubinafsishaji imekuwa ikiongoza mchakato wa ubinafsishaji kinyume na sheria, mfano Mgodu wa Kiwira, Hoteli ya Kilimanjaro na Kiwanda cha Kusindika Nyama (Tanganyika Packers Limited) cha Kawe.

9.2.3.3 Kutofanyika kwa Tathmini na Ufuatiliaji Usioridhisha wa Utekelezaji wa Mikataba ya Uuzaji

Mikataba ya uuzaji ina vipengele vinavyoonyesha shughuli zitakazofanywa na mnunuzi ili kuinua mashirika kupitia uwekezaji katika mitambo na teknolojia. Mipango hii ya uwekezaji ina muda maalum wa utekelezaji. Imebainika kwamba kumekuwepo na udhaifu katika muundo wa ufuatiliaji na tathmini wa kuiwezesha Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma/Shirika Hodhi la Mali za Serikali kufuatilia mipango ya utekelezaji wa mashirika yaliyobinafsishwa. Zaidi ya hayo tafiti hii haikupata vielelezo vya kuthibitisha kwamba Shirika Hodhi la Mali za Serikali lilichukua hatua kutekeleza vipengele vya mikataba. Hali hii ina maana kwamba hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kuhusiana na utekelezaji wa mikataba ya ununuzi.

Kutokana na uchambuzi uliofanywa, uwekezaji ambao haukupata usimamizi wa kutosha ni pamoja na uuzaji wa

NMC - makao makuu, NMC - Kurasini Wheat Complex, NMC - Tabora Rice Complex, NMC - Shinyanga Rice Complex, NMC Isaka Rice Complex, Kiwira Coal Mine Limited, Morogoro Canvas Mill Limited na Mufindi Paper Mill Limited. Mpaka kufikia wakati wa kuhitimisha ripoti hii, uwekezaji tajwa hapo juu ulikuwa haujahakikiwa juu ya utekelezaji wake na Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma/Shirika Hodhi la Mali za Serikali.

Imebainika kwamba Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma/Shirika Hodhi la Mali za Serikali haikuweka utaratibu wa kufanya ufuatiliaji wa tathmini ya utendaji kazi na wa kifedha wa mashirika yaliyobinafsishwa angalau katika kipindi cha uandaaji mpango wa uwekezaji ili kupima na kutoa taarifa juu ya mabadiliko ya uwekezaji kabla na baada ya ubinafsishaji. Ufuatiliaji na tathmini ni muhimu kwa ajili ya kutoa maamuzi sahihi kwa matokeo yaliyotarajiwa kutokana na urekebishaji wa mashirika ya umma.

9.2.3.4 Mapitio ya Mikataba ya Uuzaji

Mkataba kati mnunuzi na muuzaji ni sharti iionyeshe wajibu wa mnunuzi na muuzaji. Mkataba sharti pia uwe na vipengele vinavyokazia ufuatiliaji na utekelezaji wa mkataba kwa pande zote mbili.

Vipengele muhimu katika mkataba lazima vijumuishe miongoni mwa vitu vingine bei ya uuzaji na jinsi ya ulipaji, mpango wa uwekezaji uliokubaliwa wenye muda wa utekelezaji, haki ya muuzaji kupata taarifa kutoka kwa mnunuzi juu ya utekelezaji wa mpango wa uwekezaji na utendaji kazi ili kuweza kusaidia ufuatiliaji wa ufanisi wa ubinafsishaji. Vilevile ni muhimu kuwa kipengelea kinachosisitiza uwezekano wa mnunuzi kuendelea na biashara ileile iliyokuwa ikifanywa na shirika lililobinafsishwa na katika sekta ileile au kupanua biashara kupitia “forward and backward linkages”, utambuzi mzuri wa mali zinazouzwa ili kuepuka migogoro

katika hatua za baadae. Pia katika usitishwaji wa mkataba wa uuzaji kutokana na kuvunjwa kwa mkataba na mwekezaji utakapotokea, mali zote za biashara zinapaswa kurudishwa kwenye umiliki wa serikali bila malipo yeyote kwa mwekezaji. Mkataba lazima pia uzuie uuzaji wa mali iliyobinafsishwa kwa mtu mwingine.

Zaidi ya hayo, kila mkataba unapaswa kujumuisha kipengele kinachohusu uvunjaji wa mkataba ukionyesha hatua za kuchukuliwa kutokana na utendaji duni wa kazi, kama kushindwa kutekeleza mpango wa uwekezaji kulingana na muda uliopangwa na kushindwa kulipa pesa ya manunuzi kulingana na vipengele vya mkataba. Kushindwa kutekeleza vipengele vya mkataba ni ukiukwaji ambao unampa nguvu muuzaji kusitisha mkataba bila kulipa chochote kwa mnunuzi.

Katika mikataba mingi iliyopitiwa imebainika kuwa kipengele cha usitishaji wa mikataba kimezingatia kushindwa kwa ulipaji wa bei ya uuzaji pekee bila kuzungumzia vipengele vingine kama vile kushindwa kutekeleza mpango wa uwekezaji na kushindwa kuendeleza biashara.

9.2.3.5 Usimamizi wa Bodi na Menejimenti za Mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya Ubinafsishwaji

Kifungu cha 39 cha Sheria ya Mashirika ya umma (Iliyorekebishwa) Na. 16 ya mwaka 1993 imetoa mamlaka ya uangalizi kwa Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma kuhusiana na mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya ubinafsishwaji. Mamlaka haya yalilenga kuhakikisha kwamba shughuli za kiutawala na uangalizi za Mashirika ya Umma zinaendeshwa katika njia ambayo itasaidia urekebishaji mzuri wa Mashirika ya Umma.

Kifungu cha 39 (2) kinatamka kwamba “Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 39(1), huhusiana na mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya ubinafsishwaji, tume inaweza-

(a) *Kusababisha uchambuzi wa kina wa kifedha na kiutendaji kufanyika;*

(g) *Kufanya majadiliano na wajumbe wa bodi, maafisa, watumishi au wawakilishi wao kuhusu mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya ubinafsishwaji ili kufikia urekebishaji wa mashirika ya umma ulio bora”;*

Kifungu cha 42 cha Sheria hiyohiyo kinatamka kwamba: “Bila kuzingatia kwamba shirika la umma limetangazwa kuwa lilitengwa kwa ajili ya ubinafsishwaji, bodi ya wakurugenzi bado ina jukumu la;

(a) *Kuhakikisha kwamba shirika linaendelea kufanya kazi zake kama ilivyo katika mpango mkakati wake na;*

(b) *Kushirikiana na maafisa na watumishi wa shirika husika na Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma ili kuwezesha urekebishaji wa mashirika ya umma wenye mafanikio”.*

Uchambuzi wa taarifa zilizopatikana hauonyeshi kwamba tume ilitekeleza majukumu yake kulingana na kifungu cha 39(2) (a) kama ilivyoelezwa hapo juu au kuwezesha bodi za wakurugenzi kutekeleza kifungu cha 42 cha sheria hiyo.

Kifungu hicho, kinatamka kwamba bodi za mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya ubinafsishwaji kuhakikisha zinaendelea kufanya kazi kulingana na mikakati ya shirika na kushirikiana na menejimenti katika urekebishaji wa mashirika ya umma.

9.2.4 Hoja Maalum

Hoja maalum za tafiti ya ubinafsishwaji iliyofanywa zinafafanuliwa katika aya zifuatazo;

9.2.4.1 Kushindwa Kufanya Ukaguzi wa Awali (pre audit) Kabla ya Uuzaji wa Mashirika

Ukaguzi ulibaini kwamba, ubinafsishwaji wa baadhi ya Mashirika ya Umma ulifanyika kabla ya ukaguzi wa awali kwa ajili ya kupata maoni huru kuhusu hali ya mali za

Mashirika ya Umma. Hii ilithibitika kwa kutokuwepo kwa ushahidi wa kufanyika kwa ukaguzi wa huo wa awali (pre audit). Mifano ya mashirika ya umma ambayo udhaifu huu ulibainika ni Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira na Hoteli ya Kilimanjaro.

9.2.4.2 Kutokuwepo kwa Ushahidi wa Mchakato wa Uuzaji

Ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa ushahidi wa mchakato wa uuzaji. Baadhi ya mashirika yaliyokosa ushahidi huo ni Shirika la Usagishaji la Taifa (Kurasini Wheat Complex), Kiwanda cha Kusindika Nyama (TPL Shinyanga) na Southern Paper Mills Limited (SPM).

9.2.4.3 Utekelezaji wa Mpango wa Uwekezaji au Mkataba wa Uuzaji Mali

Ufuatiliaji wa mpango wa uwekezaji uligundua mapungufu kama inavyoainishwa hapa chini.

Katika Mgodini wa Kiwira (KCML), mnunuzi alipaswa kuwekeza katika mgodi shilingi bilioni 46.1. Hata hivyo ilibainika kwamba uwekezaji uliofanywa na mgodi wa kiwira kama ilivyo katika ripoti za Mgodini kwa kipindi kuanzia Juni 2005 hadi tarehe 31 Disemba, 2010 ulikuwa shilingi bilioni 3.3.

Imebainika pia kwamba uwekezaji katika Hoteli ya Kilimanjaro hakufanya uwekezaji kulingana na mkataba na muuzaji hakuchukua hatua yeyote kulingana na mkataba.

Imefahamika pia kwamba ingawa mkataba wa uuzaji wa Makao Makuu ya NMC ulimpa muuzaji haki ya kupata taarifa ya kila robo mwaka kuhusu masuala ya mpango wa ukarabati uliopendekezwa na mnunuzi, hakuna ushahidi kwamba Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma/Shirika Hodhi la Mali za Serikali ilitekeleza sharti hilo lililopo katika mkataba.

Upungufu mwingine ulibainika wakati wa kutembelea kiwanda mnamo Septemba, 2012 ambapo ilibainika kwamba mtambo ulikuwa bado haujaanza kufanya kazi, yaani ulikuwa katika ukarabati na uzalishaji ulikuwa bado haujaanza ikiwa ni miaka mitano tangu uuzaji ufanyike na miaka miwili tangu tarehe iliyopangwa ya kukamilisha mpango wa uwekezaji.

9.2.4.4 Utendaji wa Mashirika Baada ya Ubinafsishaji

Mapitio yaliyofanywa na tafiti kuhusu utendaji wa mashirika baada ya ubinafsishwaji yamebaini kwamba;

Hoteli ya Kilimanjaro ilikuwa na limbizo la hasara ya kiasi cha shilingi bilioni 26.2 kati ya mwaka 2005 na mwaka 2010. Hii ilibainika baada ya kupitia nyaraka zilizowasilishwa na Shirika Hodhi la Mali za Serikali. Pia uwekezaji uliokubaliwa kufanywa kama ilivyo katika mkataba wa uuzaji haukutekelezwa kwa kiwango kikubwa.

Kwa upande wa makao makuu ya Shirika la Usagishaji la Taifa, shughuli za usagishaji zilikuwa zikifanyika. Hata hivyo, takwimu za kiutendaji hazikuweza kupatikana. Pia mkataba unampa haki muuzaji kupata taarifa za kila mwaka kuhusu utekelezaji wa mambo yahasuyo uwekezaji, hata hivyo uthibitisho wa Shirika Hodhi la Mali za Serikali kutumia haki ya kupata taarifa kuhusu complex ya NMC Kurasini haukuweza kupatikana. Ilibainika pia kwamba Complex ya Usagishaji mchele ya NMC - Isaka ilikuwa imetelekezwa.

Hakukuwa na ushahidi wowote kuonyesha kwamba Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma/Shirika Hodhi la Mali za Serikali ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkataba wa mauziano ya “Southern Paper Mills Limited (SPM)”. Ukaguzi ulibaini kuwa kiwanda kilikuwa kikifanya kazi, hata hivyo menejimenti ilikataa kutoa taarifa za utendaji na za fedha.

Takwimu zilibainisha kwamba utendaji wa Morogoro Canvas Mills ulikuwa ukiporomoka kwa miaka kadhaa sasa.

Ilibainika kwamba Kiwanda cha Matairi cha General Tyre East Africa Limited kilikuwa kimefungwa. Hata hivyo kulikuwa na ukarabati unaoendelea kufufua kampuni uliokuwa unasimamiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa. Takwimu zilionyesha kwamba ingawa Kiwanda cha Sukari Kagera kilikuwa kikifanya kazi, utendaji wake ulikuwa ukishuka kwa miaka kadhaa iliyopita.

9.2.4.5 Maendeleo ya Soko la Hisa

Ubinafsishaji na maendeleo ya masoko ya hisa yanategemeana. Ubinafsishaji husaidia makampuni kufanya kazi kwa ufanisi na kwa faida na hivyo kuyafanya yaweze kuwa na sifa ya kuorodheshwa katika soko la hisa. Soko la Hisa la Dar-es-Salaam lilianzishwa mwaka 1998 ili kusaidia mchakato wa urekebishaji wa sekta ya fedha, kuhamasisha umiliki wa hisa kwa watanzania na kusaidia mchakato wa ubinafsishaji. Soko la Hisa la Dar es Salaam lilianza na kampuni moja ya hisa ambayo ni “Tanzania Oxygen Limited (TOL)”. Mpaka hivi sasa kuna makampuni 17 yaliyoorodheshwa na soko la hisa, hati fungani (bond) sita za makampuni na hati fungani 17 za serikali. Soko la Hisa la Dar es salaam limeongeza uwekezaji kutoka shilingi bilioni 161 kama ilivyokuwa mwaka 1998 na kufikia shilingi bilioni 12,772.79 ilipofika tarehe 30 Juni, 2012 (Ripoti ya Robo Mwaka ya Soko la Hisa la Dar-es-Salaam ya mwaka 2012).

Pamoja na ukuaji huo mkubwa ulioonyeshwa na Soko la Hisa la Dar es salaam, ni mashirika 8 tu kati ya mashirika 336 yaliyobinafsishwa ndiyo yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam. Makampuni hayo ni Kampuni ya Oksijeni Tanzania, Kampuni ya Bia Tanzania, Kampuni ya Sigara Tanzania, Kampuni ya Simenti ya Simba Tanga (SIMBA), Kampuni ya Mizigo katika Viwanja vya Ndege (SWISS PORT Tanzania Limited), Kampuni ya Simenti ya Tanzania Portland, “National Microfinance Bank (NMB)” na

Kampuni ya Chai ya TATEPA. Mashirika yaliyobinafsishwa yana jumla ya asilimia 52 ya hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Kwa ujumla, Soko la Hisa la Dar es Salaam bado ni changa. Uwekezaji wake katika soko haukuweza kuvutia makampuni mengi kwa ajili ya kuorodheshwa kwa sababu makampuni mengi yaliyolengwa hayakuwa na vigezo vilivyoainishwa. Zaidi ya hayo, Soko la Hisa la Dar es Salaam halikuweza kusaidia shughuli za ubinafsishaji. Changamoto kubwa zilizoathiri maendeleo ya Soko la Hisa ni kuwa na kiwango kidogo cha mauzo na idadi ndogo za huduma zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa na mitaji.

Ukuzaji wa umiliki wa mashirika ya umma kwa watanzania ilikuwa ni moja ya malengo ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma Tanzania. Hata hivyo, mashirika mengi makubwa yalibinafsishwa na kuuzwa kwa mataifa ya kigeni.

9.2.4.6 Kutoshirikishwa kwa Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma katika Ubinafsishwaji wa Mgodhi wa Kiwira

Imebainika kwamba mchakato wa ubinafsishwaji wa Mgodhi wa Kiwira ulifanywa na Wizara ya Nishati badala ya Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma kama ilivyo katika Sheria ya Mashirika ya Umma (iliyorekebishwa) ya mwaka 1993. Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma/Shirika Hodhi la Mali za Serikali ilihusishwa wakati wa kusaini mkataba (Joint Venture Agreement).

Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma/Shirika Hodhi la Mali za Serikali iliundwa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa urekebishaji wa mashirika ya umma na kupatiwa nyenzo muhimu zilizohitajika katika urekebishaji wa mashirika ya umma. Kushindwa kutumia utaaalam wa Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma katika ubinafsishwaji kunaweza kuleta uwezekano wa kupata matokeo mabaya ya ubinafsishwaji.

Waziri wa Nishati na Madini alimwandikia Rais dokezo CDA48/171/01 ambalo halikuwa na tarehe lililokuwa likiomba kibali cha Rais kuharakisha ubinafsishwaji wa Kiwira kutokana na ombi la Tanpower. Dokezo hilo halikuonyesha kama kulikuwa na zabuni ya kiushindani ambapo TANPOWER iliibuka mshindi.

Uchambuzi haukuweza kutambua kiwango cha ushiriki wa Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma katika mchakato ambao ulisababisha kusainiwa “Subscription and Joint Venture Agreement”, isipokuwa, tume ilihusika kutia saina tu kwenye makubaliano hayo ikiwakilisha Serikali.

9.2.4.7 Kusitishwa kwa Mkataba wa Muungano wa Makampuni (Joint Venture)

Ibara ya 17 ya mkataba wa muungano wa makampuni (Joint Venture) inahusu masuala ya usitishaji wa mkataba na katika ibara ya 17.1 inatamka kwamba:

“Serikali inaweza kusitisha mkataba huu endapo mwekezaji atashindwa kufuata vipengele katika mpango wa biashara ambao ni sehemu muhimu ya mkataba huo, pia mwekezaji anaweza kusitisha mkataba huu iwapo Serikali itashindwa kutimiza majukumu yake yaliyotajwa katika mkataba huu endapo upande uliotendewa kosa utatoa taarifa ya maandishi kuhusu upande uliotenda kosa na upande uliotenda kosa ukashindwa kurekebisha kosa lake ndani ya siku 60 baadaye au ukakata rufaa”.

Ukaguzi uliofanywa haukuweza kupata ushahidi kwamba TANPOWER ilifikia kiwango cha uwekezaji na faida kinachotajwa na mpango wa uwekezaji. Hiyo kampuni ilivunja ibara ya 17.1 ya mkataba katikati ya mwaka 2009 ikiwa ni miaka minne baada ya kusaini mkataba.

Kutokana na kuvunjwa kwa mkataba, Shirika Hodhi la Mali za Serikali/Serikali ilikuwa na haki ya kuvunja mkataba bila kutoa fidia ya aina yeyote kwenda kwa TANPOWER. Tarehe 18 Oktoba, 2009 Wizara ya Nishati na Madini ililiandikia

barua Shirika Hodhi la Mali za Serikali kulitaarifu uamuzi wa Serikali kurudisha Mgodi wa Kiwira Serikalini. Hata hivyo, sikupata ushahidi kuonyesha kwamba Kampuni ya Makaa na Nishati ya Kiwira ilikabidhiwa kisheria kwenda Serikali ya Tanzania.

kukabidhiwa Kampuni ya Makaa na Nishati ya Kiwira kwa Serikali kunamaana kwamba TANPOWER inamilikisha hisa zake za asilimia 70 kwa Serikali. Hata hivyo, kanuni ilivyo ilitarajiwa kwamba wanahisa wa kampuni walitakiwa kuamua hatima ya kampuni kulingana na vifungu vya sheria ya makampuni na mkataba wenyewe. Baada ya kupokea asilimia 70 ya hisa za mgodi wa Kiwira, nguvu ya serikali kisheria kusitisha mkataba bila fidia kutokana na kuvunjwa kwa mkataba na TANPOWER inakuwa imehujumiwa.

9.2.4.8 Utumiaji wa mikopo kutoka CRDB, NSSF na PSPF katika Kampuni ya Makaa ya Mawe Kiwira

Kampuni ya Makaa ya Mawe Kiwira ina mikopo minne ya muda mrefu kutoka NSSF, PSPF na benki ya CRDB yote ikiwa haijaanza kulipwa tangu ilipochukuliwa na kuwekwa kwenye vitabu vya hesabu vya kampuni tarehe 31 Disemba, 2010. Mikopo hiyo ni:

Madeni ya Kampuni ya Makaa ya Mawe Kiwira hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2010 (Shilingi "milioni")

Mkopeshaji	Tarehe ya Mkopo	Kianzio	Riba	Jumla	Madhumuni ya Mkopo
NSSF	10/07/2007	9,009	6,286	15,295	Fedha za kuinua mtaji
PSPF	11/11/ 2005	5,422	4,204	9,626	Fedha za Ukarabati na Upanuzi
CRDB	11/11/2005 & 19/09/2006	2,508	1,569	4,077	Kazi ya mgodi wa makaa na mtambo wa nishati
Jumla		16,939	12,059	28,998	

Chanzo: Mahesabu yaliyokaguliwa ya Kampuni ya Makaa ya Mawe Kiwira mpaka tarehe 31 Disemba, 2010

Kuhusiana na mikopo hiyo imegundulika kuwa Kampuni ya Mgoji wa Makaa ya Mawe Kiwira haijaanza kulipa na hivyo kusababisha kulimbikizwa kwa riba ya mikopo hiyo.

Uchunguzi zaidi umebaini kuwa hesabu zilizokaguliwa za Kampuni ya Mgoji wa Makaa ya Mawe Kiwira hazikuonyesha ni kwa jinsi gani kiasi kikubwa cha mkopo kilichochukuliwa kilivyotumika hasa mkopo wa CRDB na PSPF ambayo ililengwa kwa ajili ya mtaji. Hata hivyo kampuni haijanunua aina yeyote ya mali zitokanazo na mkopo kabla na baada ya kupata mkopo.

9.2.4.9 Dhamana za Serikali chini ya “Export Credit Guarantee Scheme (ECGS)” kwenda kwa Kampuni ya Mgoji wa Makaa ya Mawe Kiwira

Mkopo wa NSSF wa shilingi bilioni 9.009 ulidhaminiwa na Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ambayo ilitoa dhamana ya shilingi bilioni 6.65 (sawa na asilimia 75 ya mkopo) chini ya “Export Credit Guarantee Scheme - ECGS” ili kufidia pengo la mtaji.

Hata hivyo, Kampuni ya Mgoji wa Makaa ya Mawe Kiwira haikuwa na vigezo ya kupata dhamana ya Serikali chini ya “ECGS” kutokana na kanuni za “ECGS” (ECGS Rules of 1993). Mikopo chini ya ECGS hutolewa kwa makampuni yanayouza bidhaa nje ya nchi, kwa msambazaji au mzalishaji wa bidhaa chini ya mkataba wa mauzo kati ya kampuni na muuzaji bidhaa nje ya nchi na Mikopo itolewayo kuhusiana na “deemed export transactions”. Bidhaa zinazokidhi vigezo ni bidhaa za kitanzania kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi na kipaumbele kinatolewa kwa bidhaa zilizoongezwa thamani.

Kipindi cha dhamana ni kama ifuatavyo au itakavyopangwa na mpango wa ECGS;

- Dhamana ya kipindi kabla ya kusafirisha bidhaa - siku 270,
- Dhamana ya mkopo wa uzalishaji - siku 70 ,
- Dhamana ya mkopo baada ya kusafirisha bidhaa - siku 60,
- Dhamana wakati wa utendaji (performace) - siku 270.

9.2.4.10 Kutokuchukua Hatua Kuhusiana na Ukaguzi Maalum Uliofanywa na PKF

Tarehe 11 Juni, 2011, Shirika Hodhi la Mali za Serikali lilisaini mkataba na mshauri PKF Tanzania, kampuni ya wahasibu na washauri wa biashara kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa Kampuni ya Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira toka mgodini uchukuliwe na TANPOWER mpaka tarehe 31 Disemba, 2010.

Ripoti hii ilitoa hoja mbalimbali za msingi kuhusiana na menejimenti ya Kampuni ya Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira na hali yake ya kifedha mpaka tarehe 31 Disemba, 2010. Kutokana na ripoti hiyo Tanzania na Shirika Hodi la Mali za Serikali linatakiwa kuchukua hatua za haraka kuhusiana na ukaguzi huo maalum kabla ya kukabidhiwa mradi huo kwa Serikali.

9.2.4.11 Upitiaji wa Mikataba ya Huduma ya Menejimenti

Hatukuweza kupata ushahidi wa kuwepo kwa menejimenti ya kigeni yenye sifa ulioajiriwa na TANPOWER kuendesha Kampuni ya Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira kama ilivyo katika Mikataba wa huduma za menejimenti kati ya TANPOWER na Kampuni ya Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira.

Tarehe 18 Octoba, 2005, Kampuni ya Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira iliingia mkataba na TANPOWER ambapo walikubaliana kwamba TANPOWER itatoa huduma ya menejimenti (kama wakala wa menejimenti kwa KCML (baadae Kampuni ya Mgodini wa Makaa ya Mawe Kiwira).

Mkataba huo ulitakiwa kudumu katika kipindi chote cha “joint venture” kati ya TANPOWER, KCML na Serikali ya Tanzania au mpaka kampuni itakapovunjwa kutegemea na kitakachotangulia.

Sehemu B ya mkataba wa huduma ya kimenejimenti inatamka kwamba mkataba umesainiwa kulingana na masharti yaliyopo kwenye mkataba wa “joint venture”. Hata hivyo, pendekezo la TANPOWER la tarehe 4 Januari, 2005 linatamka kwamba “..... Pendekezo letu litajumuisha menejimenti ya kampuni. Kwa sababu hiyo, Tan-Power Resources Company Limited itaajiri timu ya kimenejimenti ya kigeni inayoaminika.....”

Kwa mujibu wa mkataba, kazi ya kufanywa na wakala wa kimenejimenti ni pamoja na:

- (i) Usimamizi wa ujumla wa kampuni wakati wa usimamizi wa mradi,
- (ii) Kufanya utafiti wa kiufundi na upembuzi yakinifu ili kukuza mgodi wa makaa, mradi wa makaa kwenda nishati na miradi midogo ya kusambaza nishati,
- (iii) Kukusanya fedha kwa kukopa au kukuza mtaji ili kugharamia shughuli za kampuni kama vile ukarabati wa mgodi na kufanya upembuzi yakinifu na tafiti nyingine za kiufundi na kama wakala wa kimenejimenti akiona inafaa, kufanya tafiti kuhusu utekeleaji wa mradi.

Ibara ya 3(i) ya mkataba inatamka kwamba “...fidia kamili kwa ajili ya huduma zilizotolewa kwa kampuni zilizofanywa na wakala wa menejimentii katika kufanya shughuli zake katika kipindi cha miaka minne baada ya tarehe ya mkataba, kampuni itatakiwa kumlipa wakala wa menejimenti ada ipatayo dola za marekani milioni 2.4 kwa mwaka (iliyokokotolewa kwa kutumia dola za marekani 200,000 kwa mwezi).

Ibara ndogo ya pili ya mkataba wa menejimenti kuhusu pande husika za mkataba inatamka kwamba kampuni haitatakiwa kulipa ada ya menejimenti mpaka kuanza kwa uzalishaji wa makaa ya mawe. Ada itarekodiwa kwa ulimbikizaji, itarekodiwa kama deni mpaka kampuni itakapoweza kulipa au, kwa uchaguzi wa wakala wa menejimenti, kutengwa kama malipo ya utangulizi wa ununuzi wa hisa na endapo wakala wa kimejimenti atasitisha kuwa mwanahisa katika kampuni, wakala wa menejimenti atatakiwa kulipwa kutokana na mtaji wa uwekezaji kwa kuzingatia ada iliyolimbikizwa.

Kwa kuwa hatukuweza kupata ushahidi wa uajiri wa menejimenti ya kigeni yenye uzoefu katika Kampuni ya Mgodu wa Makaa ya Mawe Kiwira kama ilivyoainishwa katika mkataba wa huduma ya kimejimenti, hakukuwa na uthibitisho kwa Kampuni ya Mgodu wa Makaa ya Mawe Kiwira kulipa limbikizo la ada la shilingi milioni 19,477 kwa TANPOWER hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2010.

9.2.4.12 Usimamizi wa Mchakato wa Ubinafsishwaji wa Hoteli ya Kilimanjaro

Katika uuzaji wa hoteli ya Kilimanjaro, kulifanyika duru tatu za utangazaji kati ya mwaka 1996 na 1999, lakini hatukuweza kupata maelezo zaidi ya duru hizo na kwa nini hazikufanikiwa kumpata mnunuzi. Badala yake, mwekezaji alipatikana mwaka 2003 bila zabuni na wala Tume ya Uboreshaji wa Mashirika ya Umma kuhusishwa.

Shughuli zilizohusu uuzaji wa Hoteli ya Kilimanjaro zilianzishwa, kusimamiwa na kuhitimishwa na Serikali kuu, Tume ya Uboreshaji wa Mashirika ya Umma ikiachiwa kuandaa mkataba. Aina hii ya utendaji inaweka vikwazo kwenye uwajibikaji kati ya serikali na Tume ya Uboreshaji wa Mashirika ya Umma kuhusishwa /Shirika Hodhi la Mali za Serikali na pia kuondoa uwazi.

9.2.4.13 Uuzaji wa mali za Makao Makuu ya NMC kutoendana na Sera ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma

Tafiti ya mashirika yaliyobinafsishwa umebaini kwamba uuzaji wa mali za Shirika la Usagishaji la Taifa haukufanywa kwa kuzingatia mpango wa mauzo ambapo mwekezaji alipaswa kuwa na hisa kati ya asilimia 51 na 75 na nyingine kuchukuliwa na wawekezaji wadogo wa ndani, mifuko ya amana, wafanyakazi, pamoja na umma kwa ujumla.

Tume ya Uboreshaji wa Mashirika ya Umma ilitoa “Information Memorandum” juu ya Shirika la Usagishaji la Taifa ikitaja nia ya Serikali kutafuta wabia ambao wako tayari kuwekeza kwenye sekta ili kuinua teknolojia na kupanua sekta ili kukidhi mahitaji ya ndani. Serikali ililenga kutengeneza “joint venture” mpya kwa mwekezaji ambaye atakuwa kwenye mali za Shirika la Usagishaji la Taifa za Dar es salaam kama ilivyoonyeshwa katika kundi la mashirika yatakayobinafsishwa.

Nia ya Serikali katika uuzaji huo inaendana na sera ya urekebishaji wa mashirika ambayo ni kuhamasisha ushiriki mkubwa wa wananchi katika kumiliki na kusimamia biashara. Hata hivyo uuzaji ulifanywa kwa asilimia 100 kwa mwekezaji kinyume na njia ya uuzaji iliyopendekezwa.

Ingawa mmoja wa mzabuni alitaka ifanyike “joint venture” na serikali katika uwiano wa asilimia 75 kwa 25 ambapo serikali ingeshikilia hisa chache ikiwa inaendana na malengo ya serikali. Tume ya Uboreshaji wa Mashirika ya Umma ilihitimisha uuzaji wa shirika kwa mzabuni tofauti kwa asilimia 100. Uamuzi huo ulikuwa ni kinyume na sera za serikali na malengo ya ubinafsishaji.

9.2.4.14 Utekelezaji wa Mkataba wa Uuzaji wa Mali za Shirika la Usagishaji Makao Makuu

Ibara ya 8.3 ya mkataba wa uuzaji wa mali za Shirika la Usagishaji la Taifa Makao makuu inampa muuzaji haki

kupata taarifa za kila robo mwaka kuhusu utekelezaji wa ukarabati uliopendekezwa na mnunuzi. Hakuna ushahidi kuonyesha kwamba Shirika Hodhi la Mali za Serikali lilisimamia utekelezaji wa mpango wa uwekezaji uliopendekezwa.

Mpango wa uwekezaji ni nyenzo muhimu katika mkataba na unatumika kutathmini au kutafuta zabuni iliyoshinda kwa kuwa inaonyesha uwezekano wa mnunuzi mtarajiwa kutekeleza malengo ya sera za Serikali.

Ufuatiliaji usio wa kutosha kuhusu utekelezaji wa mkataba wa uuzaji mali ulisababisha kushindwa kwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali kufuatilia, kutathmini na kutoa mapendekezo kwa Serikali jinsi urekebishaji wa mashirika ya umma unavyoendelea kwa kulinganisha na madhumuni na nini kingefanyika zaidi kulinganisha utekelezaji wa sera.

9.2.4.15 Ulipaji kwa Kubadilishana Madeni Kinyume na Mapendekezo Yaliyowasilishwa Kwa Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma Kuhusu Uuzaji wa Shirika la Usagishaji la Taifa - Kurasini

Kulingana na pendekezo la kifedha lililowasilishwa kwa Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma na mnunuzi, kampuni ya “21st Century Limited” inayomilikiwa na Mohamed Enterprises ilitakiwa kulipa kwa taslimu na si kwa kubadilishana madeni. Hata hivyo, ununuzi ulifanywa kwa kubadilishana madeni. Hatukuweza kufahamu ni kwa jinsi gani ununuzi kwa kubadilishana madeni ulifanyika.

Kinyume na njia ya ulipaji iliyopendekezwa na mnunuzi katika pendekezo lake la kifedha, tumebaini kwamba ibara ya 3.0 ya mkataba wa ununuzi iliruhusu ulipaji kamili wa dola za marekani milioni 6.2 kwa kubadilishana madeni kama ilivyoidhinishwa na Wizara ya Fedha kupitia barua yenye kumbukumbu namba TYC/C/240/27/1 ya tarehe 16 Septemba, 2005.

Pia tulibaini kwamba ulipaji wa namna hiyo haukuwa wa kawaida katika Tume. Kulingana na ibara ya 22(3) ya sheria ya mashirika ya umma (iliyorekebisha) ya mwaka 1993, Tume ya Urekebisha wa Mashirika ya Umma ni sharti ifanye mawasiliano kwa maandishi kutoka Hazina na kwa waziri anayehusika na kilimo na ushirika na Mwanasheria Mkuu. Hatukuweza kupata ushahidi kuonyesha kwamba Tume ya Urekebisha wa Mashirika ya Umma/Shirika Hodhi la Mali za Serikali iliomba idhini ya kubadilishana madeni kutoka hazina na waziri husika pamoja na mwanasheria wa Serikali.

9.2.4.16 Usimamizi na Tathmini ya Ubinafsishaji wa Shirika la Usagishaji la Taifa - Kurasini

Mkataba wa uuzaji wa mali haukuonyesha viashiria vya tathmini ya utendaji/ufanisi kwa ajili ya kufanya usimamizi na tathmini. Kiashiria pekee kilikuwa, kuongeza uzalishaji maradufu hadi kufikia tani 500 kwa siku na pia kuongeza uwezo kuhifadhi bidhaa kwa tani 12,000 zaidi ifikapo mwisho wa hatua ya pili ya uwekezaji wa dola za marekani milioni 10.76 ambao ulipangwa kukamilika ifikapo mwisho wa mwaka wa tano wa ubinafsishwaji.

Ingawa ibara ya 7.3 ya mkataba inampa muuzaji haki ya kupata taarifa za mwaka kuhusu utekelezaji wa uwekezaji, hatukuweza kupata ushahidi ya kwamba Shirika Hodhi la Mali za Serikali lilitumia haki hiyo ili kufuatilia utekelezaji wa ibara hiyo muhimu.

Hatukuweza pia kupata ushahidi wa kwamba Tume ya Urekebisha wa Mashirika ya Umma/ Shirika Hodhi la Mali za Serikali ilichukua hatua kufuatilia utekelezaji wa ibara hiyo ya mkataba.

Hatukuweza kupata taarifa za fedha kabla na baada ya ubinafsishwaji ili kuweza kutoa maoni juu ya ufanisi wa utendaji kifedha kabla na baada ya ubinafsishwaji. Hali

hii inaonyesha kwamba usimamizi na tathmini ya ubinafsishwaji wa Shirika la Usagishaji la Taifa - Kurasini Complex haukufanywa kiasi cha kuridhisha.

9.2.4.17 Mkataba wa Uuzaji wa Mali za Isaka (Isaka Rice Mill Complex)

Tumebaini kwamba ibara ya 13.1 ya kuvunja mkataba wa uuzaji wa mali inaelezea usitishaji wa malipo ya mauzo kama ilivyo katika jedwali la ulipaji. Mkataba wa mauzo sharti uwe na vipengele vingine muhimu vihusavyo utekelezaji wa mpango wa uwekezaji na viashiria vingine vya ufanisi wa utendaji kifedha ambavyo vinaweza kusitishwa kwa mkataba kama havikutekelezwa. Kukosekana kwa vipengele hivyo katika mkataba inamaanisha kwamba mnunuzi hana majukumu yoyote ya kimkataba kutekeleza mpango wa uwekezaji wa shilingi bilioni 2.2 au kuweka kiwanda katika wigo mkubwa wa kibiashara.

Ukaguzi haukuweza kumpata mnunuzi. Taarifa za kiwanda baada ya ubinafsishwaji hazikuweza kupatikana. Iligundulika pia kuwa kiwanda cha kusagisha nafaka cha Isaka kilikuwa hakifanyi kazi. Hatukuweza kufahamu ni kwa muda gani kiwanda hicho kilibaki bila kufanya kazi. Juhudi za kumpata mmiliki hazikuweza kuzaa matunda.

9.2.4.18 Utekelezaji wa Mkataba wa Uuzaji wa Mali za Isaka (Isaka Rice Mill Complex)

Hatukuweza kupata ushahidi wowote unaoonyesha Shirika Hodhi la Mali za Serikali lilifanya tathmini ya utekelezaji wa uuzaji wa mali hizo.

Mkataba wa uuzaji haukueleza jinsi ya utekelezaji wa mkataba huo na pia haukuwa na vipengele muhimu ambavyo Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma ingepaswa kusesitiza ili kuhakikisha utendaji wa mnunuzi

baada ya ubinafsishaji unaendana na sera na malengo ya Serikali.

Kukosekana kwa vipengele hivyo muhimu katika mkataba kama vile mpango wa uwekezaji inafanya ufuatiliaji wa baada ya ubinafsishwaji kutokuwa wa mafanikio kwa kuwa mnunuzi hana jukumu lolote la kutekeleza mpango wa uwekezaji na vipengele muhimu kwa ajili ya ubinafsishwaji wenye manufaa ambao utahakikisha sera na malengo ya Serikali kuhusiana na uuzaji wa mali unapata mafanikio.

9.2.4.19 Muda na Mchakato wa Uuzaji wa Shinyanga Rice Mill

Uuzaji wa Kiwanda cha Usagishaji cha Shinyanga ulichukua miaka kumi kukamilika na imeripotiwa kuwa uuzaji ulitangazwa na ulivutia wazabuni katika matukio zaidi ya matatu. Kushindwa kukamilisha uuzaji kwa wakati kulitokana na bei ndogo iliyopendekezwa na wanunuaji ikilinganishwa na taarifa ya tathmini ya thamani ya mali hizo. Ikumbukwe kuwa jinsi muda unavyopita kati ya tarehe ya tathmini ya mali na tarehe ya mauzo, matumizi ya taarifa ya uthamini hupungua na kutokuwa na umuhimu katika maamuzi.

Juhudi za kuuza kinu cha usagishaji zilianza tangu mwaka 1995 wakati Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma ilipotoa kazi ya kutathmini thamani ya mali, lakini uuzaji ulikamilika tarehe 20 April, 2005, ikiwa ni miaka kumi baadae na hivyo kusababisha mali kukaa bila kufanya kazi ambayo inasababisha kushuka kwa thamani ya vinu au kusababisha wizi wa mali hizo. Hii haikuwa tu na madhara hasi kwenye bei ya uuzaji bali pia inapunguza umuhimu zoezi la uthamini wa mali na zoezi zima la utoaji maamuzi.

9.2.4.20 Kutokuwepo kwa Usimamizi wa Mashirika Yaliyotengwa kwa Ajili ya Ubinafsishaji Kinu cha Usagishaji Shinyanga

Kukosekana kwa usimamizi wa karibu wa Shirika Hodhi la Mali za Serikali kwa mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya urekebishwaji kungesababisha menejimenti kuchukua maamuzi ambayo si sahihi kwa ajili ya mpango wa uuzaji wa mali uliopangwa.

Wakati wa hatua za mwisho za uuzaji, iligundulika na Tume ya Urekebishaji wa Mashirika Yaliyobinafsishwa kuwa Shirika la Usagishaji la Taifa lilikodisha moja ya maghala yake kwa Mohammed Enterprises (T) Limited na kodi ya pango ikilipwa katika Shirika la Usagishaji la Taifa. Wizara ya Kilimo na Chakula ilikuwa na taarifa kuhusu mpango huo, hata hivyo taarifa hiyo haikuweza kufikishwa Tume ya Urekebishaji wa Mashirika Yaliyobinafsishwa.

Ukodishaji huo uliingiwa baada ya uuzaji wa mali kutangazwa na hivyo kuingilia mpango wa urekebishaji wa Mashirika ya Umma.

Hakukuwa na ushahidi kuonyesha kwamba Shirika Hodhi la Mali za Serikali lilifanya uthamini wa shughuli za kinu cha kukoboa mchele cha Shinyanga “Shinyanga Rice Mill” baada ya ubinafsishaji.

Kutokana na kutembelea kinu hicho mwezi Septemba, 2012, tulibaini kwamba, kinu hicho kilikuwa kinamilikiwa na Kampuni ya “Mohammed Enterprises Limited”, badala ya Kampuni ya Best Lint (Tanzania) Limited walionunua kinu hicho kutoka Serikalini na kusaini mkataba wa uuzaji.

Ilibainika pia kwamba, mkataba wa uuzaji, haukuleza masuala ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkataba wa uuzaji. Pia mkataba huo haukuwa na vipengele

muhimu ambavyo Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma, ungepaswa kusisitiza ili kuhakikisha kwamba mwenendo wa mnunuzi unakuwa sambamba na sera za serikali kuhusu uuzaji huo.

Mkataba huo, unakosa vifungu muhimu kama vile kushindwa kutekeleza mpango wa uwekezaji kulipaswa kuwa sehemu ya makubaliano yatakayoruhusu uvunjwaji wa mkataba. Kipengele pekee kinachoruhusu kusitishwa kwa mkataba, ni kushindwa kulipa bei ya ununuzi kama ilivyokubaliwa na mkataba wa uuzaji. Mkataba wa uuzaji ulipaswa pia kuwa na viashiria vya ufanisi ili kuhakikisha usimamizi na tathmini ya mashirika ya umma baada ya ubinafsishaji utakaofanywa na Shirika Hodhi la Mali za Serikali kuwa mzuri.

9.2.4.21 Utekelezaji wa Mkataba wa Uuzaji wa Mali katika ubinafsishaji wa Tabora Rice Mill

Imebainika kwamba, mkataba wa uuzaji mali haukuwa na vipengele vinavyohusu usimamizi wa utekelezaji wa mkataba wa uuzaji. Pia mkataba huo haukuwa na vipengele muhimu ambavyo Tume ya Urekebishaji wa Mashirika yaliyobinafsishwa ingesisitiza ili kuhakikisha kwamba mwenendo wa mnunuzi katika mali zilizobinafsishwa unaendana na sera ya Serikali katika uuzaji huo.

Ni hali isiyo sawa kwa mnunuzi kutokuwa na majukumu yoyote ya kimkataba katika kutekeleza mpango wa uwekezaji au kuweka kinu katika wigo mpana wa biashara. Mkataba wa manunuzi haukuwa na vipengele vya kumfanya mnunuzi kuwajibika katika utekelezaji wa mkataba.

Mkataba unakosa vipengele muhimu kama vile kushindwa kutekeleza kwa mpango wa biashara. Mkataba uliopo unaeleza sababu moja tu ya kusitisha mkataba nayo ni kushindwa kulipa pesa ya ununuzi iliyotajwa kwenye jedwali la malipo. Zaidi ya hayo,

mkataba wa uuzaji ulitakiwa kuwa na viashiria vya ufanisi wa utendaji na sharti la kutoa taarifa kwa vipindi mbalimbali kwa ajili ya kuongeza ubora katika kufanya tathmini kunakofanywa na Shirika Hodhi la Mali za Serikali.

Hakukuwa na ushahidi wowote ulioonyesha kwamba Shirika Hodhi la Mali za Serikali lilifanya tathmini ya shughuli za shirika baada ya ubinasfishwaji.

9.2.4.22 Ucheleweshaji katika utekelezaji wa Mkataba wa Ubinafsishaji wa Kiwanda cha Kusindika Nyama “Tanganyika Packers Limited Kawe”

Katika kupitia mkataba wa uuzaji wa mali ilibainika kwamba, wakati mnunuzi akiwa amekamilisha wajibu wake katika mkataba, muuzaji alishindwa kutimiza masharti chini ya mkataba kwa kushindwa kukabidhi kwa mnunuzi hati kama ilivyo katika ibara cha 2.2. Kwa msingi huo muuzaji alikiuka mkataba wa uuzaji.

Hata baada ya kugundua kuwa imekiuka mkataba, Serikali haikuchukua hatua yoyote kusuluhisha suala hilo. Muuzaji amesababisha ukiukwaji ambao ungeweza kurekebisha, ambapo chini ya kifungu 11 cha mkataba wa uuzaji, hali hii inaweza kusababisha usuluhishaji wake kufuata kanuni za Tume ya Biashara ya Kimataifa ya Umoja wa Mataifa (UNCITRAL Arbitration Rules).

Suala hilo limebaki bila kutatuliwa kwa takriban miaka kumi tangu kusainiwa kwa mkataba huo mnamo mwaka 2002.

Ucheleweshwaji wa utekelezaji wa majukumu ya kimkataba unaweza kusababisha madai makubwa na kuharibu taswira ya Serikali kama kituo cha uwekezaji.

9.2.4.23 Ucheleweshwaji wa Uuzaji wa Mali za Kiwanda cha Usindikaji Nyama “Tanganyika Packers Shinyanga”

Ucheleweshaji wa muda mrefu wa uuzaji wa mali baada ya tathmini ya thamani waweza kusababisha kushuka

kwa thamani ya mali za muuzaji na pia kusababisha kuchakaa kwa mali husika. Tathmini ya Julai, 1998 ya mali za Tanganyika Packers Shinyanga uliofanywa na “LET Consultants” ulitaja thamani ya mali za Tanganyika Packers Limited za Shinyanga kuwa shilingi milioni 1,090.52 (kadirio la juu) na shilingi milioni 732.95 (kadirio la chini). Zaidi ya hayo, taarifa nyingine ya mwaka 1994 iliyofanywa na “Feser Valuers” ilitoa taarifa ya thamani kuwa ni shilingi milioni 1,508.8 (replacement value) na shilingi milioni 904.62 ikiwa ni thamani iliyopatikana kwa kutumia njia ya kukokotoa uchakavu.

Mkataba wa uuzaji ulisainiwa kati ya Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma na Triple S Beef Limited tarehe 15 Oktoba, 2007, miaka tisa baada ya tathmini ya thamani kwa bei ya shilingi milioni 63.25 kiasi ambacho ni asilimia kumi pungufu ya kiwango cha chini ya tathmini ya mwaka 1998.

- 9.2.4.24 **Upungufu katika utekelezaji wa mpango wa uwekezaji wa Tanganyika Packers Limited - Mali za Shinyanga**
Katika kutembelea kiwanda cha Tanganyika Packers cha Shinyanga mwezi Septemba, 2012, ilibainika kwamba mtambo ulikuwa hauifanyi kazi, bado ulikuwa katika ukarabati na uzalishaji ulikuwa bado kuanza, ikiwa ni miaka mitano baada ya uuzaji kukamilika na miaka miwili baada ya tarehe ya kukamilika kwa mpango wa uwekezaji.

Hatukuweza kupata taarifa za kutosha kuhusu kiwango cha uwekezaji kilichofanywa mpaka wakati wa kukamilika ukaguzi huu. Pia muda uliopangwa katika ukarabati na muda tarajiwa wa kuanza kutumika kwa kiwanda haukuweza kupatikana.

Ingawa mkataba wa uuzaji wa mali ulimpa muuzaji mamlaka ya kuratibu mpango wa uwekezaji na kuweka

vigezo vya kusitisha mkataba kutokana na kushindwa kutekeleza mpango wa uwekezaji (ibara ya 7 ya mkataba). Muuzaji hakufanya kilichotarajiwa na mnunujaji kuachwa huru.

Mpango huo ulikuwa ni wa uwekezaji wa Dola za kimarekani milioni 236.6 katika kipindi cha miaka mitatu kikiwa na mpango wa uwekezaji unaoonyesha kwamba mpaka kufikia Januari, 2011, mradi utakuwa katika uwezo wake kamili kiuzalishaji.

9.2.4.25 Ubinafsishaji wa Southern Paper Mills (SPM)

Jitihada za kubinafsisha SPM zilianza mwaka 1991 kabla ya kuanzishwa kwa Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma. Jitihada hizo zilianzishwa na kuratibiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa kwa msisitizo wa wafadhili wa kigeni wa SPM wakiwemo Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uswidi, Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Canada, KfW na Benki ya Dunia. Mwaka 1992 Serikali iliunda kikundi kazi cha wizara kwa ajili ya ubinafsishaji wa SPM ambao ulihusisha Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) kama mshauri kwa ajili ya ubinafsishaji wa SPM. Mwaka 1993 Shirika la Fedha la Kimataifa lilikutana na zaidi ya makampuni 160 ya karatasi na wawekezaji wengine duniani kujaribu kutangaza uuzaji wa SPM kama fursa inayovutia ya kuwekeza. Hata hivyo, wawekezaji wengi walikuja na masharti ambayo hayakuwa mazuri na hivyo kusababisha Serikali kujitoa kwenye majadiliano. Mwaka 1994, Shirika la Fedha la Kimataifa lilijitua kutoka kwenye kazi ya kiushauri na Tume ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma ikachukua madaraka ya mchakato wa ubinafsishaji.

Chini ya Tume hiyo, mwaka 1999 seti ya wazabuni wanne ilipokelewa kutoka kwa makampuni ya M.A. Kharafi & Sons (MAK), MIDROC Ethiopia Pvt. Limited, Khoday India Limited na AJ Group. Kampuni ya MAK, ambayo iliibuka mshindi wa zabuni, ilialikwa kwa ajili ya majadiliano ingawa kulikuwa na kutokukubaliana

kwenye vivutio, kanuni na masharti yaliyotolewa na MAK. Matokeo yake, SPM iliuzwa kwa kampuni ya Rai Group ya Kenya kwa bei ya dola za kimarekani milioni 26. Mkataba wa uuzaji wa mali kati ya Tume ya Urekebishaji wa Mashirika Yaliyobinafsishwa na kampuni ya Rai Group ulisainiwa tarehe 16 Januari, 2004. Mkataba huu ulitamka kwamba bei iliyokubaliwa ni dola za kimarekani milioni 26 itakayolipwa kama ifuatavyo; Dola za marekani milioni moja wakati wa kusaini mkataba, dola za marekani milioni tatu kuwekwa kwenye “escrow account” na dola za marekani milioni ishirini na mbili kutumika na mnunuzi (i)kuwekeza katika kampuni katika kipindi cha miaka miwili ya kwanza (dola za marekani milioni 16.2) na (ii) dola za marekani milioni 5.8 katika mwaka wa tatu. Ilikubaliwa pia kwamba kiasi kilichowekwa kwenye “escrow account” kitolewe na mwekezaji baada ya kuweka uwekezaji wa jumla ya dola za kimarekani milioni 22.

Kwa kuzingatia ukweli kwamba dola za marekani milioni 3 zilizowekwa kwenye “escrow account” zitarejeshwa kwa mwekezaji na dola za marekani milioni 22 zitawekezwa kwenye SPM, kiasi kinachobaki ni dola za marekani milioni moja tu kuwa bei halisi ya kuuzia mali za SPM. Kwa maoni yetu, hii ina maana kwamba kama bei ya kuuzia ni dola za marekani milioni 26 ina maana kwamba mali za SPM hazikuuzwa kwa mwekezaji lakini inamilikiwa na Serikali kwa kuwa malipo yaliyofanywa kwa mali za SPM hazikwenda kwa Serikali bali ziliwekezwa katika SPM. Kiasi cha dola za marekani 22 zilizowekwa SPM kama sehemu ya bei ya kuuzia zilitakiwa kufanywa kama sehemu ya uwekezaji wa serikali katika SPM.

Zaidi ya hayo, hakuna ushahidi kwamba Tume ya Urekebishaji wa Mashirika Yaliyobinafsishwa/Shirika Hodhi la Mali za Serikali ilifanya usimamizi na tathmini ya ubinafsishaji na utekelezaji wa mkataba wa uuzaji.

SURA YA KUMI

MATOKEO YA KAGUZI MAALUM

10.0 Utangulizi

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa Mamlaka chini ya Kifungu Na. 29(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 ya kufanya ukaguzi maalum. Pia anaweza kufanya ukaguzi maalum kufuatia maombi ya Mtu Binafsi, Taasisi, Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma.

Kufuatia kifungu hicho cha sheria, katika mwaka huu wa fedha Ofisi yangu ilifanya jumla ya kaguzi maalum sita katika Mashirika ya Umma. Mashirika hayo ni Benki ya Posta Tanzania (TPB), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bodi ya Korosho ya Tanzania na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade).

Matokeo ya kaguzi maalum yameainishwa kwenye ripoti hii kwa muhtasari, kwa hiyo taarifa za kina zinapatikana katika ripoti husika ambazo hupatikana katika Mamlaka zilizoomba kufanyiwa kaguzi hizo.

Yafuatayo ni matokeo ya kaguzi maalum zilizofanyika na kukamilika katika kipindi cha mwaka huu wa ukaguzi:-

10.1 Benki ya Posta Tanzania (TPB)

Ukaguzi maalum wa Benki ya Posta Tanzania (TPB) ulifanyika kufuatia barua iliyoandikwa na wafanyakazi wa Benki ya Posta kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikieleza kuwa Benki ya Posta Tanzania kumefanyika ufisadi wa shilingi milioni 185, kumekuwa na utoaji wa zabuni kwa njia za kifisadi na ajira za upendeleo na pia kutozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005.

10.1.1 Ukarabati wa Nyumba ya Mkurugenzi Mkuu

Ukaguzi maalum ulibaini kuwepo kwa mkataba wa kukarabati nyumba ya Mkurugenzi Mkuu wa TPB iliyopo kiwanja Na. 24 kitalu Na. 186157 - katika eneo la Ursino Kinondoni Dar es Salaam. Kazi hii ilipewa kampuni ya Kiaren Investment Ltd na mkataba wa kazi hiyo ulisainiwa tarehe 15 Novemba, 2011. Mkataba wa kazi hiyo ulikuwa wa jumla ya shilingi milioni 92.630. Ilibainika kuwa kiasi kilicholipwa kwa Mkandarasi huyo kilikuwa ni shilingi milioni 104.572. Menejimenti ya TPB haikuwa tayari kutoa maelezo ya malipo ya ziada ya kiasi kilichoainishwa kwenye mkataba jumla ya shilingi milioni 11.942. Utaratibu wa manunuzi uliotumika ulikuwa ni ule wa kugawa zabuni maalum (Restricted tendering method), ambapo wazabuni watano walishiriki kwenye mchakato huo ikiwepo kampuni ya Kiaren Investment Ltd. Hata hivyo, kampuni zote zilizoshiriki hazikukidhi vigezo vya kushiriki utaratibu huo wa manunuzi.

Benki ya Posta Tanzania ilitoa zabuni ya kubuni michoro na kuandaa mchanganuo wa gharama (BOQ) ya ukarabati wa nyumba ya Mkurugenzi Mkuu kwa kampuni za Aeroproject Tanzania Ltd na kampuni ya Technician Image. Menejimenti ya Benki ya Posta haikuweza kutoa maelezo ya utaratibu uliotumika kutoa zabuni hiyo kwa kampuni hizo.

Benki ya Posta Tanzania haikuwa na msimamizi (meneja wa mradi) mwenye sifa ya kusimamia kazi ya ukarabati wa nyumba ya Mkurugenzi Mkuu, badala yake Afisa Utawala ndiye aliyekuwa akisimamia kazi hiyo. Afisa huyo hakuwahi kufanya mkutano "site meeting" yoyote na mkandarasi ingawa ndiye aliyemshauri Mkurugenzi Mkuu kuwa mkandarasi huyo apewe kazi za ziada.

Kazi za ziada za ukarabati wa nyumba ya Mkurugenzi Mkuu zenye thamani ya shilingi milioni 71.137 zilitolewa kwa kampuni ya Kiaren Investment Ltd. Ukaguzi ulibaini

kuwa kazi za ziada zilifanyika pia na kampuni ya Havillah Business ambayo ilipewa kazi hizo bila kufuata taratibu za sheria ya manunuzi. Ilibainika kuwa Mkurugenzi Havillah Business pia alikuwa anafanya kazi katika kampuni ya Kiareni Investment Ltd. Vilevile, Kampuni ya Havillah Business haikuwa imesajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB). Malipo yaliyolipwa kwa kampuni ya Havillah Business yalikuwa ni shilingi milioni 16.692 yaliyojuimuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ambayo hayakurejeshwa katika Mamlaka ya mapato ya Tanzania (TRA) na kampuni hiyo.

Cheti cha usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) cha kampuni ya Havillah Business ndicho kilichotumiwa na kampuni ya NACOD Enterprises, kampuni iliyopata asilimia 50 ya mikataba ya ujenzi kutoka Benki ya Posta Tanzania kwa kipindi cha mwaka 2011 hadi August 2013. Pia, ilibainika kuwa kazi za ujenzi zilizokuwa ikipewa kampuni ya NACOD Enterprises Ltd hazikuzingatia utaratibu wa Sheria ya Manunuzi. Kampuni ya NACOD Enterprise ililipwa jumla ya shilingi milioni 463.388 na Benki ya Posta Tanzania kwa mikataba hiyo. Kodi ya ongezeko la thamani ya kiasi cha shilingi milioni 61.851 kilikusanywa na kampuni hiyo lakini hakikurejeshwa katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa sababu kampuni zote mbili zilitumia cheti kimoja cha kughushi cha usajili wa VAT.

- 10.1.2 Ukarabati wa Jengo la Benki ya Posta Tawi la Mkwepu
Kampuni ya Kiaren Investment Ltd ilipewa kazi ya ukarabati wa jengo la Benki ya Posta tawi la Mkwepu. Benki ilitoa kazi hiyo bila kufuata taratibu za Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005. Mkataba kwa ajili ya kazi hiyo ulisainiwa tarehe 15 Novemba, 2011 na ulikuwa wa thamani ya kiasi cha shilingi milioni 86.344. Zabuni hiyo ilitolewa pia kwa njia ya kugawa zabuni maalum (Restricted Tendering) ambapo wazabuni walioshiriki

katika tenda hiyo wote hawakukidhi vigezo vya kushiriki zabuni kwa njia hiyo.

Kazi za ziada za kiasi cha shilingi milioni 144.316 zilitolewa kwa Kampuni ya Kiaren Investment Ltd na kampuni ya Havillah Business Company kwa pamoja. Utaratibu uliotumika kutoa kazi hizo za ziada haukwenda sambamba na matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma, pia ilibainika kutokuwepo kwa mikataba iliyosainiwa kati ya kampuni hizo na Benki ya Posta kwa kazi hizo za nyongeza.

Mchanganuo wa gharama (BOQ) kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Mkwepu ziliandaliwa na mtumishi wa utawala wa Benki ya Posta, ambaye pia alikuwa ni mjumbe kwenye kamati ya kuanzisha tawi la Mkwepu. Mtumishi huyo alikuwa pia mjumbe wa kamati ya tathimini ya zabuni na ndiye aliyekuwa meneja wa kusimamia kazi hiyo ya ukarabati. Pia, alikubali kazi za nyongeza kwamkandarasi huyo na kumshauri Mkurugenzi Mkuu kuzipitisha bila kufuata taratibu za Sheria ya Manunuzi. Malipo yote yaliyolipwa kwa kampuni hizo yalilipwa bila kuwasilishwa kwa cheti cha ukamilifu wa kazi (Interim certificates).

10.1.3 Utaratibu wa Ajira na Masuala ya Rasilimali Watu

- (i) Benki ya Posta Tanzania iliajiri wafanyakazi 40 kwenye nafasi mbalimbali kuanzia Julai, 2012 hadi Aprili, 2013. Ajira hizo zilikuwa zikitangazwa kupitia anuani za barua pepe za ndani (internal emails) ambazo ni [Benki ya Posta Tanzania.all@postalbank.co.tz](mailto:Benki_ya_Posta_Tanzania.all@postalbank.co.tz) na branches@postalbank.co.tz tu na kuwawezesha wale wenye “password” kuona tangazo hilo. Ajira hizo zilikuwa zikitangazwa kwa njia ya matangazo ya ndani kupitia barua pepe ambazo zinaonekana kwa wafanyakazi wa ndani tu au mtu husika aliyetumiwa barua pepe ya tangazo. Mtu yeyote asiye na “password” hawezi kuona tangazo husika. Hali hii

ilitoa mwanya kwa wafanyakazi kuwaleta marafiki, jamaa au ndugu ili kupata fursa hizo.

- (ii) Benki ya Posta iliajiri wafanyakazi watatu katika nafasi za juu na za kudumu ambao walipewa viwango vya mishahara tofauti na vilivyoainishwa kwa nafasi hizo katika Muongozo wa Utumishi wa Benki ya Posta Tanzania. Mmoja aliyepewa nafasi ya “Senior Manager Treasury -Trading”, aliajiriwa tarehe 30 Aprili, 2012 kwa mishahara wa shilingi milioni 3.6. Kulingana na viwango vya mishahara vilivyoainishwa kwenye Muongozi wa Utumishi wa Benki, mishahara uliopangwa kwa nafasi hiyo ni kati ya shilingi milioni 2.418 na 2.495 kwa mwezi. Mtumishi mwingine aliajiriwa tarehe 2 Mei, 2012 katika nafasi ya “Senior Manager Treasury - Sales” na kupewa mishahara wa shilingi milioni 5. Kulingana na Muongozo wa utumishi wa Benki ya Posta mishahara kwa nafasi hiyo ni kati ya shilingi milioni 2.418 na 2.495 kwa mwezi.

Pia ilibainika kwamba, Benki ilimuajiri Meneja Mkuu wa mikopo tarehe 10 Aprili, 2012 kwa makubaliano ya mishahara wa shilingi milioni 5.5 wakati mishahara wa nafasi hiyo ulikuwa ni kati ya shilingi milioni 3.370 na 3.466 kwa mwezi.

Ukaguzi huu maalum ulibaini kuwa taratibu za ajira kwa watumishi hao watatu hazikuwa za wazi na hazikuzingatia taratibu za ajira za Benki. Ilionekana kuwa meneja waandamizi na wakurugenzi wa benki hiyo walikuwa wakilipwa mishahara kama ilivyoainishwa kwenye muongozo wa utumishi ambayo ilikuwa midogo ukilinganisha na mishahara ya waajiriwa wanya.

10.2 Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA)

Ukaguzi maalum wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga ulifanyika kufuatia ombi la Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya kufanya ukaguzi huo maalum kwa mwaka 2010/2011 hadi Machi 2012. Matokeo ya ukaguzi huo yalikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Taasisi za Serikali zikiwemo shule, ofisi za serikali, hospitali, Polisi na vyuo zimekuwa hazilipi ankara za maji kwa Mamlaka. Kufikia tarehe 30 June, 2012 kulikuwa na malimbikizo ya madeni ya kiasi cha shilingi milioni 147.420 ya taasisi hizo. Mnamo mwaka 2000 Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji alitoa maelekezo kuwa Mamlaka isitishie huduma ya maji kwa taasisi zote za serikali ambazo hazilipi ankara za maji kwa wakati. Mamlaka ilishindwa kutimiza agizo hilo kutokana na kwamba Taasisi hizo zimekuwa zikiizuia Mamlaka hiyo kusitisha huduma ya maji ikiwa ni pamoja na kutoa vitisho kwa Mamlaka.

10.3 Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)

Ukaguzi maalum wa Ranchi za Taifa (NARCO) ulifanyika kufuatia barua kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi na barua nyingine kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Matokeo ya ukaguzi huu yalikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Mishahara ya wafanyakazi wa Shirika imekuwa ikikatwa makato ya kodi na mifuko ya jamii lakini haikupelekwa kwenye Mamlaka husika kama TRA, NSSF, PPF kwa usahihi na kwa wakati. Jumla ya shilingi milioni 716.238 zimekatwa katika mishahara ya wafanyakazi kwa kipindi cha kuanzia Juni, 1992 hadi Julai, 2012 lakini hazikupelekwa kwenye taasisi husika. Kampuni itatakiwa kulipa faini kwa ajili ya ucheleweshwaji.

- (ii) Shirika lilipata mkopo kutoka Benki ya Rasilimali ya Tanzania (TIB) na benki ya CRDB ya jumla ya shilingi bilioni 3.280. Mkopo kutoka TIB ulikuwa jumla ya shilingi bilioni 2.860 na kutoka benki ya CRDB ulikuwa shilingi milioni 420. Mikopo hiyo ilikuwa kwa ajili ya kuendesha mradi wa kununua ng'ombe, kuwanenepesha na kuwauza ikiwa ni pamoja na kukarabati miundo mbinu ndani ya ranchi za Taifa.

Mapungufu yafuatayo yalionekana katika matumizi ya mikopo hiyo:-

Mkopo wa TIB ulikuwa na riba ya asilimia 16 kwa mwaka na mkopo wa benki ya CRDB ulikuwa na riba ya asilimia 17 kwa mwaka. Riba hizo zilikuwa juu sana ukilinganisha na faida. Kampuni ya Ranchi za Taifa imeshapata hasara ya jumla ya shilingi milioni 325.901 kutoka mwaka 2011 hadi Aprili, 2013 kutokana na riba kubwa inayotozwa kwenye mikopo hiyo.

- (iii) Thamani ya ng'ombe wa mradi ambao bado hawajauzwa ni ndogo ukilinganisha na kiasi cha deni la mkopo ambao haujarejeshwa benki. Hali hii inaiweka NARCO kwenye hatari ya kuuza mali zake za ranchi zilizowekwa rehani kwa ajili ya kufidia deni la mkopo huo. Mradi uliotumia fedha za mkopo wa benki ya CRDB ulikuwa na salio la ng'ombe 380 wenye thamani ya shilingi milioni 123.806 waliopo kwenye ranchi wakati deni la mkopo ambao haujarejeshwa ni shilingi milioni 149.139 hadi kufikia mwezi Aprili, 2012. Ni wazi kuwa salio la ng'ombe waliopo hawatoshelezi kulipa deni la mkopo lililobaki.
- (iv) NARCO haikuwa na udhibiti wa ndani ulio madhubuti kwenye kuangalia fedha za mauzo ya ng'ombe. Kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 2.242 kilikusanywa

kutoka mradi uliokuwa unafadhiliwa na fedha za mkopo wa TIB ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1.820 ilikuwa ni mauzo ya fedha taslimu, kiasi cha shilingi bilioni 1.427 kiliwekwa benki na kiasi cha shilingi milioni 392.911 hakikupelekwa benki. Kiasi ambacho hakikupelekwa benki kilidaiwa kuwa kilitumika katika matumizi ya mradi lakini hakukuwa na uthibitisho uliowasilishwa kwa wakaguzi kuonyesha matumizi hayo. Kitendo hicho kilikuwa ni kinyume na matakwa ya sheria za fedha za NARCO namba 4.3.1 kinachosema kuwa, fedha zote za makusanyo zipelekwe benki kabla ya kufanyiwa matumizi mbalimbali.

- (v) Ukaguzi maalum ulibaini upotevu wa ng'ombe 376 kutoka katika Ranchi ya Ruvu katika kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Aprili, 2013. Upotevu huo ulisababisha hasara ya shilingi milioni 224.650. Hasara hiyo ilitokana na kutokuwa na mfumo sahihi na madhubuti wa kuweka kumbukumbu ya idadi ya ng'ombe kwenye vitabu. Vilevile utaratibu wa utoaji wa ng'ombe kwenye maboma na kupelekwa malishoni haukufuata utaratibu unaostahili kwani wahusika kama mkuu wa boma, mlinzi wa boma na mchungaji wa ng'ombe hawakuwa wakitia saini vitabu hivyo kuonyesha makabidhiano.

10.4 Bodi ya Korosho Tanzania

Ukaguzi maalumu wa Bodi ya Korosho Tanzania ulifanyika kufuatia barua iliyoandikwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara (RAS) iliyomuomba Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum katika matumizi ya fedha za ruzuku ya pembejeo na fedha za ushuru wa korosho ghafi zinazotolewa kwa Bodi ya Korosho Tanzania kwa ajili ya pembejeo.

Matokeo ya ukaguzi yalikuwa kama yafuatavyo:-

- (i) Uwepo wa sheria mbili zinazokinzana yaani ile ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 na Sheria ya Bodi ya

Korosho Tanzania ya mwaka 2009 iliyorekebishwa mwaka 2010 ambapo kila moja inazipa mamlaka hizo jukumu la kutunza na kupanga matumizi ya fedha za ushuru wa mauzo nje ya nchi. Hali hii inasababisha kuwepo kwa mgogoro usioisha kati ya Bodi ya korosho na Halmashauri ya Wilaya za Mkoa wa Mtwara kwenye matumizi ya fedha za ruzuku na fedha za ushuru wa mauzo ya Korosho nje ya Nchi.

- (ii) Ukaguzi ulibaini kuwa Kampuni za Mukpar Tanzania Ltd na Equatorial Africa Ltd zililipwa kiasi cha shilingi milioni 223.815 na Bodi ya Korosho ikiwa ni malipo yote kwa ajili ya pembejeo za kilimo kwa msimu wa 2009/2010. Fedha hizo zililipwa kwa mkupuo kinyume na makubaliano yaliyotaka malipo ya asilimia 50. Hadi ukaguzi huo unakamilika tarehe 26 Septemba, 2013 pembejeo hizo zilikuwa hazijapokelewa na hakuna juhudi zozote zilizofanyika kuhakikisha pembejeo hizo zinawasilishwa.
- (iii) Mnamo tarehe 30 Aprili, 2009, Afisa Kilimo wa Wilaya ya Masasi alipitisha vibali vya kununua pembejeo za ruzuku kwa makampuni ya Mukpar Tanzania Ltd na Equatorial Africa Ltd zenye thamani ya shilingi milioni 292.375. Afisa Kilimo wa wilaya aliandika barua tarehe 20 Aprili, 2009 akiyaomba makampuni hayo kukubali sehemu ya malipo kwa asilimia 50 na asilimia hamsini 50 ya pembejeo ambazo hazijalipiwa ziendele kutunzwa kwenye ghala la Mukpar kwa uangalizi wa pamoja kati ya Mfuko na makampuni hayo. Mfuko ulikiri kupokea pembejeo zote na hivyo kumwezesha Mukpar kulipwa shilingi milioni 292.375 pamoja na usafiri wa shilingi milioni 2.880. Hii ni baada ya kuwasilisha vielelezo ikiwemo idhini ya kulipa kutoka mkoani kwenye Bodi ya Korosho vinavyothibitisha kupokelewa kwa pembejeo zote wakati baadhi ya

pembejeo hizo bado zilikuwa kwenye maghala ya kampuni ya Mukpar Tanzania Ltd.

- (iv) Ukaguzi maalum ulibaini kuwa kiasi cha shilingi bilioni 1.075 kilitumiwa na Bodi ya Korosho kulipia matumizi mbali mbali ya ofisi ikiwemo mishahara, gharama za matengenezo, ankara za umeme na gharama nyinginezo ikiwa ni kinyume na maelekezo ya sheria inayotaka fedha hizo zitumike kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho Mtwara.
- (v) Halmashauri za Mtwara (M), Newala, Masasi na Nanyumbu hazikuweza kupokea kiasi cha shilingi milioni 735.082 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya wakulima wa Halmashauri hizo kutoka Bodi ya Korosho ya Tanzania. Hata hivyo Bodi ya Korosho haikutoa vielelezo vinavyoonesha uwepo wa bakaa hiyo kwa maelezo kwamba fedha zimekuwa zikitumika kulipia madai ya pembejeo hata kama hazikutumika kwenye Halmashauri husika. Kitendo hicho kinaaminika kuwa siyo sahihi na haki kwa zile Halmashauri ambazo zilikuwa zifaidike na mgao huo.

10.5 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

Ukaguzi maalum katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulifanyika kufuatia maombi ya Bodi ya Wakurugenzi wa Mfuko kupitia barua ya tarehe 11 Julai, 2013 iliyoainisha hadidu za rejea katika kufanya ukaguzi huo maalum. Ukaguzi ulikuwa mahususi kuangalia malipo yanayofanywa na Mfuko kwa mwaka unaoanzia tarehe 1 Julai, 2012 hadi tarehe 30 June, 2013. Hii ni kufuatia kuwepo kwa tuhuma za wizi unaofanywa na Watumishi wa Mfuko waliopo kwenye vituo vya afya.

Matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulionekana kutokuwa na taarifa sahihi na za kutosha kwenye

mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za wanachama wa Mfuko. Mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za wanachama haukuwa na taarifa muhimu za wanachama kama vile vitambulisho, majina, tarehe za kuzaliwa na jinsia. Kadi ambazo hazikuwa na majina zilikuwa 27, kadi za wanachama zilizokosewa tarehe za kuzaliwa zilikuwa 9,195, kadi zilizokuwa hazina tarehe za kuzaliwa zilikuwa 29,221, kulikuwa pia na kadi za wanachama 27 ambazo hazikuonyesha kama mwanachama ni mwanandoa au la na kadi 25,873 hazikuonyesha jinsia za wanachama.

- (ii) Ukaguzi ulibaini kuwa kuna watu ambao si wanachama wa Mfuko ambao walipata huduma za afya kwa kupitia kadi za wanachama wa Mfuko kinyume na mwongozo wa madai ya huduma za afya.
- (iii) Kuna madai ya bima ya afya yaliyopokelewa na kuingizwa kwenye mfumo wa kompyuta wa usimamizi wa madai (Claims Management Information System - CMIS) kwa wanachama ambao hawajarekodiwa kwenye mfumo huo. Kwa madai ambayo majina hayapo kwenye kumbukumbu za wanachama, Mfuko ulikuwa ukiingiza taarifa za wanachama hao kwa mikono kwa wale ambao taarifa zao hazikuwa kwenye mfumo huo. Kiasi cha shilingi milioni 254 kililipwa na Mfuko kwa wanachama ambao taarifa zao hazikuwa kwenye mfumo wa (CMIS) kwa mwaka 2012/2013.
- (iv) Malipo ya madai ya bima ya afya wakati mwingine yalionekana hayaidhinishwi na maafisa wa Mfuko. Kuna malipo ya kiasi cha shilingi milioni 520.117 yaliyolipwa kwa Kituo cha huduma za afya cha Regency tarehe 20 Disemba, 2012 bila kuwepo kwa uthibitisho wa kuidhinishwa na kusainiwa katika madokezo sabili ndani ya mafaili husika.

- (v) Watumishi wa Mfuko na watoa huduma za afya hawakuzingatia sera ya kupanga bei kama ilivyoainishwa kwenye mikataba ya kutoa huduma za afya. Mapungufu hayo yalionekana katika kubadilishwa kwa bei mara kwa mara, kitendo kilichofanywa na watumishi wa Mfuko wanao hakiki ubora. Kitendo hiki kimekuwa kikiendelea bila Mfuko kuchukua hatua za makusudi kusimamisha hali hiyo kwenye vituo vya huduma za afya. Kiasi cha shilingi 174.422 kililipwa na Mfuko zaidi ya bei za kawaida kwa Hospitali za Regency, TMJ, Mikocheni, IMTU na Tumaini.
- (vi) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulilipa kiasi cha fedha zaidi ya madai ya yaliyopokelewa kutoka vituo vya afya. Hospitali ya TMJ ililipwa zaidi kwa kiasi cha shilingi milioni 1.098 zaidi ya madai yaliyowasilishwa na kituo hicho. Ilionekana pia kiasi kilichothibitishwa na wahakiki ubora wa Mfuko nacho kilikuwa cha chini ukilinganisha na kiasi kilicholipwa. Kwa upande mwingine ilionekana hospitali ya TMJ ililipwa kiasi cha shilingi milioni 14.859 zaidi ya kiasi cha madai ya madawa yaliyokuwa yamerekodiwa na duka la dawa la hospitali hiyo.
- (vii) Mfuko ulifanya malipo kwa Zahanati ya Sattelite ambayo haijathibitishwa iliyo chini ya Kituo cha afya cha Regency. Katika madai ya kituo cha afya cha Regency yalijumuishwa pia madai ya kiasi cha shilingi milioni 99 ya Zahanati hiyo. Malipo yote yaliyofanyika kwa Zahanati hiyo yalikuwa juu ya kiwango cha kawaida kama vile Zahanati zilizopitishwa kwa kuleta madai ya kiwango hicho cha juu (Special Package) badala ya kutoza kiwango cha kawaida kwa Zahanati. Kiasi cha shilingi milioni 3.181 kilikuwa ni malipo zaidi ya kiwango cha kawaida ambacho kingetakiwa kulipwa katika mwezi Machi, 2013.

- (viii) Hospitali ya TMJ ilipeleka madai ya daktari kutembelea wagonjwa waliosafishwa figo (dialysis) mara kwa mara kwenye Mfuko. Madai hayo yalipelekwa kama madai tofauti na yale ya daktari kumwona mgonjwa kawaida. Kutokana na maelezo ya Kaimu Mkurugenzi wa mambo ya kiufundi na huduma za afya (Acting Director of Technical and Medical Services DTMS), alisema kwamba madai hayo hayastahili kulipwa isipokuwa panapojitokeza tatizo kubwa linalohitaji uangalizi wa karibu. Kiasi cha shilingi milioni 20.375 ya madai hayo yasiyo sahihi yalilipwa na Mfuko licha ya kuwa gharama hizo za uangalizi wa mara kwa mara kwa wagonjwa waliosafishwa figo kujumuishwa kwenye matibabu hayo mwanzoni.
- (ix) Hospitali ya Misheni Mikocheni haikuomba kibali kutoka Mfuko wa Bima ya Afya cha kuruhusu kulaza wagonjwa zaidi ya siku 10 katika wodi za hospitali hiyo. Kiasi cha madai ya jumla ya shilingi milioni 7.200 yaliwasilishwa na kulipwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambayo yalikuwa ni madai ya siku za kulazwa wagonjwa zaidi ya siku 10 bila idhini kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Hapakuwa na barua iliyotoka katika hospitali hiyo kuomba idhini ya kuendelea kuwalaza wagonjwa ambao ni wanachama wa Mfuko kwa zaidi ya siku 10. Ilionekana wazi kuwa pamoja na mapungufu hayo malipo hayo hayakusitishwa na wahakiki wa uhalisia wa madai ndani ya Mfuko.
- (x) Kulikuwa na malipo ya madai yaliyolipwa na Mfuko ambayo majina ya wagonjwa hayakuwa yamejumuishwa kwenye orodha ya madai yaliyowasilishwa na vituo vinavyotoa huduma za afya. Regista za wagonjwa waliotibiwa katika Hospitali za TMJ na Tumaini zilionesha wagonjwa ambao majina yao ni tofauti na yale yaliyopo kwenye madai yaliyowasilishwa Bima ya

Afya kwa ajili ya malipo. Jumla ya malipo yaliyofanyika Hospitali za TMJ na Tumaini kwa wagonjwa ambao majina yao hayakuonekana kwenye regista za hospitali hizo yalikuwa ni kiasi cha shilingi milioni 21.287 kwa hospital ya TMJ na shilingi milioni 20.697 kwa Hospital ya Tumaini.

10.6 Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade)

Ukaguzi maalumu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), ulifanyika kufuatia ombi la Wakurugenzi wa Bodi ya TanTrade kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kufanya ukaguzi kufuatia madai mbalimbali ambayo yalihatiji kufanyiwa uchunguzi hasa kwenye maeneo yafuatayo:- uwepo wa tiketi za kughushi za kuingia kwenye maonyesho, kuhakiki usahihi wa madeni ya Mamlaka kwa mwaka 2011/12 na robo ya kwanza ya 2012/13, kukagua utaratibu mzima katika manunuzi ya bidhaa na huduma, kukagua utaratibu uliotumika katika ukodishaji wa mabanda katika viwanja vya kimataifa vya maonyesho ya kimataifa Dar es salaam na kukagua namna ambavyo rasilimali za Mamlaka zinavyosimamiwa.

Matokeo ya Ukaguzi wa TanTrade ni kama ifuatavyo:-

- (i) **Uwepo wa Tiketi na Stika Zisizo Halisi (feki)**
Kiasi kikubwa cha mapato ya Mamlaka kinatokana na maonyesho ya Sabasaba (DITF), hivyo kuhujumiwa kwa zoezi la maonyesho kunaweza kusababisha athari kubwa katika mapato. Katika maonyesho ya 36 ya DITF uwepo wa tiketi feki ulisababisha asilimia 30 ya tiketi za watu wazima na asilimia 11 ya stika za maegesho kutouzwa ambapo jumla ya shilingi milioni 158.817 ambazo zingeweza kukusanywa.

(ii) **Kukosekana Udhhibiti wa Uwanja.**
Ukaguzi ulibaini kuwa Menejimenti ya TanTrade haikuchukua hatua stahili katika kudhibiti uwanja kwa kuainisha na kuulinda mipaka yake. Eneo la Uwanja lilivamiwa na wafanyabiashara wadogowadogo na eneo lingine kumegwa na Shule ya Msingi Mtoni Sabasaba na Barabara ya Kilwa. Hakukuwa na fidia kwa Mamlaka iliyotokana na eneo lililomegwa na barabara.

(iii) **Umilikishwaji wa Mabanda kwa Watu Binafsi**
Ilibainika kuwa Menejimenti ya Tantrade haina kumbukumbu muhimu zinazothibitisha uhusika wake katika kutoa idhini na maelekezo kwa wamiliki binafsi ambao walijenga mabanda ndani ya uwanja.

Pia kukosekana kwa mikataba na utaratibu stahili juu ya ujenzi wa mabanda ndani ya viwanja vya maonyesho kulisababisha taasisi na watu binafsi kujenga mabanda yao bila utaratibu maalum.

Hakukua na orodha sahihi ya wamiliki wa mabanda kwa vipindi tofauti vya umiliki wao, kutokana na utunzaji mbovu wa nyaraka.

Hali hiyo imesababisha mamlaka kukosa mapato kwa baadhi ya mabanda kama ya 'Carnival Bar & Restaurant' kutokana na uwepo wa shauri mahakamani, ambapo hadi sasa anayeshikilia umiliki huo anaendelea kulitumia kwa biashara za kukodisha ukumbi bila mamlaka kuingiza kipato chochote.

(iv) **Ukaguzi wa Madeni ya Mamlaka**
Madeni yenye jumla ya shilingi milioni 184.339 yalihakikiwa. Kiasi cha shilingi milioni 108.487 ya madeni yaliyohakikiwa yalibainika kuwa na mapungufu yafuatayo; kiasi cha shilingi milioni 22.089, kilidaiwa zaidi ya gharama halisi, kiasi cha shilingi milioni 51.500 kilichodaiwa hakikuthibitika uhalisia wake, kiasi cha shilingi milioni

15.100 kilichodaiwa hakikuwa na ushahidi wa mikataba, deni la kiasi cha shilingi milioni 14.098 lilikuwa na nyaraka pungufu, na kiasi cha shilingi milioni 5.700 ni madeni yaliyokiuka taratibu. Aidha madeni yaliyohakikiwa yametokana na huduma mbalimbali zilizotolewa kwa Mamlaka katika vipindi tofauti ambapo baadhi ya huduma zilizotolewa hazikuthibitika.

- (v) **Mapungufu Katika Ufuatiliaji wa Mali za Bodi ya Biashara za Ndani (BIT) na Bodi ya Biashara za Nje (BET)**
Kuunganishwa kwa majukumu ya BIT na BET kupitia Sheria Na.4 ya 2009, kulihitaji utambuzi wa mali zote za zilizokuwa BET na BIT ili kuwezesha usimamizi mzuri wa mali hizo. Ukaguzi huu ulibaini kuwa zoezi hili muhimu halikuzingatiwa kutokana na kutofanyika kwa utambuzi stahiki wa mali na madeni ya Bodi hizo kabla ya kuunganika pamoja na kuunda TanTrade. Baadhi ya taarifa zilionyesha kuuzwa kwa baadhi ya mali kwa njia ya MEBO (Management Employees Buy Out) lakini hakukua na ushahidi juu ya hatua zilizochukuliwa na TanTrade katika kufuatilia uhalali na taratibu zilizotumika katika uuzwaji wa mali husika. Vilevile zipo mali za BIT zilizokabidhiwa kwa Wakala wa Majengo kwa usimamizi ambazo wakala huo ulithibitisha kuhusika na uangalizi wake.
- (v) **Magari ya Mamlaka Yaliyotoweka Baada ya Usajili wake**
Katika kipindi cha Mwezi Augosti na Mwezi Septemba, 2012, Magari 11 yaliyosadikiwa kuwa ni ya Mamlaka yalisajiliwa kwa namba binafsi. Ildhibitika kuwa magari hayo hayakupokelewa na TanTrade baada ya usajili. Ilibainika pia kuwa Mamlaka haikujulishwa yalikopelekwa magari hayo.

Katika kutaka kujua umiliki wa magari hayo na sehemu yalipo, wakaguzi waliwasiliana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wizara ya Viwanda na Biashara lakini hadi wakati ukaguzi huu unakamilika Mwezi Februari, 2013 hakuna majibu yaliyokuwa yamepokelewa.

SURA YA KUMI NA MOJA

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

11.0 Mtazamo wa Jumla

Sura hii inatoa hitimisho na mapendekezo ya mambo yaliyojadiliwa katika ripoti hii na ambayo yanahitaji kutazamwa na kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Mashirika ya Umma. Mambo yote yaliyomo katika ripoti hii ni ya ujumla na ambayo ni muhtasari wa ripoti moja moja zilizopelekwa kwenye menejimenti za mashirika na mambo mengine muhimu yaliyojitokeza ambayo yanafaa kwa ajili ya umma kuyafahamu.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa nguvu na Kifungu cha 12 cha Sheria Na.11 ya Ukaguzi wa umma ya mwaka 2008 kutoa mapendekezo ambayo yatasaidia kuzuia au kupunguza matumizi ya fedha za umma yasiyo na tija, kuongeza ukusanyaji wa mapato, na kuondoa hasara ambazo zinasababishwa na uzembe, kutojali, wizi, ukosefu wa uaminifu, ubadhilifu na vitendo vya rushwa katika mali za umma ili kuboresha utoaji wa huduma kwa umma.

Ripoti hii inajumuisha taarifa za fedha za mashirika ya umma ambazo zimetengenezwa kwa vipindi vilivyoishia tarehe 30 Septemba, 2012, 31 Disemba, 2012 na 30 Juni, 2013. Kwa kutumia madaraka niliyopewa chini ya sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 napenda kuhitimisha na kutoa mapendekezo kutokana na kaguzi zilizofanyika.

11.1 Mapendekezo Maalum

11.1.1 Maoni ya Ukaguzi na Ripoti Zilizokamilika

Nimefanikiwa kuhitimisha kaguzi 103 kati ya kaguzi 179 zilizotakiwa kukaguliwa na ambazo zipo chini ya mamlaka yangu ya ukaguzi. Kati ya kaguzi zilizohitimishwa, ripoti za

kaguzi za mashirika 93 ziliridhiwa na bodi za wakurugenzi na hati za ukaguzi kutolewa, wakati mashirika 10 hayakuwa na Bodi za Wakurugenzi wa kuidhinisha hesabu hizo kufikia tarehe 7 Machi, 2014. Hesabu za Mashirika ya Umma 51 zilizosainiwa zilipata hati inayoridhisha wakati hesabu za mashirika 41 zilipata hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo. Pia, hesabu ya shirika 1 ilipata hati yenye shaka na suala la msisitizo. Katika kipindi cha mwaka huu hakuna shirika lililopata hati isiyoridhisha wala mbaya.

Kaguzi 74 zilizobaki zilikuwa katika hatua mbalimbali za ukaguzi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuchelewa kuwasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi, mashirika mengine kutoandaa vikao vya Bodi za wakurugenzi kwa wakati na kushindwa kwa baadhi ya wakaguliwa kujibu hoja za wakaguzi kwa wakati hali iliyopelekea kuchelewesha zoezi la ukaguzi kumalizika kwa wakati. Ninashauri mamlaka husika, kuhakikisha kwamba Bodi za wakurugenzi zinateuliwa kwa wakati pindi muda wake unapokwisha.

Lazima ikumbukwe kwamba masuala ya msisitizo yalitolewa kwa vigezo kwamba kumekuwepo kwa hali ya uzorotaji ya kiutendaji na matatizo ya kifedha yanayozikabili baadhi ya Taasisi za Umma. Hali hii ilitokana na uzorotaji wa hali ya kifedha uliochangiwa na hasara kwa zaidi ya miaka miwili mfululizo na matatizo ya kifedha yanayokwamisha mashirika ya umma kulipa madeni ya muda mfupi yanayowakabili kila yanapohitajika kulipa. Hii imepelekea uwepo wa mashaka iwapo taasisi hizi zinaweza kuendelea na kazi zake za kila siku.

Bodi za wakurugenzi na Menejimenti za Mashirika ya Umma zinatakiwa kuangalia njia mbadala za kujiongezea mapato kwa kutilia mkazo swala la kuongeza vyanzo vya mapato na kupunguza matumizi. Undani na mchanganuo wa maoni haya ya ukaguzi yameainishwa kwenye sura ya pili ya ripoti hii.

11.1.2 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ripoti Zilizopita

Katika ripoti zangu za miaka iliyopita niliweza kutoa mapendekezo ambayo yanahitaji kuingiliwa kati na kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za wakurugenzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa ajili ya ufumbuzi. Kuna baadhi ya mapendekezo yamefanyiwa kazi na mengine yapo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji.

Ofisi yangu ina jukumu la kuhakikisha kuwa mapendekezo yanayotolewa kwenye ripoti yanaleta mafanikio katika Taifa. Lakini, Kitu muhimu ambacho kinaweza kuongeza motisha ya kazi katika ofisi yangu ni kutambua jitihada zinazofanywa na ofisi yangu na kuchukua hatua za kutekeleza mapendekezo ya taarifa zangu. Ni jukumu la Serikali na wadau wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kutambua umuhimu wa mapendekezo yanayotolewa na ije na mikakati ya utekelezaji kwa ajili ya kurekebisha mapungufu hayo. Ikumbukwe kwamba mapendekezo yanayotolewa kwenye ripoti zangu za kila mwaka yanakusudia kuleta ufanisi na kufuata njia bora na sahihi za kuendesha Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Napenda kukiri kupokea majibu ya Serikali ya ripoti yangu iliyopita kupitia barua ya Mlipaji Mkuu wa Serikali yenye Kumbukumbu Na. No.EB/AG/AUDIT/12/VOL.I/53 ya tarehe 25 June, 2013. Majibu niliyoyapokea kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali hayajitoshelezi kujibu mapendekezo yote niliyoyatoa katika taarifa yangu ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ya mwaka 2011/2012. Kuna mapendekezo mengi hayajafanyiwa kazi na baadhi yako katika hatua za utekelezaji. Naiomba Serikali kuingilia kati hasa kwa yale mapendekezo yanayohusiana na Utawala Bora kwa kuwa yasipotekelzwa ndio chanzo cha matatizo kwani yanasababisha Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kutofikia malengo kutokana na muingiliano wa kimaslahi kati ya watendaji na waliopewa jukumu la usimamizi.

Kuna mapendekezo yanayohusu shirika husika la Umma na mengine ni ya jumla. Ninaomba Serikali kupitia Wizara Mama za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo, Bunge, Kamati za Hesabu za Bunge, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Bodi za Wakurugenzi kuhakikisha kuwa mapendekezo ambayo hayajafanyiwa kazi yanafanyiwa kazi ili kuongeza uwajibikaji na matumizi mazuri ya rasilimali za Taifa katika Mashirika.

11.1.3 Masuala Muhimu Ambayo Hayakutolewa Taarifa Katika Ripoti ya Mwaka Uliotangulia

Menejimenti ya makao makuu ya VETA inatakiwa kuhamisha mali zisizotumika katika kituo cha Mpanda zenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1, na kupelekwa kwenye vituo vingine ambavyo vina uhitaji wa mashine hizo. Zaidi ya hapo, Menejimenti pia inatakiwa kuhakikisha wakufunzi wote wanapelekwa mafunzo ili waweze kutumia mashine zote badala ya kutelekeza mashine hizo, ambazo ziliigharimu VETA fedha nyingi wakati wa manunuzi. Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo ambazo hazijatumika katika kituo cha Kihonda na Dakawa, napendekeza shughuli zote zilizo pangwa kufanyika kulingana na bajeti ya mwaka husika zinatekelezwa na Menejimenti ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kuepuka gharama ambazo sio muhimu kwa sababu ya ucheweleshwaji wa utekelezaji.

11.1.4 Usimamizi wa Sheria ya Manunuzi na Mikataba

Kupitishwa kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 kumeleta mabadiliko makubwa katika usimamizi wa manunuzi katika sekta za umma. Hata hivyo, licha ya uwepo wa sheria hii baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yameonekana kutotii sheria hii. Kwa hali hii inaonekana kuwa, bado kuna uelewa mdogo kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma katika kutekeleza matakwa ya sheria na kanuni zake. Haya yanathibitishwa na matokeo ya ukaguzi yaliyoanishwa kwenye sura ya tano ya ripoti hii.

Kadhalika, matokeo ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yalionyesha kuwa michakato ya manunuzi katika baadhi ya taasisi haikuwa na uwazi. Ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya taasisi hazikusimamia vyema mikataba ya manunuzi. Natoa ushauri wa jumla kwa menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kubadili mitazamo yao juu ya usimamizi makini wa mikataba wanayoingia na kandarasi mbalimbali. Mikataba hii inahitaji uangalizi wa kina mara tu baada ya kusainiwa. Usimamizi na uchambuzi wa kina juu ya mikataba iliyosainiwa na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma unahitajika ili kuepuka upotevu wa rasilimali za umma.

Kwa kuzingatia muhtasari wa matokeo ya ukaguzi katika ripoti hii natoa ushauri kwa menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuhakikisha zinaifuata kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005.

Mihimili mikuu ya manunuzi ambayo ni Mkuu wa Taasisi, Kitengo cha Manunuzi, Bodi ya Zabuni, Kamati ya Tathimini ya Zabuni na Mtumiaji lazima ifanye kazi bila muingiliano ukizingatia kazi zao na mamlaka waliyopewa kisheria chini ya kifungu cha 38 cha sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2004.

Watendaji wakuu wa taasisi wakishirikiana na vitengo vya manunuzi wanapaswa kuhakikisha kuwa mipango ya manunuzi ya mwaka inaandaliwa na pasiwepo na manunuzi yatakatofanywa bila kuidhinishwa na bodi ya zabuni

Bidhaa na huduma kabla ya kupokelewa na taasisi lazima zikaguliwe kuthibitisha ubora wake. Tatizo la muda katika mchakato wa manunuzi pamoja na gharama zidhibitiwe kwa kuzingatia miongozo na maagizo yanayotolewa na mamlaka husika (PPRA).

Nashauri pia kwamba Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ziendeele kutii sheria ya manunuzi kwa kuhakikisha zabuni zote zinashindanishwa ili kuleta uwazi na unafuu wa bei. Vitengo vya manunuzi vihakikishe kuwa manunuzi yote ya umma yanafanyika kwa mujibu wa bajeti na kwa kufuata mipango ya manunuzi kama inavyoelekeza kanuni ya 46 (9) ya tangazo la Serikali Na.97 la kanuni za sheria ya manunuzi za mwaka 2005. Nyaraka muhimu za manunuzi zinatakiwa kutunzwa vizuri kwa mujibu wa kifungu cha 56 cha sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2004 na kanuni ya 19 (1) ya kanuni ya manunuzi ya umma ya mwaka 2005.

Ni matarajio yangu kuwa vyombo vya serikali vinavyohusika na maadili ya utumishi wa umma vitachukua hatua stahiki kwa maafisa wote waliotajwa katika ripoti kwa ukiukwaji wa sheria ya manunuzi na kanuni zake.

11.1.5 Usimamizi wa Rasilimali

Ni muhimu kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kusimamia vizuri rasilimali zake ili kuongeza tija na ufanisi na kuhakikisha yanatoa huduma bora kwa jamii. Kutosimamiwa vizuri kwa rasilimali hupelekea upotevu wa mali na huweza kusababisha kufilisika kwa Shirika au Taasisi. Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinapaswa kutumia vizuri rasilimali zake ili kuzalisha mapato zaidi.

Udhibiti makini unapaswa kuwepo katika kupunguza madeni ya muda mrefu kwa kutumia sera madhubuti za ukusanyaji wa madeni kutokana na huduma zilizotolewa na kuongeza juhudi katika ufuatiliaji wa madeni ya muda mrefu ili kuhakikisha yanalipwa ndani ya kipindi kifupi kadiri inavyowezekana. Pia, malipo ya awali, yafanyike pale kunapokuwa na uhakika kuwa huduma au bidhaa zitapokelewa ndani ya kipindi kifupi.

Shughuli zinazohusu fedha taslimu na zile za kibenki zinapaswa kuangaliwa kwa ukaribu na umakini ili

kuhakikisha usalama wa fedha zilizokasimiwa kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Fedha zinazokaa benki bila kazi maalum zinapaswa kuwekezwa ili kuzalisha faida na kuongeza mapato. Kwa kuwa fedha ni rahisi zaidi kuibiwa, usuluhishi wa taarifa za benki na zile za Mashirika unapaswa kufanywa mara kwa mara.

Njia madhubuti zichukuliwe na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhubiti wa Nishati na Maji (EWURA) katika kuhakikisha eneo lililopo Ubungo Maji lililotengwa na Wizara ya Maji kwa ajili ya EWURA linaendelezwa mara moja. Kwa kufanya hivyo, EWURA itaweza kuokoa kiasi cha fedha kinacholipwa kama kodi ya pango ambacho kilikuwa ni shilingi bilioni 1.2 katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.1 katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Kuhusiana na 'flow meters' zilizotelekezwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania, maafisa wote walioshiriki katika zoezi la manunuzi wanapaswa kuwajibishwa kwa kununua bidhaa zisizo na ubora. Pia, hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya maafisa wa Wakala wa Vipimo ambao mwanzoni walitoa mapendekezo ya kutumika kwa mita hizo, na baadae kusema hazikidhi viwango. Ni wazi kuwa, hapakua na thamani ya fedha katika matumizi ya shilingi bilioni 2.5 katika ununuzi wa mita hizo.

Kwa bidhaa zilizopo ghalani ambazo hazitumiki zenye thamani ya shilingi bilioni 1.5, Mamlaka ya Bandari Tanzania inapaswa kutafuta njia ya bora ya kutumia vifaa hivyo kwani kuendelea kuvihifadhi bila matumizi yoyote kunasababisha kuongezeka kwa gharama za uhifadhi na pia inapelekea kupungua thamani kwa vifaa hivyo kwa kupitwa na teknolojia.

11.1.6 Usimamizi wa Rasilimali Watu

Kama ilivyoelezwa katika sura ya saba ya ripoti hii, usimamizi wa rasilimali watu ni eneo muhimu katika

uendelezaji wa wa mashirika ya umma kwa kuwa ina mchango mkubwa katika kutoa mwelekeo wa ujumla wa ofisi na utimizaji wa malengo ya taasisi.

Ili kuyafikia manufaa yaliyotarajiwa ya usimamizi wa rasilimali watu, inashauriwa kwamba kwa ujumla mapendekezo yote yaliyotolewa yanatekelezwa na mashirika ya umma.

Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ni sharti zihakikishe, zinakuwa na wafanyakazi wa kutosha wenye mchanganyiko unaokubalika kulingana na ujuzi walionao. Mashirika ya umma pia yafanye ufuatiliaji wa karibu kwenye Ofisi ya Rais inayoshughulikia Utumishi wa Umma kuhakikisha wanapata vibali vya ajira kwa wakati kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma pia zinashauriwa kuhakikisha kwamba taratibu za kiuteendaji kazi zinaboreshwa mara kwa mara kukidhi mahitaji kwa wakati. Pia mashirika yahakikishe makato ya kisheria ya wafanyakazi yanawasilishwa kwa wakati. Vilevile ili kudhibiti ukuaji uliokithiri wa deni la mikopo ya wafanyakazi, mashirika ya umma ni sharti waandae sera za ukopeshaji kwa wafanyakazi itakayoelekeza jinsi ya kutoza riba na kuweka ukomo wa utoaji wa mikopo kwa wafanyakazi.

Zaidi ya hayo, inashauriwa kwamba mashirika yahakikishe yanaongeza udhibiti wa uandaaji wa mishahara ya wafanyakazi kwa kufanya usuluhishi wa mishahara inayoandaliwa na hazina na ile ya shirika husika.

Pia ikiwa ni njia ya kuimarisha udhibiti wa matumizi na kulinda fedha za umma, menejimenti ya Mamlaka ya Bandari Tanzania, isimamishe malipo ya zaidi ya mara moja kwa siku kuhusiano na mikutano ya mabaraza ya wafanyakazi. Zaidi ya hayo, Serikali kupitia Msajili wa

Hazina itoe taarifa inayoeleza utaratibu wa ulipaji posho kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, badala ya kila shirika kujipangia jinsi ya ulipaji wa posho hizo.

11.1.7 Utawala Bora

Mafanikio ya shirika lolote lile kwa kiwango kikubwa hutegemea sana uadilifu kwa namna linavyoendeshwa. Kuzingatia kanuni za utawala bora ni muhimu katika kupunguza uwezekano wa kutumia madaraka vibaya na maafisa wa mashirika husika. Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kutenganisha shughuli za uendeshaji za kila siku na zile za kulisimamia shirika.

Pamoja na mapendekezo kadhaa ambayo nimekuwa nikiyatoa katika ripoti zangu za kila mwaka, bado kuna mapungufu katika idara za ukaguzi wa ndani na kamati za ukaguzi katika mashirika mbalimbali. Kwa hiyo, ninapenda kukumbushia mapendekezo niliyoyatoa katika ripoti zilizopita kuwa uongozi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma uimarishe vitengo vya ukaguzi wa ndani na kamati za ukaguzi. Uimarishwaji huu unapaswa kufanywa kwenye maeneo ya kupanga namna ya kukagua, kuhakikisha kuwa idadi ya watumishi katika idara hizo inakidhi haja, kuandaa na kuidhinisha miongozo ya ukaguzi wa ndani na kamati za ukaguzi na kuhakikisha mipango kazi ya idara za ukaguzi inaridhiwa na kamati za ukaguzi baada ya kuandaliwa.

Maelekezo yatolewayo na wizara mama kwa mashirika yaliyopo chini ya wizara hizo ni ya muhimu kwa uendeshaji wa mashirika. Mashirika na Taasisi Nyinginezo za umma hupata nyaraka, sera, maelekezo na miongozo ambayo inahusika katika uendeshaji wa shirika. Hata hivyo, ni vema kama uhusiano kati ya wizara na mashirika yakahusu mambo ya sera peke yake. Wizara kujihusisha katika shughuli za kiutendaji za kila siku inaingilia wajibu na uwajibikaji ambao umekasimiwa kwa Bodi za Wakurugenzi.

Kuna haja ya kupitia sheria na taratibu ambazo zinayapa mashirika haki ya kupata asilimia fulani au kiwango maalum kwenye mapato ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Bodi ya Wadhamini ya TANAPA inatakiwa kuishauri wizara mama na serikali juu ya mzigo wa michango mbalimbali inayotoa kwa mashirika mengine. Hali hii isipodhibitwa inaweza kuathiri utendaji wa majukumu ya uanzishwaji wa TANAPA.

Pia napendendekeza kwa menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuhakikisha wanapanga vizuri shughuli na mikutano ya Bodi za Wakurugenzi ili kutokuwa na mikutano mingi na ya mara kwa mara isiyo na ulazima. Hii itasaidia katika matumizi mazuri ya rasilimali za fedha na zisizo za fedha.

Kwa upande wa Bodi za Wakurugenzi, naendelea kuisitiza mapendekezo yangu katika ripoti zilizopita kwamba ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe kuna daftari (rejista) linaloonyesha muda wa kumalizika kwa Bodi husika ili kuandaa uteuzi wa Bodi zinazofuatia. Ikumbukwe pia kuwa kaguzi za baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma hazikukamilika kutokana na mashirika hayo kutokuwa na bodi za wakurugenzi na hivyo hazikutolewa maoni ya uwajibikaji katika maswala ya fedha.

11.1.8 Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma

Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma unaongozwa na Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1996. Sheria hii inatoa mamlaka, mwongozo na makujukumu kwa Tume ya Urekebishaji wa Mashirika Yaliyobinafsishwa/Shirika Hodhi la Mali za Serikali katika utekelezaji wa sera ya ubinafsishaji. Tangu kufanyika kwa ubinafsishaji, mambo kadhaa ya ukiukwaji wa sheria yamebainika. Napenda kuishauri serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika Hodhi la Mali za Serikali kuzingatia sheria ya mashirika ya umma ili kuondokana na uwezekano wa mgongano wa kimaslahi baina ya serikali na vyombo vingine

vilivyopewa majukumu ya kusimamia kwa mujibu wa sheria. Pia kuzingatia sheria, kufuatilia na kudhibiti mashirika yaliyobinafsishwa ili kuhakikisha kuwa yanafanya kazi sawa na mipango ya uwekezaji iliyowekwa kwa mujibu wa makubaliano katika mikataba ya mauzo.

Ninapenda pia kupendekeza kwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii ili kutathmini utendaji wa mashirika yaliyobinafsishwa na kubaini kama yanafanya kazi kwa kuzingatia makubaliano ya mikataba ya mauzo. Pia kwa mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya kuuzwa, usimamizi kwa Bodi za Wakurugenzi uimarishwe ili kuhakikisha kuwa mashirika hayo yanaendelea kufanya kazi kulingana na madhumuni ya uanzishwaji wake.

Katika kufuatilia utendaji wa mashirika kumi (10) yaliyobinafsishwa, nilibaini kuwa tarehe 11 Juni, 2011, Shirika Hodhi la Mali za Serikali lili saina mkataba na kampuni binafsi ya PKF Tanzania ili kufanya ukaguzi maalum katika kampuni ya “Kiwira Coal and Power Limited” kuanzia lilipochukuliwa na TANPOWER Resources Limited hadi tarehe 31 Disemba, 2010. Ripoti hii imebainisha mapungufu kadhaa kuhusu utendaji wa “Kiwira Coal and Power Limited” na taarifa zake kufikia tarehe 31 Disemba 2010. Serikali inahitaji kuchukua hatua za haraka kuhusu mambo yalioibuliwa na ripoti hiyo kabla ya serikali kuitwaa “Kiwira Coal Mine”.

Kwa upande wa kukuza mtaji, ifahamike kuwa soko la hisa la Dar es Salaam (DSE) lilianzishwa ili kusaidia zoezi zima la ubinafsishaji kwa kuleta mageuzi kwenye sekta ya fedha kwa kuhimiza umiliki wa hisa kwa watanzania. Ni muhimu kwa DSE ambayo ni soko pekee la hisa kufanya uhamasishaji kwa watanzania ili kuinua ufahamu wa watanzania juu ya uendeshaji wa soko la hisa na kutambua fursa zilizopo. Kwa upande mwingine, serikali ihakikishe sera na mipango iliyoidhinisha inafanyiwa kazi hususani kwa mashirika yaliyosalia kubinafsishwa ili watanzania wapate

fursa ya kuyamilki. Na kwa mashirika yaliyokwisha binafsishwa yasiyofanya vizuri serikali iyatwae kwa kuzingatia vifungu vilivyopo katika mikataba. Serikali ijitoe kwenye maamuzi ya uwekezaji ambayo yanakinzana na sera zake.

11.1.9 Matokeo ya Kaguzi Maalumu

Menejimenti ya Benki ya Posta Tanzania (TPB) inatakiwa kufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005 katika manunuzi. Usajili wa kampuni zinazopewa kazi na Benki ya Posta uhakikiwe kupitia Mamlaka husika kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB) kabla ya kuingia mikataba na kampuni hizo. Malipo ya ziada ya Kiasi cha shilingi milioni 11.942 kwa Kampuni ya Kiareni Investment zitolewe maelezo na kiasi cha VAT ya shilingi milioni 61.851 ambazo hazikuwasilishwa TRA ziwasilishwe. TPB inashauriwa kuangalia upya mishahara ya wafanyakazi ili kuondoa mapungufu yaliyoonekana, na Menejimenti ya Benki inatakiwa kutoa maelezo ya kutofuata mishahara iliyoainishwa kwenye muongozo wa utumishi (scheme of service) kwa maafisa waandazimi walioajiriwa na benki. Menejimenti ya Machinjio ya Taifa (NARCO) inashauriwa kurejesha malimbikizo ya makato ya mishahara ya watumishi ya kiasi cha shilingi milioni 716.238 kwa mamlaka husika ili kuepuka adhabu. Upembuzi yakinifu ufanyike kwenye miradi kabla ya kuomba mikopo kutoka benki ili kuhakikisha kuwa fedha za mikopo zinawekezwa kwenye miradi yenye tija. Menejimenti ya NARCO ihakikishe kuwa makusanyo ya fedha taslimu yahifadhiwe benki ili kuepuka kufanyika matumizi yasiyo ya muhimu. Hatua za makusudi zichukuliwe katika kuandaa vitabu vya kutunza kumbukumbu ya idadi ya Ng'ombe na kufuatilia mienendo yao.

Katika Bodi ya Korosho ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itoe mwongozo wa sheria mbili zinazokinzana kama Sheria ya Bodi ya Korosho ina nguvu

zaidi ya Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ihakikishe kuwa pembejeo zilizohifadhiwa kwenye maghala ya Kampuni ya Mukpar zinapelekwa kwa wakulima wa Masasi ili kuepusha hasara ya shilingi milioni 223.815. Hatua za kinidhami zichukuliwe dhidi ya watumishi wa Mfuko wa Pembejeo wa wilaya ya Masasi kwa kutotimiza wajibu wao inavyopaswa kwa kusababisha pembejeo za wakulima kutowafikia kwa kipindi cha miaka mine. Bodi ya Korosho ya Tanzania irudishe kwa wakulima kiasi cha shilingi bilioni 1.075 ambazo Bodi ilitumia katika matumizi ya kawaida ya ofisi. Bodi inashauriwa pia kulipa kwa wakulima wa Newala, Masasi na Nanyumbu kiasi cha shilingi 735.082 zilizokuwa ni mgawo wa mapato kwa wakulima wa wilaya hizo.

Menejimenti ya NHIF ihakikishe kuwa malipo ya madai ya bima ya afya yanalipwa kwa wanachama sahihi wa Mfuko. Pia yawe ni malipo ambayo yanaendana na sera za kulipa madai ya wanachama na kuacha kulipa madai mengine yote yasiyo endana na miongozo na sera ya madai. Kurugenzi ya Uendeshaji (Directorate of Operations) itoe kipaumbele kwenye zoezi la kuhakikisha kuwa, taarifa za wanachama zinakuwa sahihi kwenye mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu na kuhakisha taarifa zisizo sahihi kwenye mfumo huo zinafanyiwa marekebisho ili kupunguza udanganyifu na matukio yanayosababishia Mfuko hasara. Menejimenti ya Mfuko iangalie namna ya kuboresha mfumo wa kompyuta wa kusimamia madai (Claims Management Information System CMIS) ili kuwasaidia wahakiki madai kuweza kuoanisha madai kutoka maduka ya dawa na hospitali husika ambako madai hayo hutokea na pia kusaidia kuepuka ulipaji wa malipo ya madai mara mbili.

Menejimenti ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) inashauriwa kuboresha na kukarabati miundo mbinu na majengo yaliyopo kwenye viwanja vya maonyesho. Menejimenti ya TanTrade inashauriwa pia kuweka mfumo wa digitali katika ukusanyaji wa tiketi,

sambamba na kutumia teknolojia ya kamera (surveillance) ili kurahisisha usimamizi kwenye maeneo ya kuingilia uwanjani. Bodi ya Wakurugenzi ikishirikiana na Menejimenti ichukue hatua za haraka kuikomboa mipaka ya uwanja ikiwa ni pamoja na maeneo yaliyovamiwa. Bodi na Menejimenti zifuatilie na kuzirejesha/kuziomba mali za iliyokuwa Bodi ya Biashara za Ndani (BIT) zilizorejeshwa serikalini kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Msajili wa Hazina(TR) na Shirika Hodhi la Mali za Serikali(CHC) ili kuongeza uwezo wa rasilimali katika kusaidia shughuli za mamlaka.

11.2 Mapendekezo ya Jumla

11.2.1 Uhitaji wa Kuboresha Manunuzi ya Umma na usimamizi wa Mikataba

Manunuzi ya Umma hutumia zaidi ya asimilia 70 ya bajeti ya Serikali na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, hivyo kuwepo kwa udhibiti na uangalizi madhubuti ni muhimu sana.

Kwa miaka mingi sasa, Nchi imekuwa ikishuhudia usimamizi na maandalizi yasiyoridhisha ya mikataba. Ilibainika kuwa, mapungufu yanayoonekana kwenye mikataba hutokana na kutokuwa makini kwa wenye dhamana ya uongozi katika Mashirika na Taasisi za Umma. Viongozi hao huingia mikataba hiyo yenye mapungufu aidha kwa makusudi fulani au bila kujua ambapo husababisha hasara kwa Umma. Ili kuepukana na upotevu wa rasilimali za umma na hasara napendekeza mambo yafuatayo:-

- i. Serikali iijengee uwezo ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuiongezea rasilimali watu na fedha kuiwezesha kupitia mikataba yote kwa umakini kabla ya kusainiwa. Ofisi hiyo itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mikataba yote inakuwa ya manufaa kwa Umma. Pia, Maofisa watakao hakiki mikataba hiyo watawajibika kwa mikataba ambayo haitakua ya maslahi na manufaa kwa taifa.

- ii. Serikali na Taasisi zake zote zianzishe Kamati za Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba ambazo zitakuwa zikipitia na kuhakiki mikataba ya manunuzi iliyosainiwa na Taasisi za Umma. Uanzishwaji wa Kamati hizo uwekwe kisheria kwa kuongeza kipengele katika Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011. Kamati hizo ziwe ni kamati ndogo za Bodi za Wakurugenzi katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Katika Wizara kamati hiyo iwe chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ilihali katika Halmashauri za Serikali za Mitaa kamati hiyo iwe chini ya Baraza la Madiwani.

Wajumbe wa Kamati zilizopendekezwa, zijumuishe wajumbe wenye upeo wa kina na utaalumu kwenye shughuli za Manunuzi na usimamizi wa mikataba. Kamati hizo ndogo zitakuwa na mamlaka ya kupitia na kuridhia au kutengua maamuzi ya bodi ya zabuni wakati ambapo ikidhihirika kuwa maamuzi ya kamati yatakuwa ya manufaa kwa Umma bila kuathiri kiwango au ubora wa kazi iliyofanyika au mali inayonunuliwa.

- iii. Maafisa Masuuli (Wakuu wa Mashirika), Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika na Taasisi za Umma na wale watakaopewa dhamana kupitia mapendekezo ya kuunda Kamati ya Usimamizi wa Mikataba na Manunuzi, watatakiwa kwa muda wote kuitisha taarifa za maendeleo ya miradi ili kuhakikisha kwamba, miradi hiyo inatekelezwa kwa kuzingatia makubaliano na vigezo vilivyoainishwa kwenye mikataba iliyosainiwa.
- iv. Japokuwa Kifungu cha 60 (9) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 9 ya mwaka 2011 na Kanuni ya 59 ya Tangazo la Serikali (GN) 449 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, imeainisha ukomo kwa mikataba inayozidi shilingi milioni 50 kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ni maoni yangu kuwa, ukomo huo bado ni mdogo ukizingatia kwamba ni mikataba mingi sana inaingiwa na Serikali na Taasisi zake. Kuna haja ya kufanya utafiti kwa lengo la kupandisha kiwango cha ukomo huo ili kuipunguzia mzigo Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuharakisha mchakato wa manunuzi.

11.2.2 Mamlaka za Udhibiti Zinategemea Ushuru Unaotozwa na Taasisi Wanazozisimamia kama Moja ya Vyanzo vyake Vya Mapato

Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri Majini na Nchi Kavu (SUMATRA) ni mamlaka za udhibiti ambazo ni muhimu sana katika kuhakikisha kuwa, uendeshwaji wa mashirika mbalimbali yakiwemo mashirika ya umma yanayotoa huduma kwa wananchi, yanaendeshwa vizuri. Serikali inategemea sana mamlaka za udhibiti katika kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa na Taasisi hizo kwa wananchi ni zenye ubora wa kutosha.

Mamlaka mbalimbali za udhibiti Tanzania zinapata asilimia fulani ya mapato yake kutoka kwenye taasisi zinazozisimamia. Taasisi hizo zinapoongeza ushuru kwa wateja ndipo Mamlaka za Udhibiti zinavyozidi kufaidi katika uongezekaji wa mapato yake, hivyo kusababishia mgongano wa kimaslahi katika utendaji. Utaratibu huu unaweza kushawishi mamlaka za udhibiti katika kuhamasisha ongezeko la ushuru, hivyo kusabisha mzigo wa gharama kwa watumiaji wa huduma ambao ndio wanapaswa kulindwa na mdhibiti.

Miongoni mwa kazi ya mdhibiti ni kuhakikisha kuwa bei zinazopangwa na taasisi husika ni za kuridhisha na sio za kuumumiza mtumiaji. Endapo kutakuwa na ombi la ongezeko la ushuru kwa mtumiaji, uwezo wa Mdhibiti katika kuidhinisha ushuru huo utakuwa sio huru kwenye maamuzi, kwa sababu Mdhibiti ni mmoja kati ya watakapo nufaika kwenye ongezeko la mapato hayo endapo ataidhinisha ushuru huo. Mfumo huo wa Mamlaka za Udhibiti kujipatia kiasi fulani cha mapato kutoka kwenye taasisi hizo unaweza ukasababisha/ kuleta migogoro

mikubwa ya kimaslahi, hivyo Mdhibiti kuwa kwenye hatari ya kutosimamia vizuri mashirika hayo kama chombo huru.

Ni maoni yangu kwamba, mapato hayo ya Mamlaka za Udhibiti hayapaswi kutokana na mapato ya taasisi ambazo zinasimamiwa. Serikali inapaswa kufanya utafiti ili kupata vyanzo mbadala vya mapato kwenye mamlaka hizo ili kuepuka mgongano wa kimaslahi ambao unazikabili mamlaka hizo kwa sasa, au kutafuta jinsi ya kupunguza mgongano huo wa kimaslahi kama utaratibu huu utaendelea.

11.2.3 Kuongeza Tija na Ufanisi wa Mabaraza ya Watumiaji wa Huduma

Nimebaini kwamba serikali imekuwa ikianzisha mabaraza mbalimbali ya kuwatetea watumiaji wa huduma (Consumer Consultative Council - CCC) nchini kwa ajili ya kushughulikia haki za watumiaji wa huduma kwenye taasisi zinazoshughulikia huduma. Mabaraza mbali mbali yaliyoanzishwa yana lengo moja la kumwakilisha mtumiaji wa huduma ambapo yanatumia gharama kubwa ambazo zingeweza kupunguzwa kama mabaraza haya yangeweza kufanya kazi kama chombo kimoja. Kwa sasa kuna mabaraza manne ya kuwatetea watumiaji wa huduma/walaji kama vile Baraza la kuwatetea watumiaji/walaji wa nishati na maji (EWURA CCC), Baraza la kuwatetea watumiaji wa huduma ya usafiri wa nchi kavu na majini (SUMATRA CCC), Baraza la kuwatetea wafugaji Ngorongoro (Ngorongoro CCC) na Baraza la kuwatetea watumiaji wa Mawasiliano (TCRA CCC).

Ninaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuunganisha mabaraza hayo ili yaweze kufanya kazi kama chombo kimoja hali itakayosaidia kupunguza gharama za uendeshaji kwa kuwa na Mkurugenzi Mtendaji mmoja akisaidiwa wakurugenzi watacaoongoza kurugenzi mbalimbali za sekta husika kwa vile wote wanahudumia/kuiwakilisha jamii ile ile yenye mahitaji yanayoendana.

Pia kwa kuyaunganisha mabaraza itasababisha yawe na nguvu ya pamoja miongoni mwa mabaraza hayo na hivyo kuwa na jukwaa la pamoja kwa ajili ya kushughulikia malalamiko ya watumiaji wa huduma.

Baada ya kuanzisha taasisi hiyo, serikali italazimika kuangalia namna bora ya kuiwezesha kuwa na uhuru wa kifedha kwa kuja na njia sahihi za kufadhili shughuli za uendeshaji kinyume na sasa ambapo mabaraza haya yanategemea huruma ya mamlaka za udhibiti.

11.2.4 Mali Zinazotelekezwa au Kukosa Wamiliki

Mali zilizotelekezwa zinaweza zikawa ni fedha zilizohifadhiwa kwa niaba ya mmiliki halali ila kwa sababu moja au nyingine mmiliki halali ameziacha kwa muda mrefu bila kuchukuliwa na mwenyewe.

Nimegundua kuwa fedha/mali hizi mara nyingi hukaa bure katika taasisi za fedha kwa muda mrefu bila wamiliki wake kufahamika walipo. Fedha hizi zinajumuisha magawio yasiyochukuliwa, mishahara ya watu waliostaafu, mapato ya bima, amana zilizowekwa mahakamani, pensheni na mafao ya uzeeni, fedha za wadhamini, “escrow accounts”, akaunti za benki zisizotumika kwa muda mrefu, hati za amana zilikomaa na hundi za kusafiria. Kimsingi hizi sio mali za taasisi ambapo fedha zimewekwa kama amana au zinazozitunza bali ni za wamiliki ambao hawafahamiki walipo. Kama mali/fedha hizi hazitakuwa na usimamizi wa kutosha kuna hatari ya kufanyiwa ubadhirifu au kutumika kwa matumizi yasiyo sahihi kwa wanaohifadhi fedha hizo.

Mojawapo ya sababu zinazosababisha fedha hizo kuachwa kwa muda mrefu ni makato ya kisheria ya wafanyakazi waliofukuzwa kazi au kufa ambapo hazina bado inaendelea kupeleka michango yao kwenye mifuko ya hifadhi za jamii, amana zilizoachwa kwenye mabanki kutokana na kifo cha mmliki wake wakati huo ndugu zake hawana taarifa juu ya fedha zilizopo benki, akaunti za watoto ambazo

hufunguliwa na wazazi bila watoto kufahamu pindi wazazi wanapokufa na nyingine ni hisa zilizoachwa katika makampuni yaliyopo kwenye soko la hisa. Sababu nyingine ni amana zilizoachwa na wamiliki wao kwa sababu ya kukutwa na matatizo kama la biashara ya fedha haramu, kuhujumu uchumi na ukimbizi wa kisiasa.

Suala la mali zilizotelekezwa ni tatizo linalotambulika kitaifa linalohitaji uangalizi wa ziada kwa kuweka mifumo ya udhibiti na uhamasishaji wa umma. Katika kanuni za kisheria serikali ndio yenye mamlaka ya kutunza mali zilizotelekezwa kwa niaba ya wamiliki katika taifa lolote. Kutokana na hali hiyo nchi nyingi zilizoendelea zimeanzisha mfumo wa kisheria wa jinsi ya kutunza mali zilizotelekezwa. Mali hizi zilizotelekezwa na wenyewe zinaweza kuwa chanzo cha mapato ya serikali kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Kutokana na utawala bora ili kuweka mali zilizotelekezwa katika hali ya usalama endapo jitihada za kumtafuta mwenye mali zimeshindikana mali hizo inabidi zipelekwe kwenye idara ya mapato inayohusika na uangalizi wa mali za Umma ambayo ni Hazina.

Hivi sasa Tanzania hakuna sheria inayoelekeza jinsi ya kushughulikia fedha ambazo wenyewe hawafahamiki. Kwa hali hiyo kuna haja ya serikali kufanya utafiti wa kiwango cha mali ambazo hazina wenyewe ili kutunga sheria inayozitaka taasisi zinazoshikilia mali hizo waziwasilishe hazina kwa sababu mali hizo sio za kwao. Kama mhusika wa mali atapatikana baadae basi kabla malipo hayajafanyika lazima Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Serikali azifanyie uhakiki kujua usahihi wa madai hayo.

Orodha ya Kampuni Binafsi za Ukaguzi

S/N	Name of Audit Firm
1.	AA - Adolph Associates
2.	ABA Alliance
3.	AMAS Associate
4.	ABS Consultants
5.	ATEKAY Accountants and Auditors
6.	Auditax International
7.	BK Associates & David Malishee
8.	BAAS Associates & EVK
9.	Citizen Certified Partners Consortium
10.	Co-operative Audit and Supervision Corp
11.	Claritas International
12.	CT & Associates & Chabegan & Associates
13.	BDO Tanzania
14.	Deloitte & Touche
15.	Ernst & Young
16.	Elite Financial Managers
17.	Fincare & Company
18.	Global Finance and Business Solution
19.	Globe Accountancy Services
20.	ISM Consultants
21.	INNOVEX Auditors
22.	KPMG
23.	Martec & Company
24.	MATSAB & Company
25.	MEKONSULT Auditors
26.	MGK Certified Public Accountants
27.	MM Micro Business Consultants
28.	MURL-AATEC Associates
29.	PAN Associates
30.	Paul Clem Associates
31.	PIMA ASSOCIATES
32.	PKF Tanzania
33.	PricewaterhouseCoopers
34.	Philips & Company

S/N	Name of Audit Firm
35.	Quintex Financial Services
36.	R&S Associates
37.	Reliable Consultants,
38.	RS & Partners
39.	SBC Consultancy Services
40.	Shebrila & Co
41.	SMW
42.	TAB Consultants
43.	Tanna Sree Kumar Co.
44.	TAG System Associates
45.	Tax Pro Associates
46.	TAC Associates
47.	TANSCOTT
48.	TMC Associates/TOP Consultants Consortium
49.	Trion & Company
50.	VA Business Assurance Services
51.	WISCON Associates

Hali halisi ya Ukaguzi

	Taasisi za Fedha, Mifuko ya Pensheni na Mashirika Mengineyo	Hesabu Zimepokelewa	Ukaguzi Unae-ndelea	Kuhakiki Ubora wa Ripoti	Ripoti zilizokamili ka lakini hazina Bodi ya wakurugenzi	Hesabu Zinasubiri Kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi	Ripoti Zilizoka milika Maoni
1.	Benki Kuu ya Tanzania (BOT)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
2.	Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali za Mitaa (GEPF).	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
3.	Bodi ya Mfuko wa Bima za Amana	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
4.	Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
5.	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
6.	Mamlaka ya Ukanda wa Uwekezaji Tanzania (EPZA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
7.	Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
8.	Mfuko wa Mafao ya Wafanyakazi wa Umma (PSPF)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
9.	Benki ya Raslimali Tanzania (TIB)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
10.	Benki ya Posta Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
11.	Benki ya Twiga	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
12.	Mfuko wa Kuwekeza Tanzania (UTT)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	-
13.	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
14.	Shirika la bima la Taifa (NIC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
15.	Soko la Hisa Dar es salaam (DSE)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
16.	Mamlaka ya Udhibiti wa Hisa na Mitaji (CMSA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
17.	Bohari ya Dawa (MSD)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo

18.	Shirika la Utangazaji Tanzania(TBC)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
19.	Shirika la Masoko ya Kariakoo	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
20.	Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
21.	Shirika la Maendeleo la Vivanda Vidogo Vidogo (SIDO)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
22.	Shirika la Madini Tanzania (STAMICO)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
23.	Kampuni ya Mbolea Tanzania.	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
24.	“Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization” (TEMDO)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	-
25.	Shirika la Mafuta Tanzania (TPDC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
26.	Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
27.	Shirika la Magazeti Tanzania.	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
28.	Shirika la Nyumba Tanzania	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
29.	Ubungo Plaza Co. Ltd	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
30.	Jengo la IPS la NHC/PPF	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
31.	Shirika la posta Tanzania	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
32.	Mfuko wa Benjamin William Mkapa	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
33.	Shirika Hodhi la Rastimali za Mashirika ya Umma(CHC)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
34.	Shirika la Hifadhi ya Bahari Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
35.	Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
36.	Hifadhi za Taifa za Tanzania (TANAPA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
37.	Kituo cha Uwekezaji Tanzania	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	-
38.	Kampuni ya Kusimamia Raslimali za Shirika	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-

	la Reli Tanzania (RAHCO)						
39.	Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
40.	Mamlaka ya Bandari Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
41.	Mamlaka ya Elimu Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
42.	Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
43.	Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
44.	Kampuni ya Maendeleo ya Kiwanja cha Ndege Kilimanjaro	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
45.	Baraza la Wafugaji Ngorongoro	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
B.	Bodi, Mabaraza, Kamisheni na Mamlaka za udhibiti	Hesabu Zimepokelewa	Ukaguzi unaeendelea	Kuhaki-ki Ubora wa Ripoti	Ripoti zilizokamilika lakini hazina Bodi ya wakurugenzi	Hesabu zinasubiri Kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi	Ripoti Zilizokamilika
1.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu na Wasanifu majenzi (AQRB)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
2.	Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi (NLPC)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	Ndiyo
3.	Tume ya Ushindani (FCC)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
4.	Mamlaka ya Usajili wa Bima Tanzania (TIRA)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
5.	Shirika la Nguvu za Atomiki	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
6.	Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
7.	Baraza la Taifa la Biashara Tanzania (TNBC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
8.	Baraza la Kiswahili Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
9.	Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkuu Dodoma (CDA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo

10.	Bodi ya Usajili ya Wakandarasi	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
11.	Bodi ya Usajili ya Wahandisi	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
12.	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
13.	Baraza la Sanaa Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
14.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
15.	Bodi ya Manunuzi (PSPTB)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
16.	Baraza la Ujenzi la Taifa (NCC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
17.	Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
18.	Baraza la Taifa la uwezesaji wa kiuchumi (NEEC)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
19.	Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
20.	Baraza la Michezo Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
21.	Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
22.	Bodi ya Pareto Tanzania	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
23.	Mamlaka ya maendeleo ya Bonde la Rufiji (RUBADA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
24.	Bodi ya sukari Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
25.	Bodi ya Tumbaku Tanzania	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
26.	Bodi ya katani Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
27.	Bodi ya Korosho Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
28.	Shirika la Viwango Tanzania (TBS)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
29.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu Na Majini (SUMATRA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
30.	Mamlaka ya anga Tanzania (TCAA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
31.	Bodi ya Kahawa Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
32.	Makumbusho ya Taifa	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
33.	Mamlaka ya	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo

	Kudhibiti manunuzi ya Umma (PPRA)						
34.	Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
35.	Bodi ya Pamba Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
36.	Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
37.	Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
38.	Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania(TFNC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
39.	Bodi ya Chai Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
40.	Bodi ya Utalii Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
41.	Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHDA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
42.	Shirika la Haki Miliki Tanzania (COSOTA)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
43.	Bodi ya Maziiwa Tanzania	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
44.	Bodi ya Usajili wa Maghala Tanzania (TWLB)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
45.	Bodi ya Biashara ya Nje (TANTRADE)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
46.	Mamlaka ya Udhibiti ya Mifuko ya Kijamii Tanzania (SSRA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
47.	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
48.	Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri Majini na Nchi Kavu. (SUMATRA CCC)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
49.	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
50.	Bodi ya Nyama Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	-
51.	Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea	Ndiyo	-	Yes	-	-	-

52.	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
53.	Tume ya Usuluhishi(Fair Competition Tribunal)	Ndiyo	-	-	-	-	-
54.	“Universal Communications Services Access Fund”	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo

C.	Vyuo vya Elimu ya Juu, Tafiti na Mafunzo	Hesabu Zimepokelewa	Ukaguzi Unaendelea	Kuhakiki Ubora wa Ripoti	Ripoti zilizokamilika lakini hazina Bodi ya wakurugenzi	Hesabu zinasubiri Kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi	Ripoti Zilizoka milika
1.	Chuo Kikuu cha Ardhi	Ndiyo	-	-	-		Ndiyo
2.	Chuo Cha Elimu ya Biashara	Ndiyo	-	-	-		Ndiyo
3.	Taasisi ya Taifa ya Sukari	Ndiyo	-	-	-	-	-
4.	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania(TCU)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
5.	Chuo cha Teknolojia Dar es salaam	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
6.	Shirika la Tija la Taifa (NIP)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	-
7.	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
8.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
9.	Chuo cha Uhasibu Arusha	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
10.	Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
11.	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
12.	Chuo cha Usimamizi wa Fedha	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
13.	Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	-
14.	Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW)	Ndiyo	-	-	-		Ndiyo
15.	Shirika la Elimu	Ndiyo	-	-	-		Ndiyo

	Kibaha						
16.	Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere	Ndiyo	-	-	-		Ndiyo
17.	Chuo Kikuu Cha Mkwawa	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
18.	Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Kijijini CARMATEC	Ndiyo	-	-	-		Ndiyo
19.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Masomo ya Biashara Moshi	Ndiyo	-	-	-		Ndiyo
20.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi ya Afya Muhimbili (MUCHS)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
21.	Chuo cha Wanyama Pori (MWEKA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
22.	Chuo Kikuu cha Mzumbe	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
23.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
24.	Chuo cha Usafirishaji (NIT)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
25.	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
26.	Chuo Kikuu Cha Sokoine.	Ndiyo		-	-	Ndiyo	-
27.	Taasisi ya Saratani Ocean Road	Ndiyo	Ndiyo				
28.	Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
29.	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
30.	Chuo Kikuu cha Dodoma	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
31.	Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
32.	Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania(TAFORI)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	-
33.	Taasisi ya Utafiti na Uvuvi Tanzania (TAFIRI)	Ndiyo	-	-	-	-	-
34.	Taasisi ya Utafiti ya Wanyama Pori (TAWIRI)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
35.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa (TPRI)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
36.	Centre for Foreign Relation	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-

37.	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	-
38.	Shirika la Kutengeneza Magari (NYUMBU)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	-
39.	Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
40.	Chuo cha Ufundi Arusha	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo

D.	Mashirika ya Kutoa Huduma	Hesabu Zimepokelewa	Ukaguzi Unaendelea	Kuhakiki Ubora Ripoti	Ripoti zilizokamilika lakini hazina Bodi ya wakurugenzi	Hesabu zinasubiri Kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi	Ripoti Zilizokamilika
1.	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
2.	Mamlaka ya udhibiti wa Nishati na maji (Ewura)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
3.	Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura CCC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
4.	Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
5.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
7.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
8.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
9.	Shirika la Usambazaji wa Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam(DAWASCO)	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
11.	Mamlaka ya Maji	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo

	Safi na Usafi wa Mazingira Iringa						
12.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kigoma	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
13.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
14.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
15.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
16.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
17.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Moshi	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
18.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
19.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
20.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbinga	Ndiyo	-	-	-	-	-
21.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Rukwa	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
22.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Singida	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
23.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
24.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
25.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
26.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
27.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tukuyu	Ndiyo	-	-	-	-	-
28.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kyela	Ndiyo	-	-	-	-	-
29.	Mamlaka ya Maji	Ndiyo	-	-	-	-	-

	Safi na Maji Taka Ngara						
30.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Korogwe	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
31.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mpanda	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	-
32.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Njombe	Ndiyo	-	-	-	-	-
33.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Namtumbo	Ndiyo	-	-	-	-	-
34.	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
35.	Usafiri Dar-es-Salaam (UDA)	Hapana	-	-	-	-	-
36.	Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)	Ndiyo	-	-	-	-	-
37.	Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
38.	Kampuni ya Huduma ya Bahari	Hapana	-	-	-	-	-
39.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo
40.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama shinyanga	Ndiyo	-	-	-	-	Ndiyo

Aina ya Maoni ya Ukaguzi Yaliyotolewa 2012/2013

Hati Inayoridhisha	
Na.	Shirika au Taasisi
1.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha
2.	Bodi ya Mfuko wa Bima za Amana
3.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Soko la Mtaji (CMSA)
4.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavuu na Majini (SUMATRA)
5.	Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)
6.	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania
7.	Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)
8.	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
9.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama
10.	Chuo cha Wanyama Pori (MWEKA)
11.	Mamlaka ya Udhhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA)
12.	Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkuu Dodoma (CDA)
13.	Benki Kuu ya Tanzania
14.	Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE)
15.	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya
16.	Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO)
17.	Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB)
18.	Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (LAPF-Pension Fund)
19.	Jengo la IPS la NHC/PPF
20.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu na Majenzi (AQRB Wasanifu)
21.	Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha (AICC)
22.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza
23.	Baraza la Kiswahili Tanzania
24.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma
25.	Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)

26.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro
27.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora
28.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati
29.	Kampuni ya Maendeleo ya Kiwanja cha Ndege Kilimanjaro
30.	Chuo cha Usimamizi wa Fedha
31.	Benki ya Rasilimali Tanzania
32.	Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF Pension Fund)
33.	Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali za (GEPF)
34.	Mamlaka ya Udhhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA)
35.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga
36.	Chuo Kikuu Mzumbe
37.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA)
38.	Chuo cha Ardhi
39.	Mamlaka ya udhibiti wa Nishati na maji (EWURA)
40.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa
41.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Moshi
42.	Mfuko Benjamin William Mka
43.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga
44.	Shirika la Viwango Tanzania-TBS
45.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kigoma/Ujiji
46.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bukoba
47.	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania(TCU)
48.	Soko la Hisa Dar es salaam (DSE)

49.	Mamlaka ya Anga Tanzania (TCAA)
50.	Mamlaka ya Udhhibiti ya Mifuko ya Kijamii Tanzania (SSRA)
51.	Universal Communications Services Access Fund
Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo	
Na.	Shirika/Taasisi
1.	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)
2.	Chuo Cha Elimu ya Biashara
3	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea
4	Baraza la Taifa la Uwezesaji wa Kiuchumi (NEEC)
5.	Bodi ya Chai Tanzania
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga
7.	Baraza la sanaa Tanzania
8.	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam
9.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar-es-Salaam (DAWASA)
10.	Benki ya Posta Tanzania
11.	Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)
12.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi
13.	Shirika la Madini Tanzania (STAMICO)
14.	Shirika Hodhi la Rasilimali za Mashirika ya Umma(CHC)
15.	Chuo cha Uhasibu Arusha
16.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida
17.	Mfuko wa Mafao ya Wafanyakazi wa Umma (PSPF)
18.	Hifadhi za Taifa za Tanzania (TANAPA)
19.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya
20.	Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE)
21.	Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW)
22.	Tume ya Ushindani (FCC)
23.	Shirika la Usambazaji wa Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam(DAWASCO)

24.	Mamlaka ya maendeleo ya Bonde la Rufiji. (RUBADA)
25.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga (KASHWASA)
26.	Shirika la Elimu Kibaha
27.	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma
28.	Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)
29.	Shirika la Hifadhi ya Bahari Tanzania
30.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Masomo ya Biashara Moshi
31.	Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)
32.	Bodi ya Korosho Tanzania
33.	Bodi ya kahawa Tanzania
34.	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania
35.	Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)
36.	Bodi ya Pamba Tanzania
37.	Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CARMATEC)
38.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa (TPRI)
39.	Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)
40.	Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA)
41.	Chuo cha Ufundi Arusha
Hati Yenye Shaka	
Na.	Shirika/Taasisi
Hati Yenye Shaka na Suala la Msisitizo	
Na.	Shirika/Taasisi
1.	Mamlaka ya Majisafi na usafi wa Mazingira Mtwara
Hati mbaya	
Na.	Shirika /Taasisi

Kiambatisho IV

Na.	Shirika	Uzorongaji wa utendaji wa hali ya kifedha		Hali Halisi ya Matatizo ya Ukwasi	
		Upungufu wa mwaka huu	Upungufu wa kipindi Kilichopita	Mali za Shirika za mda Mfupi kwa mwaka huu	Madeni ya Shirika ya kipindi kifupi kwa mwaka huu
1	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga(KASH WASA	1,827,525,431	1,889,742,427	1,349,810,700	1,647,756,019
2	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga	63,025,244	268,569,758	663,938,005	1,004,518,595
3	Shirika la Madini Tanzania (STAMICO)	1,338,999,887	1,356,387,914	1,137,233,596	1,411,825,134
4	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)	177,399,000,000	43,349,000,000		
5	Bodi ya Pamba Tanzania	377,635,000	63,059,000		
6	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea	1,937,413,157	1,358,554,497	264,139,721	903,070,019
7	Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Kiuchumi (NEEC)	326,291,000	135,392,000	866,270,000	671,948,000
8	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania	2,736,352,171	1,768,265,400	269,077,703	577,277,100
9	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida	323,861,478	239,943,691	279,313,524	955,241,832
10	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam	446,093,759	474,277,833		
11	Shirika la Elimu Kibaha	1,883,980,523	933,572,789	1,524,131,642	2,420,500,553
12	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma	386,899,359	359,821,784	3,082,332,757	3,260,852,761
13	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar-es-Salaam	17,159,383,000	21,052,000,000	23,782,145,000	43,406,185,000

	(DAWASA)				
14	Mamlaka ya Elimu Tanzania(TEA)	1,709,827,613	1,316,040,395		
15	Shirika la Hifadhi ya Bahari Tanzania	823,838,000	593,704,000	269,883,000	385,969,000
16	Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Masomo ya Biashara Moshi	3,211,691,000	1,070,787,000		
17	Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW)	176,560,476	327,690,023		
18	Bodi ya Korosho Tanzania			870,194,000	1,230,461,000
19	Bodi ya kahawa Tanzania	439,256,000	751,552,000		
20	Mamlaka ya Majisafi na usafi wa Mazingira Mtwara	514,961,118	161,923,287	2,091,975,023	5,565,169,133
21	Chuo cha Uhasibu Arusha	95,933,723	582,014,133		
22	Chuo Cha Elimu ya Biashara	877,479,799	226,913,649		
23	Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA)	277,000,000	363,000,000		
24	Baraza la sanaa Tanzania	187,250,723	214,734,495	108,025,719	307,043,986
25	Tume ya Ushindani (FCC)	330,655,632	615,499,071		
26	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa (TPRI)	386,015,000	936,752,000		
27	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi	260,256,810	143,756,293	135,412,932	1,228,905,238
28	Chuo cha Ufundi Arusha	1,261,430,323	1,566,014,581	768,180,045	965,557,241